

**TASWIRA YA MWANAMKE KIONGOZI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA
KISWAHILI TANGIA MWAKA 2000 HADI 2016**

NA:

OGONDA SAMUEL SINZORE

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MASENO

©2019

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile. Haki zote zimehifadhiwa. Unakili wa tasnifu hii kwa mfumo wowote ule bila idhini yangu na /au Chuo Kikuu cha Maseno hauruhusiwi kamwe.

Sahihi..... Tarehe.....

Ogonda Samuel Sinzore

PG/MA/00042/2013

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa kibali chetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo cha Maseno:

Sahihi..... Tarehe.....

DKT. DEBORAH NANYAMA AMUKOWA

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Afrika

Chuo Kikuu cha Maseno

Sahihi..... Tarehe.....

DKT. BEVERLYNE AMBUYO ASIKO

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Afrika

Chuo Kikuu cha Maseno

SHUKRANI

Kwanza nimshukuru Maulana kwa kunipa afya, hekima na stahamala kutekeleza kazi hii. Shukrani natoa kwa Chuo Kikuu cha Maseno hasa idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunisajili, kunipa mafunzo na kudhamini tasnifu hii. Pongezi zangu za dhati natoa kwa wasimamizi na washauri wangu: Dkt. Asiko Beverlyne na Dkt. Nanyama Deborah Amukowa kwa kunishauri na kunielekeza. Hawa walijitolea kusoma na kuhakiki kazi hii. Nilipoelekea kulegea, walinipa moyo. Katu siwezi kumsahau Prof. Indede Florence, Mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Maseno, kwa mafunzo na mahimizo. Namshukuru kwa udhati wa moyo Dkt. Imbayi Ronald, Mchungaji wa kanisa la Word of Faith Church Majengo-Vihiga kwa motisha na maombi. Namshukuru mke wangu wa dhati, Bi. Maureen Juma kwa mengi yasiyo mfano aliyotenda kuhakikisha kuwa kazi hii imetimilika. Nawashukuru binti zangu wawili: Hephzibahope Hadasa na Beula Glory kwa stahamala yao nilipokuwa nikiufanya utafiti huu. Shukrani ziwaendee wazamili wenzangu wakiongozwa na Bw. Peter Ochieng'. Wakati bahari ya masomo ilikumbwa na mawimbi, tulihimizana kuwa tutafika ufuoni. Siwezi kusahau kushukuru Tume ya Kuajiri Walimu nchini Kenya na Bw. Henry Biggedi, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Upili ya Dr. Maurice Dang'ana. Kuna watu wengi waliofaulisha kazi hii. Siwezi kuwataja wote kwa majina. Natambua mchango wao na naomba Rabana awabariki.

TABARUKU

Kwa mamangu mpendwa, Florence Afandi Ogonda, kama si wewe singejiunga na shule ya upili wala singeyakamilisha masomo yangu ya shule ya upili.

IKISIRI

Fasihi ni kioo cha jamii. Kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi na matukio katika jamii. Vijenzi vya fasihi ni fani na maudhui na mojawapo ya vipengele vya fani ni wahusika. Fasihi andishi ya Kiswahili ina tanzu nne: riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Taswira ya wahusika katika tamthilia hubainika kupitia kwa mazungumzo na matendo yao. Tafiti nyingi zilizofanywa kumhusu mhusika mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za kabla mwaka 2000 zilimsawiri mwanamke kwa ujumla bila kuangazia uongozi wake. Chache zilizomwangazia mwanamke kiongozi zilimsawiri kwa njia hasi. Uongozi ni swala lenye umuhimu katika jamii. Ingawa kumekuwepo na wanawake viongozi kabla ya mwaka 2000, hadhi yao imekuwa ya chini. Mabadiliko yaliyotokea katika jamii kuanzia mwaka wa 2000 yameleta hali ambapo hadhi ya mwanamke kuhusiana na suala la uongozi inaimarika na jamii kuonekana kukubali uongozi wake. Baadhi ya waandishi wa tamthilia kuanzia mwaka 2000 wanamsawiri mwanamke kwa njia chanya kupitia kwa tamthilia zao. Kuna haja ya kuwepo na tafiti ambazo zitachunguza iwapo mwanamke kiongozi katika tamthilia za Kiswahili kuanzia mwaka 2000 bado amesawiriwa kwa njia hasi au ikiwa taswira hii imebadilika. Mwaka 2000 ni tarehe muhimu katika ukuaji wa sura ya mwanamke kiongozi kwa kuwa ni kuanzia mwaka huu ndipo kuna ongezeko la waandishi wa tamthilia wanaomsawiri mwanamke kwa njia chanya. Utafiti huu ulilenga kuchunguza taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahsusi yafuatayo: kupambanua sifa za mwanamke kiongozi zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000; kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule; kutathmini athari ya taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia teule. Nadharia iliyoteuliwa kwa utafiti huu ni nadharia ya udenguuzi iliyoasisiwa na Derrida (1966) na kuelezwa na Ntaragwi (2004). Misingi ya nadharia hii ni pamoja na: lugha, muktadha na mitazamo. Utafiti huu ulichunguza namna mitindo ya lugha, matendo na mitazamo ya wahusika inavyomsawiri mwanamke kiongozi. Athari ya taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke vilevile ilichunguzwa. Muundo wa kiuchanganuzi ulitumiwa. Utafiti huu uliangazia tamthilia ishirini na tatu za Kiswahili zilizotungwa kuanzia mwaka wa 2000 kwa kuwa ni katika kipindi hiki ambapo hadhi ya mwanamke kiongozi inaimarika na jamii kuonekana kukubali uongozi wa mwanamke. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu, utafiti huu uliteua tamthilia 4: *Pango* (Wamitila, 2003), *Posa za Bikisiwa* (Mohammed & King'ei, 2008), *Kimya Kimya Kimya* (Mohammed, 2011) na *Kigogo* (Kea, 2016). Mbinu ya maktaba ilitumiwa kukusanya data. Tamthilia teule zilisomwa na data kunukuliwa kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi. Data hii ilipangwa kisha ikachanganuliwa kwa njia ya uhakiki wa yaliyomo. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Imeibuka kupitia utafiti huu kwamba mwanamke kiongozi katika tamthilia za kuanzia mwaka 2000 hadi 2016 amesawiriwa kwa njia chanya. Aidha, imeibuka kuwa mitindo ya lugha imechangia kuchora picha ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule. Isitoshe, utafiti huu umebaini kuwa tendo la mwanamke kujitokeza kuongoza linamletea changamoto mbalimbali. Hata hivyo, mwanamke kiongozi anakabiliana na changamoto hizi na kuibuka mshindi.

ABSTRACT

Literature is the mirror of society. There is a big relationship between literature and the happenings in society. Aspects of literature are in style and theme and characters are one of the aspects of style. Swahili written literature has four genres: novel, play, short stories and poetry. Characters' image in the play is usually brought out through their conversations and actions. Many studies that have been conducted on female characters in plays before 2000 portrayed the woman generally without focusing on her leadership. Few which focused on the female character portrayed her negatively. Leadership is an aspect of significance in society. Although we have had women leaders before 2000, their status has been low. The changes in society since 2000 have brought about a situation whereby the status of women leaders is improving and the society seemingly accepts their leadership. Some of the play writers since 2000 are portraying the woman positively through their plays. There is need of having studies that will investigate if the woman leader in Swahili plays since 2000 is still being portrayed negatively or if this portrayal has changed. The year 2000 is a key date in the growth of the image of the woman leader because it is from this year that there is an increase in the number of play writers who are portraying the woman positively. This study aimed at investigating the portrayal of the woman leader in selected Swahili plays since 2000. This study was guided by the following specific objectives: describe the characterization of the woman leader in selected Swahili plays since 2000; analyze stylistic devices used to portray the woman leader in selected Swahili plays since 2000; evaluate the impact of the portrayal of the woman leader on women leadership in selected plays. The theory that is adopted for this study is the Deconstruction Theory that was propounded by Derrida (1966) and explained by Ntaragwi (2004). The tenets of this theory include: language, context and perceptions. This study investigated how stylistic devices, perceptions and actions of characters portray the woman leader. The impact of this portrayal to women leadership was also investigated. Analytical research design was employed. This study focused on 23 Swahili plays that have been written since 2000 because it is in this period that the status of women leaders is improving and the society seemingly accepts their leadership. Through purposive sampling technique, this research sampled 4 plays: *Pango* (Wamitila, 2003), *Posa za Bikisiwa* (Mohammed & King'ei, 2008), *Kimya Kimya Kimya* (Mohammed, 2011) and *Kigogo* (Kea, 2016). Library method was used to collect data. Selected plays were read and data recorded with the help of an observation checklist. This data was organized and analyzed through content analysis. Findings were presented through explanation. It has emerged through this study that the woman leader in selected Swahili plays has been portrayed positively. Similarly, it has emerged that stylistic devices have contributed towards portraying the woman leader in selected Swahili plays. Moreover, this study has demonstrated that the woman leader's action of coming out to lead brings her various challenges. However, the woman leader in selected Swahili plays since 2000 to 2016 faces these challenges and emerges victorious.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
SHUKRANI.....	iii
TABARUKU	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ORODHA YA VIFUPISHO	x
MAELEZO YA ISTILAHU.....	xi
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Usuli.....	1
1.2 Swala la Utafiti	6
1.3 Maswali ya Utafiti.....	7
1.4 Madhumuni ya Utafiti.....	7
1.5 Upeo wa Utafiti.....	7
1.6 Misingi ya Uteuzi wa Mada.....	8
1.7 Dhima ya Utafiti	9
1.8 Misingi ya Kinadharia.....	10
SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI.....	15
2.1 Utangulizi.....	15
2.2 Nafasi ya Taswira katika Tamthilia ya Kiswahili	15
2.3 Nafasi ya Mitindo ya Lugha katika Kujenga Taswira ya Mhusika.....	25
2.4 Mapitio Kuhusu Nadharia ya Utafiti.....	27
2.5 Hitimisho.....	29
SURA YA TATU: NJIA NA MBINU ZA UTAFITI	30
3.1 Utangulizi.....	30
3.2 Muundo wa Utafiti	30
3.3 Muktaba wa Utafiti	30
3.4 Kundi Lengwa.....	31
3.5 Sampuli na Usampulishaji	31
3.6 Mbinu za Ukusanyaji data	32
3.7 Uaminifu na Uthabiti wa vifaa vya kukusanya data	33

3.8 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data.....	34
3.9 Masuala ya Kimaadili	34
3.10 Hitimisho.....	35
SURA YA NNE: TASWIRA MWANAMKE KIONGOZI KATIKA TAMTHILIA TEULE.....	36
4.1 Utangulizi.....	36
4.2 Sifa za Mwanamke Kiongozi.....	36
4.2.1 Mwanamke kama Kiongozi Mwenye Msimamo Thabiti.....	36
4.2.2 Mwanamke kama Kiongozi Mzindushi na Mtetezi wa Haki.....	43
4.2.3 Mwanamke kama Kiongozi Jasiri.....	47
4.2.4 Mwanamke kama Kiongozi Mshawishi.....	53
Kingi anakiuka amri ya Majoka ya kuwapiga wananchi risasi.....	57
4.2.5 Mwanamke kama Kiongozi Msema Ukweli kwa Uwazi.....	57
4.2.6 Mwanamke kama Kiongozi Mzalendo	61
4.2.7 Mwanamke kama Kiongozi Mkakamavu	63
4.2.8 Mwanamke kama Kiongozi Anayejiheshimu na Kuheshimu Wengine.....	67
4.2.9 Mwanamke Kama Kiongozi Mwerevu na Mwenye Busara	69
4.2.10 Mwanamke kama Kiongozi Mwenye Lengo na Maono	73
4.2.11 Mwanamke kama Kiongozi Msomi	76
4.2.12 Mwanamke kama Kiongozi Mlumbi	77
4.3 Mitindo ya Lugha Inayojenga Taswira ya Mwanamke Kiongozi.....	78
4.3.1 Takriri	79
4.3.2 Maswali ya balagha.....	88
4.3.3 Methali	95
4.3.4 Jazanda.....	98
4.3.5 Tashbihi.....	102
4.3.6 Nahau na Misemo	106
SURA YA TANO: ATHARI YA TASWIRA YA MWANAMKE KIONGOZI KWA UONGOZI WA MWANAMKE.....	112
5.1 Utangulizi.....	112
5.2 Athari Hasi za Taswira ya Mwanamke Kiongozi kwa Uongozi wa Mwanamke	112
5.2.1 Kudharauliwa na Kukejeliwa kwa Mwanamke Kiongozi	112
5.2.2 Mwanamke Kiongozi Kusingiziwa maovu.....	124
5.2.3 Kutishwa, Kupigwa, Kukanwa na Kutengwa kwa Mwanamke Kiongozi	127

5.3 Athari Chanya za Taswira ya Mwanamke Kiongozi kwa Uongozi wa Mwanamke katika Tamthilia teule za Kiswahili.....	133
5.3.1 Kubadilika kwa Mitazamo Hasi Kumhusu Mwanamke Kiongozi.....	133
5.3.2 Kuheshimiwa, Kusherehekewa na Kusifiwa kwa Mwanamke Kiongozi	136
5.3.3 Ushindi wa Mwanamke Kiongozi.....	140
5.4 Hitimisho.....	144
SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.....	145
6.1 Utangulizi.....	145
6.2 Muhtasari wa Tasnifu	145
6.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	146
6.4 Hitimisho la Utafiti	147
6.6 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye.....	149
MAREJELEO	150
VIAMBATISHO	160
Kiambatisho 1: Sifa za Mwanamke Kiongozi	160
Kiambatisho 2: Mitindo ya Lugha	161
Kiambatisho 3: Athari ya Taswira ya Mwanamke Kiongozi kwa Uongozi wa Mwanamke	162
Kiambatisho 4: Barua ya idhini Kutoka Tume ya Kimaadili.....	163
Kiambatisho 5: Barua ya Kuidhinisha Pendekezo la Utafiti.....	164

ORODHA YA VIFUPISHO

TUKI: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Bw.: Bwana

AAUW: American Association of University Women

WHO: World Health Organisation (Shirika la Afya Ulimwenguni)

tz - tazama

uk. - ukurasa

MAELEZO YA ISTILAHU

1. Taswira: Jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana; pia usawiri.
2. Mwanamke: Mtu yeyote wa jinsia ya kike bila kuzingatia umri. Pia mhusika wa jinsia ya kike au mhusika wa kike.
3. Kiongozi: Mtu ambaye huwaelekeza na kuwachochea watu kutekeleza shughuli fulani.
4. Uongozi: Shughuli yenye kuathiri au kuelekeza watu kufikia lengo fulani.
5. Mwanamke kiongozi: Mtu yeyote wa jinsia ya kike ambaye huwachochea na kuwaelekeza watu kutenda jambo fulani. Pia atarejelewa kama mwanamke wa jinsia ya kike.
6. Mtindo: Jinsi ya kufanya kitu kwa kufuata utaratibu fulani.
7. Lugha: mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa kwa mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake.
8. Mitindo ya lugha: Jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake.
9. Mukadha: Mazingira au hali ambamo tukio au jambo hutendeka.
10. Mtazamo: jinsi mtu huchukulia au kufikiria kuhusu jambo fulani; mawazo ya mtu juu ya jambo fulani.

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Usuli

Fasihi ni kioo cha jamii. Kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi na matukio katika jamii (Matti, 2003). Kwa mujibu wa Wamitila (2003) vijenzi vya fasihi ni fani na maudhui. Mojawapo ya vipengele vya fani ni wahusika. Isitoshe, fasihi hugawika katika tanzu na mojawapo ni tamthilia.

Kulingana na TUKI (2014), tamthilia ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo na aghalabu huweza kuigizwa.

Mwanamke ni mtu yeyote wa jinsia ya kike (TUKI, 2014). Kimatumizi, neno mwanamke huashiria mtu wa jinsia ya kike aliye na utu uzima au aliyekomaa na kufikia umri wa kuolewa ilhali mwanamke mchanga au yule ambaye bado hajaolewa huitwa msichana katika tamaduni nyingi ulimwenguni (Hora, 2014). Hata hivyo, neno mwanamke hutumiwa wakati mwingine kumtambulisha binadamu wa jinsia ya kike bila kujali umri. Mathalani, tunaposema haki za mwanamke tunaashiria haki ambazo mtu yeyote wa jinsia ya kike anazo pasi na kujali umri. Kwa minajili ya utafiti huu, dhana mwanamke ilitumiwa kwa maana ya mtu yeyote wa jinsia ya kike bila kuzingatia umri.

Kulingana na TUKI (2014) kiongozi ni mtu anayesimamia na kuelekeza watu au kikundi cha watu, wafanyakazi au shughuli fulani. Inaendelea kueleza kiongozi kama mkuu fulani. Mdee, Njogu & Shafi (2011) wanaeleza kiongozi kama mtu mwenye madaraka ya kuelekeza watu wengine. Kwa mujibu wa Kohlrieser (2006) kiongozi ni mtu ambaye huwashawishi watu wengine kumfuata na kuwachochea watu kufikia malengo fulani. Yeye huijua njia na kuonyesha wengine njia hiyo (Farewell, 2011; Hora, 2014). Kutokana na fasiri hizi, ni bayana kwamba kiongozi ni mtu ambaye huelekeza na kuchochea watu kutekeleza shughuli fulani. Huenda kiongozi asiwe mkuu aliyechaguliwa kwa njia rasmi bali watu hutaka kumfuata kwa ajili ya mawazo mapya aliyo nayo. Utafiti huu ulizingatia mwanamke kiongozi kama mtu yeyote wa jinsia ya kike ambaye huwachochea na kuwaelekeza watu kutenda jambo fulani. Utafiti huu ulimwangazia kiongozi wa jinsi katika tamthilia teule.

Mirikau (2011) anaibua hoja kuwa taswira ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Anaendelea kusema kwamba picha hii aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa kupitia mambo yanayompitikia akilini mwa binadamu na kwamba mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Kutokana na maelezo haya ya Mirikau, inabainika kwamba taswira ya mhusika hudhirika kupitia kwa matendo na mitazamo yake na ya wahusika wengine. Kwa maoni ya Wamalwa (2005) taswira ya wahusika huwa ni mwangwi au fumano la jamii na kwamba wahusika huweza kusawiriwa kama kwamba hao ni viumbe wanaoishi katika jamii halisi. Ni bayana kutokana na mawazo ya Wamalwa kuwa muktadha wa jamii husika huwa muhimu katika kuchunguza taswira ya wahusika katika fasihi. Kulingana na Onyoni (2012) kufahamu muktadha kunatusaidia kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika katika fasihi. Kunayo miktadha mbalimbali, ya: kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiuchumi (Wamitila, 2003). Ni katika misingi hii ambamo picha za wahusika zinaweza kubainika vyema (Murumba, 2011). Kwa kuchunguza taswira ya mwanamke kiongozi, utafiti huu umejikita katika miktadha ya kisiasa, kijamii na kitamaduni ya tamthilia teule.

Kulingana na TUKI (2014) mtindo ni jinsi ya kufanya kitu kwa kufuata taratibu fulani. Lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa kwa mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake (Trudgil, 1974; TUKI, 1990). Wamitila (2003) anaibua hoja kuwa mitindo ya lugha ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Mitindo ya lugha ni muhimu katika kuibua maudhui ya kazi za fasihi (Mugambi, 1982; Murungi, 2013). Syambo & Mazrui (1992) wanasisitiza umuhimu wa lugha kwa kusema kwamba, lugha inahitaji kuwatofautisha wahusika kulingana na jinsia yao. Kulingana na Njogu na Chimera (1999) taswira hutokana na ufundi wa msanii katika kuteua na kupanga maneno yake ya kazi fulani ya kifasihi. Ipo haja ya kuhusisha mitindo ya lugha na suala la uongozi wa mwanamke kwani ni kupitia lugha ambapo taswira ya mwanamke kiongozi inaweza kubainika.

Uongozi ni suala muhimu katika jamii yoyote ile. Uongozi ni shughuli yenye kuathiri au kuelekeza watu kufikia lengo fulani (TUKI, 2014). Uongozi katika jamii wafaa kuwa jumuishi: umshirikishe mwanamume pamoja na mwanamke. Kwa maoni ya Mcclullough (2015) kumekuwepo na wanawake viongozi hata kabla ya mwaka wa 2000. Mifano ya wanawake ambao wamekwea ngazi ya uongozi katika mataifa mbalimbali ya ulimwengu kabla ya 2000 ni: Margaret Thatcher wa Uingereza, Corazon Aquino wa Ufilipino, Golda Meir wa Israeli, Indira

Gandhi wa India, Bhutto wa Pakistan na Angela Merkel wa Ujerumani. Hadhi na idadi ya wanawake viongozi kabla mwaka wa 2000 ilikuwa ndogo ikilinganishwa na viongozi wanaume (Afkhami, 2003).

Hadhi na idadi ya wanawake ulimwenguni imebaki duni ikilinganishwa na ya wanaume (Jalalzai & Krook, 2010). Ingawa sehemu kubwa ya idadi ya watu ulimwenguni huchukuliwa na wanawake, wao hawashirikishwi katika maamuzi ambayo yanaathiri jamii zao (Afkami, 2003; Mapunjo, 2014). Kwa maoni ya Donald (2000) kati ya kampuni elfu moja zilizo maarufu nchini Marekani katika mwaka wa 2000, ni kampuni tatu tu zilizokuwa na wanawake viongozi. Asilimia ya wanawake waliokuwa wakishikilia nafasi za usimamizi katika nchi zilizoendelea kufikia mwaka wa 2003 ilikuwa karibu thelathini na tatu. Barani Afrika ilikuwa asilimia kumi na tano na katika bara Asia na visiwa vya Pacific ilikuwa asilimia kumi na tatu. Katika Umoja wa Mataifa, wanawake walishikilia asilimia tisa tu ya vyeo vya ngazi za juu, asilimia ishirini na moja vyeo vya ngazi za uandamizi na asilimia arobaini na nane ya vyeo vya ngazi za chini kufikia mwaka wa 2003 (Afkhami, 2003). Kwa mujibu wa Migiro (2013) baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 nchini Kenya, nchi ya Kenya ilikuwa na idadi ndogo ya wabunge wa jinsia ya kike katika bunge la taifa (asilimia kumi na tisa pekee) ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika Mashariki. Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Usawa nchini Kenya, Bi. Winfred Lichuma, akiwa mjini Kwale tarehe 26 Novemba 2015 alilalamikia kubaguliwa kwa wanawake katika uteuzi wa mawaziri uliokuwa umefanywa na rais wa Kenya, Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, ambapo wanawake watano na wanaume kumi na tano waliteuliwa mawaziri (Murimi, 2015). Katika uchaguzi wa mwaka wa 2017, idadi ya wanawake viongozi waliochaguliwa ilikuwa ndogo ikilinganishwa na ya viongozi wa kiume (Munysia & Wandiemba, 2017; Oluoch, 2017).

Viongozi mbalimbali wa ulimwengu wametambua hali duni ya mwanamke na wamejitokeza kusesitiza umuhimu wa usawa wa kijinsia katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katibu wa Umoja Mataifa Bwana Ban Ki-Moon mnamo tarehe 7 Machi mwaka wa 2014 akiwa Vienna (Austria) alisema kuwa, usawa kwa wanawake ni maendeleo kwa wote (Moon, 2014). Waziri wa mambo ya nje wa zamani wa Marekani, Bi Hillary Clinton, mnamo tarehe 7 Machi mwaka wa 2014 akiwa Vienna alisema kuwa, wanawake wanaposhinda, ulimwengu unashinda na hivyo ajenda mpya ya maendeleo ni lazima iwe jumuishii (Clinton, 2014). Rais wa Marekani Bwana

Barack Obama akihutubia taifa akiwa Washington D.C tarehe 20 Januari mwaka wa 2015 alilitaka bunge la Marekani kupitisha sheria itakayohakikisha usawa baina ya wanawake na wanaume (Obama, 2015).

Hali katika jamii kwa sasa imeanza kubadilika. Kwa mujibu wa Mulila (2009) wanawake sasa wanashikilia nyadhifa za uongozi katika nyanja mbalimbali za ulimwengu. Kunao wanawake viongozi katika vyuo vikuu, mabaraza ya mawaziri, mabunge, mashirika na makampuni mbalimbali ya ulimwengu. Wanawake 16 walichaguliwa kama wabunge wa bunge la taifa katika uchaguzi mkuu wa 2013 nchini Kenya (Mwende, 2015, Oluoch 2017). Katika uchaguzi mkuu wa 2017 nchini Kenya, jumla ya wanawake 23 walichaguliwa kuwa wabunge katika bunge la taifa, 3 kuwa maseneta katika bunge la seneti na 3 kuwa magavana wa majimbo (Oluoch, 2017). Ikumbukwe kwamba katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 hakuna mwanamke alichaguliwa kuwa seneta au gavana nchini Kenya. Idadi ya wanawake waliochaguliwa katika uchaguzi mkuu nchini Kenya mwaka wa 2017 ni ya juu zaidi kuwahi kutokea katika historia ya nchi ya Kenya. Kwa mujibu wa Munyaneza (2013) nchi ya Rwanda imejitahidi kuwakweza wanawake kwenye viti vya uongozi. Wanawake nchini humo wanashikilia asilimia sitini na nne ya nyadhifa bungeni. Kulingana na Mureithi (2015) kati ya vyuo vikuu ishirini na viwili vya umma nchini Kenya, vinne vinaongozwa na machansela wanawake. Hadhi ya viongozi wa jinsia ya kike imeendelea kuimarika ulimwenguni kote (Jalalzai & Krook, 2010; Hussen, 2016).

Kunazo tafiti zilizofanywa katika fasihi kuhusu wahusika wa kike na kiume. Tafiti nyingi zilizofanywa kuwahusu wahusika wa kike zimedhihirisha nafasi duni aliyopewa mwanamke (Chesaina, 1987; Muniu, 2013). Wamalwa (2005) akimnukuu King'ei (2002) anasema kwamba tahakiki nyingi zilizofanywa kuhusu suala la mwanamke katika fasihi ya Kiswahili zimelalamikia hoja ya kukandamizwa na kutoshirikishwa kwa mwanamke katika vipengele muhimu vya maisha ya jamii. Chacha (2013) anasema kwamba, katika baadhi ya kazi za kifasihi, aghalabu mwanamke husawiriwa kama kiumbe dhaifu, mnyonge, mtu asiye na haki, mwoga na pia kama chombo kisichotamanika. Anaendelea kudai kuwa, wakati mwingine wasanii huchora wanawake kama watu wanaodharauliwa na kukosa ushirikiano baina yao. Hali hii imefanya mwanamke kutoangaziwa pakubwa kama kiongozi katika fasihi ya Kiswahili. Selden (1989) naye anaibua maoni kuwa, historia ya fasihi imetawaliwa na mamlaka ya kuumeni ambapo wanawake wamedunishwa. Senkoro (1982) anadai kwamba, wanawake wa Kiafrika

wanaumia mikononi mwa waandishi wanaume. Hali hii ndiyo inamfanya Indede (2011) kupendekeza kuwa, ili kujikomboa na kujinasua kutokana na minyororo ya ukandamizwaji wa kijamii, wasanii (wanafasihi) wafaa wajitokeze kama watetezi wa haki na ukombozi wa mwanamke katika ngazi mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kijinsia. Kuna haja ya kuchunguza namna waandishi wa Fasihi tangia mwaka wa 2000 walivyoliangazia suala la uongozi wa mwanamke katika kazi zao.

Taswira hasi ya mwanamke katika tafiti za awali inatokana na namna waandishi wa kazi za fasihi walivyomsawiri mhusika mwanamke kwani fasihi ni kioo cha jamii. Tamthilia huwa mwafaka katika kubainisha taswira ya wahusika kwa sababu husheheni mazungumzo na matendo yanayomwezesha msomaji kuchanganua tabia zao (Mulokozi, 1996; Wamitila, 2008). Kwa mujibu wa Murungi (2013) tamthilia nyingi kabla mwaka wa 2000 zilimsawiri mwanamke kwa njia hasi. Mathalani, tamthilia za: *Afadhali Mchawi* (Hyslop, 1957); *Nakupenda Lakini* (Kuria, 1957); *Mfalme Edipode* (Sophocles, 1971); *Mashetani* (Hussein, 1971); *Mbio za Sakafuni* (Muslimi, 1976) na *Uasi* (Kitsao, 1980) zilimsawiri mwanamke kwa njia duni hata mwanamke anapojitahidi kujiendeleza. Kwa maoni ya Onyoni (2012) suala la uongozi wa mwanamke katika tamthilia hizi halikuangaziwa kwani utamaduni na mila hazikumruhusu mwanamke kuyaingilia masuala ya uongozi. Ingawa suala la uongozi linabainika katika tamthilia ya *Mgeni Karibu* (Hyslop, 1957), mwandishi hakutumia wahusika wanawake hata kidogo. Tamthilia ya *Visiki* (Ongeti, 1984) nayo ilimsawiri mwanamke kama kiongozi ila kwa njia hasi. Said Ahmed Mohammed katika tamthilia yake ya *Kivuli Kinaishi* (1990) alionyesha namna mwanamke hawezi kuwa kiongozi na kwamba mwanamke ni katili (Mapunjo, 2014). Tamthilia ya *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1981) imebainisha hisia za ukombozi wa kijamii (Mugambi, 1982). Ingawa viongozi wengi katika tamthilia hii ni wanaume, Lanina amejitokeza kuongoza vita vya ukombozi. Inabainika kwamba mwanamke ana uwezo wa kuiongoza jamii vyema iwapo atapewa nafasi, hata hivyo Lanina hakupewa nafasi hiyo baada ya kutiwa kizuizini. Kuna hitaji la kuchunguza iwapo mwanamke katika tamthilia za Kiswahili kuanzia mwaka 2000 bado amesawiriwa kwa njia hasi kuhusiana na suala la uongozi au taswira hii imebadilika kadiri miaka ilivyoendelea kusonga.

Isitoshe, nyingi ya tafiti zilizofanywa katika tamthilia ya Kiswahili zimemwangazia mwanamke kijumla bila kumwangazia anavyojitokeza kuongoza jamii yake (Mbughuni, 1982; Momanyi,

1998). Ipo haja ya kuchunguza iwapo mwanamke katika tamthilia za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 amesawiriwa kijumla kama mwanamke au kama mwanamke anayejitokeza kuongoza jamii yake.

Baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi zilizotungwa kuanzia mwaka wa 2000 wamemsawiri mwanamke kwa njia chanya. Usawiri huu unatokana na mabadiliko yaliyotokea katika jamii ambapo hadhi ya wanawake inaimarika kuliko ilivyokuwa awali. Waandishi wa tamthilia kama *Zilizala* (Njogu & Chimera, 2006) na *Chamchela* (Arege, 2007) wamemsawiri mwanamke kwa njia chanya kinyume na waandishi wa awali (Mulila, 2009). Utafiti wa mwanamke katika tamthilia za tangia mwaka wa 2000 wafaa kufanyika ili kubaini ikiwa mwanamke amesawiriwa kwa uchanya kama kiongozi kinyume na tafiti za hapo awali. Mwaka wa 2000 ni tarehe muhimu katika ukuaji wa sura ya mwanamke katika tamthilia kwa kuwa ni kuanzia mwaka huu ndipo kuna ongezeko la waandishi wanaomchora mwanamke kwa njia chanya ikilinganishwa na miaka kabla mwaka 2000 (Onyoni, 2012).

1.2 Swala la Utafiti

Fasihi ina tanzu mbalimbali kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Utanzu wa tamthilia huwa mwafaka katika kubainisha taswira ya wahusika kwa sababu huwa na matendo na mazungumzo yanayoweza wasomaji kuchanganua tabia za wahusika. Tafiti nyingi za tamthilia ya Kiswahili kabla ya mwaka 2000 zilimsawiri mwanamke kwa njia hasi. Nyingi yazo zilimwagazia mwanamke kwa ujumla bila kuangazia uongozi wake. Chache zilizomwagazia mwanamke kiongozi zilimsawiri mwanamke kiongozi kwa njia hasi. Usawiri huu ulitokana na hali kwamba tamthilia nyingi zilikosa kuangazia uongozi wa mwanamke na chache zilizofanya hivi zilimchora mwanamke kiongozi kwa njia hasi. Taswira hii ilikuwa zao la hadhi duni aliyokuwa amepewa mwanamke katika jamii. Uongozi ni swala muhimu katika jamii. Ingawa kumekuwepo na wanawake viongozi kabla ya mwaka 2000, hadhi yao imekuwa ya chini. Mabadiliko yaliyotokea katika jamii kuanzia mwaka wa 2000 yameleta hali ambapo hadhi ya mwanamke kuhusiana na suala la uongozi imeimarika na jamii kuonekana kukubali uongozi wa mwanamke. Baadhi ya waandishi wa fasihi baada ya mwaka 2000 wamemsawiri mwanamke kwa njia chanya. Kuna haja ya kuwepo na tafiti ambazo zitachunguza ikiwa mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili tangia mwaka 2000 bado amesawiriwa kwa njia hasi kuhusiana na suala la

uongozi au iwapo taswira hii imebadilika namna hadhi ya mwanamke inavyoendelea kuimarika. Utafiti huu ulichunguza taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- a. Ni sifa zipi za mwanamke kiongozi zinajitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016?
- b. Ni mitindo ipi ya lugha inayochangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016?
- c. Taswira ya mwanamke kiongozi ina athari zipi kwa uongozi wa mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016?

1.4 Madhumuni ya Utafiti

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000. Ili kutimiza lengo la utafiti huu, utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahsusi yafuatayo:

- a. Kupambanua sifa za mwanamke kiongozi zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016.
- b. Kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016.
- c. Kutathmini athari ya taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016.

1.5 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umejikita kwenye taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016. Utafiti huu umechunguza mitindo ya lugha iliyotumiwa na waandishi wa tamthilia teule kujenga taswira ya mwanamke kiongozi. Mitazamo na matendo ya wahusika wa kike ambao ni viongozi wanapotagusana na wahusika wengine kupitia kwa lugha

imechunguzwa ili kubaini inavyomsawiri mwanamke kiongozi. Aidha, utafiti huu umechunguza namna matendo na mitazamo ya wahusika wengine inavyojenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike. Utafiti huu umepiga hatua na kutathmini athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016. Nadharia iliyofaulisha utafiti huu ni nadharia ya udenguzi. Misingi ya nadharia hii: lugha, muktadha na mitazamo iliufaa utafiti huu.

1.6 Misingi ya Uteuzi wa Mada

Momanyi (1998) anapendekeza kuwa, wahakiki wa kisasa wanafaa wawajibike katika kuhakiki usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Kulingana naye, hii itasaidia katika kubadilisha mielekeo ya watu kuhusu mwanamke kama kiambatisho au kitegemezi cha mwanamume. Utafiti huu ulitekeleza pendekezo hili la Momanyi kwa kuchunguza namna mwanamke alivyosawiriwa kama kiongozi katika tamthilia za Kiswahili. King’ei (2002) anadai kuwa, ni tafiti chache sana (hasa zile za tasnifu) zilizozingatia kipengele cha matumizi ya lugha katika kubainisha masuala ya kiuana katika fasihi ya Kiswahili. Anashikilia kwamba, huo ni udhaifu mkubwa kwani lugha ndiyo njia muhimu zaidi inayotumika katika malezi na elimu, nyanja zinazochangia utu na mielekeo ya kijamii kuhusu uana kwa jumla. Utafiti huu umeziba pengo hili analolizungumzia King’ei kwa kuchunguza mitindo ya lugha inayochangia kujenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike.

King’ei (2002) anaibua hoja kuwa, tahakiki nyingi zilizofanywa kuhusu suala la uana katika fasihi ya Kiswahili zimeishi kulalamikia hoja ya kukandamizwa, kudharauliwa, kupuuzwa na kutoshirikishwa kwa mwanamke katika vipengele muhimu vya maisha ya kijamii kama uongozi (King’ei, 2002). King’ei anatoa hoja kwamba, ingawa wanawake bado wanachukua nafasi za chini wakilinganishwa na wenzao wa kiume, si kweli kwamba matabaka ya juu na kati yenye uwezo yanamilikiwa na wanaume pekee, wanawake pia wamo. Utafiti huu ulimwagazia mhusika mwanamke ambaye ni kiongozi. King’ei anapendekeza kwamba badala ya kuwalaumu wanaume pekee kama asili ya maonevu yote dhidi ya wanawake, wakati umefika wa kuchunguza mchango wa wanawake viongozi kwa dhuluma ya wanawake wenzao. Utafiti huu ni chanzo cha kuafikiwa kwa pendekezo la King’ei kwani kwa kuchunguza taswira ya mwanamke kiongozi na

athari ya taswira hii kwa uongozi wa mwanamke, msingi wa kuchunguza mchango wa uongozi wa mwanamke kwa mwanamke mwenzake umewekwa.

1.7 Dhima ya Utafiti

Kothari (1990) anajadili hoja kuwa, utafiti katika sayansi jamii huhusisha kuweza kuibua maarifa mapya na vilevile matumizi tendaji ambapo mwanasayansi–jamii hupata ufahamu ili kuweza kulitenda jambo vyema au kwa njia bora. Mawazo ya Kothari yanatiliwa mkazo na Mugenda & Mugenda (2003) wanaosema kwamba utafiti huvumbua maarifa na tafsiri mpya. Wanaendelea kusema kuwa, kuna vyanzo vingi vya maarifa lakini utafiti unasalia chanzo bora na cha kutegemewa zaidi kwani hulenga na kudhihirisha ukweli. Watafiti wameshughulikia nafasi na taswira ya mwanamke katika fasihi. Kwa ujumla, utafiti huu umeangazia suala la uongozi wa mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili.

Tafiti nyingi za fasihi ya Kiswahili zimemhusu mhusika mwanamke kwa ujumla. Suala la uongozi wa mwanamke halijabainishwa katika nyingi ya tafiti hizi. Watafiti wengi wa fasihi katika tafiti zao wamehitimisha kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni na mtegemezi wa mwanaume (Momanyi, 1982; Katola, 2006). Kwa kumwangaia mhusika mwanamke kiongozi, utafiti huu umeibua maarifa mapya kuhusu suala la uongozi wa mwanamke. Utafiti huu huenda ukawapa hamasa watafiti wa baadaye kulishughulikia suala la uongozi wa mwanamke katika tafiti zao.

Maarifa mengine mapya yaliyoibuliwa na utafiti huu ni kuhusu mitindo ya lugha. Kwa mujibu wa King’ei (2002), watafiti wengi wa kazi za kifashi na hasa wanaotafitia masuala ya kiuana hawajazingatia kipengee cha lugha katika tafiti zao. Kulingana naye, huu ni udhaifu mkubwa kwa kuwa lugha ni kipengele muhimu katika kubainisha masuala ya kiuana katika fasihi. Utafiti huu umebainisha namna mitindo ya lugha inavyochangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi. Huenda watafiti wa baadaye wakahochewa na utafiti huu kuzingatia mitindo ya lugha katika tafiti zao.

Idadi na hadhi ya wanawake viongozi ulimwenguni imesalia ya kiwango cha chini ikilinganishwa na ya wanaume (Afhami, 2003). Utafiti huweza kulenga kutoa suluhu kwa tatizo

fulani (Kothari, 1990). Kwa kuwa fasihi huakisi mambo yanayotendeka katika jamii (Wamitila, 2003), fasihi yafaa kutoa suluhisho kwa matatizo yanayokumba jamii. Huenda utafiti huu ukawa chanzo cha kusuluhisha tatizo la ubaguzi wa wanawake katika nyadhifa za uongozi. Utawajua wanawake viongozi kuhusu namna wanavyosawiriwa. Viongozi hawa wa jinsia ya kike huenda wakakuzwa, kuhimizika na kuchochewa kuhusu uongozi wa mwanamke kupitia utafiti huu. Athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke huenda zikawatia hamasa wanawake viongozi wanaopitia changamoto mbalimbali katika juhudi zao za kuleta mabadiliko ya kiuongozi na kuwafanya kutokata tamaa hivyo kuibuka washindi. Momanyi (1998) anapendekeza kuwa wahakiki wa kisasa wanafaa waajibike katika kuhakiki usawiri wa wanawake katika fasihi ya Kiswahili. Kulingana naye, hii itasaidia kubadilisha mielekeo ya watu kuhusu mwanamke kama kiambatisho au kitegemezi cha mwanamume. Kwa kuangazia usawiri wa mwanamke kiongozi na athari za usawiri huu kwa uongozi wa mwanamke, utafiti huu huenda ukachangia kubadilisha mielekeo hasi iliyopo kumhusu mwanamke na hasa mwanamke kiongozi jambo litakaloendeleza na kuboresha uongozi wa mwanamke katika jamii.

Tafiti nyingi ambazo zimefanywa katika Kiswahili na zinazomhusu mwanamke hazijazingatia nadharia ya udenguzi. Nyingi ya tafiti kumhusu mwanamke zimetumia nadharia ya Ufeministi (Katola, 2006; Mirikau, 2011; Muniu, 2013; Mapunjo, 2014). Utafiti huu huenda ukawatia shime watafiti wa baadaye kutumia nadharia ya udenguzi kufanya utafiti wao kwa kujikita sio tukwa tamthilia bali tanzu nyinginezo za fasihi.

1.8 Misingi ya Kinadharia

Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni nadharia ya udenguzi iliyoasisiwa na Jacques Derrida (1966) na kuelezwa na Ntaragwi (2004). Nadharia hii hutupilia mbali dhana kuwa matini ya kifasihi huwa na lengo au maana moja (Miller, 1976). Nadharia hii hushikilia kuwa, kila msomaji binafsi huumba lengo na maana mpya na ya kibinafsi au ya kipekee katika matini (Ntaragwi, 2004). Nadharia hii huhusishwa na maendeleo kutoka kwa kazi za Derrida (1966, 1973, 1976), Berthes (1977), Lacan (1977), Kristeva (1981, 1984, 1986), Althusser (1971), Miller (1976); Foucault (1978, 1979 a; 1979 b, 1981, 1986) (Ntaragwi, 2004). Katika mhadhara wake wa 1966, Derrida alieleza kuhusu mapinduzi ya kiusomi aliyoyafananisha na mchezo. Mapinduzi haya yalikuwa mabadiliko kutoka kwa umuundo hadi umuundo mpya. Kwa mujibu

wa Derrida (1973) maana ndani mwa matini ni kitu ambacho hakiwezi kuelezwa moja kwa moja. Hivyo basi, fasiri ya matini kwa wahakiki haiwezi kuelezwa kwa namna moja. Kila mhakiki ataeleza maana kwa namna yake. Kulingana na Derrida, maana ndani mwa matini zinaweza zikafanana au zikatofautiana.

J. Hillis Miller vilevile alikuwa mfuasi wa nadharia hii. Miller (1976) alimpinga Abrams aliyekuwa amepinga nadharia ya udenguzi katika mhadhara wake wa mwaka wa 1980. Abrams alikuwa amedai kuwa matini huwa na maana moja tu na iwapo nadharia ya udenguzi itatumika basi hapawezi kuwepo na historia. Miller alimjibu kuwa, kuwepo kwa maana moja ndani mwa matini ni jambo lisilowezekana kwa sababu maneno ndani mwa matini husheheni maana mbalimbali. Kila neno kulingana naye huwa na maana iliyojengwa ndani mwake na aghalabu huhusiana na neno lingine. Miller (1976) alisema kwamba kuhakiki matini kupitia nadharia ya udenguzi huibua maana mpya.

Berthes (2011) alidai kuwa, 'kifo' cha mwandishi ni chanzo cha kuaminika cha maana ya matini husika. Alidai kuwa, matini yoyote huwa na maana nyingi na kwamba mwandishi ni chanzo cha kimsingi cha maana. 'Kifo' cha mwandishi kulingana na Berthes ilikuwa 'kuzaliwa' kwa msomaji. 'Kifo' cha mtunzi anachozungumzia Berthes ni maana tofauti ambazo huweza kuzaliwa na wasomaji bila kutilia maanani maana ya mtunzi. Kutokana na mawazo ya Berthes, ni bayana kuwa nadharia ya udenguzi hutegemea usomaji wa kina wa matini ili kuibua maana. Mtazamo huu hushirikisha kutambua changanuzi za maana zilizopo na zinazohusiana na ambazo zaweza kuibuliwa ndani mwa matini. Utambuzi na uchanganuzi huu huwa ni kazi ya msomaji wa matini kulingana na Berthes.

Kulingana na nadharia hii, lugha huweza kubeba maana mbalimbali. Kutokana na anayoyasema mtu tunaweza kupata maana kuhusu suala fulani ambayo huenda ikatofautiana na maana tunayoweza kupata kutoka kwa mtu mwingine kuhusu suala lilo hilo. Nadharia ya udenguzi huchukulia kwamba maana hujengwa katika lugha na kwamba msikilizaji au msomaji ataweza kuibua maana kupitia kwa lugha iliyotumiwa. Hivyo, udenguzi husisitiza kuwa, maana hukuzwa kupitia kwa lugha.

Kutokana na mawazo ya wanaudenguzi hawa, kilicho muhimu katika uhakiki wa matini ni usomaji wa kina wa matini ili kuibua na kufasiri maana mbalimbali zilizofichama. Maana hizi

zinaweza kufanana au kutofautiana na maana zilizoibuliwa na wahakiki wengine (Derrida, 1973). Ni kwa mawazo haya ndipo usomaji wa kina wa tamthilia za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 ulifanywa. Ufasiri wa taswira ya mwanamke kiongozi uliibuliwa kutokana. Taswira hii huenda imetofautiana na taswira ya mwanamke iliyoibuliwa na watafiti wengine wa awali.

Ntaragwi (2004) anatoa maoni kuwa nadharia ya udenguzi huwa na mihimili mitatu mikuu: lugha, muktadha na mtazamo. Utafiti huu uliongozwa na mihimili hii mitatu. Kulingana naye, nadharia hii hushikilia kuwa, lugha ni kipengele muhimu cha matini au usemi na kwamba lugha hubeba maana mbalimbali. Kwa mujibu wa Derrida (1973), lugha iliyotumiwa ndani mwa matini huwa muhimu katika kuibua maana. Kulingana naye maana hujibua mbele ya mhakiki namna zulia linavyojikunjua mbele ya mtu anayelifungua kupitia kwa uchanganuzi wa lugha iliyotumiwa. Mawazo haya ndiyo yaliwafanya Njogu & Chimera (2007) kusema kuwa kutokana na nadharia ya udenguzi hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hivyo basi, wahakiki kwa misingi ya nadharia hii wanaweza kutoa fasili tofautitofauti za jambo moja kwa kuchunguza lugha iliyotumiwa. Fasili hizi kulingana na wawili hawa zinaweza kutofautiana au kufanana.

Kwa maoni ya Bakhtin (1981) lugha hubeba maana nyingi ndani mwa matini. Lugha mbalimbali pamoja na matumizi mbalimbali ya lugha moja huugawa ulimwengu na kuupa maana mbalimbali. Kwa hivyo, hakuna maana moja ya neno au fungu la maneno katika kazi ya fasihi. Hadhira huibua maana mbalimbali kutokana na maneno aliyoyateua na kuyatumia mtunzi. Wahusika wa kazi ya fasihi wanapozungumza huleta maana mbalimbali zinazofasiriwa na wahusika wengine au wasomaji tofautitofauti. Kipengele hiki cha lugha huchangia wingi-maana wa matini au mazungumzo. Escholt (1982) anaeleza kuwa, matumizi ya lugha ndiyo yanayokuza na kupalilia mawazo yenye taasubi za kiume na kike. Anasema kwamba, ubaguzi wa kiuana hujitokeza kupitia ishara za lugha ya kitamathali katika asasi kama vile ukoo, uana, kazi au maelezo kuhusu maumbile na matumizi mengineyo ya lugha. Mhimili wa lugha uliuwekea utafiti huu msingi wa kuchunguza namna lugha ya wahusika wa kike na kiume katika tamthilia teule ilivyojenga taswira ya mwanamke kiongozi. Lugha hii ilibainika kupitia kwa mitindo mbalimbali ya lugha iliyotumiwa katika tamthilia teule. Ni kupitia kwa mitindo hii ambapo taswira ya mwanamke kiongozi ilibainika.

Mhimili wa muktadha kulingana na Ntaragwi (2004) hushikilia kuwa, maana ya kisa ni amana ya msomaji na kwamba kuna fasili mbalimbali za kisa kulingana na muktadha. Muktadha ni mazingira au hali ambamo tukio au jambo hutendeka (TUKI, 2004). Bakhtin (1981) anaeleza kuwa, hakuna uumbaji wa maana katika lugha ambao hauathiriwi na muktadha wa kimatumizi. Mawazo yake yanaoana na ya Fairclough (1992) anayesema kwamba, uchanganuzi wa watu na matini huathiriwa na suala la muktadha. Hivyo basi, maana hutokana na muktadha. Kwa mtazamo wa nadharia hii, msomaji huchukuwa sehemu muhimu ya uchunguzi. Wanaudenguzi huchunguza vianzo vingine vya maana kando na mtunzi wa matini. Vianzo hivi ni kama: mila na desturi, kipindi cha wakati, mazingira, mitazamo ya wasomaji na matini mengine (Peck & Coyle; 1984). Neno ‘mama’ kwa mfano linaweza kuwa na maana inayobadilika kutokana na mazingira. Maana hizi ni kama: mzazi, mlezi, mfadhili, mtoto, bibi, mke wa kiongozi fulani au mwanamke yeyote yule.

Katika kuchunguza taswira ya mwanamke kiongozi, utafiti huu umejikita katika miktadha ya kisiasa, kijamii na kitamaduni ya tamthilia teule. Kulingana na wanaudenguzi, uelewa wa muktadha husaidia msomaji kufasiri matini hivyo kuelewa maana ndani mwa matini hayo. Kwa mujibu wa Onyoni (2012) kufahamu muktadha kunatusaidia kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika katika fasihi.

Kwa maoni ya Ntaragwi (2004) msingi mwingine wa udenguzi ni dhana ya mitazamo. Mtazamo ni jinsi mtu huchukulia au kufikiria kuhusu jambo fulani; ni mawazo ya mtu juu ya jambo fulani (TUKI, 2004). Ntaragwi anaibua hoja kuwa, mhakiki wa kazi ya fasihi anayetumia nadharia ya udenguzi anaweza kutumia mitazamo mbalimbali kuumba uchanganuzi wa matini wenye mtazamo mpana. Levinas (2003) anasema kwamba maneno huashiriwa kutokana na ulimwengu na mtazamo ambamo mtu hutazama jambo fulani. Utafiti huu ulichunguza namna mitazamo ya wahusika wa kike na kiume (ilivyoashiriwa kupitia kwa maneno) inavyochangia kujenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike kwa mujibu wa tamthilia teule. Hooks (1988) naye anasema kwamba kuibua maana kutoka kwa mtazamo mpana huibua maswali mapya na changanuzi mpya. Kutokana na mitazamo ya wahusika katika tamthilia teule, utafiti huu uliibua maswali yafuatayo: Je, mitazamo ya wahusika mbalimbali katika tamthilia teule imechangia kumsawiri mwanamke kama kiongozi au kama kiumbe dhaifu asiyefaa kuongoza? Je, mitazamo ya wahusika ina athari zipi kwa uongozi wa mwanamke? Mitazamo ya mhusika mwanamke

kiongozi na wahusika wengine katika tamthilia teule ilichunguzwa. Mitazamo ilidhihirika kupitia kwa matendo na lugha ya wahusika na hivyo kusaidia utafiti huu kuibua taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike na athari za taswira hii kwa uongozi wa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia teule za Kiswahili.

Nadharia ya udenguzi iliteuliwa kuwa dira ya utafiti huu kwa sababu ya mihimili yake. Kulingana nayo, lugha; muktadha na mtazamo ni mambo muhimu ambayo yafaa kuzingatiwa na mchanganuzi wa matini. Kwa kutumia mihimili hii, tamthilia teule za Kiswahili zimesomwa huku lugha iliyotumiwa na wanawake viongozi pamoja na wahusika wengine ikichunguzwa ili kubaini inavyojenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike. Kulingana na wanaudenguzi, lugha hii sharti ieleweke katika muktadha mahususi. Muktadha wa kisiasa na kijamii katika tamthilia teule umesaidia utafiti huu kubainisha mitazamo na matendo ya wahusika inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi. Muktadha wa kitamaduni katika tamthilia teule umewezesha utafiti huu kuelewa mitazamo ya baadhi ya wahusika inayozuia ukweaji wa mwanamke katika ngazi ya uongozi na namna mwanamke anavyokabiliana na mitazamo hii na kuibuka kiongozi. Hivyo uelewa wa muktadha huu umesaidia kubainisha taswira ya mwanamke kiongozi na athari ya usawiri huu kwa uongozi wa mwanamke. Vilevile, mitazamo ya mwanamke kiongozi na wahusika wengine (ambayo ilibainika kupitia matendo na lugha ya wahusika) ilichunguzwa kwa lengo la kubaini mchango wake katika kumsawiri kiongozi wa jinsia ya kike.

1.8 Hitimisho

Katika sura hii, utafiti huu umeweka msingi kwa kushughulikia usuli, suala, maswali, madhumuni, upeo, dhima, misingi ya uteuzi na kinadharia ya utafiti. Imebainika kuwa tafiti nyingi za fasihi ya Kiswahili kabla ya mwaka 2000 zilimsawiri mwanamke kwa ujumla bila kuangazia uongozi wake. Chache zilizomwangazia mwanamke kiongozi zilimsawiri kwa njia hasi. Utafiti huu umechunguza taswira ya mwanamke kiongozi kwa kuangazia sifa za mwanamke kiongozi, mitindo ya lugha inayojenga picha ya mwanamke kiongozi na athari za taswira ya mwanamke kwa uongozi wa mwanamke. Utafiti huu umejikita kwenye mihimili mitatu ya nadharia ya udenguzi: lugha, mitazamo na muktadha na kuteua tamthilia nne za Kiswahili za tangia mwaka 2000 hadi 2016.

SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia uhakiki wa maandishi. Dhana ya tamthilia inashughulikiwa. Aidha, nafasi ya mitindo ya lugha, wahusika na taswira katika fasihi inabainishwa. Isitoshe, mapitio ya nadharia ya udenguuzi ambayo imetumiwa na utafiti huu ni suala linalojadiliwa katika sura hii.

2.2 Nafasi ya Taswira katika Tamthilia ya Kiswahili

Njogu & Chimera (1999) wanafafanua dhana ya taswira kama mkusanyiko wa picha zinazotokana na ufundi wa msanii katika kuteua na kupanga maneno yake ya kazi fulani ya kifasihi. Kutokana na wawili hawa, lugha iliyotumiwa katika kazi ya fasihi ni muhimu katika kuibua taswira. Mirikau (2011) naye anatoa hoja kuwa, taswira ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Taswira hii kulingana naye aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa kupitia mambo yanayopitikia akilini mwa binadamu na huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Kwa mujibu wa maoni haya ya Mirikau, taswira ya mhusika hutokana na sifa za mhusika huyo. Utafiti huu ulichunguza sifa za mwanamke kiongozi zinazojenga picha ya mwanamke kiongozi. Kutokana na mawazo ya Njogu & Chimera (1999) na Mirikau (2011), taswira katika fasihi hudhihirika kupitia kwa matendo, mitazamo na lugha ya wahusika. Utafiti huu ulichanganua mitindo ya lugha inavyojenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike pamoja na mitazamo ya wahusika mbalimbali kwa mwanamke kiongozi kwa kurejelea tamthilia teule.

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza uhusika kama umithilishaji wa vitendo vya viumbe vya hadithini na vile vya viumbe katika ulimwengu razini. Kulingana nao, vitendo vya viumbe hao husababishwa na kuingiliana na mazingira ya ubunifu, kama ambavyo vitendo vya viumbe razini huwa vimesababishwa na maingiliano baina yao wao wenyewe na mazingira yao ambayo ni razini. Murumba (2011) akimnukuu Wamitila (2003) anasema kwamba uhusika ni mbinu na mikakati ambayo hutumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Anaendelea kusema kuwa baadhi ya maandishi ambao hutilia mkazo suala la uhusika huwa wanaamini kuwa, kilicho na uzito na maana katika fasihi ni jinsi matukio yanayopatikana katika kazi yanavyoathiri wahusika. Athari hiyo huwa na matokeo mengi kuhusu mikabala yao sambamba na matukio

yaliyotokea. Utafiti huu ulimchunguza mhusika wa jinsia ya kike aliye uongozini anapotagusana na wahusika wengine katika tamthilia teule.

Kwa mujibu wa Muniu (2011) wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi ili wawe sauti yake katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Maoni yake yanashabihiana na ya Wamitila (2003) anayeeleza wahusika kama viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya kifasihi. Forster (1927) anaibua hoja kuwa wahusika katika fasihi aghalabu huwa watu kwani hata kama wakitumiwa, saikolojia yao haijulikani wazi kwa binadamu. Hii ndiyo sababu Muniu (2011) anasema kwamba wahusika katika tamthilia huwa watu na hivyo huwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na yale wanayoyatenda au yale yanayosemwa na msimulizi au wahusika wengine. Sifa za mhusika mwanamke aliye uongozini zilichunguzwa na utafiti huu ili kuchanganua namna zinachangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi.

Dhima ya wahusika katika kazi ya fasihi inasisitizwa vyema na Wamalwa (2005) anayesema kuwa, msanii huwashirikisha wahusika hadithini kwa minajili ya kujenga au kuendeleza maudhui na dhamira. Kulingana naye, wahusika hupewa sifa zinazowasaidia kutekeleza matendo fulani nayo matendo haya huelekezwa kwenye maudhui na dhamira. Chambilecho Wamitila (2011) wahusika ni nguzo kuu ya matendo ya kidrama. Semzaba (1997) anasema kuwa wahusika ndiyo nyenzo muhimu inayosababisha mtiririko wa matukio.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) wahusika husawiriwa kupitia kwa mbinu kama maelezo ya msimulizi au mwandishi, maelezo au maneno ya wahusika wengine, matendo au matumizi ya mazungumzo (mbinu ya kidrama), majazi, ulinganuzi na mwingiliano matini. Matendo ya wahusika hutuelekeza katika kuelewa tabia, imani, mategemeo au matumaini, hisia, kero, ndoto au hata udhaifu wao (Njogu & Chimerah, 1999; Wamitila, 2008; Murumba, 2011). Wahusika wa tamthilia hudhihirishwa na kukuzwa vyema kwa matumizi ya mazungumzo (Wamitila, 2003). Wamalwa (2005) anasema kwamba, mintarafu mazungumzo ya wahusika, msomaji anaweza kupata picha ya mahusiano yao kijamii na kitamaduni hasa baada ya kuzisoma na kuzichunguza fikra zao. Wamitila (2008) anaibua hoja kuwa, maneno ya wahusika ni msingi mkubwa wa kuwakuza na kuwaendeleza hao hao wahusika. Kupitia kwa matendo na mazungumzo ya wahusika, wasomaji wanaweza kuzichanganua tabia zao.

Mazungumzo huchukuliwa kama njia ya kuendeleza mgogoro au tendo lililoko katika kazi ya kifasihi au dhamira au maudhui (Murumba, 2011). Mulokozi (1996) anatoa hoja kuwa, hadithi ya tamthilia husonga mbele kwa njia ya vitendo na mazungumzo ya wahusika. Anasisitiza kwamba, bila wahusika hata mazungumzo hayawezi kuwepo. Kupitia kwa matendo na mazungumzo ya wahusika wasomaji wanaweza kuzichanganua tabia zao (Wamitila, 2008). Utafiti huu basi ulichunguza namna matendo na lugha ya wahusika mbalimbali katika tamthilia teule yalivyomsawiri mhusika mwanamke ambaye ni kiongozi.

Were (2012) kwa kutumia nadharia ya umuundo alichunguza namna vipengele vya fani: wahusika, ploti, monolojia na dayolojia vinavyohusiana na kufaulisha ujenzi wa tamthilia ya *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1981) na *Kijiba cha Moyo* (Arege, 2009). Alipolizungumzia suala la wahusika, Were alirejelea jinsi nne: nafasi ya wahusika, usemi wao, umakundi wao na ulinganuzi wao. Anasema kuwa kupitia kwa mhusika Lanina katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* mwandishi anaonyesha uwezo alio nao mwanamke licha ya changamoto zinazomkumba. Utafiti huu ulichunguza dai hili la Were kwa lengo la kubaini uwezo wa kuongoza walio nao wanawake viongozi na namna wanavyodhihirisha uwezo huu kwa mujibu wa tamthilia teule. Were alishughulikia wahusika wa jinsia ya kike na kiume kwa kurejelea tamthilia za *Kilio cha Haki* (1981) na *Kijiba cha Moyo* (2009). Utafiti huu ulimchunguza mhusika mwanamke kiongozi kwa kurejelea tamthilia za *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016).

Mugambi (1982) alihakiki maudhui katika tamthilia zilizochapishwa nchini Kenya kati ya mwaka wa 1957 hadi 1981. Kwa kuitumia nadharia ya umaksi, Mugambi alionyesha namna waandishi walivyoendeleza maudhui mbalimbali kama udhalimu, nafasi ya mwanamke katika jamii na utetezi wa haki za mwanamke. Kwa kuangazia tamthilia ya *Zinduko* (Ryanga, 1986), Mugambi alidai kuwa wanawake wamesawiriwa kama viumbe duni ambao wanatumiwa na wanaume kuendeleza maslahi yao, viumbe dhifu ambao hawana upeo mkubwa wa kisiasa na ambao wanatarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa waume wao bila ukinzani. Anasema kuwa mwanamke katika tamthilia hii hana nafasi ya kushiriki katika siasa kama kiongozi bali jukumu lake kuu ni kuwahimili wanaume. Utafiti huu ulichunguza taswira hii ya Mugambi kwa lengo la kubaini iwapo taswira hii inafanana na ya mwanamke kiongozi katika tamthilia zilizotungwa tangia mwaka 2000 hadi 2016.

Mugambi anatazama kuwa, *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1981) ndiyo tamthilia ya kipekee ya Kiswahili iliyofikia kilele katika kubainisha hisia za ukombozi wa kijamii. Kulingana naye, tamthilia hii, kando na kubainisha mapambano ya wafanyikazi dhidi ya udhalimu, inatudhihirishia nafasi ya mwanamke katika jamii iliyo na mifumo kandamizi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lanina ambaye ni mhusika mkuu anajitokeza kama mwanamke jasiri aliyejikomboa kimawazo kuongoza mapambano ya wafanyikazi. Utafiti wa Mugambi ulifaa utafiti huu. Kupitia utafiti wa Mugambi, picha mbalimbali za mwanamke Lanina ziliibuliwa na kuhusishwa na tamthilia teule. Picha hizi ni kama zinazohusu ujasiri, utetezi wa haki na msimamo thabiti wa mwanamke. Mugambi aliangazia ukombozi wa mwanamke. Utafiti huu ulimwagazia mwanamke kiongozi kinyume na Mugambi aliyemzungumzia mwanamke kwa ujumla. Isitoshe, utafiti huu ulilenga kubaini namna lugha ya wahusika inavyochangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi.

Aidha, Mugambi alionyesha mbinu zilizotumiwa na waandishi wa tamthilia hizo katika kuendeleza maudhui mbalimbali. Alishughulikia mazingira, wahusika, matumizi ya lugha na hasa matumizi ya jazanda na tamathali za usemi kama mbinu muhimu katika ujenzi wa maudhui. Ufaafu wa utafiti wa Mugambi kwa utafiti huu ni kutokana na alivyotumia mbinu za kimtindo kuendeleza maudhui. Utafiti huu ulichunguza ikiwa kipengele cha lugha alichokizungumzia Mugambi kinasaidia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia husika. Utafiti wa Mugambi ulijikita katika tamthilia zilizoandikwa baina ya mwaka wa 1957 na 1981. Utafiti huu ulirejelea tamthilia nne zilizoandikwa kuanzia mwaka 2000 hadi 2016. Aidha, utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia teule.

Mule (1991) alihakiki tamthilia za *Zinduko* (Ryanga, 1986), *Mama Ee* (Mwachofi, 1987) na tamthilia za: Muhando, Matteredu na Chongo. Anasema kwamba, mwanamake katika tamthilia hizi wamesawiriwa kama viumbe dhaifu ambao hawana upeo mkubwa wa kisiasa. Katika hitimisho lake, Mule aliafiki maoni ya watafiti mbalimbali waliomtangulia kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni na mtegemezi wa mwanamume. Utafiti huu ulichunguza madai haya. Mule alijikita katika kubainisha taswira ya mwanamke kijumla wala si ya mwanamke kiongozi. Utafiti huu ulichunguza taswira ya mwanamke kiongozi kupitia kwa lugha ya wahusika kwa mujibu wa tamthilia teule.

Kiango (1992) aliangalia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Katika kazi yake, Kiango alisema kwamba mwanamke amesawiriwa kwa njia hasi kama kiumbe tofauti na mwanamume. Kulingana naye, mwanamke ameumbwa kama mtu anayeendeleza maudhui mabaya kwa kuwa amesawiriwa kama: mzinifu, mbaya, muuaji, mwaviaji mimba na mtu asiye na mwelekeo thabiti. Utafiti huu ulilenga kubainisha ikiwa picha ya mwanamke aliyoiibua Kiango inafanana au inatofautiana na ya mwanamke kiongozi katika tamthilia za Kiswahili za tangia mwaka 2000 hadi 2016. Kiango alimwangazia mwanamke kwa ujumla. Utafiti huu ulimwangazia mwanamke ila ulijikita kwenye uongozi wake. Utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza namna lugha inavyochangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi na athari ya taswira hii kwa uongozi wa mwanamke.

Mosoti (1993) kwa kutumia nadharia ya uyakinifu wa kijamaa alihakiki maudhui katika tamthilia nne za Emmanuel Mbogo: *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981a), *Watoto wetu* (1981b) na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988). Alihakiki maudhui ya dhuluma, usaliti, ubinafsi, ukombozi na nafasi ya mwanamke. Uhakiki wake wa maudhui ya nafasi ya mwanamke uliweka msingi wa kuibua taswira ya mwanamke kiongozi kwa kurejelea tamthilia teule. Mosoti anaonekana kukubaliana na maoni ya watafiti mbalimbali kuwa mwanamke amechorwa kama kiumbe duni. Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo usawiri wa mwanamke kulingana na Mosoti unaoana au unatofautiana na wa mwanamke katika tamthilia za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Utafiti huu ulipiga hatua na kubainisha mitindo ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi pamoja na kutathmini mchango wa wahusika katika kujenga taswira ya mwanamke kiongozi. Utafiti huu ulitumia nadharia ya udenguzi kinyume na Mosoti aliyetumia nadharia ya uyakinifu.

Sarara (1997) amehakiki maudhui katika tamthilia ya S.A Mohamed kwa kuchunguza tamthilia tatu: *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaisha* (1990) na *Amezidi* (1995). Sarara amejikita katika misingi ya uyakinifu wa kisosholista. Katika kushughulikia masuala ya kijamii, ameshughulikia maudhui kama: ufnisadi, ukombozi, umaskini na dhuluma dhidi ya mwanamke. Uhakiki wake wa maudhui ya dhuluma dhidi ya mwanamke umesaidia utafiti huu kuchunguza mitazamo ya baadhi ya wahusika inavyochangia kujenga taswira ya mwanamke katika tamthilia teule. Ni taswira hii ya mwanamke ndiyo iliyosaidia kuibua picha ya kiongozi wa jinsia ya kike. Utafiti huu ulichunguza ikiwa mwanamke kiongozi katika tamthilia teule anadhulumiwa na iwapo dhuluma hizi zinamzuia kuongoza jamii yake. Sarara alitumia nadharia ya uyakinifu wa kisosholista ambayo

husisitiza kuwa kazi ya fasihi lazima idhihirishe hali halisi katika jamii. Utafiti huu umetumia nadharia ya udenguzi ambayo hushikilia kuwa matini hubeba maana mbalimbali ambazo zaweza kuibuliwa na msomaji.

Katola (2006) kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kiafrika alihakiki tamthilia nne: *Hatia* (Muhando, 1972) *Mama Ee* (Mwachofi, 1987), *Buriani* (Yahya & Mulwa, 1983) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (Mohammed, 2000). Alishughulikia udhalimu dhidi ya wahusika wa kike kwa kurejelea tamthilia hizi. Anasema kuwa, mifumo ya kijamii iliyojaa taasubi za kiume imechangia katika kumdhulumu mwanamke. Anaendelea kusema kuwa, mhusika wa kike amedhulumiwa sana na kupewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Kwa ujumla, anataja maonevu yote ya kimwili wanayofanyiwa wanawake. Baadhi ya dhuluma alizotambua ni wanawake kutishwa, kutusiwa, kuoza bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii. Matokeo ya dhuluma hizi kulingana naye ni mitazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Utafiti huu ulichunguza iwapo mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia za kuanzia mwaka 200 hadi 2016 anadhulumuwa na ikiwa dhuluma hizi zinamzuia kuongoza. Tamthilia nne zilizorejelewa katika utafiti huu ni tofauti na za Katola kwa misingi ya waandishi na vipindi vya uandishi.

Mulila (2009), kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, alitafiti kuhusu usawiri wa wahusika wanawake katika tamthilia za *Zilizala* (Njogu na Chimera, 2006) na *Chamchela* (Arege, 2007). Amebainisha namna mwanamke alivyochorwa kama mwalimu, mwenye msimamo thabiti, mfanyikazi, mwenye busara, mwenye uwezo na mwenye nia safi. Utafiti huu ulichunguza ikiwa taswira hii ilivyobainishwa na Mulila inafanana au kutofautiana na ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule. Mulila anadai kwamba hakuna ithibati kuwa wanaume wana uwezo wa kuongoza kuliko wanawake. Utafiti huu ulilenga kuchunguza dai hili. Katika hitimisho lake, Mulila anadai kwamba mwanamume ndiye kisiki kikubwa cha ukombozi wa mwanamke. Utafiti huu ulichunguza dai hili kwa mujibu wa tamthilia teule. Mulila kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika aliangazia ukombozi wa mwanamke; utafiti huu umeangazia uongozi wa mwanamke kwa kurejelea nadharia ya udenguzi.

Mirikau (2011) alishughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia tatu za Wamitila: *Wingu Jeusi* (1999), *Pango* (2003) na *Seserumbe* (2009) kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Alifafanua dhana ya taswira kama jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha

kamili ya namna anavyoonekana. Alieleza kuwa, picha hii mara kwa mara ni zao la anavyofikiriwa mtu kupitia mambo yanavyomfikia binadamu akilini. Dhihirisho la mambo haya laweza kuwa katika matendo halisi anayotendewa. Alitamatisa kwa kusema kwamba, taswira hii ni kuhusu ngazi katika jamii ambayo mwanamke hujikuta amekwea na kukabiliana na uamuzi ambao humfanya atukuzwe au adhalalishwe na hata kujidhalilisha mwenyewe. Ufafanuzi wa Mirikau kuhusu taswira ulifaa utafiti huu kwani utafiti huu ulichunguza namna mwanamke kiongozi alivyochorwa kwa mujibu wa tamthilia teule. Hili limetekelezwa kwa kuchunguza, matendo, mitazamo na lugha inayomwashiria mwanamke kiongozi. Utafiti huu umeshughulikia suala la taswira ila umemwangazia mwanamke kiongozi kinyume na Mirikau aliyeshughulikia mhusika mwanamke kijumla bila kuangazia uongozi wake.

Mwenderani (2012) alishughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1981) na *Pango* (Wamitila, 2003). Alichunguza taswira hasi na chanya aliyopewa mwanamke katika tamthilia hizi mbili pamoja na njia ambazo mwanamke anaweza kuzitumia ili kujikomboa. Taswira ya mwanamke aliyoiibua Mwenderani ilihusishwa na tamthilia teule za utafiti huu kwa lengo la kubaini iwapo inamhusu mhusika mwanamke aliye uongozini. Baadhi ya sifa za mwanamke zinazomsawiri mwanamke kichanya kama ujasiri na utetezi wa haki alizozishughulika Mwenderani zilisaidia kubainisha taswira ya mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia zilizotungwa tangu mwaka 2000 hadi 2016. Mwenderani alishughulikia taswira ya mwanamke kiujumla. Aliegemea suala la ukombozi wa mwanamke ilhali utafiti huu umepiga hatua na kuangazia suala la uongozi wa mwanamke linavyobainika kupitia kwa mitindo ya lugha katika tamthilia teule.

Onyoni (2012) kwa kutumia nadharia ya Ufeministi alichunguza usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala* (Mberia, 1997) na *Mama Ee* (Mwachofi, 1987). Alipoichunguza tamthilia ya *Natala*, Onyoni anasema kwamba mhusika Natala amechorwa kama mtu: jasiri, anayewajibika, mwenye urembo wa kiakili na mwenye mapenzi kwa watu wa familia yake. Kutokana na sifa hizi, taswira ya mwanamke kiongozi iliibuliwa kwa mujibu wa tamthilia teule. Onyoni alishughulikia sifa za kijumla zinazomchora mhusika mwanamke. Utafiti huu umeangazia sifa za mwanamke ambazo zinajenga uongozi wake.

Aidha, Onyoni alichunguza matumizi ya lugha katika tamthilia hizi ili kuona namna inavyojenga taswira ya mwanamke. Alibainisha mbinu mbalimbali za lugha kama ama vile: methali, tashihisi,

jazanda, istiari na kinaya. Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo mbinu hizi za lugha alizoziainisha Onyoni zinajenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike. Utafiti huu umemlenga kiongozi wa jinsia ya kike kinyume na Onyoni ambaye hakumbainisha mwanamke kama kiongozi moja kwa moja. Isitoshe, tamthilia alizochunguza pamoja na nadharia aliyoitumia ni tofauti na iliyotumiwa na utafiti huu.

Keter (2013) alishughulikia nafasi na utambulisho wa mwanamke katika tamthilia za *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (1981). Kwa kuangazia tamthilia hizi, Keter aliweza kuchunguza namna mwanamke alivyodhalilishwa. Alidai kuwa nafasi ya mwanamke imeshushwa kwa kumchora kama chombo cha kumfurahisha mwanamume, kiumbe duni kisichoweza kumiliki chochote, mtegemezi wa mwanamume, mwovu, mgomvi na asiye na shukrani, mmbeya, msaliti anayetosheka na hali yake, barakala, kiumbe duni asiyestahili heshima, mwenye hasira za mkizi na mtu anayedanganywa kwa haraka. Aidha, Keter alishughulikia nafasi chanya aliyopewa mwanamke. Utafiti huu ulichunguza iwapo usawiri huu unafanana na wa mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za kuanzia mwaka wa 2000 hadi 2016. Anasema kuwa mwanamke katika tamthilia hizi mbili amechorwa kama mtu jasiri, mtu anayehitaji kuwa huru kimawazo, mlezi mwema wa watoto, mtu mwenye akili tambuzi, mkakamavu, mwerevu, mwenye bidii, mwenye mapenzi ya dhati na mzalendo. Utafiti huu ulichunguza iwapo usawiri huu wa Keter unafanana na wa mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za kuanzia mwaka wa 2000 hadi 2016. Keter anaibua wazo kwamba mwanamke ni mwanajamii anayeweza kujibidiisha vilivyo katika ujenzi wa jamii mpya. Dai hili lilichunguzwa na utafiti huu.

Vilevile, Keter alishughulikia changamoto zinazomkabili mwanamke katika harakati za kujikomboa. Changamoto hizi ni pamoja na: utamaduni, ndoa, uhafidhina, wanawake kutoshirikishwa katika maamuzi, hali ya kutojua miongoni mwa wanawake wenyewe, mfumo wa kiuchumi na ukosefu wa ushirikiano miongoni mwa wanawake wenyewe. Keter alishughulikia nafasi mbili za mwanamke: hasi na chanya kinyume na watafiti wengine walioegemea upande mmoja tu. Utafiti huu umechunguza ikiwa nafasi hizi chanya na hasi kumhusu mwanamke alizozungumzia Keter zinavyojitokeza katika tamthilia za *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016) na namna zinajenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike. Changamoto alizozibainisha zimewezesha utafiti huu kuchanganua mitazamo iliyopo kumhusu mwanamke. Usawiri wa mwanamke kiongozi unaeleweka vyema katika misingi ya mitazamo hii. Aidha mitazamo kumhusu mwanamke

inayotokana na changamoto hizi alizozibainisha Keter zilisaidia utafiti huu kuibua athari za taswira ya mwanamke kiongozi. Utafiti wa Keter ulijihusisha na taswira ya mwanamke kwa kurejelea tamthilia za *Kifo Kisimani* (2004) na *Natala* (1997). Utafiti huu hata hivyo umeangazia taswira ya mwanamke kiongozi (wala si mwanamke tu) katika tamthilia za *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016). Mitindo ya lugha inayojenga taswira hii imechunguzwa; jambo ambalo halikujitokeza katika utafiti wa Keter.

Muniu (2013) alishughulikia ujingina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango* (2003). Anatoa tafsili ya jingina kwa kusema kuwa, jingina ni mtu wa kike au kiume ambaye ni binadamu wa kawaida lakini anayeyatenda matendo mbalimbali hata kama ni hatari. Kimsingi, Muniu alizungumzia ushujaa katika tamthilia ya *Pango* kwa kuchanganua majingina chanya, hasi na pwaya. Alichunguza namna ujingina wa Katango unavyodhihirishwa miongoni mwa wazee, pingamizi na changamoto zinazomkabili mhusika Katango katika kudhihirisha ujingina wake na namna wahusika wengine walivyochangia ujingina wa mwanamke katika *Pango*. Katika kuhitimisha, Muniu anasema kwamba wahusika wa kike na kiume wanachangia katika kudhihirisha ujingina wa mwanamke katika *Pango* (2003). Hitimisho hili liliwezesha utafiti huu kuchunguza taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike na athari za taswira hii kwa uongozi wa mwanamke katika tamthilia teule. Kwa kuwa tamthilia ya *Pango* (2003) ni mojawapo ya tamthilia zilizorejelewa na utafiti huu, utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa wahusika aliowabainisha Muniu katika kumsawiri mwanamke kiongozi lakini kupitia lugha. Utafiti huu wa Muniu ni muhimu kwa utafiti huu kwani suala la uongozi wa mwanamke ni suala la kishujaa. Hata hivyo, ushujaa ni sifa mojawapo ya kiongozi. Utafiti huu umepiga hatua na kuchunguza sifa za mwanamke kiongozi mbali na ushujaa kwa kurejelea tamthilia teule.

Murungi (2013) alitafiti kuhusu namna mtindo unavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala* (1997). Alishughulikia namna wahusika wanavyosaidia kujenga maudhui. Anaonyesha namna Natala ametumiwa kama kielelezo cha utetezi wa haki na utambulisho wa mwanamke; Tango Mwina kama ishara ya utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume na Wakene kama mwakilishi wa mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke. Kupitia kwa wahusika Natala na Tango Mwina, Murungi alituchorea picha ya mwanamke katika tamthilia ya *Natala*. Utafiti huu ulisaidia utafiti huu kuchunguza mchango wa wahusika wa kike na kiume katika kujenga taswira ya mwanamke kiongozi. Murungi alimwangazia mhusika mwanamke kwa ujumla. Utafiti huu

ulimhusu mwanamke kiongozi na uliangazia tamthilia za Kiswahili tangia mwaka wa 2000: *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016).

Mapunjo (2014) alichunguza usawiri wa mwanamke kama kiongozi katika tamthilia ya *Nguzo mama* (Muhando, 1982) na *Kivuli Kinaisha* (Mohammed, 1990). Ameangalia namna mwanamke alivyochorwa kama kiongozi kwa mujibu wa tamthilia husika. Baadhi ya picha alizoziibua ni pamoja na mwanamke kama: mwenye maamuzi, mfuata sheria, mtetezi wa wanawake, anayependa elimu na mwenye huruma kwa wenzake. Baadhi ya taswira alizozibainisha Mapunjo zilichunguzwa ili kubainisha iwapo zinajitokeza katika tamthilia zilizotungwa tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 ikikumbukwa kwamba tamthilia alizozirejelea ziliandikwa kabla mwaka wa 2000.

Aidha, Mapunjo alishughulikia changamoto zinazomkabili kiongozi wa jinsia ya kike na namna ya kuzitatua changamoto hizo. Kutokana na changamoto hizo, utafiti huu uliibua baadhi ya mitazamo iliyopo kumhusu mwanamke kiongozi. Mitazamo hii ilisaidia utafiti huu kupambanua athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke. Mapunjo alimwangazia mhusika mwanamke ambaye ni kiongozi namna utafiti huu ulivyofanya. Vilevile, utafiti wa Mapunjo ulijikita katika utanzu wa tamthilia sawa na utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wa Mapunjo ni tofauti na huu. Mapunjo aliangazia changamoto zinazomkabili kiongozi wa kike na namna ya kukabiliana nazo. Utafiti huu hata hivyo umechunguza jinsi mitindo ya lugha inavyojenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike. Kwa mujibu wa Mugambi (1982) na Murungi (2013) mitindo ya lugha ni muhimu katika kuibua maudhui ya kazi ya fasihi. Mitindo ya lugha ni kipengele muhimu sana katika kubainisha masuala ya kiuana katika fasihi (King'ei, 2002). Utafiti huu umepiga hatua na kuchunguza athari za usawiri wa mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke: suala ambalo hakuliangazia Mapunjo. Mapunjo alirejelea tamthilia zilizotungwa kabla ya mwaka wa 2000. Utafiti huu umeangazia tamthilia zilizotungwa tangia mwaka 2000 hadi 2016 ambapo hadhi ya wanawake viongozi imeendelea kuimarika na jamii kuonekana kukubali mabadiliko haya (Oluoch, 2017; Munyasia & Wandiemba, 2017). Hivyo taswira iliyobainishwa na utafiti huu inaoana na mabadiliko ya kiutunzi tangia mwaka wa 2000.

Aidha, tamthilia alizozirejelea Mapunjo ni tofauti na za utafiti huu. Mapunjo alirejelea *Nguzo Mama* (1982) na *Kivuli Kinaisha* (1990). Utafiti huu umerejelea *Pango* (2003), *Posa za Bi Kisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016). Isitoshe, utafiti huu umetumia

nadharia ya udenguzi kinyume na Mapunjo aliyetumia nadharia ya ufeministi. Mapunjo katika utafiti wake anawapendekezea watafiti wa baadaye kutafiti kuhusu suala la uongozi wa wanawake kwa kurejelea utanzu wa tamthilia au tanzu zingine za kifasihi kwani kulingana naye suala hili halijashughulikiwa katika tafiti nyingi za Kifasihi. Utafiti huu umetimiza pendekezo hili kwa kujikita kwa utanzu wa tamthilia.

2.3 Nafasi ya Mitindo ya Lugha katika Kujenga Taswira ya Mhusika

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) vijenzi vya fasihi ni fani na maudhui. Fani hujumuisha: mtindo, muundo, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari (Msokile, 1993, Wamitila, 2003). Lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa kwa mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake (Trudgil 1974; TUKI 1990). Kwa mujibu wa Ntaragwi (2004) lugha ya fasihi huwa tofauti na lugha ya kawaida. Kulingana naye, fasihi huwa na lugha yake ambayo yaweza kuhakikiwa. Isitoshe, lugha hii huwa ya kuzua na kulisimua hisia za msomaji. Syambo & Mazrui (1992) wanatoa hoja kuwa ni muhimu lugha inayotumika katika utanzu wa tamthilia iwe na uwezo wa kuzua na kuendeleza matendo ya wahusika wake kwani mazungumzo ya wahusika ndiyo yanayotupeleka mbele katika plati. Isitoshe, utafiti unaochunguza wahusika katika tamthilia hauna budi kuchunguza lugha iliyotumiwa kwani matendo ya wahusika huibuliwa na kuendelezwa na lugha. Utafiti huu ulichunguza lugha katika tamthilia teule kwani ni kutokana na lugha hii ambapo taswira ya mwanamke kiongozi iliibuliwa.

Ntaragwi (2004) analinganisha lugha na mtambo anaotumia mtunzi kusafirisha maudhui yake kwa hadhira yake. Wamitila (2003) anasema kwamba lugha ndiyo nyenzo kuu ya kazi ya fasihi na kwamba dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi hayawezi kuwasilishwa na kuwafikia wasomaji bila kuweko lugha. Kulingana naye, lugha hii humsaidia mtunzi kuwasawiri wahusika wake na kudhihirisha dhamira yake. Utafiti huu ulichunguza namna lugha ilivyomsawiri mwanamke kiongozi.

Mtindo ni jinsi ya kufanya kitu kwa kufuata taratibu fulani (TUKI, 2014). Mbatia (2001) anatoa fasili ya mtindo kama namna mtunzi wa kazi ya kifasihi anavyotumia lugha kujieleza. Msanii huwa na wazo analotaka kuwasilisha kwa hadhira yake. Wazo hili ataliwasilisha kupitia kwa lugha. Atateua miundo ya lugha inayoweza kuwasilisha na kufanikisha mawazo yaliyo katika kazi yake (Mwangi, 2005). Wamitila (2003) anaibua hoja kuwa, mtindo ni jumla ya mbinu au

sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Kulingana naye, dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Anasema kwamba katika kuchunguza mtindo, mhakiki huangalia uteuzi wa msamiati, mbinu za lugha, mbinu za sanaa, mbinu ya kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya na uakifishaji wake.

Kulingana na Mbatia (2001) uchanganuzi wa mitindo ya lugha huhusu mambo kama uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi na kwa jumla vipengele vyote vya lugha. Senkoro (1982) anatoa hoja kwamba, kuna aina mbalimbali ya mitindo ya lugha kama: mbinu za lugha, mbinu za sanaa, lahaja, uchaguzi wa msamiati na miundo ya sentensi. Anafafanua tamathali za usemi kama maneno, sentensi au misemo inayotumiwa na Wanafasihi kuwasilisha kazi zao. Kwa mujibu wa Mbatia (2001) tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi katika maana na mpangilio wa maneno. Mbinu za sanaa ni jumla ya njia anazotumia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake ambazo huwa ni zao la ubunifu na uzoefu wake (Wamitila, 2003). Mbinu za lugha hushirikisha: tashbihi, sitiari, tasfida, tashihisi, chuku, maswali balagha, tabaini, jazanda, kinaya, kejeli, semi, majazi na takriri na mbinu za sanaa hujumuisha: taharuki, sadfa, ndoto, nyimbo na kisengere nyuma (Wamitila, 2003). Katika kuchunguza mitindo ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi, utafiti huu ulijikita kuchunguza mbinu za lugha katika tamthilia za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000.

Mwangi (2005) alichunguza fani katika tamthilia za Wamitila za *Wingu la Kupita* (1999) na *Pango* (2003). Kwa kurejelea tamthilia hizi, alishughulikia matumizi ya lugha kitamathali. Alichunguza lugha ya vijana na wazee katika tamthilia hizi. Alichunguza vipengele vya tamathali za lugha kama: kejeli, misemo, tashbihi na sitiari. Baadhi ya tamathali za lugha alizozibainisha Mwangi kama misemo, tashbihi na sitiari zilichunguzwa na utafiti huu ili kuona namna mwanamke kiongozi anavyosawiriwa kwazo. Anaeleza kuwa ploti ya tamthilia ya *Pango* (2003), inaangazia utata wa kisiasa, uchumi, uongozi na migogoro ya wimbi la ukale na usasa. Utafiti huu ulithibitisha maelezo ya Mwangi kuwa ploti ya tamthilia hii inaangazia suala la uongozi ila utafiti uliegemea uongozi wa mwanamke kinyume na Mwangi aliyeangazia uongozi wa mwanamumme aitwaye Ngwese. Kando na tamthilia ya *Pango* (2003), utafiti huu ulirejelea tamthilia za *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016). Mwangi alichunguza suala la fani; utafiti huu umepiga hatua na kuchunguza namna baadhi ya vipengele vya fani alivyobainisha Mwangi vinavyomsawiri mhusika mwanamke aliye uongozini.

Nguta (2011) alishughulikia fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Pango* (2003) na *Mama Ee* (1987) kwa kutumia nadharia ya urasimu na ufeministi. Aliangazia namna wahusika walivyotumia lugha katika mazungumzo baina yao na uzungumzi nafsia. Kipengele cha lugha alichokishughulikia Nguta ndicho kilichofanya utafiti wake kuwa faafu kwa utafiti huu. Mitindo ya lugha aliyoizungumzia Nguta ilichunguzwa kwa lengo la kujua ikiwa mitindo hii imetumiwa katika tamthilia teule kumsawiri mwanamke kiongozi. Alishughulikia tamthilia ya *Pango* ambayo ni tamthilia mojawapo iliyojielewa na utafiti huu. Picha ya mwanamke aliyoiibua katika tamthilia hii kama ujasiri na usomi iliwezesha utafiti huu kuibua taswira ya mwanamke kiongozi. Utafiti wa Nguta ulijikita tu katika usawiri wa mhusika mwanamke kwa ujumla; haukushughulikia mwanamke kiongozi namna utafiti huu ulivyofanya.

Murungi (2013) alichunguza namna mtindo ulivyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala* (1997). Aliangazia namna mbinu za lugha na sanaa kama: tashihisi, kinaya, jazanda, taswira, maswali balagha, semi, sitiari, usemajikando na uzungumzi nafsia zilivyoendeleza maudhui. Mitindo ya lugha aliyoieleza Murungi ilichunguzwa kwa minajili ya kubainisha iwapo inachangia kujenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike kwa mujibu wa tamthilia teule. Murungi anatamatisha kwa kusema kuwa mtindo umechangia pakubwa kujenga na kuendeleza maudhui katika *Natala*. Utafiti huu ulibaini mchango wa mitindo ya lugha katika kumsawiri mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia teule. Murungi alishughulikia wahusika wa jinsia zote mbili: kike na kiume katika tamthilia ya *Natala*. Utafiti huu umemwangazia mhusika wa jinsia ya kike kwa namna ambavyo anajitokeza kama kiongozi kwa kurejelea tamthilia za teule za Kiswahili kuanzia mwaka 2000 hadi 2016.

2.4 Mapitio Kuhusu Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya udenguzi imetumiwa katika baadhi ya tafiti za fasihi. Mwamzandi (2013) alitumia nadharia hii kuhakiki riwaya teule za karne ya ishirini na moja. Aliangazia riwaya za *Dunia Yao* (Mohammed, 2006) na *Nyuso za Mwanamke* (Mohammed, 2010). Mwamzandi alichunguza namna kipengele cha ukinzani wa jozi za maneno kilivyojitokeza ndani mwa matini. Alichunguza namna mhusika mkuu katika *Nyuso za Mwanamke* ambaye ni Nana anavyotumia jozi za maneno yanayokinzana kama: kuwepo/kutokuwepo, ukweli/uwongo, umoja/wingi, weusi/weupe, wema/uovu na uuke/uume. Kwa kutumia mhusika Ndi ambaye ni mhusika mkuu katika *Dunia Yao*, Mwamzandi alieleza kuhusu dhana ya kivuli cha maana. Kulingana naye,

kivuli cha maana ni ile sehemu ya pili ya neno au dhana ambayo aghalabu huenda ikaachwa nje na isizungumziwe waziwazi na mwandishi. Kipengele hiki cha ukinzani wa jozi za maneno alichokifafanua Mwamzandi kinaoana na maneno ya Berthes (2011) aliyesema kwamba matini huwa na maana mbalimbali. Kwa kudengua jozi za maneno, maana hizi mbalimbali huweza kubainika. Utafiti wa Mwamzandi ulisadia utafiti huu kuchunguza maneno mbalimbali katika tamthilia husika ili kubaini namna yanavyojenga picha ya kiongozi wa jinsia ya kike. Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo dhana ya kivuli cha mana alioieleza Mwamzandi inajitokeza katika tamthilia teule na inavyochangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule. Kwa kutumia nadharia ya udenguzi, Mwamzandi alihakiki riwaya za karne ya ishirini na moja. Kwa kutumia nadharia ya udeenguzi, utafiti huu ulihakiki tamthilia za teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016.

Mung'atha (2012) alichunguza ufumbuaji wa mashairi ya Kiswahili kwa kuangazia diwani za *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita* kwa kutumia nadharia za udenguzi na uhistoria Mpya. Aliteua mashairi kumi kutoka diwani hizi mbili kwa kuzingatia mada za unyumba, majonzi na maliwazo. Mung'atha alibainisha vipengele vya lugha vilivyochangia kufumba maana au ujumbe wa mwandishi. Aidha, alidhihirisha namna ya kupata fasiri tofauti za maana ya shairi ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Kipengele cha lugha alichotumia Mung'atha ni mhimili mojawapo wa nadharia ya udenguzi ambao umetumiwa na utafiti huu. Katika kuchunguza namna vipengele vya lugha vinachangia uibuaji wa fasiri mbalimbali ndani mwa shairi, Mung'atha alsisitiza mawazo ya wanaudenguzi kuwa kwa kuchunguza kwa makini maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini, mhakiki aweza kuibua maana mbalimbali ambazo zilikuwa zimefichama. Utafiti huu umechunguza namna mitindo ya lugha inavyojenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule.

Manyama (2014) alichunguza ujitokelezaji wa wahusika wa tamthilia za Kiswahili kwa kutumia nadharia ya udenguzi. Aliangazia tamthilia zifuatazo: *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (Hussein, 1976) *Mkutano wa Pili wa Ndege* (Amadi na Lihamba, 1992), *Nguzo mama* (Mlama, 1981), *Heshima Yangu* (Mlama, 1974), *Mashetani* (Hussein, 1971), *Kivuli Kinaisha* (Mohammed, 1990), *Lina Ubani* (Mlama, 1984), *Aliyeonja Pepo* (Topan, 1973) na *Morani* (Mbogo, 1993). Alidhihirisha namna wahusika wa fasihi simulizi walivyojitokeza kiudenguzi katika tamthilia za *Mkutano wa Pili wa Ndege* na *Jogoo Kijijini na Ngano za Jadi*. Dhana aliyoshirika Manyama

katika dhihirisho hili ni dhana ya unyume. Kwa mujibu wa Mishra (2018), udenguzi hulenga kubainisha unyume, utata, kinaya, ukinzani, utofauti na mwachano ndani mwa matini. Kulingana naye, udenguzi wa mhusika Chizi katika *Nguzo Mama* unatokea anapotumiwa na mwandishi kueleza kuhusu demokrasia ambalo ni jambo la muhimu na la kimsingi ilhali jamii inamwona kwamba hawezi kusema kitu chochote cha maana. Hii ni dhana ya kinaya.

Kwa mujibu wa Manyama, udenguzi katika tamthilia ya *Mashetani* unabainika pale mwandishi anapodengua uhusika wao kwenye uhusika wa kishetani na kibinadamu. Katika *Mashetani*, mwandishi amezifumba sifa kwa kutumia wahusika Shetani na Binadamu ili kuakisi maisha halisi ya Kitaru na Juma. Manyama anasema kwamba, udenguzi wa wahusika katika tamthilia ya *Kivuli Kinaisha* unatokea pale Bi Kirembwe anapochorwa kama mwenye amri na sauti ya kuwatisha hadi wanaume licha ya kwamba yeye ni mwanamke wa Kiafrika. Kwa kutumia nadharia ya udenguzi, Manyama ameangazia utanzu wa tamthilia namna utafiti huu ulivyofanya. Hata hivyo, ameangazia udenguzi wa wahusika tu. Utafiti huu umetumia nadharia ya udenguzi kwa mapana zaidi ili kuonyesha namna mihimili ya lugha, muktadha na mtazamo inavyochangia kujenga picha ya mwanamke ambaye ni kiongozi. Tamthilia alizorejelea Manyama zilitungwa kabla ya mwaka wa 2000. Utafiti huu umeangazia tamthilia za kuanzia mwaka 2000 hadi 2016.

2.5 Hitimisho

Sura ya pili imeshughulikia mapitio ya maandishi. Katika sura hii, imebainika kuwa tafiti nyingi za fasihi kumhusu mhusika mwanamke zimemsawiri mwanamke kwa njia hasi. Isitoshe, nyingi yazo zimemwangazia mwanamke kwa ujumla bila kuangazia uongozi wake. Aidha, imedhihirika kuwa mitindo ya lugha ni kipengele muhimu katika tamthilia ya Kiswahili na utafiti wa kifasihi. Utafiti huu kupitia sura hii umebaini kuwa, kazi ya fasihi husonga mbele kupitia kwa wahusika ambao waweza kusawiriwa kupitia kwa lugha, matendo na mitazamo.

SURA YA TATU: NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa sampuli na usampulishaji na mbinu za ukusanyaji data. Aidha, uaminifu na uthabiti wa vifaa vya kukusanya data unaangaziwa.

3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kithamano ambapo muundo uliozingatiwa ni wa kiuchanganuzi. Kothari (1990) anatoa maoni kwamba, utafiti wa kithamano ni utafiti wa ubora ambao huchunguza tabia za binadamu na huzama katika kujibu maswali kama vile: mbona watu hufikiri na kutenda vitu fulani. Utafiti huu ni wa kithamano kwa sababu ulijikita katika kuchunguza namna lugha, matendo na mitazamo ya mhusika mwanamke kiongozi pamoja na wahusika wengine inavyojenga taswira ya mwanamke kiongozi. Mwanje (2001) anatoa hoja kuwa, muundo wa kiuchanganuzi ni bora kwa makala ya kimatini. Muundo huu uliteuliwa kwa ufaafu wake wa kuafikia malengo ya utafiti katika kuchanganua matini ambayo ni tamthilia nne. Uchanganuzi huu ulishughulikia mitindo ya lugha inavyojenga taswira ya mwanamke kiongozi, matendo na mitazamo ya mwanamke kiongozi pamoja na wahusika wengine wanaojenga taswira hii.

3.3 Mukadha wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa tamthilia katika fasihi ya Kiswahili. Fasihi ya Kiswahili ina tanzu zingine kama vile: riwaya, hadithi fupi na ushairi. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) na Murumba (2011) tamthilia hujengwa kupitia matendo na mazungumzo ya wahusika. Utafiti huu ulijikita kwa utanzu wa tamthilia kwani ni kupitia matendo na mazungumzo ya moja kwa moja ya wahusika ndipo taswira ya mwanamke kiongozi imebainika (Wamitila, 2003; Onyoni, 2012). Aidha utanzu wa tamthilia ndio ambao umemsawiri mhusika mwanamke kupitia kwa mazungumzo na matendo. Nyingi ya tamthilia hasa zile za kabla mwaka wa 2000 zilimdunisha mhusika mwanamke (Onyoni, 2012; Murungi, 2013). Tamthilia zilizoteuliwa na utafiti huu ni zile zilizotungwa tangia mwaka 2000 hadi 2016 na ambazo zina mhusika mwanamke ambaye ni

kiongozi. Utafiti huu uliangazia tamthilia zilizotungwa tangia mwaka 2000 hadi 2016 kwa kuwa ni kuanzia mwaka huu ambapo kiongozi wa jinsia ya kike ameangaziwa pakubwa si tu katika jamii bali pia katika fasihi ikilinganishwa na miaka ya awali.

3.4 Kundi Lengwa

Utafiti huu ulilenga tamthilia zilizoandikwa tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 ambapo hadhi ya mwanamke kiongozi imeendelea kuimarika na jamii kuonekana kukubali uongozi wa mwanamke (Mulila, 2009). Tamthilia zilizotungwa nchini Kenya na Tanzania tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 ni ishirini na tatu (Gromov, 2014; Muthui, 2019). Hizi ni pamoja na: *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (Mohammed, 2000); *Upotovu* (Kimunyi, 2000); *Siri* (Topan 2000); *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001); *Pango* (2003); *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (Mberia, 2004; *Mazonge* (Rashid, 2004); *Safari* (Omwaka, 2004); *Sudana* (Mazrui & Njogu, 2005); *Sumu ya Bafe* (Wamitila, 2006); *Zilizala* (Njogu & Chimera, 2006); *Migogoro* (Mbatia, 2006); *Chamchela* (Arege, 2007); *Posa za Bikisiwa* (Mohammed & King'ei, 2008); *Mstahiki Meya* (Arege, 2009); *Seserumbe* (Wamitila, 2009); *Amri ya Wakati* (Mohammed, 2009); *Vitanzi vya Tamaa* (Omar, 2009); *Janga la Werevu* (Mohammed, 2011); *Kimya Kimya Kimya* (Mohammed, 2011); *Kijiba cha Moyo* (Arege, 2012), *Mbaya Wetu* (Walibora, 2014) na *Kigogo* (Kea, 2016).

3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ya utafiti huu ilikuwa tamthilia nne: *Pango* (Wamitila, 2003); *Posa za Bikisiwa* (King'ei & Mohammed, 2008), *Kimya Kimya Kimya* (Mohammed, 2008) na *Kigogo* (2016). Utafiti huu ulilenga tamthilia zilizotungwa tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Kuna jumla ya tamthilia ishirini na tatu zilizotungwa tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 kutoka nchi za Kenya na Tanzania. Nchi hizi zimeangaziwa kwa kuwa zina waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili (Bertoncini, 2009; Gromov, 2014; Olali, 2015). Tamthilia teule ziliteuliwa kupitia kwa mbinu ya usampulishaji dhamirifu. Kwa mujibu wa Patton (1990), kuna mikakati mbalimbali ya usampulishaji dhamirifu. Utafiti huu ulitumia mkakati wa usampulishaji dhamirifu wa kivigezo. Kulingana na Patton, mkakati huu huteua sampuli ambayo huwa imeafiki kigezo fulani muhimu kwa minajili ya uchambuzi wa kindani. Mkakati huu uliwekea utafiti huu msingi wa kuteua tamthilia nne: *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2008) na *Kigogo*

(2016). Kila tamthilia iliyoteuliwa iliafiki kigezo cha kuwa na mhusika mwanamke ambaye ni kiongozi.

Creswell (2003) anaibua hoja kuwa, usampulishaji dhamirifu ni mbinu ya usampulishaji ambapo mtafiti huteua sampuli kwa sababu inasaidia uelewa wa suala la utafiti na mada kuu ya utafiti. Kulingana na Mugenda & Mugenda (2003) mtafiti hutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu wakati ambapo sampuli husika huwa na data muhimu kwa utafiti wake kwa mujibu wa madhumuni yake. Oso & Onen (2009) nao wanadai kuwa, katika mbinu hii mtafiti huamua nani au nini cha kusampulisha kulingana na mada yake ya utafiti. Wanasema kwamba, kwa kufanya hivi, mtafiti huweza kuteua sampuli iliyo muhimu pekee kwa utafiti wake. Maoni haya yanaoana na ya Patton (1990) anayesema kwamba, utafiti wa kithamano huzama ndani ya sampuli ndogo hata zingine moja tu zilizoteuliwa kidhamirifu.

Morse (2000) anaibua hoja kuwa, ukubwa wa sampuli hutegemea mambo kama: ubora wa data, upeo wa utafiti, mada, mbinu ya utafiti na idadi ya mahojiano. Ni kwa msingi wa kigezo cha mada alichozungumzia Morse (2000) ndipo utafiti huu uliteua tamthilia nne kwa kuwa zinashughulikia maudhui ya uongozi wa mwanamke. Isitoshe, tamthilia hizi zimeandikwa katika miaka tofautitofauti ya kipindi kati ya mwaka 2000 hadi 2016. Utafiti huu ulilenga kubainisha namna mwanamke kiongozi anavyosawiriwa katika miaka hii tofauti ili kuwa na picha kamili ya mwanamke kiongozi tangia mwaka wa 2000 hadi 2016.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji data

Mbinu ya maktaba ilitumiwa kukusanya data. Tamthilia teule: *Pango*, Wamitila (2003); *Posa za Bikisiwa*, Kinge'i & Mohammed (2008), *Kimya Kimya Kimya*, Mohammed (2011) na *Kigogo*, Kea (2016) zilisomwa kwa lengo la kudondoa sifa za mwanamke kiongozi, mitindo ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi na athari za usawiri wa mwanamke kwa uongozi wa mwanamke. Sifa za mwanamke kiongozi ziliibuliwa kwa kuchunguza matendo, mitazamo na lugha ya wahusika katika tamthilia teule. Baada ya kuibuliwa, sifa hizi zilinukuliwa kwenye daftari. Orodha ya uchunguzi ilisaidia katika kuhakikisha kuwa sifa mbalimbali za mwanamke kiongozi zimeibuliwa katika kila tamthilia teule (rejelea kiambatisho 1 uk.160). Mitindo mbalimbali ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi ilinukuliwa katika usomaji wa tamthilia hizi kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi iliyokuwa imetayarishwa kimbele (rejelea

kiambatisho 2 uk. 161). Orodha hii iliandaliwa kwa kuzingatia uanishaji wa mitindo ya lugha kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Athari za usawiri wa mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke ziliibuliwa kutokana na mitazamo, matendo na lugha ya wahusika na kunukuliwa kwenye daftari kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi (rejelea kiambatisho 3 uk. 162).

3.7 Uaminifu na Uthabiti wa vifaa vya kukusanya data

Kwa mujibu wa Kothari (1990), utafiti wa kithamano wafaa kuwa thabiti na wa kutegemewa. Ili kuafikia hili, vifaa vya utafiti vyafaa kuwa thabiti na sahihi (Mugenda & Mugenda, 2003). Utafiti huu ulitumia orodha ya uchunguzi kukusanya data.

Kwa mujibu wa Ritchie & Lewis (2003) matumizi ya data iliyokusanywa hupeana ithibati ambayo hufaa sana wakati wa kuchanganua na kufasiri data. Utafiti huu ulikusanya data kutoka kwa tamthilia teule. Uchanganuzi na ufasiri wa data ulitokana na data iliyokuwa imekusanywa. Kulingana na Golafshani (2003), uaminifu wa utafiti hupatikana wakati mtafiti huthibitisha data iliyokusanywa kabla ya kuibua ufasiri kutokana na data hiyo. Data iliyokusanywa ilithibitishwa kwa kurejela tamthilia teule kwa minajili ya kuhakikisha kuwa data hii ni sawa na yaliyomo katika tamthilia teule na orodha ya uchunguzi.

Kwa kurejelea Golafshani (2003), utafiti utakuwa wa kuaminika ikiwa mhakiki atahakikisha kuwa ameyapa matokeo yake nguvu ambazo kulingana naye hutokana na ubora wa data iliyokusanywa. Uchanganuzi wa data na ufasiri wa matokeo haujatendeka katika ombwe tupu. Umejikita katika data iliyokusanywa kupitia orodha ya uchunguzi. Ni kutokana na uchanganuzi na ufasiri huu ndipo mahitimisho yametolewa. Maoni ya wataalamu yamerejelewa ili kuhakikisha kuwa matokeo ni ya kutegemewa. Isitoshe utafiti huu umehakikisha kuwa taswira ya mhusika mwanamke na mitindo ya lugha iliyobainishwa kwa kutumia orodha ya uchunzaji ni ile inayopatikana katika tamthilia teule. Ithibati imetolewa kuhusu sifa na mitindo hii kwa kurejelea tamthilia teule.

Golafshani (2003) anasema kwamba, utafiti sharti uwe wa kutegemewa hivi kwamba iwapo utafiti huo waweza kurudiwa kwa misingi ya utafiti wa awali, matokeo hayatakuwa tofauti. Iwapo utafiti huu unaweza kurudiwa kwa mujibu wa madhumuni, nadharia na tamthilia teule, matokeo yatafanana. Kwa kuwa utafiti huu umerejelea matini yaliyokwisha kuandikwa, mtu yeyote anaweza kurejelea tamthilia rejelewa ili kuthibitisha data ambayo imekusanywa.

3.8 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Baada ya data kuhusu taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili kupangwa, ilichanganuliwa. Mbinu ya uhakiki wa yaliyomo ilitumiwa kuichanganua data iliyokuwa imekusanywa. Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa, uhakiki wa yaliyomo ni mbinu ambayo huchunguza uzito ambamo maneno fulani hutumiwa na hueleza kwa utaratibu umbo au undani wa matini. Wanaendelea kusema kuwa, mbinu hii ya uchanganuzi humpa mtafiti nafasi ya kuhakiki kwa makini vipengele kama vile muktadha na mazingira ya kazi fulani ya sanaa na maana inayoibuka kutokana na vipengele vya sanaa hiyo. Mbinu hii ilitumiwa kwa kuwa utafiti huu ulichunguza matini ya tamthilia teule kwa umakini ili kubaini taswira ya mwanamke kiongozi iliyomo. Baada ya kuibua data, ilipangwa. Kwa mujibu wa White & Marsh (2008), mtafiti anayetumia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo afaa apange data katika vijishehemu vidogovidogo kabla ya kuichanganua. Kwa msingi huu, data kuhusu sifa za mwanamke kiongozi na mitindo ya lugha inayomsawiri mwanamke kiongozi ilipangwa kwa kuzingatia tamthilia ambamo data hiyo imeibuliwa. Aidha, athari za usawiri wa mwanamke kwa uongozi wa mwanamke kiongozi zilipangwa katika makundi mawili: hasi na chanya. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yalifasiriwa kutokana na data hiyo na mahitimisho kutolewa kwa mujibu wa madhumuni. Matokeo yenyewe yalizingatia hali halisi mintarafu suala la utafiti, mihimili ya nadharia ya udenguzi na madhumuni ya utafiti.

3.9 Masuala ya Kimaadili

Masuala ya kimaadili yalipewa kipaumbele katika utafiti huu. Masuala ya kimaadili huibuka katika aina zote za utafiti: utafiti wa takwimu na wa kithamano (Padgett, 2002). Creswell (2003) anaibua hoja kuwa, katika uandishi na usambazaji, mtafiti hafai kudanganya, kuzima au kubatilisha matokeo ya utafiti ili kutimiza mahitaji yake au ya hadhira. Usahihi wa matokeo ya utafiti huu ulizingatiwa kwa kuhakikisha kuwa matokeo hayabatilishwi kwa vyovyote vile. Kila kazi iliyosomwa na kurejelewa katika utafiti huu imetambuliwa. Haki miliki za watunzi zimezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa yaliyoandikwa kwenye vitabu vilivyotumiwa katika utafiti huu hayapunguzwi au kuongezwa. Aidha, utafiti huu uliidhinishwa na Tume ya Kimaadili ya Chuo Kikuu cha Maseno (rejelea barua ya idhini katika kiambatisho 4, uk.163). Isitoshe, taratibu zote zilizowekwa na Chuo Kikuu cha Maseno zilifuatwa. Mathalani, pendekezo la utafiti

liliidhinishwa na Chuo (Rejelea Barua ya Kuidhinisha pendekezo la utafiti katika uk. 164). Katika kujadili mawazo, utafiti huu ulihakikisha kuwa usiri wa watunzi kwa mfano; uraibu, falsafa na sifa zao umezingatiwa na maisha ya kibinafsi ya watunzi wa kazi husika hayajaingiliwa.

3.10 Hitimisho

Sura hii imebainisha kuwa utafiti huu ni utafiti wa kithamano uliojikita katika tamthilia nne za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000: *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016). Muundo wa kiuchanganuzi umetumiwa. Data imekusanywa kupitia njia ya makataba na kupangwa kisha kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo Data imewasilishwa kwa njia ya maelezo.

SURA YA NNE: TASWIRA MWANAMKE KIONGOZI KATIKA TAMTHILIA TEULE

4.1 Utangulizi

Utafiti huu katika sura hii unashughulikia taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi. Katika kufanya hivi, utafiti huu unaangazia sifa za mwanamke kiongozi na mitindo ya lugha inayochangia kujenga taswira hii. Sifa hizi zimebainishwa kwa kuchunguza mitazamo, lugha na matendo ya wahusika katika tamthilia teule. Aidha, sura hii inashughulikia mitindo ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi. Tamthilia teule zilisomwa huku sifa za mwanamke kiongozi, mitindo ya lugha pamoja na mitazamo ya wahusika inayochora picha ya mwanamke kiongozi ikinukuliwa kwenye kijitabu kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi. Baadaye, data hii ilipangwa na kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo.

4.2 Sifa za Mwanamke Kiongozi

Katika sehemu hii, utafiti huu umerejelea sifa ambazo zinajenga taswira ya mwanamke katika tamthilia teule. Kwa mujibu wa Mdee, Njogu & Shafi (2011) sifa ni mambo mazuri au mabaya ya mtu au kitu. Sifa za mhusika zaweza kuwa chanya au hasi (Wamitila, 2003). Katika fasihi, sifa hizi hubainika kupitia kwa matendo, mitazamo na lugha ya wahusika (Njogu & Chimera, 2007; Mirikau, 2011). Kwa maneno ya Muniu (2011), wahusika katika tamthilia huwa watu na hivyo huwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na yale wanayoyatenda au yale yanayosemwa na msimulizi au wahusika wengine. Katika kuchunguza sifa za mhusika mwanamke kiongozi, utafiti huu umeangazia matendo, mitazamo na lugha ya mwanamke kiongozi na wahusika wengine.

4.2.1 Mwanamke kama Kiongozi Mwenye Msimamo Thabiti

TUKI (2014) inaeleza msimamo kama maoni ya mtu juu ya jambo fulani na thabiti kama -enye nguvu, -siyotetereka, imara, madhubuti. Kwa kusema mtu ana msimamo thabiti ina maana kuwa mtu huyo ana maoni au falsafa madhubuti au imara isiyotetereka.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Pango* (2003) Katango anakataa kupashwa tohara. Babake Katango anadhihirisha hali hii anapomwambia Katango kwa hasira:

.... *Wewe tangu ugomee kupashwa... (uk.19).*

Mwamzandi (2013) katika utafiti wake alitumia nadharia ya udenguzi. Anasema kwamba kuna maana ambayo huwa imefichama ndani mwa matini na ambayo huenda isiibuliwa pasipo usomaji wa kina wa matini hayo. Wanaudenguzi husisitiza usomaji wa kina wa matini ili kubaini maana mbalimbali zilizomo. Kwa kurejelea maneno ya babake Katango katika usemi huu twaweza kumwona Katango kama mtu anayehisi utamaduni wake. Hata hivyo kwa kuchunguza maneno haya kwa undani na kulingana na muktadha wa jamii ya Pango, maana nyingine yaweza kuibuka. Kwa mujibu wa Wanaudenguzi, uelewa wa muktadha unasaidia uelewa wa maana ndani ya matini (Ntaragwi, 2004). Kulingana na muktadha wa utamaduni wa jamii ya Pango, mwanamke alipaswa kupashwa tohara. Tendo la Katango kukataa kukeketwa licha ya shinikizo kutoka kwa utamaduni wa jamii yake linamsawiri kama kiongozi mwenye msimamo thabiti.

Utafiti wa Shirika la Afya Ulimwenguni umebaini kwamba ukeketaji wa mwanamke ni jambo linalioendelea katika jamii mbalimbali za Afrika (World Health Organisation [WHO], 1998). Kwa mujibu wa Cheserem (2011) ukeketaji wa wanawake ni jambo linaloendelea nchini Kenya. Kulingana naye, asilimia 38 ya wanawake wa miaka 15 hadi 49 waliripoti kukeketwa. Hili linatendeka licha ya maendeleo yaliyotokea katika jamii tangia mwaka wa 2000 pamoja na juhudi za serikali, mashirika na dini mbalimbali kukomesha ukeketaji wa mwanamke. Ingawa utamaduni wa jamii ya Katango ulimshurutisha mwanamke kukeketwa, Katango ana mtazamo kuwa tendo hili lingemdunisha.

Umuhimu wa muktadha katika kuibua maana ndani ya matini ni jambo ambalo husisitizwa na wanaudenguzi (Ntaragwi, 2004). Kwa mujibu wa muktadha wa utamaduni wa *Pango*, mwanamke hakufaa kuwania wadhifa wa uongozi. Uongozi ulikuwa jukumu la mwanamume. Mtazamo huu wa kitamaduni ulitokana na imani kuwa mwanamke kamwe hawezi kuongoza kwa sababu ya jinsia yake. Kulingana na Katola (2006) kuna mifumo ya kijamii iliyojaa taasubi ya kiume ambayo huchangia katika kumdhulumu mwanamke. Mifumo hii kulingana naye humfanya mwanamke kudhulumiwa na kupewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Mfumo wa jamii ya Pango ulikuwa na taasubi ya kiume ambayo ilimpinga mwanamke kuwania wadhifa wa

uongozi. Ni katika muktadha huu wa kitamaduni ambapo babake Katango anataka Katango aache kumpinga Ngwese kwani ana mtazamo kuwa mwanamke ni kiumbe duni ambaye hafai kuongoza wala kumpinga mwanamume. Anamwuliza Katango:

Kwanza nawe kwa nini unajitia ushujaa wa kwenda kinyume na utamaduni wetu? (uk.35).

Isitoshe mamake Katango kwa kuona madhila aliyokuwa akiyapitia mwanawe katika ushindani wa kuongoza anamwambia Katango aache kugombea uongozi wa Pango. Wakati Katango anavamiwa njiani, Sota anaenda kumwita Mama. Ajapo, anamshauri Katango kuachana na harakati za kuwania uongozi wa Pango. Katango anakataa kufanya hivyo. Mamake anarudia ushawishi huu:

Ni afadhali ukawazia tena...Katango mwanangu, wimbo wa mjinga huchezwa na wajinga wenzake... (uk.34).

Pindi mamake atamkapo maneno haya, Katango kwa mara ya pili anasisitiza kuwa hawezi kabisa kuacha kugombea uongozi wa Pango. Ngwese (mpinzani wake wa kisiasa) anamtisha ili aache kumpinga. Licha ya pingamizi kutoka kwa babake na Ngwese pamoja na shinikizo kutoka kwa mamake, Katango anasimama imara na kuendelea kuwania uongozi. Tendo la Katango kusimama imara kuwania uongozi wa Pango linamdhihirisha kama kiongozi asiyeteterika. Anamwambia mamake:

Ndio mama (Ngwese) anataka niache nia ya kumpinga lakini siwezi... (uk. 34).

Mtu I, anamgusa Katango kimapenzi na kumwambia:

Huoni raha, hivyo au tuseme hutaki kupendwa na...kuguswaguswa... (uk.32).

Kwa mujibu wanaudenguzi, matini huwa na maana mbalimbali. Kwa kudengua jozi za maneno ndani mwa matini, maana hizi mbalimbali hubainika (Berthes, 2011; Mwamzandi, 2013). Kwa msingi wa maoni haya, taswira mbili za Katango zaweza kubainika ndani mwa usemi wa Mtu 1. Taswira ya kwanza ni ya mwanamke kutazamwa kama chombo cha mapenzi licha ya uongozi wake. Taswira ya pili inatokana na tendo la Katango kukataa kupumbazika kwa maneno ya Mtu I. Tendo hili linamsawiri Katango kama kiongozi mwenye msimamo thabiti.

Kikubi ambaye ni mwanamume waliyesoma pamoja na Katango anasema kuwa wakiwa shuleni, Katango:

...aliwahenyeshwa wanaumme ile mbaya kutokana na misimamo yake (uk.25).

Njia moja ya kubaini sifa ya mhusika katika fasihi ni kuchunguza maneno anayosema mhusika fulani kumhusu mhusika mwingine (Wamitila, 2008). Kwa mujibu wa Miller (1976) wanaudenguzi hushikilia kuwa maneno ndani mwa matini husheheni maana. Maneno ya Kikubi yanamsawiri Katango kama mtu mwenye misimamo thabiti.

Kulingana na tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011), Mpya ni msichana wa Mfalme aitwaye Bw. Binafsi. Mpya anaamua kujitokeza kupinga uongozi wa babake na kutetea haki za wananchi hasa haki ya kusema. Yeye ni msichana wa nyumba kuu kwa kuwa babake ni Mfalme anayaeongoza nchi. Utamaduni katika jamii hiyo haukumruhusu kuongea na kuteta dhidi ya uongozi mbaya wa babake. Sauti inamkumbusha jambo hili:

A-a, Bi Mpya, hapa kwenu watu hawasemi waziwazi wala hawasemi kwa kelele.

Hawaruhusiwi kufanya hivyo! (uk.27).

Nadharia ya udenguzi hulenga kuibua maana ambayo huwa imefichama ndani mwa matini ambayo huenda isiibuliwe pasipokuwepo na uchunguzi wa kina wa matini husika (Mung'atha, 2012; Mwamzandi, 2013). Kwa kurejelea maneno ya Sauti katika usemi huu, kusema waziwazi na kwa kelele kunaibua maana ya kutetea haki na kupinga uongozi mbaya. Katika muktadha wa utamaduni wa jamii ya Mpya, mwana wa mfalme hakutarajiwa kupinga uongozi wa babake. Kinaya ni kuwa Mpya anaamua kutumia ulimi wake kuongoza maandamano ya wananchi dhidi ya uongozi mbaya wa Bw. Binafsi. Anakemewa na sauti, kukanywa na kubururwa kama gunia na babake ila haya hayabadili msimamo wake. Mugambi (1982) alipohakiki tamthilia nchini Kenya mwaka wa 1957-1981 anasema kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe ambaye hana nafasi ya kushiriki katika siasa kama kiongozi. Ingawa Mpya anajaribu kunyimwa nafasi ya kuongoza, yeye anajitokeza na kuipigania nafasi hii.

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008), Bikisiwa ni mtoto wa pekee wa babake aitwaye Mfalme ambaye ni kiongozi wa nchi. Mtindo wa uongozi katika nchi hii ulikuwa ni wa kurithisha uongozi. Babake na mamake Bikisiwa ni wakongwe wa miaka. Inatarajiwa kuwa Bikisiwa ndiye atakuwa kiongozi wa nchi. Hata kabla ya mabadiliko haya kutokea, Bikisiwa anajitokeza kuongoza jamii yake kwa kutetea haki ya jamii yake. Anataka posa itakayozingatia maslahi ya jamii yake. Anawakataa wachumba wote wanaokuja kumposa: Hassan, Chachi, Biss

na Sogoramaneno kwa misingi kuwa hawajali maslahi yake na ya jamii yake. Babake (Mfalme) anathibitisha hili anaposema:

Waposaji wote waliokuja kukuposa uliwapuuzza (uk.18).

Anashikilia msimamo kuwa mwanamume atakayetaka kumwoa sharti azingatie maslahi ya pande zote. Anasema:

Nangojea posa za hapa petu, bila shaka zikiwa posa za maslahi ya pande zote (uk.67).

Msimamo wake thabiti unabainika anaposema:

Nasema tu kwa ufupi kuwa posa yetu mimi na Sogoramaneno haiwezi kuendelea (uk.21).

Aliponialika Sogoramaneno kitandani nilikataa. Tokea siku zile mpaka leo na nadhani daima na milele (uk.60).

Mugambi (1982) katika uhakiki wake wa tamthilia alidai kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe dhaifu ambaye anatarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa mwanamume bila ukinzani. Taswira inayobainika katika tamthilia hii ni tofauti na ya Mugambi. Bikisiwa anamkataa mume ambaye babake alimpendekezea.

Mwamzandi (2013) alipoitumia nadharia ya udenguzi katika utafiti wake anazungumzia dhana ya kivuli cha maana. Kulingana naye, kivuli cha maana ni ile sehemu ya neno au dhana ambayo huenda isibainishwe waziwazi bila uchunguzi wa kina wa matini. Kwa kuchunguza kwa kina dhana ya posa katika tamthilia ya *Posa za Bikiswa* (2008), inabainika kuwa posa ilirejelea uhusiano wa kimataifa kati ya nchi ya Bikisiwa na nchi zingine. Bikisiwa anazungumzia uhusiano huu ambao umemithilishwa na posa anaposema:

Ushirikiano umekuwepo tokea enzi zamani. Biashara imedumu karne nyingi sana miongozi mwa watu duniani kote. Lakini katika karne zote hizo biashara imekuwa ikiweka misingi ya dhuluma (uk.73).

Kwa mujibu wa Chacha (2013), mwanamke anatendewa matendo ya kushangaza katika jamii. Kiongozi Bikisiwa anatendewa matendo na wanaume waposaji ya kumshawishi akubali posa zao. Wanaume waposaji wajapo kuomba posa ya Bikisiwa, wanakuja na zawadi tele na maneno matamu kwa lengo la kumshawishi akubali. Licha ya vichocheo vya zawadi na maneno matamu, Bikisiwa anakataa kuyumbishwa kuhusu suala la posa. Bikisiwa anathibitisha hili anaposema:

Niliwakana kwa kuwa sikuona hata mmoja aliyenifaa... Walikuja kwa ujanja huku wakinimwagia sifa za uwongo na kunipangia rundo za zawadi (uk.18).

Hassan anampa Bikisiwa zawadi nyingi kama vile magauni ya herini, herini za dhahabu, kidani cha dhahabu na manukato. Isitoshe, anamwinamia kwa heshima na taadhima (uk.33). Hata hivyo, Bikisiwa anakataa kukubali posa yake. SS anampa zawadi tele: pete ya dhahabu, sakini za vita, magauni ya hariri, vyombo vya mapambo, farasi na hata watumishi ila vitu vyote hivi havimshawishi Bikisiwa kutetereka katika uamuzi wake wa kumchagua mchumba wa kumwoa (uk.39).

Wanaume waposaji katika *Posa za Bikisiwa* (2008) wana mtazamo kuwa mwanamke Bikisiwa atashawishika kupitia kwa maneno na matendo na hatimaye kukubali posa zao. Hii ndiyo sababu wanamjia Bikisiwa na kumsifu, kumwinamia na kumpa zawadi nyingi zenye thamani. Hata baada ya Bikisiwa kumsisitizia Hassan kuwa yeye hawezi kuolewa naye kwa kuwa hampendi, Hassan anamwambia kuwa atashauriana na babake. Hassan ana mtazamo kuwa Bikisiwa atakuja kushawishika na kukubali kuolewa naye. Anamwambia Bikisiwa:

Pamoja na hayo, asiyepeleka mwanzo huenda akapenda mwisho. Nitabaki hapa penu. Najua siku moja utabadili mawazo (uk.33).

Kulingana na Hassan, mwanamke hata akikataa jambo mara ya kwanza huenda akabadili mawazo na kukubali iwapo ataendelea kushawishwa. Licha ya mitazamo hii, kiongozi wa jinsia ya kike katika tamthilia teule za Kiswahili amejitokeza kama mtu aliye na msimamo madhubuti na asiyetereka katika maamuzi yake.

Keter (2013) alipohakiki tamthilia za *Kifo Kisimani* (1981) na *Natala* (1997) alidai kuwa mwanamke amechorwa kama kiumbe anayedanganywa na kushawishika kwa urahisi. Taswira ya Kiongozi Bikisiwa ni tofauti na taswira iliyoibuliwa na Keter. Bikisiwa anajitokeza kama kiongozi aliye na msimamo thabiti. Hapumbazwi na vishawishi vingi anavyopewa.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016), Tunu ni mhusika mwanamke ambaye anajitokeza kuupinga uongozi mbaya wa Majoka na kuwazindua wananchi kuzijua na kuzitetea haki zao. Anatumia maandamano, diplomasia, vyombo vya habari na mikutano ya kisiasa ili kuleta mabadiliko ya kiuongozi katika jimbo la Sagamoyo. Mtazamo wa kiongozi Tunu ni kuwa sharti soko ambalo ndilo tegemeo kuu la kiuchumi la Wanasagamoyo lifunguliwe (uk.58). Anasisitiza

kuwa hawezi kulegeza msimamo wake hadi soko la Chapakazi lifunguliwe. Majoka alikuwa amelinyakua ili ajenge hoteli ya kifahari (uk.45).

Majoka anamshawishi Tunu aolewe kwa mwanawe aitwaye Ngao Junior. Lengo la pendekezo hili ni kumfanya aaache kumpinga kisiasa. Tunu anakataa pendekezo la Majoka la kuolewa kwa mwanawe, Ngao Junior licha ya ushawishi wa Majoka anayemwambia:

Usitazame kwa moyo Tunu. Tazama kwa macho uione kesho. Ione fanaka kwa Ngao (uk.42).

Baada ya Tunu kuvamiwa na kuvunjwa mguu, Tunu anataka kwenda kukutana na watekelezaji wa kitendo hicho cha unyama. Ni wakati huu ambapo mamake aitwaye Hashima anamwambia:

Tunu, huwezi kujipeleka kwenye pango la joka katika hali hii yako (uk.55).

Hata baada ya ushauri huu, Tunu haachi kwenda. Makanyo ya mamake hayabadilishi msimamo wake wa kwenda.

Matendo ya Tunu ya: kusesitiza kuwa lazima soko lifunguliwe, kukataa pendekezo la ndoa kutoka kwa Majoka na kusesitiza kuwa sharti aende kukutana na watu waliomvamia yanambainisha Tunu kama kiongozi mwenye msimamo madhubuti.

Muktadha kulingana na nadharia ya udenguzi huwa muhimu katika kufasiri maana ndani mwa matini. Kwa mujibu wa Bakhtini (1981) hakuna uumbaji wa maana katika lugha ambao hauathiriwi na suala la muktadha. Katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika, mwanamke alisawiriwa kama mtu asiye na msimamo imara (Hora, 2014). Kiango (1992) alipochunguza taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili (kabla mwaka wa 2000) alidai kuwa mwanamke amesawiriwa kama mtu asiye na mwelekeo thabiti. Keter (2012) alipotafitia nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Kifo Kisimani (1981)* na *Natala (1997)* anasema kwamba mwanamke kwa mujibu wa tamthilia hizi amechorwa kama mtu anayedanganywa kwa haraka. Hii ina maana kuwa mwanamke katika tafiti hizi alisawiriwa kama mtu asiye na msimamo imara. Kulingana na Miller (1976) uhakiki wa matini kupitia nadharia ya udenguzi huibua maana mpya. Kinyume na tafiti za awali zilizomsawiri mwanamke kama mtu aliye na msimamo wa kuyumbayumba, mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 amechorwa kama kiongozi mwenye msimamo thabiti.

4.2.2 Mwanamke kama Kiongozi Mzindushi na Mtetezi wa Haki

Kwa kurejelea tamthilia ya *Pango* (2003), kiongozi Katango anatetea haki yake ya kuongoza kupitia kwa matendo. Katango anajitokeza kuwazindua wanawake na Wanapango wote kuhusu haki zao na kuzitetea haki hizi kwa udi na uvumba. Anatetea haki za wanawake wenzake. Baadhi ya wanajamii na hata baadhi ya wanawake katika tamthilia ya *Pango* walikuwa na mtazamo kuwa ilikuwa vigumu kwa mwanamke kuongoza. Katango anatetea usawa wa kijinsia katika jamii ya Pango iliyojaa kasumba ya utamaduni ulioshikilia kuwa katu mwanamke hawezi kuongoza na kwamba sehemu ya mwanamke ni nyumbani na hasa jikoni. Mbabekazi anapotilia shaka uwezo wa Katango kuliongoza Pango, Katango anatetea haki yake na ya mwanamke kuongoza:

Mwanamke ana nini, si ni mwanapango pia? Si anaweza kuongoza? (uk.27).

Kwa mujibu wa Mishra (2018) nadharia ya udenguzi hulenga kuibua maana mbalimbali kwa kubainisha kinaya, utata, unyume, ukinzani au mwachano uliomo ndani mwa matini. Usemi huu wa Katango unabainisha kinaya kuwa ingawa kulikuwepo na wanawake wenye uwezo wa kuongoza, hawakuruhusiwa na utamaduni kufanya hivyo. Maana nyingine tuipatayo katika usemi huu ni kuwa, Katango yu tayari kuenda kinyume na utamaduni uliombagua mwanamke na kuongoza. Usemi huu unabainisha mtazamo wa kiongozi Katango kuwa wanawake wana haki ya kuongoza kwani ni Wanapango sawia na wanaume kama Ngwese. Katango anasisitiza kuwa ana haki ya kuliongoza *Pango* kama Mwanapango yeyote yule. Ni mtazamo huu ndio unaomfanya akiuke tamaduni zinazomdunisha mwanamke katika jamii yake na kuwania uongozi wa *Pango*. Maana ndani mwa matini kulingana na udenguzi huathiriwa na mitazamo iliyopo (Ntaragwi, 2004). Mtazamo huu wa Katango unamsawiri kama kiongozi anayejua haki yake na kuitetea kwa udi na uvumba.

Aidha, Katango anatetea haki ya watoto ya kuchota maji. Ngwese anawazuia watoto (Sota na Susa) kuchota maji kwa madai kuwa kisima ki katika ardhi yake na kwamba mali yake si kama ng'ombe wa kijiji anayekamuliwa na kila mtu. Sota arejeapo nyumbani anamwambia mamake:

Pamezungushwa seng'enge na mwenyewe...Ngwese alitufukuza kama ndege...anasema yale ni maji yake! (uk.16).

Baba yao haonekani kuwatetea ila anasisitiza kuwa madai ya watoto kwamba walifukuzwa na Ngwese ni uongo mtupu. Katango anajitokeza kutetea watoto wapate haki hii ya kimsingi kwani tujuavyo maji ni uhai. Anaeleza kugadhabika kwake na jambo hili. Kwa hasira anamkosoa Ngwese:

Watoto gani? Hata hamnazo huahi? Hivi unadhani watu hatuna macho?... Hukuwafukuza ndugu zangu waliokuja kutafuta maji wewe, hukuwawinga kama ndege wewe? (uk.10).

Isitoshe, kiongozi Katango anatetea haki ya usawa katika jamii yake iliyozungwa na tatizo la ubaguzi na ubinafsi. Anajitokeza kupinga ubaguzi na ubinafsi huu na kutetea usawa pangoni Anawaambia Kibwana, Kikubi na Mbabekazi:

Ehhh mara hii asali ya Pangoni lazima iwafaidi wote... (uk.28).

Katango anagadhabishwa na hali ambapo Ngwese anavuna asali ya *Pango* pekee na kufaidi watu wa karibu naye tu (uk.40). Asali katika muktadha huu imetumiwa kijazanda kuashiria rasilimali za *Pango* ambazo zinachukuliwa na Ngwese ili kumfaidi yeye na watu walio karibu naye. Katango anaamua kugombea uongozi ili kuleta ugavi sawa wa rasilimali (uk.28). Mwenderani (2012) alipohakiki tamthilia za *Kilio cha Haki (1981)* na *Pango (2003)* anasema kwamba mwanamke amejitokeza kama mtetezi wa haki. Katika uhakiki wake Mwenderani aliangazia ukombozi wa wanawake: Lanina na Katango. Kwa kuangazia mhusika Katango, utafiti huu umeegemea namna uongozi wake unavyobainika anapotetea haki za Wanapango.

Kupitia tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya (2011)*, mwanamke amejitokeza kama kiongozi anayetetea haki. Mpya anatetea haki yake ya kusema (uk.51-52). Mpya hajitetei tu. Anatetea haki ya wananchi kusema. Anaitetea jamii yake ipate: katiba mpya, uongozi bora utakaojali maslahi ya umma, huduma za kijamii, kuondoa ufisadi na kulinda rasilimali za nchi (uk.72-74). Mwisho wa uongozi wa Bw. Binafsi ni ishara kwamba Mpya akishirikiana na wazalendo wengine amefaulu kuitetea jamii yake (uk.87-88).

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa (2008)*, Mtambaji katika hadithi yake anasema kuwa Bikisiwa alikuwa binti:

...mwenye msisimko mkubwa juu ya haki zake, haki za wanawake wa nchi yake na haki za raia wa nchi yake ... (uk.13).

Kiongozi Bikisiwa anatetea haki yake, ya wanawake wenzake na ya jamii yake. Kiongozi yeyote hawezi kutetea haki za wafuasi wake ikiwa hazielewi si tu haki za wafuasi wake bali haki zake mwenyewe. Bikisiwa anazifahamu na kuzielewa haki zake. Mathalani, anatambua kuwa na haki ya kuchagua mchumba amtakaye. Anatetea hali hii asemapo:

Ni haki yangu mimi kijana

Ndoa ni haki yangu mwanamke

Ndoa ni haki yako mwanamume

Ni haki yangu kama ilivyo haki yako

Ndoa ni haki ya mwanamke

Kama ilivyo haki ya mwanamume (uk.6)

Utamaduni wa Kiafrika ulimfanya mwanamke kukubali hadhi yake ya chini katika jamii; jambo lililochangia udhalilishaji wa mwanamke (Katola 2006; Muniu, 2013). Uelewa wa muktadha wa matini kwa mujibu wa nadharia yetu ya utafiti huu ni muhimu katika uibuaji wa maana ndani mwa matini hayo (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa nchi ya Bikisiwa, vijana walikuwa wakichaguliwa wachumba na wazazi wao. Kinyume na mwanamke katika muktadha wa utamaduni huu, Bikisiwa anazinduka. Alichaguliwa mchumba (Sogoramaneno) na babake. Hata hivyo, Bikisiwa alimkataa kwa sababu alimwona kama mtu asiyejali nchi yake. Kiongozi Bikisiwa anatetea uhuru wa kumchagua mchumba amtakaye. Anasema:

Naikana posa ya udhalimu. Nadai uhuru wangu. Au nadai usawa (uk.23).

Anamwambia Bwana Chachi kuwa yeye hataki kelele tupu. Anataka ajue namna watu wake watafaidika. Anatetea haki ya jamii kwa kusisitiza kuwa anataka posa ya kufaidi jamii:

Nini itakuwa hatima ya ndoa yetu pindi tukioana? Watu wangu watafaidi nini? (uk.49).

Kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi, matini huwa na maana mbalimbali ambazo huweza kuibuliwa na mhakiki kupita usomaji na uchambuzi wa kina (Berthes 2011). Wanaudenguzi hulenga kuchunguza matini kwa makini ili kuibua maana iliyojificha ndani mwa matini hayo (Mung'atha, 2012; Mwamzandi, 2013). Kwa kuchunguza tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* inabainika kuwa dhana ya ndoa inayozungumziwa katika usemi huu inarejelea uhusiano wa kimataifa kati ya nchi ya Bikisiwa ambayo ni ya Kiafrika na nchi za kigeni (uk.72-73). Kwa Bikisiwa kusema kuwa ndoa ni haki yake (uk.6) anamaanisha kuwa nchi yake ina haki ya

kuingia katika uhusiano wa kibiashara, kisiasa au kijamii na nchi ambayo italeta manufaa kwa nchi yake.

Kupitia tamthilia ya *Kigogo* (2016), kiongozi Tunu anajitokeza kutetea haki ya watu wa jimbo la Sagamoyo. Anasema kwamba tangu wakiwa viongozi wa chama cha wanafunzi chuoni, walikula kiapo na Sudi kutetea haki za Wanasagamoyo hata kama ni kwa pumzi zao mwisho (uk.18). Tunu anatumia vyombo vya habari kulalamikia hali ambapo soko la Chapakazi limefungwa badala ya kusafishwa na serikali ya Majoka (uk.32). Kenga anamripotia Majoka:

Mara pesa za kusafisha soko zimefujwa, mara tukaamua kufunga soko badala ya kulisafisha...sijui haki za wauzaji, sijui haki za kina nani zimefanyiwa nini...mara hawataulegea msimamo wao hadi soko lifunguliwe...(uk.32).

Anatetea kufunguliwa kwa soko hili ambalo lilifungwa na Majoka kwa lengo la kujenga hoteli ya kifahari katika ardhi hiyo. Anamwambia Majoka kuwa ugatuzi si unyakuzi na kwamba Wanasagamoyo wana haki ya kuishi. Anaapa kutolegeza msimamo wake hadi soko lifunguliwe (uk.45). Isitoshe, anatetea haki za wachuuzi (uk.44).

Muktadha kama kipengele mojawapo cha nadharia ya udenguzi huwa muhimu katika kufasiri maana ya matini (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika, mwanamke alidunishwa kutokana na mifumo ya kijamii iliyojaa taasubi ya kiume (Hora, 2014). Katola katika utafiti wake wa tamthilia za: *Hatia* (1972), *Mama Ee* (1987), *Buriani* (1983) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) anasema kuwa mhusika wa kike katika tamthilia hizi amedhulumiwa sana na kupewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Ni kutokana na dhuluma na udunishaji wake ambapo mwanamke kiongozi katika tamthilia za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 anajitokeza kutetea haki yake katika jamii.

Suala la uongozi wa mwanamke halikuangaziwa katika tamthilia za awali (za kabla ya mwaka wa 2000) kwa kuwa utamaduni na mila hazikumruhusu mwanamke kuyaingilia masuala ya uongozi (Onyoni, 2012). Mugambi (1982) alipohakiki tamthilia za Kiswahili zilizochapishwa nchini Kenya kati ya mwaka 1957 hadi 1981 alidai kuwa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia hizi hana nafasi ya kushiriki siasa kama kiongozi bali jukumu lake kuu ni kuwahimili wanaume. Keter (2003) alipoihakiki tamthilia ya *Natala* (2003) anadai kuwa mwanamke ni mtegemezi wa mwanaume. Kulingana na Miller (1976) uhakiki wa matini kwa kutumia nadharia ya udenguzi

huibua maana mpya ndani mwa matini. Kulingana naye, maana hii yaweza kufanana au kutofautiana na maana ya awali. Mwanamke katika tamthilia za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 amesawiriwa kama kiongozi mzindushi na mtetezi wa haki kinyume na tafiti za awali zilizomdunisha mwanamke. Kiongozi huyu anajitokeza kupigania haki zake, za wanawake wenzake na za jamii nzima kwa ujumla. Anawazindua wanawake na jamii nzima kwa ujumla kupigania haki zao.

4.2.3 Mwanamke kama Kiongozi Jasiri

Kwa mujibu wa TUKI (2014) ujasiri ni hali ya kukabili jambo bila ya hofu. Mdee, Njogu & Shafi (2011) wanaeleza ujasiri kama utendaji wa jambo bila kuogopa. Kiongozi sharti awe jasiri (Afkami, 2003). Uelewa wa muktadha kulingana na wanaudenguzi husaidia kubainisha maana ya matini (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa Pango, mwanamke hakufaa kuwa kiongozi. Mtu wa I anamkumbusha Katango hili:

Kigoda cha pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? Hilo halijawahi kutokea katika historia ya huku kwetu na halianzi nawe, unasikia? (uk.32).

Kigoda ni kiti kifupi sana kinachochongwa kwa mti, chenye miguu mitatu iliyoshikamana na kitako (Mdee, Njagi & Shafi, 2011). Mtu wa I anatumia maneno: kigoda cha Pango kuashiria uongozi wa Pango. Kulingana naye, mwanamke katika muktadha wa utamaduni wa jamii hii hakuwahi na hangeweza kuwa kiongozi kwa kuwa mila na tamaduni za Pango hazikumruhusu.

Kando na mwanamke kujitokeza kuongoza, mwanamke anatenda matendo yanayomsawiri kama kiongozi. Chacha (2013) anadai kwamba mwanamke anajitendea matendo ya kushangaza katika jamii. Ni matendo haya ndiyo yanayochangia kumsawiri mwanamke kwa uchanya au uhasi (Murumba 2011. Kwa kurejelea *Kigogo* (2016), Tunu anatetea haki za wananchi kwa ujasiri. Majoka anapomweleza kuwa juhudi zake za kuongoza maandamano ya wafanyikazi na wachuuzi hazitampeleka popote, Tunu anamjibu kiujasiri:

Lakini zitawapeleka Wanasagamoyo ndani ya soko lao na kuwafuta tongo (uk.44).

Alipopokea habari za maandamano ya wafanyikazi katika Majoka and Majoka Company ambayo yalisababisha mauaji ya vijana watano na kujeruhiwa kwa wachuuzi, Tunu aliwashauri Sudi, Boza na Kombe waende kuko huko (uk.17). Tendo hili ni la kijasiri kwa vile Tunu

hayahofii maisha yake. Isitoshe, Tunu kwa ushirikiano wa Ashua anawaongoza Sudi, Boza na Kombe (wanaumme) kwenda kumkabili mshauri mkuu wa Majoka aliyekuwa akiwahutubia wahuni wa kulipwa chini ya mti (uk.18).

Kupitia tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) tunaona Bikisiwa akimkosoa kinagaubaga babake ambaye ni mfalme. Anamkosoa kwa kutoshauriana na raia (hata mamake Bikisiwa) kuhusu posa yake. Tendo hili ni la kijasiri.

Njia moja ya kubaini sifa za mhusika katika kazi ya fasihi ni kupitia kwa matendo anayotendewa na wahusika wengine katika kazi hiyo (Wamitila, 2008, Murumba, 2011). Kunayo matendo ambayo wahusika wengine wanamtendea mhusika mwanamke katika tamthilia za Kiswahili tangia mwaka wa 2000. Baadhi ya matendo haya yanamsawiri mwanamke kama kiongozi jasiri. Kwa kurejelea tamthilia ya *Pango* (2003), Katango wakiwa na Kibwana wanavamiwa njiani na watu waliotumwa na Ngwese. Hata baada ya Kibwana kupigwa na kuangushwa na Mtu I, Katango hatishiki na tendo hili. Tunamtarajia Katango kuingiwa na woga na hata kutoroka. Hata hivyo anamgeukia Mtu I aliyemchapa Kibwana na kushutumu ukatili wake pamoja na kumwuliza sababu ya kutenda hivyo. Hakomei hapo Katango. Anamwendea Mtu I na kutaka kumvua vazi alilokuwa amejifunika kuuficha uso wake usionekane (uk.31).

Matendo anayotendewa mwanamke Katango yanadhihirisha ujasiri wake. Katango anafinywa, anabanwa na kutaka kupigwa kofi na Mtu I (uk.32-33). Lengo la matendo haya ni kumwogofya Katango aache kumpinga Ngwese katika uwaniaji wa uongozi wa pango. Kinaya ni kwamba Katango haogopi. Anampiga Mtu I kumbo linalomrudisha kinyume. Mtu II anapokuja juu na kujaribu kumgusa Katango, Katango anautupa mkono wa Mtu II hadi unampiga (uk.33).

Tunu katika *Kigogo* (2016) anatendewa tendo la unyama na majangili waliotumwa na kufadhiliwa na serikali ya Majoka. Hata baada ya kuumizwa, Tunu anaamua kwenda kukutana na majangili waliomvamia licha ya makatazo kutoka kwa mamake (uk.55-56).

Tunu akiwa katika ofisi ya Majoka anazungumza kwa ujasiri. Haogopi kamwe. Ni katika ofisi hii ambapo Majoka anampendekezea Tunu mpango wa Tunu kuolewa na mwanawe Ngao Junior. Tunu anapinga pendekezo hili kiujasiri (uk.44).

Nadharia ya udenguzi hushikilia kuwa muktadha huathiri uumbaji wa maana katika lugha (Bakhtini, 1981). Katika muktadha wa utamaduni wa Pango, mwanamke hakufaa wala

kuruhusiwa kujibizana na mwanamume. Katango anakiuka utamaduni wa Pango uliomwogofya mwanamke. Kwa uhodari anajibizana na Ngwese. Kwa ujasiri, Katango anamweleza kuwa babu yake alikuwa kibarakala wa wakoloni na hakuonewa wivu na wazee wa Katango alivyodai Ngwese (uk.13).

Ngwese anapotishia kumpiga Katango makofi, Katango anasimama kiujasiri na kumwambia Ngwese:

Huu ni wakati mwingine (uk.14).

Maana ndani mwa matini kulingana na wanaudenguzi hutokana na uchunguzi wa maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini. Uchunguzi wa semi huu wa Katango unadhihirisha mtazamo aliokuwa nao kiongozi Katango kuwa tendo la wanaume kuwapiga wanawake ni tendo lililopitwa na wakati. Kwa mujibu wa udenguzi, uelewa wa mitazamo iliyopo husaidia uelewa wa maana katika lugha (Levinas, 2003). Mtazamo wa Katango unaopinga tendo la kumpiga mwanamke unamsawiri kiongozi Katango kama mtu jasiri. Aidha, mwanaume Kikubi anasifia ujasiri wa Katango:

Lakini kusema kweli, ana ujasiri mkubwa sana yule Katango! (uk.25).

Mpya katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) anazungumza kwa ujasiri. Anasema:

Hili ndilo tambiko letu. Tambiko la uhai wa nchi zetu. Tambiko la kusema ukweli bila ya kuhofu wala kuogopa (uk.23).

Ni ujasiri unaomfanya Mpya awe tofauti na wanawake wengine kama mamake aitwaye Bi Shoo na hata vijana wenzake kama Mussa na Zanga ambao ni ndugu zake. Mamake Mpya hawezi kusimama kwa ujasiri na kumkosoa mumewe kwa uongozi mbaya kwa kuwa anahofia kuwa ndoa yake itavunjika. Mussa na Zanga vilevile wanaogopa kusema kwa uwazi japo wana hamu ya kusema. Mpya ananena na babake ambaye ni mfalme na hata kuwahutubia wananchi kwa ujasiri.

Kwa mujibu wa muktadha wa utamaduni wa Kiafrika mwanamke alifaa kusalia chini ya mume, kumtii na kumheshimu (Hora, 2014; Mapunjo, 2014). Hakufaa kujibizana naye au hata kukataa anachosema. Jibu lake kwa mwanamume sharti lilikuwa ndio. Alihitajika kuwepo tu aonekane yupo ila asichangie katika mijadala na wanaumme. Sehemu yake ilikuwa kukaa nyumbani na kutekeleza majukumu ya kinyumbani kama kupika, kufua, kuzaa na kutunza watoto (Mapunjo,

2014). Hali hii ilimfanya mwanamke huyu kuwa mwoga. Usawiri wa mwanamke katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) ni tofauti na usawiri wa mwanamke katika muktadha wa kitamaduni. Bikisiwa anawakabili wanaumme waposaji: Hassan, Chachi, Sogoramaneno, SS na Biss kwa ujasiri mkubwa. Mathalani anamwambia Hassan:

Tuseme ni lipi lililokuleta hapa?... Hebu sema hasa unataka nini hapa?... Sema haraka nisikie lilokuleta (uk.31).

Katola (2006) katika uhakiki wake wa tamthilia nne: *Hatia* (1972), *Mama eeh* (1987), *Buriani* (1983) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) anahitimisha kwamba mhusika amedhulumiwa sana na kupewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Katika tamthilia ya *Pango* (2003) mwanamke Katango anakataa kupewa nafasi ya pili baada ya mwanamume kwa kujitokeza kijasiri na kuwania uongozi. Kupitia *Pango* (2003), Katango anajitokeza kiujasiri kuwania uongozi wa Pango katika jamii iliyokuwa imetawaliwa na utamaduni uliomkandamiza mwanamke. Keter (2013) anadai kuwa mwanamke ni mwanajamii anayeweza kujibidiisha vilivyo katika ujenzi wa jamii mpya. Ujasiri wa Katango unabainika anavyojibidiisha kuwa kiongozi kwa kugombea na hata kupiga kampeni (uk.41-46).

Mwanamke Mpya katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) anaamua kupinga uongozi mbaya wa babake na kuwazindua wananchi ili kukomesha uongozi huo mbaya. Katika nchi ya Mpya mwanamke hakuwahi kuwa kiongozi. Anasema:

Nimechoka kusubiri. Nimechoka kungojea. Nimechoka kunyamaza (uk.31).

Kulingana na Mung'atha (2012) maneno yatumiwayo ndani mwa matini hubeba maana. Kwa Mpya kusema kuwa amechoka kunyamaza anamaanisha kuwa amechoka kuona babake akiongoza nchi vibaya na ameamua kujitokeza kupinga uongozi mbaya wa babake. Tendo la yeye kujitolea kuleta mabadiliko nchini mwake ni tendo la kijasiri kwa kuwa utamaduni wa nchi ya Mpya haukumruhusu mwana wa kiongozi kupinga uongozi wa babake (uk.27).

Kwa kurejelea *Posa za Bikisiwa* (2008) mwanamke katika nchi ya Bikisiwa aliyekataa kuozwa aliozwa kwa lazima. Sogoramaneno anamwambia Bikisiwa:

Iwapo mwanamke atasitasita, basi nina haki ya kumpiga mwereka hadi nyumbani kwangu...(uk.58).

Ujasiri wa Bikisiwa unabainika anapokata uchumba kati yake na Sogoramaneno licha ya kuwa Sogoramaneno alikuwa pendekezo la babake kwake. Kwa mujibu wa Mwamzandi (2013) kwa kutumia nadharia ya udenguzi, mhakiki aweza kuibua maana nyingine ambayo huenda imejificha ndani mwa matini. Ingawa usemi huu unarejelea Bikisiwa kuingizwa katika ndoa kwa lazima, uchunguzi wa kina wa tamthilia hii unabaini kuwa dhana ya ndoa imetumika kurejelea uhusiano wa kibiashara, kisiasa na kijamii (uk.73). Tendo la Bikisiwa kukata uhusiano na Sogoramaneno licha ya kupendekezewa na babake linaashiria namna kiongozi Bikisiwa anakataa nchi yake kuhusiana na nchi dhalimu. Kwa ujasiri, Bikisiwa anamkosoa babake kwa kutoshairiana na raia kuhusu posa yake (uk.22-23).

Kupitia tamthilia ya *Kigogo* (2016) mwanamke Tunu anajitokeza kupigania uongozi bora wa jimbo la Sagamoyo. Anaongoza maandamano na kuwahutubia wananchi na wanahabari (uk.32). Tendo la Tunu kujitokeza kuongoza maandamano ili kuleta mabadiliko ni tendo la kijasiri kwani wanawake hawakuwahi kuongoza jimbo la Sagamoyo. Awali jimbo hili lilikuwa limeongozwa na wanaume kama Ngao na Marara (uk.4). Ndiposa Kenga anasema kwamba Sagamoyo haijawahi kuwa na wanawake viongozi (uk.10). Jamii ya Sagamoyo wakati huo haikumruhusu mwanamke kufanyika kiongozi si kwa sababu hakuwa na uwezo wa kuongoza ila utamaduni ulisisitiza kuwa mwanamke alikuwa kiumbe duni asiyefaa kuongoza.

Mapunjo (2014) alipohakiki tamthilia ya *Kivuli Kinaisha* (1990) anadai kuwa mwanamke alisawiriwa kama kiumbe asiyeweza kuwa kiongozi. Utafiti huu umebaini kuwa mwanamke katika tamthilia teule za tangia mwaka wa 2000 hadi 2017 amesawiriwa kama kiongozi. Mapunjo aliporejelea tamthilia ya *Nguzo Mama* (Muhando, 1982) anaibua madai kuwa ingawa mwandishi wa tamthilia hii ameonyesha kwamba wanawake wana uwezo wa kuwa viongozi, ameonyesha pia kuwa wanawake wanategemea kupewa nafasi za uongozi na wameridhika na hali hiyo. Mwanamke katika tamthilia teule hategemei kupewa uongozi. Anainuka kijasiri na kutetea haki yake ya kuongoza. Katango katika *Pango* (2003) hategemei kupewa uongozi wa Pango. Anawania uongozi huu (uk.41-46). Mpya katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) anajitokeza kupigania uongozi bora kwa kupinga uongozi mbaya wa babake (uk.72-74), Bikisiwa katika *Posa za Bikisiwa* (2008) anapigania uhusiano usioitelea nchi yake faida (uk.64). Tunu katika *Kigogo* (2016) anapigania uongozi bora kupitia maandamano na hotuba (uk.32).

Kulingana na Mugambi (1982), wanawake ni viumbe ambao hawana upeo mkubwa wa kisiasa na ambao wanatarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa wanaumme wao bila ukinzani. Keter (2013) alipohakiki tamthilia ya *Natala* (1997) alidai kwamba mwanamke ni mtegemezi wa mwanamume. Tukirejelea tamthilia ya *Kigogo* (2006) mwanamke Tunu hamtegemei mwanamume aitwaye Sudi katika harakati zake za kupigania uongozi bora wa Sagamoyo. Kinaya ni kuwa Sudi ndiye anayemfuata na kumtegemea Tunu. Mathalani, Tunu ajapo na kuwataka Sudi, Kombe, Ashua na Boza waende kusambaratisha njama ambayo Majoka alikuwa akipanga na wahuni chini ya mbuyu, Sudi ndiye anamfuata (uk.15). Sudi anapoelekea kutamauka na kuachana na vita dhidi ya uongozi mbaya wa Majoka, Tunu ndiye anayemhimiza Sudi asikate tamaa (uk.18). Hata baada ya kuvunjwa mguu na wahuni wa kulipwa waliotumwa na Majoka, Tunu kwa ujasiri wake anaamua kwenda kukabiliana na watu waliomvamia (uk.55). Ikumbukwe kuwa Tunu wakati huu hakujua mahali alipokuwa Sudi. Kulikuwa na tetesi kuwa Sudi alikuwa amemsaliti (uk.54-55). Badala ya kukaa na kumsubiri mwanamume Sudi, Tunu anajitokeza kijasiri kwenda kukabiliana na wahuni waliokuwa wamemvamia. Isitoshe, ni mwanamke Tunu anayemkosoa na kumwelekeza Sudi aliyeelekea kupoteza lengo la wao kwenda Mangweni kulikoandaliwa pombe (uk.64). Sudi anamfuata na kumtegemea kiongozi Tunu hadi Ngurumo anamwambia:

Wafikiri kila mtu ametiwa ndani ya kirinda na huyu Tunu kama wewe? (uk.64).

Kwa kurejelea *Kimya Kimya Kimya* (2011) Mpya hategemei kupewa uongozi na babake. Anajitokeza pekee yake kupigania uongozi bora bila kuwategemea nduguze wa kiume: Mussa na Zanga (uk.42). Mwanamke Bikisiwa katika *Posa za Bikisiwa* (2008) anajitokeza kupigania uhusiano wa kuletea nchi yake faida bila kutegemea pendekezo la babake (uk. 64). Isitoshe Katango kwa mujibu wa *Pango* (2003) anajitokeza kuwania uongozi bila kutegemea uungwaji mkono kutoka kwa wanaumme kama Ngwese na babake aitwaye Seki. Seki aliunga mkono uongozi wa Ngwese na kumpinga Katango. Kwa ujasiri, Katango anamwambia babake:

Ndio maana lazima ateuliwe kiongozi afaaye! (uk21).

Kulingana na wanaudenguzi, uhakiki wa maana kwa kutumia nadharia ya udenguzi huzua maana mpya ambayo huenda ikafanana au ikatofautiana na maana za wahakiki wa awali (Derrida, 1976; Miller, 1976). Kwa msingi wa mawazo haya ya wanaudenguzi, utafiti huu umebaini kuwa kinyume na usawiri wa mwanamke katika utafiti wa Mugambi (1982) na Keter (2013),

mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka 2000 hadi 2016 ana upeo mkubwa wa kisiasa na anajitokeza kuongoza bila kutegemea mwanaumme.

Wamalwa (2005) akimnukuu King'ei (2002) anasema kuwa tahakiki nyingi zilizofanywa kuhusu suala la mwanamke katika fasihi ya Kiswahili zimelalamikia hoja ya kukandamizwa na kutoshirikishwa kwa mwanamke katika vipengele vyote vya maisha ya jamii (uongozi ukiwemo). Japo mwanamke kiongozi katika tamthilia teule anakandamizwa na kutoshirikishwa katika shughuli za kiuongozi katika jamii yake, anajitokeza kwa ujasiri na kutetea nafasi yake ya kushiriki katika siasa na uongozi.

Katika muktadha wa kisiasa nchini Kenya, ni wanawake wachache sana hujitokeza kuwapinga wanaumme katika kugombea nyadhifa za kisiasa ikilinganishwa na wapinzani wa kiume. Mathalani katika uchaguzi mkuu nchini Kenya mwaka wa 2013, idadi ya wanawake waliojitokeza kuwania nyadhifa za ubunge, useneta na ugavana ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya wanaume (Migiro, 2013). Kwa mujibu wa tamthilia teule, tendo la wanawake: Katango, Mpya na Tunu kugombea uongozi katika jamii zao ni tendo la kijasiri ikizingatiwa muktadha wa kisiasa wa jamii hizi na hata jamii ya kisiasa nchini Kenya.

4.2.4 Mwanamke kama Kiongozi Mshawishi

Kwa mujibu wa TUKI (2014), kushawishi ni kitenzi kilicho na maana ya kumpa mtu maelezo ili kutaka kumfanya akubali kufuata fikra au maelezo yako au kumfanya mtu avutike kutenda jambo fulani. Kutokana na maelezo haya, inabainika kwamba mtu anaweza kumshawishi mwingine kupitia kwa maneno (maelezo) au vitendo. Kiongozi yeyote yule: mbaya ama mzuri lazima awe na wafuasi (American Association of University Women [AAUW], 2016). Kiongozi hawezi kujidai ni kiongozi kama hana wanaomfuata. Wafuasi hawa hupatikana kupitia ushawishi. Kiongozi bora sharti awe na uwezo wa kuwashawishi wengine na kuwafanya kusonga na kuelekea katika upande fulani (Hora, 2014). Wafuasi hushawishika kutokana na maono, maneno, mitazamo au matendo ya kiongozi husika. Katika muktadha wa kisiasa, jambo ambalo laweza kumfanya kiongozi kuibuka mshindi uchaguzini katika nchi zenye demokrasia

komavu ni uwezo wake wa kuwashawishi wapiga kura wengi iwezekanavyo. Katika nchi hizi, kiongozi katu hawezi kuibuka mshindi iwapo hataweza kuwashawishi wananchi.

Kwa kurejelea *Pango* (2003) Kiongozi Katango anawashawishi Wanapango kumpigia kura kupitia kwa hotuba yake katika mkutano wa kisiasa wa kuwania uongozi wa Pango (uk.40-45). Athari ya ushawishi huu ni wakati watu wanapomsheherekea, kumwinua na kumbeba juu kwa juu kwa muda Katango (uk.45). Aidha, watu walioshawishwa na mtazamo, tabia, maneno na matendo ya Katango wanafuatana huku wakicheza na kuimba kwa furaha na kwa sauti ya juu wakati Ngwese unapobanduliwa mamlakani (uk.88)

Katika *Posa za Bikisiwa* (2008), Bikisiwa anamshawishi mamake mzazi kuhusu suala la posa yake kupiti uneni wake:

Wewe mama u kama mimi...Siko tayari kuingia ndani naye (uk.21).

Baada ya kumsikiza, mamake anashawishika kuwa ndoa baina ya Bikisiwa na Sogoramaneno yafaa kubatilishwa. Anasema:

Hapana jambo lingine mume wangu ila kuibatilisha ndoa hii. Au tuitafutie misingi inayofaa (uk.22).

Hata babake Bikisiwa ambaye ni Mfalme anashawishika kwa maneno na mustakabali wa Bikisiwa. Hatimaye anaamua kuwaita raia kwenye uwanja mkuu ili kushauriana nao kuhusu posa ya bintiye. Ingawa ulikuwa wajibu wa wazazi kuwachagulia wanao wachumba kwa mujibu wa muktadha wa jamii ya Bikisiwa (uk.17), Mfalme anashawishika kwa maneno ya Bikisiwa na kuamua kumpa uhuru wa kuchagua mchumba atakaye. Hili ndilo jambo analouambia umati uliokusanyika katika uwanja mkuu:

Ndipo nikasema mtoto wa kisasa (Bikisiwa) amepevuka kuliko wazee wake (uk.62).

Ametalii na kuyaelewa mengi kutoka kila kipembe cha ulimwengu (uk.62-63).

Kwa kurejelea muktadha huu wa kisiasa, Bikisiwa anafaulu kuwashawishi wananchi kuwa yafaa mchumba atakayemposa awe anayejali maslahi yake na ya nchi. Tendo la wananchi (baada ya Bikisiwa kuongea nao) kusheherekea kwa kucheza na kurukaruka huku wakiendelea kuita jina la Bikisiwa mfululizo ni ishara ya athari ya ushawishi huu (uk.64).

Mpitanjia anapomwambia Mtambaji kuwa yeye (Mtambaji) ndiye aliyekuwa akiwaongoza, Mtambaji anapinga hili kwa kusema;

Hapana, sasa Bikisiwa ndiye aliye mbele yetu. Ndiye anayeongoza (uk.67).

Mugambi (1982) katika uhakiki wake wa tamthilia zilizotunga tangia mwaka wa 1957 hadi 1981 anasema kwamba mwanamke katika tamthilia ya *Zinduko* (1986) hana nafasi ya kushiriki katika siasa kama kiongozi. Mapunjo (2014) anasema kuwa mwanamke katika tamthilia ya *Kivuli Kinaisha* (1990) amechorwa kama mtu asiyeweza kuongoza. Kupitia usemi huu wa Mtambaji, mwanamke Bikisiwa amasawiriwa kama kiongozi aliyefaulu kuwashawishi wananchi.

Tabia za wahusika hubainika kupitia kwa maneno na matendo yao (Mulokozi, 1996, Murumba, 2011). Kwa mujibu wa *Kimya Kimya Kimya* (2011), Mpya anawashawishi Kulia na Kushoto waache kukinzana (waungane pamoja) kwa maslahi ya nchi nzima (uk.22).

Mwanzoni mamake Mpya (Bi. Shoo) ni mwoga. Uoga wake unaeleweka vyema kwa misingi ya muktadha wa utamaduni wa nchi ya Mpya. Kulingana na nadharia ya udenguzi, uelewa wa muktadha husaidia mchanganuzi wa matini kubaini maana ndani mwa matini hayo (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa nchi ya Mpya, mwanamke alikuwa kiumbe dhalili. Hili linabainika kutokana na taswira anayotuchorea Mpya:

Tazama mama 'angu ameketi katika ukingo wa dunia. Ana hofu za kuanguka na kuangamia. Anamhofu baba. Anaihofu ndoa. Anaogopa kuvunjika... (uk.32).

Baada ya kusikiliza maneno ya Mpya, kuona mtazamo na matendo yake, Bi. Shoo anashawishika kujasirika. Yeye pamoja na wanawe wanaondoka nyumbani. Anamwambia mumewe:

Sivezi kumtupa mtoto wangu hasa kwa sababu ni msema kweli. Heri tuondoke sisi sote (uk.43).

Athari ya ushawishi wa Mpya kwa mamake unabainika mwishoni mwa tamthilia tunapomwona Bi. Shoo akiwa na msimamo tofauti wa kisiasa na mumewe na kumshauri mumewe ajiuzulu (uk.86).

Mpya vilevile anawashawishi nduguze, Mussa na Zanga kusimama na umma kutetea haki za wananchi. Baada ya Mpya kunena nao, Zanga anasema kuwa sasa ameshajua naye Mussa anakiri kuwa sasa wameshatambua ishara kuwa wawili hawa wamepata kushawishika na maneno ya

Mpya (uk.55). Zanga na Mussa wanaanza kuongoza maandamano ya wananchi wakiwa na Mpya. Hii ni ishara kuwa Zanga na Mussa walishawishiwa na maneno ya Mpya.

Kiongozi Mpya anawashawishi wananchi kutetea haki zao kwa utulivu bila fujo. Anawaambia wananchi kuwa ingawa fujo zinapangwa na wapinzani wake, wao hawataki fujo. Wananchi wanashawishwa na mtazamo huu wa Mpya wa kutetea haki zao kwa Amani (uk.86).

Athari ya ushawishi wa Mpya kwa wananchi unabainika pale Bw. Naona, waziri wa nchi, anamwambia Bw. Binafsi:

Naona sasa kundi linalojua na kutambua limekua, limejaa na kumiminika. Kila aina ya raia yumo humo. Wazee na vijana, wanawake na wanaume, wagonjwa na wazima, wa mjini, majijini na mashambani, waliosoma na wasiosoma, walimu, madaktari, wafanyabiashara, wakulima, mabingwa wa kilimo, wavuvi, mawakili, wanasheria na baadhi ya wanasiasa wa upinzani. (uk.66).

Aidha, Bi Shoo anamweleza Bw. Binafsi kuwa jeshi la wananchi wanaomfuata Mpya ni kubwa na hata wanajeshi wake wengine wameamua kujiunga na kundi hili.

Katika tamthilia ya *Kigogo* (2016), Tunu anawashawishi Wanasagamoyo kutetea haki zao na kupigania Sagamoyo mpya. Sudi anaelekea kukata tamaa na kuacha kushirikiana na Tunu kuleta mabadiliko ya kiuongozi jimboni Sagamoyo. Hii ni baada ya Boza kumshauri akae nyumbani kukidhi mahitaji ya familia yake na hasa wanawe ambao wana njaa. Tunu anamshawishi Sudi kuendelea kupigania wananchi wa jimbo la Sagamoyo (uk.18).

Isitoshe, Tunu anawashawishi wananchi kuandamana kutetea haki zao. Majoka anasema:

Ala! Tunu aliongoza maandamano? Tena aliandamana na hawa wanaojiita wanaharakati! (uk.32).

Uongozi ni uwezo wa mtu kushawishi, kumotisha na kuwawezesha watu wengine kushiriki ufanisi wa shirika ambalo wao ni wanachama (Hora, 2014). Kiongozi Tunu anawashawishi na kuwapa motisha wananchi kutetea haki. Anafanya hivyo kupitia kwa maneno, matendo na mtazamo yake. Kupitia kwa maneno, matendo na mitazamo ya mhusika; sifa zake hubainika (Mulokozi, 1996). Tunu anawashawishi wananchi wengi hadi wanatoa maoni kuwa Tunu awanie

uongozi wa Sagamoyo. Asilimia zaidi ya sitini kwa mujibu wa gazeti alilokuwa nalo Majoka wako tayari kumpigia kura (uk.33).

Isitoshe, Tunu anawashawishi Wanasagamoyo wakutane katika lango kuu la Chapakazi siku ya kuadhimisha miaka sitini ya uhuru. Akiwa ameandamana na Sudi na Siti, wanaenda kwa Mamapima ambako shughuli ya ulevi ilikuwa imenoga na kuwaalika wote kwa mkutano huo (uk.56). Siku hii inapowadia ushawishi wa Tunu unabainika wazi. Wanasagamoyo wanasusia mkutano wa Majoka katika uwanja wa ikulu na kukusanyika katika lango kuu la soko la Chapakazi alivyowataka Tunu. Kenga anashangaa kuona kuwa ni watu kumi pekee ndio waliofika katika uwanja wa mkutano wa Majoka, ilhali kidehuri uwanja huu huwa umejaa pomoni kufikia saa nne za asubuhi wakati wa mikutano kama hii (uk.86). Tunu anafaulu kuwashawishi baadhi ya watu waliokuwa wafuasi wa Majoka kumuunga mkono. Mwishoni mwa tamthilia, tunawaona Kingi ambaye ni mkuu wa polisi na Mamapima wakijiunga na upande wa Tunu jambo linaloashiria kuwa wawili hawa waliokuwa wafuasi wa mpinzani wa Tunu wa kisiasa wameshawishika kumfuata Tunu (uk.90-92). Kingi anamwambia Majoka:

Sina ruhusa ya kuwavamia watu ambao hawajavunja sheria. Samahani msheshimiwa (uk.90).

Kingi anakiuka amri ya Majoka ya kuwapiga wananchi risasi.

4.2.5 Mwanamke kama Kiongozi Msema Ukweli kwa Uwazi

Kiongozi Bikisiwa katika *Posa za Bikisiwa* (2008) anawaambia wanaume waposaji waziwazi bila kuficha kuwa yafaa wajali maslahi yake na ya jamii wala sis maslahi yao wenyewe. Hassan ajapo kumposa, anamwambia bayana kuwa ndoa baina yao ni jambo lisilowezezana kabisa. Bikisiwa anasema:

Mimi sitaki kuolewa na wewe kwa sababu sikupendi (uk.32).

Kwa mujibu wa wanaudenguzi, matini husheheni maana mbalimbali ambazo zaweza kubainishwa kupitia usomaji na uchunguzi wa kina wa matini. Ndoa katika muktadha huu yaweza pia kurejelea uhusiano kati ya nchi ya Bikisiwa na nchi ya Hassan (uk. 73-74). Uwazi wa Bikisiwa unamshangaza Hassan. Bikisiwa anamweleza Hassan kwamba amekuzwa kusema ukweli na kwamba katu hawezi kumdanganya kwani yeye hajazoea kusema uongo (uk.32).

Aidha Bikisiwa anataka Sogoramaneno amwambie moja kwa moja mambo aliyo nayo bila ya kumpaka mafuta (uk.55-56). Sogoramaneno anaposifia uzuri wa Bikisiwa, Bikisiwa anamwambia waziwazi kuwa uzuri ni wake na kwamba Sogoramaneno afaa aache autumie vilivyo (uk.56).

Bikisiwa hasazi kumwambia babake ukweli kibayana kuwa alifanya kosa la kutoshauriana na raia kuhusu posa yake. Anasema:

Samahani baba lakini kosa ni lako wewe kwa kutotaka kushauriana na raia kuhusu posa zangu- jambo kama hili kubwa kuliko jingine lolote katika familia yetu na katika ufalme wako hukutaka kumshauri mtu yeyote? Hata mama? (uk.18).

Mwamzandi (2013) alipoitumia nadharia ya udenguzi alizungumzia dhana ya kivuli cha maana. Anasema kuwa kivuli cha maaana ni ile sehemu ya neno au dhana ambayo huenda isizungumziwe wazawazi na mwandishi. Neno posa katika muktadha huu linarejelea uhusiano wa kimataifa baina ya nchi ya Bikisiwa na nchi zingine.

Bikisiwa katika usemi huu anamkosoa babake kwa kuingia katika mahusiano ya kimataifa bila kuhusisha wananchi. Bikikongwe anakasirishwa na watoto wanaopita wakicheza mchezo wa kutupiana risasi za bunduki. Anawaamrisha waondoke. Tukio hili linafanya Cecilia, Jane na Mpitanjia kucheka kicheko kikubwa. Bikisiwa anasikitika na kuwaambia wazi kuwa hilo si jambo la kucheka.

Mojawapo ya njia ya kubainisha sifa za mhusika fulani katika kazi ya fasihi ni kuchunguza usemi wa wahusika wengine kumhusu mhusika huyo (Wamitila, 2003). Mtambaji, Mpitanjia, Jane na Cecilia wanasema kuwa Bikisiwa ni msemu kweli:

Tuna hamu na ya kiongozi wa kike mwenye ukweli kama wewe...(uk.68).

Katika *Kimya Kimya Kimya* (2011), Mpya anasema ukweli kuwa utawala wa nyumbani wafaa uchangie utawala wa nchi na utawala wa nchi haufai kuwa wa mtu mmoja na familia yake finyu ila wa jamii (uk.53). Kwa kusema hivi, Mpya anarejelea hali nyumbani mwao ambapo babake alikuwa akiongoza nchi bila kuzingatia maslahi ya wananchi. Kinaya ni kuwa yeye alikuwa mmjowapo wa familia hii. Mpya anawaeleza Mussa Zanga kuwa kama vijana wafaa kusema ukweli hadi ukweli huo udhihiri na uwongo ujitenge (uk.54). Kiongozi Mpya anaiambia umma

ukweli na uhalisia wa jamii. Anawaambia kuwa nchi yao ni ya watu wachache (kama babake) wanaoiba mali ya nchi (uk.74). Ni ukweli huu ndio ufanyao wananchi kumuunga mkono kwani kulingana nao ukweli huu ndio wanaoujua (uk.75).

Kupitia tamthilia ya *Pango* (2006), kiongozi Katango anasema ukweli waziwazi bila kuficha. Anamkosoa Ngwese kwa uwazi na kumwambia ukweli kuwa tendo lake la kuwafukuza watoto wasichote maji ni tendo la kikatili na kibinafsi (uk.10). Isitoshe, Katango anamweleza Ngwese ukweli kwamba babu yake alikosa kuwa chifu kwa kukataliwa na wananchi kwani alikuwa kibarakala wa wakoloni kinyume na madai ya Ngwese kuwa wazee wa Katango walimwonea wivu. Ukweli huu unamkasirisha Ngwese zaidi hadi anamkaribia Katango na kutaka kumpapata makofi (uk.13-14).

Seki, babake Katango, anakataa kuamini kuwa Ngwese aliwafukuza watoto wasichote maji. Katango anamsisitizia kuwa ni kweli Ngwese alifanya hivyo. Seki haamini ukweli kuwa Katango aliviziwa njiani. Katango anamsisitizia ukweli huu:

Ni kweli baba, tuliviziwa na najua kuwa lazima walitumwa na Ngwese (uk.35).

Baada ya Katango kupokwa uongozi na Ngwese kupitia kwa mbinu ya ufisadi, Katango anaonekana kukata tamaa. Anamweleza babuye ukweli wa hali hii yake bila ya kumficha. Anamweleza kuwa heri amwachie Ngwese na watu wa aina yake kila kitu (uk.57-58). Hatimaye Wanapango wanatambua kwamba madai ya Katango kuwa Ngwese ndiye aliyekuwa anaharibu Pango yalikuwa ya kweli (uk.85).

Kiongozi wa jinsia ya kike katika *Kigogo* (2016) ni mtu wa kusema ukweli bila kuficha. Tunu akiwa ofisini mwa Majoka anamweleza Majoka ukweli mchungu kuwa ugatuzi si unyakuzi (uk.45). Majoka alikuwa amenyakua ardhi ya soko la Chapakazi ambalo lilikuwa tegemeo la kiuchumi la Wanasagamoyo wengi na kuamua kujenga hoteli ya kifahari.

Tunu na Sudi wanamtembelea Majoka ofisini kutatua matatizo ya wananchi. Majoka anatoa madai kuwa yeye na babake Tunu walikuwa ndugu wa toka nitoke. Hapo ndipo Tunu anapomweleza waziwazi kuwa kesi ya babake ilimkomaza kabla ya wakati wake. Katika kikao kiki hiki, Tunu anamwambia Majoka ukweli kuwa kesi ya babake ilikuwa mbaya sana na kuwa ikiwa mamake hangejibidiisha kwenda mahakamani basi Majoka hangewapa chochote (uk.44).

Majoka anapodai kufadhili masomo ya Tunu na hata kumtafutia ufadhili wa ng'ambo, Tunu anamweleza ukweli waziwazi kuwa babake alifia katika kampuni ya Majoka na kifo chake kilisababishwa na Majoka. Isitoshe, anamweleza kuwa mamake Tunu asingeenda mahakamani na kupigania haki yake wasingeipata haki hiyo (uk.44).

Tendo la mwanamke kiongozi kuzungumza ukweli kwa uwazi linawafanya baadhi ya watu katika jamii hizi kuwa na mtazamo kuwa mwanamke kiongozi ni mtu mkali. Kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu mitazamo ni kipengele muhimu katika kubaini maana ndani mwa matini. Kulingana nayo, uchanganuzi wa mitazamo mbalimbali iliyomo ndani mwa matini husaidia uibuaji na uelewa wa maana ndani mwa matini hayo (Levinas, 2003). Katika *Posa za Bikisiwa* (2008) Bikisiwa anawaeleza wanaume waliomjia kumposa ukweli. Anapomweleza Hassan ukweli kuwa hampendi hivyo hawezi kuolewa naye, Hassan anakuwa na mtazamo kuwa Bikisiwa ni mkali. Anamweleza Bikisiwa mtazamo huu:

Mbona Bikisiwa uko wazi hivyo? (uk.32).

Kwa uwazi, Tunu anamweleza Majoka ukweli kuhusu matatizo yanayokumba jimbo la Sagamoyo. Anamweleza bayana kuwa yeye na watu wake watalipia kila tone la damu walilomwaga Sagamoyo. Mtazamo wa Majoka ni kuwa Tunu kwa kumwambia maneno haya ni mkali. Mtazamo huu unadhihirika Majoka anapomwambia Tunu:

Hilo ni onyo ama ni tishio (uk.43).

Mwanamke katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika alisawiriwa kama kiumbe ambaye alifaa tu kuonekana bali si kusikizwa. Hakuruhusiwa kushiriki mazungumzo ya wanaume na kufanya maamuzi muhimu katika jamii na hata kumhusu yeye na wanawe (Mapunjo, 2014). Kila uamuzi alikatiwa. Utamaduni haukumruhusu kuingilia masuala ya uongozi (Onyoni, 2012). Taswira hii ni tofauti na taswira ya mwanamke kiongozi inayobainika katika tamthilia zilizotungwa tangia mwaka wa 2000. Kwa mujibu wa Miller (1976) matumizi ya nadharia ya udenguzi katika uhakiki wa matini huibua maana mpya ndani mwa matini. Maana hii iliyoibuliwa kulingana naye huenda ikafanana au ikatofautiana na maana iliyoibuliwa na wahakiki wa awali. Kinyume na tafiti za awali za fasihi zilizomsawiri mwanamke kama mtu asiyesema kwa uwazi, mwanamke katika tamthilia teule za utafiti huu amechorwa kama mwenye kusema kwa uwazi. Isitoshe,

maneno ayasemayo yamejaa ukweli mtupu hata kama ni mchungu. Kiongozi ajuaye kusema ukweli hata ukiwa mchungu ni kiongozi bora (Lemer, 2003).

4.2.6 Mwanamke kama Kiongozi Mzalendo

Kwa mujibu wa TUKI (2014), uzalendo ni hali ya mtu kuwa tayari kuifia nchi yake. Mtu mzalendo ni mtu anayeipenda nchi yake na kuwa tayari kuipigania hata kufa kwa ajili yake (Mdee, Shafi & Njogu, 2011).

Nchi katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) inakumbwa na matatizo mengi ambayo chanzo chake ni uongozi mbaya. Kutokana na matatizo mengi wanayoyapitia wananchi, upendo kwa nchi umefifia mno. Ni bayana kuwa kuna wakati kiwango cha uzalendo nchini kilikuwa juu. Wakati huo, kila mwananchi alikuwa na hisia za kizalendo au za kuipenda nchi. Hali hii ndiyo inayodhihirika kupitia usemi wa Kulia anapozungumza na kisima:

Kiza, kiza ndani ya kisima mna ombwe. Hamwonekani kitu. Sipo hapa zamani palipokuwa na bubujiko la maji yaliyonguruma mpaka Ulaya? Sipo hapa palipomfanya kila mtu awe mwananchi mwenye hisia ya kuipenda nchi hii? (uk.12).

Katika hali hii ya matatizo, uongozi mbaya, utamaushi na kufifia kwa uzalendo nchini kunatokea hitaji kubwa la wazalendo halisi watakaopenda nchi na kuipigania. Sauti Ndani ya Kisima inaamsha hisia za kizalendo kwa kusema:

Tazama mbele, usitazame nyuma. Ijali tamu ya nchi yako, usijali tamu ya siasa tupu. Ijali nchi na kuitetea (uk.11).

Neno jali katika muktadha huu lina maana ya kuhisi kwamba unahusika kwa mtu au kitu (TUKI, 2004). Sauti Ndani ya Kisima inadhihirisha uhitaji mkubwa uliokuwepo; uhitaji wa wazalendo halisi ambao wangetetea maslahi ya nchi. Mpya anajitokeza kutetea uongozi bora unaojali maslahi ya nchi (uk.73-74). Kujitokeza huku kunaleta matumaini mapya. Sauti Ndani ya Kisima inasema kuwa kujitokeza kwa Mpya ni ishara njema (uk.21). Uzalendo wa Mpya unabainika kupitia kwa tendo lake la kujitolea kuikomboa jamii yake kutokana na uongozi mbovu.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008), Bikisiwa ni mzalendo. Anasisitiza kuwa anataka posa ambayo italeta faida kwa jamii yake wala si kwake binafsi tu. Anataka uhusiano

utakaonufaisha watu wake. Hii ndiyo sababu anawakataa wachumba wanaume wanaokuja kumposa. Wanaume hawa wanamjia kwa maneno matamu na zawadi teletele ila matendo yao hayamfanyi kukosa kushikilia lengo lake la kupata mchumba atakayejali maslahi ya nchi yake (uk.64). Tendo la kiongozi Bikisiwa kukataa kuchumbiwa na wanaumme wasiojali maslahi ya nchi yake licha ya maneno matamu na zawadi kochokocho linamsawiri Bikisiwa kama kiongozi anayeipenda nchi yake. Mathalani, anamwambia SS, mmoja wa waposaji wanaomjia:

Muhimu zaidi ni kwamba ndoa yetu italeta natija gani kwako na kwangu na hasa kwa watu wangu? (uk.39).

Bikisiwa analiona gumu pendekezo la babake (Mfalme) la kumtumia yeye kupitia kwa posa ili kuweza kuokoa nchi kutokana na uvamizi. Japo ni gumu, Bikisiwa anakubali pendekezo hili kwa kuwa anapenda nchi yake na yu tayari kuifia. Anasema:

Nimekubali kwa ajili ya nchi yangu... (uk.36).

Maneno haya yanapiga mwangi Bikisiwa aondokapo jukwaani; jambo linaloonyesha ugumu na umuhimu wa usemi huu.

Mfalme ana mtazamo kuwa Bikisiwa ni kiongozi. Mitazamo kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu huathiri maana (Levinas, 2003). Mtazamo wa Mfalme unaobainika kupitia kwa maneno yake kwa Bikisiwa yanamchora Bikisiwa kama kiongozi mzalendo:

Wewe lakini si mwanamke tu, ni binti mfalme. Maslahi ya nchi hii nzima yatakuwa juu ya maungo yako ukiolewa naye (uk.35).

Mtambaji anapomhadithia Mpitanjia hadithi ya kiongozi Bikisiwa, anamweleza kuwa Bikisiwa:

Alitaka achaguwe mchumba mwenyewe kwa maslahi yake na ya watu wake (uk.13).

Katango katika Pango (2003) ni mwanamke anayeipenda jamii yake ya Pango. Mapenzi yake kwa jamii yanamchochea kujitokeza kuwania uongozi wa Pango ili kuhakikisha kuwa kuna usawa Pangoni na kwamba asali ya Pango inamfaidi kila Mwanapango. Anasema:

Ehhh mara hii asali ya pangoni lazima iwafaidi wote... (uk.28).

Katango yuko tayari kulifia Pango. Anaviziwa na Mtu I na II (walitumwa na Ngwese ambaye ni mpinzani wa Katango) wakiwa njiani na Kibwana. Anatishwa, anafinywa, anabanwa na kutaka kubakwa ila hakati tamaa (uk.31-33). Kwa kurejelea tamthilia ya Kigogo (2016), uzalendo

unamchochea Tunu kuendelea kupigania haki za Wanasagamoyo hata baada ya kupigwa na kulemazwa na serikali ya Majoka. Anazidi kutetea kufunguliwa kwa soko, huduma kuletwa karibu na wananchi na ajira kwa vijana (uk.54-56).

Mugambi (1982) katika kuhakiki maudhui katika tamthilia ya *Zinduko* (Ryanga, 1986) alidai kuwa kwa mujibu wa tamthilia hii wanawake hawana upeo mkubwa wa kisiasa. Kulingana naye, mwanamke hana nafasi ya kushiriki katika siasa kama kiongozi bali jukumu lake ni kuwahimili wanaumme. Picha ya mwanamke kiongozi inayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 ni ya mwanamke ambaye anajitokeza kujihusisha katika siasa za uongozi wa nchi yake kwa sababu ya mapenzi yake kwa jamii au nchi yake.

4.2.7 Mwanamke kama Kiongozi Mkakamavu

Kwa mujibu wa Mdee, Njogu & Shafi (2011), ukakamavu ni hali ya kuvumilia matatizo, hali ya kukataa kuvunjika moyo au kukubali kushindwa. TUKI (2014) wanaeleza ukakamavu kama hali ya kustahimili mambo; hali ya kutokubali kushindwa kwa urahisi. Kila kiongozi hukumbana na changamoto katika kuwania uongozi na hata katika kuongoza. Changamoto hizi zinaweza kumfanya mwanamke kiongozi anayewania uongozi kutamauka. Katika muktadha wa kisiasa, wanawake hupitia changamoto kadha katika kuwania nyadhifa za kisiasa. Kwa mujibu wa Houreld (2017) wanawake waliogombea nyadhifa za kisiasa nchini Kenya katika uchaguzi wa 2017 walipitia changamoto nyingi kama kupigwa, kutusiwa, kupigwa risasi, kulaaaniwa na wazee, kuchomewa nyumba na kutibuliwa kwa mikutano yao walinzi wake kuuwawa. Ukakamavu ni sifa muhimu ya uongozi. Katika jamii, viongozi huweza kupitia madhila mbalimbali. Kiongozi bora ni yule anayeyavumilia na kudhihirisha ukakamavu.

Kwa kurejelea *Pango* (2003) Katango ni kiongozi wa jinsia ya kike anayeonyesha hali hii ya kutokubali kushindwa licha ya changamoto nyingi anazozipitia. Jambo hili linabainika kupitia kwa maneno, mtazamo na matendo ya Katango. Ngwese, mpinzani mkuu wa Katango, anatishia kumpapata makofi na kumnyamazisha Katango (uk.14). Anatuma na kufadhili Mtu I na II kuwavamia Katango na Kibwana (uk.31). Katika uvamizi huu Mtu I anajaribu kumpapasa Katango kimapenzi na kumwambia namna haiwezekani mwanamke kuongoza, anamfinya, anambana na kujaribu kumpiga kofi. Isitoshe, anamtusi kwa kumwita kiruka njia na kumtisha

aache kumpinga Ngwese. Katango anastahimili madhila haya yote kutoka kwa Mtu I na II na kukataa kufa moyo katika azma yake ya kuliongoza Pango. Hajihurumii baada ya tukio hili, anaonyesha ukakamavu. Anamwuma Mtu I na kumpiga kumbo linalomrudisha kinyumenyume na kutupa mkono wa Mtu II unaompiga shavuni. Mamake Katango anapomwuliza iwapo ameumia anakana. Anamshauri mwanawe aache kupingana na Ngwese ila Katango anadhihirisha ukakamavu wake kwa kukataa kusitisha juhudi zake za kumpinga Ngwese kuwania uongozi wa pango. Anasema:

Ndiyo mama anataka tu niache nia ya kumpinga lakini siwezi...! (uk.34).

Katango anaelekea kutwaa ushindi baada ya hotuba yake kwa umma. Hata hivyo, ushindi wa Katango unabatilishwa wakati Ngwese kwa kuona anaelekea kushindwa anaamua kuwagawia wananchi matunda. Tendo hili la kifisadi linabadilisha msimamo wa watu wengi wanaotoka upande wa Katango na kumwuunga mkono Ngwese kwa madai kuwa mkono mtupu haulambwi (uk.47). Tukio hili linamshusha moyo Katango. Anaelekea kukata tamaa na kuachana na juhudi za kuwania uongozi wa pango. Anashusha mabega na kumwambia babu:

Hali itabakia kama zamani. Si ni heri tu kumwachia huyo Ngwese na watu wa aina yake kila kitu...Hata wenzangu wananiambia kuwa sisi vijana hatuna nafasi kabisa...(uk.57).

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), wanaudenguzi huchunguza lugha iliyotumiwa ndani mwa matini kwa kuwa lugha hii hubeba maana. Nahau: shusha mabega iliyotumiwa na mwandishi ina maana kuwa Katango alikuwa anakata tamaa. Sauti katika usemi huu wa Katango ni ya kutamauka. Mishra (2018) anasema kwamba nadharia ya udenguzi hulenga kuibua kinaya, utata, ukinzani, unyume au mwachano ndani mwa matini. Tendo la Katango kushusha mabega pamoja na usemi wake unabainisha kuwa Katango alikuwa amekata tamaa. Kinaya ni kuwa Katango hakati tamaa. Anendelea kupigania mabadiliko katika jamii yake ya Pango. Hali hii inamsawiri kama kiongozi mkakamavu.

Ukakamavu wa Katango unadhihirika wakati anakuwa wa kwanza kuwaambia Kibwana na Kikubi (waliomletea habari kuwa mchezo ulikuwa ukiendelea pangoni) kwamba waende waone ni kina nani walikuwa wakicheza Pangoni ili wawajulishe wengine. Hii ilikuwa baada ya tukio la kutamausha ambapo Katango alikuwa amepokwa ushindi wake (uk.59).

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008), mwanamke anatoa kicheko kilichojaa uchungu. Nadharia ya udenguzi huchunguza ukinzani, utata, kinaya au mwachano uliomo ndani mwa matini ambao huchangia kujenga maana (Mishra, 2018). Tunavyojua katika hali ya kawaida ni kuwa, kicheko huashiria hali ya furaha. Kicheko akitoacho mwanamke huyu badala ya kuashiria furaha kimejaa uchungu na kilio. Uchungu na kilio katika kicheko hiki kinaashiria udunishwaji wa miaka mingi wa mwanamke katika jamii ya Bikisiwa.

Baada ya kicheko hiki mwanamke anaanza kutongoa kwa ukakamavu:

Eeh, wewe! Angalia wewe. Hii si dunia ya kulala. Hii ni dunia ya unyang'anyi (uk.1).

Mwandishi anaeleza kuwa Bikisiwa anaingia jukwaani kwa ukakamavu (uk.1). Mtambaji anapomhadithia Mpitanjia hadithi ya Bikisiwa anasema kwamba Bikisiwa alikuwa mwanamke mkakamavu (uk.13).

Kupitia tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011), Mpya anajitokeza kama kiongozi mkakamavu. Mpya anakanywa (kwa kumtolea kidole cha shahada) na babake aitwaye Bw. Binafsi ainamishe kichwa chake walivyokuwa wamefanya ndugu zake na mamake. Babake pia anamkemea ili anyamaze. Bw Binafsi anajuta kwa kutomng'oa Mpya kutoka tumboni mwa mamake kabla azaliwe (uk.34). Si hayo tu. Babake Mpya anawaamrisha walinzi wake kumburura Mpya. Walinzi wanamshika na kumburura kama gunia la makaa. Anamwagiza Mpya aondoke nyumbani kwake (uk.41). Mpya japo anapitia dhiki hii haachi kutetea haki. Anaongoza wananchi kuimba polepole bila fujo kuelekea kwa uwanja wa bustani. Askari wanamiminika na kuingia bustanini na kuanza kuwapiga wananchi virungu (uk.61). Juhudi za Mpya za kuikomboa nchi hazisiti kwa sababu ya matumizi ya vyombo hivi vya dola kunyamazisha sauti za wananchi wanyonge.

Kwa kurejelea *Kigogo* (2016), Tunu anapitia madhila ya kutamausha. Anasingiziwa kuwa ni mpenzi wa Sudi (uk.64). Ukakamavu wa Tunu unabainika tunapomwona akivumilia singizio hizi zote; haziachi kumsababisha kuacha kuandamana na Sudi kutetea haki za Wanasagamoyo. Majoka alisababisha kifo cha babake Tunu ambaye alikuwa mfanyikazi katika kiwanda chake (u.44). Anapanga njama ya kumwua Tunu (uk.55). Kenga anapomwambia Majoka kuwa Tunu bado yuko hai, Majoka anashangaa kuwa Tunu amefufuka kutoka kwa wafu (uk.68). Kutokana

na tukio hili la kinyama, Tunu analemazwa miguu hivi kwamba inambidi atumie kiti cha magurudumu. Kenga akimrejelea Tunu anamwambia Majoka:

Hana miguu kwa sasa. Pengine atambae kwa tumbo kama nyoka (uk.69)

Akiwa katika hali hii ya ulemavu, tunatarajia kuwa Tunu ataacha shughuli za kuwahamasisha na kutetea haki za Wanasagamoyo hata kama ni kwa muda. Kinaya ni kuwa Tunu hasitishi harakati zake hata kidogo. Anaamua kwenda kukutana na majangili waliomvamia licha ya mamake kumkataza asiende. Pindi Sudi anapoingia Tunu anamwambia mamake:

Mama, nipeleke bafuni. Tutatoka sasa hivi na Sudi (uk.56).

Katika hali yake ya ulemavu, Tunu anafanikiwa kuwahamasisha Wanasagamoyo kukutana kwenye soko la Chapakazi siku ya sherehe za uhuru. Katika mkutano huu, Tunu anahutubu kwa ukakamavu:

Naomba kwanza kuukosoa uneni wa hapo awali wa viongozi wetu katika vyombo vya habari kwamba siwezi kuzipigania haki za Wanasagamoyo kwa kuwa wamenilemaza. Hali yangu hii ni ya muda tu (uk.88-89).

Tunu anapitia changamoto za kiwango cha juu sana kwa kutaka kuuawa na hatimaye kuvunjwa mguu. Inabainika katika hotuba hii kwamba Tunu anakataa kukata tamaa katika kutetea haki za Wanasagamoyo baada ya kulemazwa na watu waliotumwa na serikali ya Majoka ili kumwua. Taswira ya Tunu inayojitokeza kupitia kwa hotuba hii ni ya kiongozi mkakamavu.

Keter (2013) alipohakiki tamthilia za *Kifo Kisimani* (1981) na *Natala* (1997) alibainisha kuwa mwanamke katika tamthilia hizi anakabiliana na changamoto nyingi katika juhudi zake za kujikomboa. Mapunjo (2014) katika uhakiki wake wa tamthilia ya *Nguzo mama* (1982) na *Kivuli Kinaisha* (1990) anadai kuwa changamoto zinazowakabili wanawake zinachangia wanawake hawa kutofaulu kupata haki zao. Anatoa mifano ya Mwavita na Bi Nane katika *Nguzo mama* ambao wanaonekana kushindwa kwa sababu ya changamoto wanazokumbana nazo. Imebainika kuwa, mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2017 anapitia changamoto mbalimbali katika juhudi zake za kuongoza jamii yake. Hata hivyo, changamoto hizi hazimfanyi mwanamke kiongozi kushindwa. Anazikiuka na kuongoza jamii.

4.2.8 Mwanamke kama Kiongozi Anayejiheshimu na Kuheshimu Wengine

Kupitia tamthilia ya *Pango* (2003), hata baada ya Ngwese kutumia njia ya kifisadi kupata uongozi, Katango anaamua kutumia mdomo wake kuwashawishi watu wasipumbazwe na matunda wanayogawiwa na mpinzani wake Ngwese. Anajiheshimu kwa kuwa hashiriki katika ufisadi namna mpinzani wake alivyofanya (uk.47). Kwa mujibu wa *Posa za Bikisiwa* (2008), Bikisiwa anajiheshimu kwa kukataa kuingia katika uchumba kiholelaholela bila fikra wala majadiliano (uk.47, 64). Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kigogo* (2016), inabainika kuwa Tunu ni kiongozi anayejiheshimu. Yeye ni mwadilifu. Ingawa anasingiziwa kuwa na ushirikiano wa kimapenzi na Sudi tunamwona akiwa mwadilifu na kuhusiana na Sudi kisiasa bila kuwa na uhusiano wa kimapenzi naye (uk.49). Mpya katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) anajiheshimu. Hajihusishi katika vitendo vya ufuska.

Mwanamke kiongozi hajiheshimu tu; anawaheshimu watu wengine. Mtu hawezi kuwaheshimu wengine pasi na kujiheshimu kwanza. Kwa mujibu wa *Pango* (2003) kiongozi Katango anawaheshimu watu wengine. Tunamwona akiwa na mlahaka mwema na mama, babu, watu uwanjani na marafiki zake kama Kikubi na Kibwana. Mathalani anamkaribisha babu kwao kwa taadhima (uk.56). Ingawa ana mtazamo tofauti na babake kuhusu masuala kama ya uongozi na utamaduni, anaeleza mtazamo wake bila kumkosea heshima babake. Kwa mfano anamwambia babake:

La, baba. Huo ni ushirikina (uk.19).

Baba mambo yamebadilika (uk.20).

Kwa kurejelea tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2011), Bikisiwa ni mwanamke mwenye heshima. Tunamwona akipiga hodi kwa nyumba yao kabla ya kuingia.

Kupitia tamthilia ya *Kimya kimya* (2011), Mpya anajitokeza kama mwanamke mwenye heshima. Licha ya kuwa hapendi namna babake (Bw. Binafsi) anavyoongoza nchi, Mpya anamtambua kama babake na kumheshimu. Anasema:

Huyu ndiye baba 'angu (uk.30).

Licha ya madhila na chuki aipatayo kutoka kwa babake mzazi, Mpya anamwita ‘baba’etu mpenzi’. Heshima yake kwa babake na mamake inabainika anaposema:

Mimi nawapenda na kuwaheshimu sana wazazi wangu (uk.51).

Anawaambia nduguze: Mussa na Zanga kuwa lazima wawaheshimu wazazi na wazee wao ila lazima wazazi na wazee hawa watambue haki zao (uk.51). Mpya anamheshimu mamake na nduguze Mussa na Zanga. Ana mlahaka mwema nao. Huenda ni mlahaka huu unaowafanya Mussa na Zanga kushawishika kuungana naye kuongoza maandamano ya kuleta mageuzi nchini mwao.

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kigogo* (2016) Tunu ni mwanamke kiongozi anayejiheshimu na kuheshimu watu wengine. Tunu anamheshimu mamake Bi Hashima. Ana mlahaka mwema naye (uk.53, 56). Kando na kumheshimu mamake, Tunu anamheshimu Sudi pamoja na ndoa yake. Licha ya singizio kuwa ni mpenzi wa Sudi, Tunu hashiriki mapenzi na Sudi (uk.64). Anajiheshimu. Aidha, anawaheshimu wananchi wa Sagamoyo. Katika muktano wake wa kisiasa, anawahutubia wananchi kwa taadhima bila kuwatusi namna mpinzani wake Majoka alivyofanya (uk.88-89).

Katika juhudi za kutetea haki za Wanasagamoyo, Tunu hana kinyongo na wapinzani wake. Asiya (Mamapima) anaamrisha Tunu aondoke kwake kwa madai ya kumharibia biashara yake ya ulevi (uk.62). Licha ya mgogoro huu, Tunu anamheshimu Asiya. Hatimaye, tunamwona Tunu akimshika Asiya mkono, kumwinua na kumwambia:

Asiya, mimi sina kinyongo nawe (uk. 92).

Kiango (1992) katika uhakiki wake wa tamthilia za Kenya anaibua dai kuwa mwanamke ni mtu anayeendeleza maudhui mabaya kwa kuwa amesawiriwa kama mzinifu, mbaya, muuaji na mwaviaji mimba. Keter (2013) katika utafiti wake kuhusu nafasi na utambulisho wa mwanamke katika tamthilia za *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001) anasema kwamba mwanamke amechorwa kama mtu mwovu, mgomvi, asiye na shukrani, barakala na mwenye hasira za mkizi. Kulingana na wanaudenguzi, uhakiki wa matini kwa kutumia nadharia ya udenguzi huibua maana mpya ambayo huenda ikatofautiana na maana ya awali (Derrida, 1973; Miller, 1976). Kinyume na baadhi ya tafiti za awali zilizobainisha namna mwanamke alivyosawiriwa kama mtu mwovu na asiyejiheshimu, mwanamke kwa mujibu wa tamthilia teule za Kiswahili za tangia

mwaka wa 2000 hadi 2017 amejitokeza kama kiongozi mwadilifu anayejiheshimu na kuwaheshimu watu wengine.

4.2.9 Mwanamke Kama Kiongozi Mwerevu na Mwenye Busara

Kwa mujibu wa TUKI (2014), mtu mwerevu ni mtu mwenye akili nyingi au mwenye hila ama ujanja mwingi. Mdee, Njogu & Shafi (2011) wanaeleza mtu mwerevu kuwa mtu mwenye ufahamu mkubwa au akili nyingi. Busara ni akili au werevu wa kufikiri au kuamua kutenda jambo lifaalo (TUKI, 2014). Hekima ni muhimu sana kwa kiongozi hasa anapotaka kufanya maamuzi muhimu (Intezari, 2013).

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008), Bikisiwa anakuwa mwenye hekima katika kuchagua mchumba. Anajiwa na wanaume tofautitofauti: SS, Hassan, Chachi, Biss na Sogoramaneno. Wanamwinamia, wanampa zawadi nzuri na kummiminia sifa kochokocho. Hata hivyo, Bikisiwa hapumbazwi na matendo haya. Ni hekima inayomfanya kutopumbazwa kwa maneno matamu ya SS. Bikisiwa anazitilia shaka sifa na heshima kutoka kwa waposaji hawa kwani anazona kama zisizotoka moyoni (uk.18).

Biss, mmoja wa wanaume waposaji, anapomjia Bikisiwa anasifu umbo lake:

Bahari izungukayo mwili wako ni shwari na kina. Bandari zako zote zimesitirika. Raslimali za pekee Mungu alizokujalia ndani ya nafsi yako. Madini ni nini kuliko ardhi ya rutuba ya kuotesha kila mmea ndani ya mwili wako? (uk.32).

Kulingana na wanaudenguzi, matini hubeba maana mbalimbali ambazo hubainika kupitia usomaji na uchambuzi wa kina wa matini (Mishra, 2018). Kwa kuchunguza usemi huu, maana mbili zinaibuka. Moja ni kuwa Biss anasifia umbo la mwili wa Bikisiwa. Pili ni kuwa Biss anasifia nchi ya Bikisiwa. Uerevu wa mwanamke kiongozi unabainika anapotambua kuwa sifa hizi ni za kumpumbaza tu. Mwanamke anayeaminika kuwa Bikisiwa anasema:

A-a! Mimi naelewa lengo lenu ni nini...kunidokoa kidogokidogo, mnimalize mpaka mniache mtupu. Wacheni ujanja wenu. Sote sasa tumeshaerevuka. Tumeshatambua (uk.2-3).

Kwa maneno ya mtambaji matajiri walijaribu kutumia maneno matamu, mali, utajiri na hifadhi lakini binti mfalme alikuwa msomi mwenye akili nyingi na mjanja. Bikisiwa anaonekana kuwa na ufahamu mkubwa kuhusu nia na mitazamo ya wanaume waposaji waliomjia kuliko walivyojua wanaume hao.

Mtambaji anapomwelezea Mpitanja hadithi ya Bikisiwa anasema:

*Alikuwa mwanamke mwenye akili, busara na mkakamavu. Watu wote walitaka
Kumposa kwa sababu ya uzuri wake wa sura, umbo na wingi wa akili na busara zake
...Lakini binti huyu alikuwa msomi, mwenye akili nyingi...Yeye alitaka mapenzi si sifa, au
utajiri au sura nzuri ya mwanamume aliyetaka kumwoa. Yeye aliamini kwamba mtu
hawezi kuchaguliwa mapenzi na mtu yeyote. (uk.13).*

Kutokana na usemi huu wa, Mtambaji anamsawiri Bikisiwa kama kiongozi mwerevu na mwenye hekima. Werevu na busara yake ilimfanya kuwakataa wanaume waliotaka kumposa ila hawakumpenda.

Mwandishi Said Ahmed Mohammed Katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) amemchora mwanamke kiongozi kama mtu mwenye akili na ufahamu mkubwa kupitia kwa mhusika Mpya. Mtazamo huu wa mwandishi unabainika anapoeleza mhusika Mpya kama: mtoto wa ajabu mwenye akili kubwa kuliko mwili wake na mtoto wa kizazi kipya kinachofundishwa kutatua matatizo kwa kutumia masikio, hisia ya ngozi na mdomo wake (uk.29-30). Kulingana na nadharia ya udenguzi, maneno ndani mwa matini hubeba ujumbe na mwanaudenguzi huhitajika kuchunguza maneno hayo kwa undani ili kuibua ujumbe huo (Derrida, 1973; Mwamzandi, 2013). Maneno ya mwandishi yanaibua maana kuwa Mpya alikuwa kiongozi mwerevu aliyetatua matatizo ya jamii yake kupitia kwa masikio (mambo aliyoyasikia), hisia ya ngozi (mambo aliyoyapitia) na mdomo wake (usemi wake).

Kupitia *Kigogo* (2016), Tunu amesomea uanasheria hadi kiwango cha uzamifu (uk.32). Mawazo na vitendo vyake vinadhahirisha ukomavu wa kiakili aliokuwa nao. Hekima ndiyo imfanyayo amwambie Siti awapeleke wana wa Sudi kwao ili mamake Tunu awalishe na kuwatunza wakati Tunu na Sudi wanapoelekea sokoni na viwandani kupigania haki za Wanasagamoyo (uk.18). Tunu anakataa pendekezo la Majoka la kumwoza Ngao Junior ambaye ni mwanawe Majoka (uk.42). Hili ni tendo la kibusara kwani iwapo angekubali angepofushwa hivyo kudidimiza juhudi zake za kulikomboa jimbo la Sagamoyo.

Ni busara ndiyo imfanyayo Tunu kutaka Majoka azungumze nao (Sudi na Tunu) kwa pamoja bila kwenda chemba (uk.40). Tunu alitambua kuwa iwapo Majoka angefanya hivyo huenda angefaulu kumshawishi Sudi kuacha kupigania haki za Wanasagamoyo na kumtengenezea kinyago. Hii inatokana na hali kwamba Sudi alikuwa ameonekana kutetereka baada ya usemi wa Boza (uk.17-18). Katika mazungumzo ya Tunu na Majoka, Majoka anadai kuwa Tunu amenaswa katika utandu wa kasumba na falsafa za ukoloni mamboleo na Sudi (uk.42). Tunu anatambua kuwa Majoka anataka kumtenga na Sudi ili aendelee na uongozi mbaya. Tunu anatumia hekima kumwambia kuwa wanafaa kuzungumzia masuala yanayoathiri Wanasagamoyo sio watu.

Sudi na Ngurumo wanalumbana kuhusu keki za uroda. Hizi ni keki zilizoundwa na Mamapima kupewa wananchi ili kuwashawishi kuunga mkono uongozi mbaya wa Majoka. Keki hizi zinaitwa za uroda kwa kuwa Mamapima alishiriki mapenzi na Ngurumo ambaye ni mfuasi sugu wa Majoka kabla ya kupewa kandarasi ya kuzipika. Busara ya kiongozi Tunu inabainika pale anapogundua kuwa malumbano haya yatafanya wasiafikie lengo lililowaleta kwa Mamapima. Agunduapo hili, anamrekebishia Sudi:

Chunga tusipoteze lengo. Achana na hayo ya keki. Tujishughulishe na yaliyotuleta hapa (uk.64).

Kwa mujibu wa Murumba (2011) matendo huwa muhimu katika kuibua sifa za mhusika fulani. Tendo la kiongozi Tunu la kwenda mangweni kwa Mamapima kuliko na walevi ni la kibusara. Tunu anatambua kuwa huko ndiko kulikuwa na Wanasagamoyo wengi kwani baada ya soko la Chapakazi kufungwa, Wanasagamoyo walienda huko kujiliwaza kutokana na shida za kimaisha. Ngurumo anasema:

Tangu kufungwa kwa soko la Chapakazi, mauzo ya pombe kwa Mamapima yamekuwa maradufu (uk.60).

Ngurumo anapomwuliza Tunu ikiwa anataka kuwa kigogo wa Sagamoyo. Tunu anatumia hekima kumjibu. Anamwambia kuwa lengo kuu ni kufunguliwa kwa soko la Chapakazi, mengine ni ya baadaye (uk.58). Anasema kuwa Wanasagamoyo wanahitaji kiongozi anayeongozwa na hekima, si ubinafsi (uk.90). Wanaudenguzi hushikilia kuwa matini yaweza kusheheni maana mbalimbali. Usemi huu wa Tunu unazua maaana mbili. Moja ni kuwa Tunu

tayari alikuwa kiongozi mwenye hekima. Pili ni kuwa lengo lake lilikuwa kuongoza nchi kwa busara wala si kwa ubinafsi kama alivyofanya Majoka.

Katika tamthilia ya *Pango* (2003), Katango ni kiongozi mwerevu. Ana ufahamu mkubwa kuhusu haki zake kuliko wahusika wengine wanawake kama Mbabekazi na Kundi la wanawake lililokuwa katika uwanja wa kampeni (uk.36-49). Tendo lake katika mkutano wa kampeni la kusimulia ngano ya sungura ambapo anajinasibisha na uerevu wa sungura ni tendo la kibusara. Kupitia ngano hii Katango anapata wafuasi wengi kutoka upande wa Ngwese (uk.45).

Mpya kwa kurejelea *Kimya Kimya Kimya* (2011) ana ufahamu mkubwa wa haki zake (uk.51). Ni ufahamu huu ndio unaomfanya kuwahamasisha nduguze wajitokeze na kupigania haki za wananchi (uk.54). Ni busara ndiyo inayomfanya kusisitizia wafuasi wake kuwa maandamano watakayoyafanya lazima yafanywe kwa amani bila fujo (uk.72-73). Anasema:

Sisi hatutaki fujo. Hatutaki fujo. Ingawa fujo zinaandaliwa upande mwingine ili tuambiwe sisi wapenda fujo...Tusikejeli kiumbe chochote (uk.72-73).

Alifahamu kuwa huenda maandamano ya fujo yangeleta maafa na kudidimiza demokrasia na maendeleo ya nchi.

Ogundipe (1994) anasema kwamba wanaume husawiriwa kama watu werevu na wenye uwezo wa uongozi wa kuzaliwa ilhali wanawake hupewa majukumu yanayowasawiriwi kwa ubaya. Kwa kuangazia mhimili wa muktadha katika nadharia ya udenguzi, maana ndani mwa matini hueleweka vyema kwa kuchanganua miktadha iliyopo (Bakhtin, 1981). Mwanamke katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika alichorwa kama mtu mjinga asiye na ufahamu na ambaye daima alifaa kuamuliwa mambo (Hussein, 2005). Mugambi (1982) alipohakiki tamthilia nchini Kenya kati ya 1957 hadi 1981 alisema kuwa mwanamke amesawiriwa kama mtu duni asiyekuwa na ufahamu kuhusu masuala ya kisiasa. Kwa mujibu wa Miller (1976) maana mpya ni matokeo ya matumizi ya nadharia ya udenguzi katika uhakiki wa matini. Maana hii kulingana naye huenda ikatofautiana na maana iliyokuwa imeibuliwa awali. Taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia zilizotungwa tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 ni tofauti na taswira ya mwanamke iliyoibuliwa kupitia tafiti za Ogundipe (1994) na Hussein (2005). Mwanamke katika tamthilia hizi amesawiriwa kama mtu mwenye ufahamu mkubwa na akili nyingi. Kulingana na Hora (2014) wanawake ni werevu na watatuzi wa kutegemewa wa changamoto mbalimbali zinazokabili jamii ila wananyimwa nafasi ya kuongoza. Keter (2013) kwa kuhakiki tamthilia za

Kifo Kisimani (1981) na Natala (1997) alidai kuwa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia zake teule amechorwa kama kiumbe mwerevu na mwenye akili tambuzi. Imebainika kuwa mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016 amejitokeza kama kiongozi mwerevu na mwenye busara.

4.2.10 Mwanamke kama Kiongozi Mwenye Lengo na Maono

Lengo ina maana ya kitu kinachoangaziwa wakati wa kupiga shabaha (Mdee, Njagi & Shafi, 2011). Maono ni mtazamo wa maisha ya usoni ambao unatoa hatima bora kuliko hali ilyopo kwa wakati fulani na ambao unaafikika katika maisha ya kiuhalisia (Brecken, 2004). Kiongozi hawezi kufanikiwa ikiwa hana lengo na maono. Kiongozi akiwa na lengo na maono mahususi hatatapatapa gizani asijue anapowaelekeza wafuasi wake. Kwa mujibu wa Zate (2011) kiongozi anafaa ajue mahali anapowapeleka watu ambao anawaongoza. Kiongozi anafaa kuijua njia kabla ya kuwachochea wafuasi wake kumfuata katika njia hiyo. Maono ndiyo humsukuma na kumpa motisha kiongozi fulani kuafika malengo katika uongozi wake.

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Pango* (2003), uongozi wa Pango ulikuwa mbaya. Kwa maneno ya Seki, Pango lilikuwa limegeuzwa uwanja wa kufanyiwa kila aina ya upuuzi (uk.21). Lengo alilokuwa nalo Katango ni kuwa na uongozi bora ambao ungehakikisha kuwa kuna ugavi sawa wa rasilimali. Anasema:

Ehhh mara hii asali ya Pangoni lazima iwafaidi wote...(uk.28).

Kulingana na *Posa za Bikisiwa* (2008), Bikisiwa ana maono ya maslahi ya nchi yake kutunzwa. Lengo lake ni kupata mchumba atakayejali maslahi ya nchi yake kando na yake (uk.64). Babake anampendekezea Sogoramaneno pasi na kushauriana naye, mamake wala umma (uk.18). Bikisiwa anakataa Sogoramaneno (uk.60). Isitoshe, anakataa posa za wanaumme wengine. Mathalani, Baada ya Chachi (mmoja wa wanamume waposaji) kumpa zawadi anamwambia kuwa zawadi hazimhakikishii kitu (uk.50). Bikisiwa anataka uhusiano utakaoleta manufaa kwa kila mtu katika nchi yake.

Aidha, Bikisiwa ana maono ya kupata uhuru wa kujichagulia mchumba amatakaye:

Siku moja kila kitu kitabainika

Bikisiwa atakapokuwa huru

Kuchagua mume anayemtaka (uk.54).

Katika usemi huu, Bikisiwa anabainisha lengo alilokuwa nalo la kuwa huru kuchagua mchumba aliyemtaka bila kushurutishwa au kushawishiwa. Babake alikuwa amekubali posa kutoka kwa Sogoramaneno bila kushauriana na Bikisiwa wala mamake. Udenguzi hulenga kubaini maana mbalimbali zilizomo ndani mwa matini. Usemi huu wa Bikisiwa unaweza kuleta maana ya Bikisiwa kama mwanamke anayetaka uhuru wa kuchagua mume amtakaye au nchi inayotaka uhuru wa kuchagua uhusiano wa kimataifa bila kulazimishwa.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011), Kiongozi Mpya ana maono ya jamii iliyo na uhuru wa kusema. Aidha, ana maono ya katiba Mpya inayolinda na kutetea haki za wananchi. Bw. Naona anamwambia Bw. Binafsi kuwa wananchi wakiongozwa na Mpya wanataka katiba ya nchi ibadilishwe (uk.73). Isitoshe, Mpya ana maono ya jamii mpya ambapo wananchi wanalinda maslahi ya nchi yao. Kulingana naye, wananchi wa nchi yake hawajawajibika katika kulinda maslahi ya nchi yao ila wamethamini na kuendelea kusaidia kupatikana kwa maslahi ya nchi zingine (uk.73-74). Hii ina maana kuwa maono ya nchi hayajalengwa ipasavyo.

Aidha, Mpya ana maono ya kuhakikisha kuwa miundo-msingi muhimu imejengwa ili kuboresha Maisha ya wananchi. Miundo-msingi hii ni kama hospitali, shule na barabara (uk.74). Katika muktadha wa kisiasa kiongozi mzuri wa kisiasa ni yule anayehakikisha kuwa wananchi wamepata maendeleo haya.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2008) Mpya ana maono kuhusu utandawazi. Utandawazi ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali kama vile biashara, uchumi au siasa uliowezeshwa na maendeleo ya teknolojia ya habari yanayofanya mataifa kuwasiliana kwa urahisi (TUKI, 2004). Mpya anaunga mkono utandawazi ila anasisitiza kwamba sharti utandawazi uiletee nchi yake tija, si hasara pekee. Kulingana naye, wananchi walikuwa wakizalisha mali kisha tija ya uzalishaji huu inapelekwa katika nchi za ng'ambo huku wananchi wakiachwa bila chochote. Mpya analenga kuyakaba makampuni ya wawekezaji wa kutoka nje ya nchi kulipa ushuru namna inavyohitajika kwa misingi ya uhusiano wa kitandawazi (uk.74).

Ubinafsi ulikuwa umekithiri miongoni mwa viongozi nchini ambao walikuwa wakiiba mali ya umma na kwenda kuificha kwa mataifa ya nje. Mpya ana maono ya nchi mpya iliyo na usawa katika ugavi wa rasilimali. Anasema:

Tano tuzilinde rasilimali zetu zisisiibiwe kiho-lela. Tunataka nchi iwe yetu sote. Isiwe tena ya watu wachache wanaoiba mali ya nchi na kwenda kuikindika katika mataifa ya nje (uk.74).

Kwa mujibu wa Kigogo (2016) Tunu ni kigogo aliye na lengo na maono. Tunu, Sudi na Siti wanaenda kwa Mamapima ambapo shughuli ya ulevi inaendelea. Ngurumo na Mamapima wanajaribu kuwashawishi wanywe pombe. Mamapima anawaletea pombe iitwayo ‘spesheli’. Tunu anaikataa pombe hiyo (uk.57). Anajikita katika lengo lilomleta hapo la kuwashawishi wananchi kukutana Chapakazi kutetea kufunguliwa kwa soko (uk.59). Tendo hili ni dhahirisho la namna Tunu alivyolenga alichotaka na alivyokataa kuyumbishwa kutoka kwa azma yake.

Ngurumo anawaambia vijana kuwa kura yao watampa mzee Majoka. Tunu kusikia hivyo anasisitiza lengo lililomleta kwa Mamapima. Anasema:

Kama nilivyosema, mimi sikuja hapa kuomba kura. Nimekuja kuwaalika katika mkutano mkubwa utakaofanyika mbele ya lango kuu la soko la Chapakazi siku ya maadhimisho ya uhuru (uk.59).

Lengo la Tunu ni kuona soko la Chapakazi likifunguliwa. Ngurumo anapomwambia kuwa anasikia Tunu anataka kuwa kigogo wa Sagamoyo, Tunu anamjibu:

Tuyaache hayo. Soko la Chapakazi lifunguliwe kwanza, mengine ni ya baadaye! (uk.58).

Katika malumbano baina ya Sudi na Ngurumo, Tunu anamkumbusha Sudi kuwa hawafai kupoteza lengo lililowapeleka huko kwa Mamapima (uk.64). Aidha Tunu ana maono ya kuleta wachunguzi kutoka nje ya nchi kuchunguza upya ajali ya Jabali aliyeuawa na Kenga kwa ushirikiano wa Majoka (uk.35).

Kwa kurejelea msingi wa muktadha katika nadharia ya udenguzi, mhakiki anaweza kuibua maana mbalimbali ndani mwa matini kwa kuchunguza miktadha iliyopo (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika, lengo kuu la mwanamke lilikuwa kumfurahisha mwanamume (Hora, 2014). Mugambi (1982) katika utafiti wake anaibua madai kuwa mwanamke hana nafasi ya kushiriki katika siasa bali jukumu lake kuu ni kuwahimili wanaumme.

Keter (2013) anasema kuwa mwanamke katika tamthilia ya *Natala* (1997) amechorwa kama mtegemezi wa mwanamme na chombo cha kumfurahisha mwanamme. Kwa kuchunguza matini, mhakiki kwa misingi ya udenguzi huibua maana mpya ambayo yaweza kutofautiana na maana ya awali (Derrida 1973; Miller, 1976). Taswira ya mwanamke kama kiongozi mwenye lengo na maono inayobainika katika tamthilia teule ni tofauti na taswira ya mwanamke iliyobainika kupitia utafiti wa Mugambi (1982) na Keter (2013). Lengo na maono ya mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia teule za Kiswahili ni kuleta mabadiliko ya kiuongozi katika jamii yake.

4.2.11 Mwanamke kama Kiongozi Msomi

Kupitia tamthilia ya *Pango* (2003), Katango amesoma (uk.51). Ameelimika na kuwa mwalimu. Kikubi anakiri kusoma na Katango:

Nimesoma naye...(uk.25).

Kwa mujibu wa *Posa za Bikisiwa* (2008) mwanamke Bikisiwa amesoma. Mtambaji anasema kuwa binti mfalme (Bikisiwa) alikuwa msomi (uk.13). Kando na Bikisiwa kuwa msomi, ni msomaji. Amesoma vitabu kama *East Africa Through a Thousand Years* cha Gideon Were na *Marriages of Convenience* cha Bwana Sasa Bongokali (uk.16-17). Vitabu hivi vinasisitiza thamani ya bara la Afrika na umuhimu wa kuwepo na mahusiano ya kimataifa yanayoleta faida kwa bara la Afrika.

Kiongozi wa jinsia ya kike katika tamthilia ya *Kigogo* (2016) amelimika. Tunu amesoma na kufikia upeo wa juu masomoni. Amesoma uanasheria. Ana shahada ya uzamifu ndio maana anaitwa daktari. Tunu aliisomea shahada hii ya juu ughaibuni (uk.32).

Muktadha kama msingi mojawapo wa nadharia ya udenguzi hushikilia kuwa ili mchanganuzi aelewe maana ndani mwa matini ni sharti aelewe miktadha iliyopo (Fairclough, 1992; Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa kitamaduni, mwanamke hakupewa haki na nafasi ya kusoma kutokana na mtazamo wa kitamaduni kuwa hatima ya maisha ya mwanamke ilikuwa kuolewa na kwamba wanawake wafaa kuthibitiwa kufanya kazi za nyumba (Ruto, 2012; Hazelzet, 2013). Kwa mujibu wa Mapunjo (2014), baadhi ya jamii zetu zinamwona mwanamke kama kiumbe dhaifu asiyefaa kupelekwa shule. Kwa maoni ya Miller (1976), mhakiki anayetumia udenguzi

kuhakiki matini huibua maana mpya ambayo huenda ikatofautiana au ikafanana na maana ya awali. Taswira ya mwanamke kama kiongozi aliyesoma inayobainika katika utafiti huu ni tofauti na taswira iliyoibuliwa katika tafiti za Ruto (2012) na Hazelzet (2013).

Nadharia ya udenguzi husisitiza uchunguzi wa kina wa matini ili kutambua utata, mwachano, kinaya, unyume au ukinzani uliomo ambao unachangia kubainisha maana (Mishra, 2018). Mhusika mwanamke katika tamthilia teule za utafiti huu amesawiriwa kama kiongozi aliyeelimika. Hata hivyo, kwa kuchunguza tamthilia hizi kwa undani, utafiti huu umebaini mwachano kati ya tamthilia ya *Kigogo* (2016) na tamthilia zingine rejelewa. Kwa mujibu wa *Pango* (2003), Katango amesomea ualimu (uk.51). Katika *Posa za Bikisiwa* (2008) tunaelezwa tu kupitia kwa usemi wa Mtambaji kuwa Bikisiwa alikuwa binti aliyesoma. Hatuelezwi upeo wa elimu hii. Ingawa kiongozi Mpya katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) ni mwerevu kutokana na elimu aliyopata (uk.29-30), kiwango chake cha elimu hakibainiki. Kenga anapomwuliza Majoka: Huyu Daktari Tunu ni daktari wa nini hasa? Majoka anamweleza kuwa Tunu amesomea sheria (uk.32). Tunu ana shahada ya uzamifu katika Sheria. Tamthilia hii ndiyo ya pekee kati ya tamthilia teule za utafiti huu ambayo imemchora mwanamke kama kiongozi aliyefikia upeo wa juu wa kielimu.

4.2.12 Mwanamke kama Kiongozi Mlumbi

Kwa mujibu wa Mdee, Njogu & Shafi (2011) ulumbi ni uhodari wa kuzungumza kwa ufasaha. Mlumbi ni mtu aliye na ufasaha wa kuzungumza. Mwanamke katika tamthilia za tangia mwaka wa 2000 amechorwa kama kiongozi anayewasilisha mawazo yake kupitia kwa lugha fasaha.

Katika *Pango* (2003), kiongozi Katango ni mlumbi. Susa anapotoka Pangoni, anamletea babu yake habari kuwa Katango amefanyika bubu. Babu kupitia kwa swali la balagha anaonyesha mshangao wake kwani Katango alikuwa msemaji hodari na fasaha. Babu anasema:

Iweje Katango asiongee na ni mlumbi maarufu kijijini? Iweje kuwa haongei na ni bingwa wa kuyasanifu maneno? Iweje? (uk.69).

Kulingana na *Posa za Bikisiwa* (2008), SS anamwambia Bikisiwa:

Aaa, Bikisiwa wewe ni bingwa wa lugha (uk.38).

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011), Mpya anawahutubia wananchi kwa ufasaha jambo linalowafanya wananchi kumpenda, kumfuata na kumsheherekea Mpya (uk.72-75).

Katika *Kigogo* (2016), Tunu alipowahutubia wananchi katika lango la Chapakazi alifanya hivyo kwa ufasaha. Mathalani, anawaambia wananchi:

Hii ndiyo maana halisi ya uhuru wetu. Uhuru wa kutangamana. Uhuru wa kutendewa haki yetu. Uhuru wa kufunguliwa soko letu... (uk.89).

Kiango (1992) alpohakiki tamthilia za Kiswahili za Kenya alidai kuwa mwanamke ameumbwa kama mtu anayeendeleza maudhui mabaya kwa kusawiriwa kama mtu mzinifu, mbaya, muuaji mwaviaji mimba na mtu asiye na mwelekeo thabiti. Mugambi (1982) alpohakiki tamthilia nchini Kenya kati ya 1957 hadi 1981 alihitimisha kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni. Kwa kuhakiki tamthilia za *Kifo Kisimani* (1981) na Natala (1997), Keter (2013) alidai kuwa mwanamke amechorwa kama kiumbe duni asiyeweza kumiliki chochote, chombo cha kumfurahisha mwanamume, mwovu, mgomvi, mtegemezi wa mwanamume, barakala, asiyestahili heshima, mwenye hasira za mkizi na mtu anayedanganywa kwa urahisi. Utafiti huu umebaini kuwa mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia teule za kuanzia mwaka wa 2000 hadi 2016 amesawiriwa kwa njia chanya kinyume na tafiti za awali zilizomsawiri kwa njia hasi.

4.3 Mitindo ya Lugha Inayojenga Taswira ya Mwanamke Kiongozi

Sehemu hii inashughlika mitindo mbalimbali ya lugha katika tamthilia teule ambayo inajenga taswira ya mwanamke kiongozi. Tamthilia teule za utafiti huu zimesomwa huku mitindo mbalimbali inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi ikinukuliwa katika daftari kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi. Mitazamo mbalimbali ya wahusika pamoja na taswira ya mwanamke kiongozi imebuliwa kutokana na mitindo hii na kunukuliwa. Aidha, mitindo hii ya lugha imepangwa kwa mujibu wa kila tamthilia na kuchanganuliwa kupitia njia ya uchanganuzi wa yaliyomo. Baadaye, mitindo hii imeweza kuwasilishwa kupitia njia ya maelezo na matokeo kufasiriwa.

4.3.1 Takriri

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo kwayo maneno, sauti, wazo au vifungu fulani katika kazi ya fasihi hurudiwa (Senkoro, 1982; Ntaragwi, 2004). Kwa mujibu wa Wamitila (2003) takriri husisitiza na kushadidia ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo huo.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) Bikisiwa anatumia mbinu hii katika mazungumzo yake. Babake Bikisiwa anakubali Sogoramaneno ampose bintiye (Bikisiwa) bila hiari ya Bikisiwa. Sogoramaneno anamdhalilisha Bikisiwa hata kabla ya ndoa. Hamshirikishi katika kufanya maamuzi. Hili linabainika Bikisiwa anaposema:

Bado sijesha baba. Wacha niseme. Wacha nitoe dukuduku langu. Mwenzangu kamwe hanijali wala hanibali... Kila shauri lazima akate yeye. Chumo lote kwa nguvu atwae yeye...Imefika hadi sasa husema chake ni chake tu, na changu ni chetu sote kama hatakigeuza chake peke yake pia... (uk.22).

Kwa maoni ya Mishra (2018) nadharia ya udenguzi hulenga kuibua maana mbalimbali ndani mwa matini kupitia uchunguzi wa kina wa matini. Inaweza kuchukuliwa kuwa Bikisiwa anarejelea ndoa kati yake na Sogoramaneno ambayo imejaa udhalimu au uhusiano wa kibiashara, kijamii ama kisiasa kati ya nchi ya Bikisiwa na nchi nyingine ambao ni wa kidhalimu. Uradidi wa neno ‘wacha’ katika usemi huu wa Bikisiwa unatupa picha ya mwanamke aliye na machungu moyoni kama kutomjali, kutomshirikisha katika maamuzi muhimu, kudharauliwa na kuonewa kiuchumi Machungu haya yanaonyesha udhalilishaji wa mwanamke katika muktadha wa utamaduni wa nchi ya Bikisiwa. Uelewa wa muktadha kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu ni jambo la mtikati kwa mhakiki wa matini kwani uelewa huu husaidia kuelewa maana (Ntaragwi, 2004). Ni katika muktadha huu wa utamaduni wa nchi ya Bikisiwa ambapo Bikisiwa anajitokeza kutetea haki yake ya kumchagua mchumba kupitia takriri katika usemi huu. Kupitia takriri hii Bikisiwa anasawirika kama mtetezi wa haki yake ya kumchagua mchumba amtakaye.

Aidha Bikisiwa anatumia takriri anaposema:

Ingawa niliingizwa katika uchumba wake kwa nguvu. Tena na wazazi wangu...Lakini hayo...Ni ya zamani...Lakini hayo ya zamani...Lakini hayo ni ya zamani... (uk.60).

Kwa kurudia maneno: lakini hayo ni ya zamani, Bikisiwa anasisitiza msimamo wake kuwa katu hawezi kuolewa kwa Sogoramaneno. Uradidi huu unamchora kama mwenye msimamo thabiti.

Bikisiwa anajisawiri kama kiongozi mkakamavu, jasiri na msema wazi kupitia kwa urudiaji wa maneno ifuatavyo:

Eeh wewe...Angalia wewe...Na wewe ...Fumbua macho uone vyema. Wewe! Hii si dunia ya kulala. Si dunia ya mahubiri na maombolezo. Hii ni dunia ya unyang'anyi. Ni dunia ya ukavu (uk.1).

Wewe! Na wewe! ... Na wewe! (uk.1).

Mnataka, mnataka mnataka kila kitu changu... (uk.2)

Tokeni uwanjani. Tokeni kizani. Tokeni simameni peupe, Tokeni upenuni (uk.2).

Mbinu ya takriri inabainika vilevile Bikisiwa anaposema:

Ukweli ni kwamba hapa petu kwa mujibu wa katiba na mila zetu, hafukuzwi mgeni.

Unaweza kukaa. Unaweza kuhamia. Unaweza kuolewa...lakini huwezi kunioa

Mimi...Mimi

sitaki kuolewa na wewe. Mimi sikupendi (uk.32).

Mhimili wa lugha katika nadharia ya udenguzi hushikilia kwamba maana mbalimbali zaweza kuibuliwa kutokana na maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini fulani (Bakhtin, 1981). Uradidi wa maneno: unaweza na mimi katika usemi huu wa Bikisiwa unasisitiza ubayana wa Bikisiwa kuwa Hassan anaweza kufanya lolote katika nchi yao lakini katu hawezi kumwoa yeye. Picha ya Bikisiwa inayobainika kupitia uradidi huu ni ya kiongozi msema kweli kwa uwazi na mwenye msimamo thabiti. Kwa uwazi anamweleza Hassan kuwa hampendi na kushikilia msimamo wake kuwa katu hawezi kumwoa.

Sogoramaneno amjiapo Bikisiwa ili kutaka posa, anaanza kumpongeza kwa kurudia neno 'hongera':

Hongera kimwana...Hongera binti mzuri...Hongera sana hongera (uk.55).

Bikisiwa anamjibu kwa takriri pia:

Hongera...hongera...Hongera za nini? (uk.55).

Mwanamke Bikisiwa kupitia uradidi huu amechorwa katika muktadha huu kama kiongozi anayepewa heshima. Hata hivyo uradidi wa neno hongera katika usemi wa Bikisiwa unaonyesha

namna heshima hii haikuwa na udhati wa moyo. Kwa kurejelea mhimili wa lugha katika nadharia ya udenguzi, maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini husheheni maana mbalimbali. Maana hizi zaweza kutofautiana au kufanana (Derrida, 1973; Miller, 1976).

Taswira hii vilevile inabainika kupitia mbinu ya takriri ambapo Hassan anamsifia Bikisiwa kwa kurudia neno malkia:

Mwenye jamala na haiba. Malkia wa ulimwengu wote. Malkia wa moyo na ndoto zangu (uk. 30-31).

Kupitia mbinu ya takriri, Bikisiwa anasema:

Si vibaya kuposana iwapo posa ni yenye nia njema. Si vibaya kuoana iwapo ndoa ni ya kuheshimiana (uk.2).

Mung'atha (2012) alipotumia nadharia ya udenguzi alisema kuwa vipengele vya lugha hutumiwa na mwandishi kufumba ujumbe wa mwandishi. Kulingana naye mhakiki anayetumia nadharia ya udenguzi hulenga kuchunguza vipengele hivi ili kuibua maana mbalimbali ambazo huwa zimefichama ndani mwa matini husika. Kwa kuchunguza maneno 'si vibaya' ambayo yamerudiwa katika usemi huu wa Bikisiwa maana mbili zaweza kuibuliwa. Moja ni kuwa Bikisiwa alikataa posa. Pili ni kuwa Bikisiwa hakukataa posa ila alisisitiza kuwa posa yenyewe lazima iwafaidi wananchi. Maana hizi mbili zinamchora Bikisiwa kama mwenye msimamo thabiti.

Chachi vilevile anamjia Bikisiwa na zawadi kochokocho na maneno matamu na kumwomba apokee hidaya hizo:

Pokea hii pete ya dhahabu. Pokea pia huu huu mkufu wa dhahabu. Pokea na hiki kidani cha dhahabu. Pokea huu ushanga wa dhahabu. Kwangu mimi vitu si vitu, nitakupa vyote kwani wewe ndiye nuru yangu, ndiye malkia wangu, ndiye mpenzi wangu (uk.50).

Kwa kurejelea nadharia ya udenguzi, maneno hubeba maana (Miller, 1976). Uradidi wa maneno: dhahabu, pokea na ndiye una umuhimu. Dhahabu ni chuma kilicho na thamani kuu duniani kote. Takriri ya neno 'pokea' inaonyesha namna Chachi anavyomsihi Bikisiwa kwa heshima akubali kupokea zawadi yenye thamani kuu. Kwa kurudia maneno haya picha ya mwanamke kama kiongozi anayeheshimiwa inajengeka.

Bikisiwa anajitokeza kama mpenda jamii wakati anapowaahidi wananchi kumtambulisha mchumba kwao kabla ya kumkubali. Takriri ifuatayo inadhihirisha hili:

Naaahidi...Naahidi...Naahidi (uk. 64).

Upendo huu kwa jamii yake ndio umfanyao Bikisiwa kuahidi na kujitolea kuwalinda wananchi:

Nitakulindeni...Nitakulindeni...Nitalindeni kwa kujilinda mwenyewe (uk.68).

Kwa kurejelea nadharia ya udenguzi, matini husheheni zaidi ya maana moja. Kwa Bikisiwa kuwaambia wananchi kuwa atawalinda kwa kujilinda mwenyewe, tunaweza kumwona kama mtu anayejiipenda. Hata hivyo, uradidi wa neno: nitakulindeni unasisitiza kuwa Bikisiwa alikuwa kiongozi aliyependa jamii.

Isitoshe, pindi Bikisiwa anaporuhusiwa na mamake kuingia kwa nyumba yao, anawasabahi wazazi wote wawili kitofauti:

Shikamoo mama. Shikamoo baba (uk.15).

Kulingana na TUKI (2004), shikamoo ni salamu ya heshima itolewayo kwa mtu aliyekuzidi umri. Hivyo basi, kwa kutumia neno hili ina maana kuwa Bikisiwa aliwaheshimu wazazi wake. Uradidi wa neno hili unadhihirisha kuwa Bikisiwa aliwaheshimu wazazi wake wote bila ubaguzi na unamchora kama mwenye heshima.

Katika tamthilia hii, sauti ya mwanamume anayeaminika kuwa ni Sogoramaneno inamdunisha Bikisiwa bila kuzingatia kuwa huyu ni mwanamke kiongozi tena aliyesoma:

Eeee we Bikisiwa. Ewe mwanamke. Sikiliza maneno yangu ili upulike. Mwanamke ni mwanamke tu. Uko chini yangu. Hata uwe kisiwa. Hata uwe bahari. Hata uwe bara la nchi kavu na majabali ya milima...(uk.19).

Takriri ya maneno: mwanamke na hata katika Sauti hii inasisitiza kuwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii ya Bikisiwa, mwanamke hata aliyekuwa na elimu alidunishwa. Mtazamo huu unashikiliwa na baadhi ya wanaume katika jamii ya Bikisiwa na unawakilishwa kwa Sauti hii. Nadharia ya udenguzi hushikilia kuwa mitazamo huwa muhimu katika kubaini maana ndani mwa matini. Kulingana na mtazamo huu mwanamke hata akiwa amefikia upeo wa juu katika masuala ya uongozi, elimu na mengineyo bado ni kiumbe duni. Licha ya mitazamo huu,

Bikisiwa anajitahidi kuleta mabadiliko na maendeleo katika nchi yake. Jambo hili linamsawiri kama kiongozi mkakamavu.

Kupitia tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) tunaona namna Bw. Binafsi anawakaripia Mpya na mamake. Katika makaripio haya, uwazi wa usemi wa Mpya unabainika:

Tumechoka. Hivi hukubaini siku zote hizi? Hukubaini kama tumechoka ...uk.42.

Kwa kutumia uradidi wa neno ‘tumechoka’, Mpya anamsisitizia babake kwa uwazi ukweli kuwa yeye, mamake, Zanga na Mussa walikuwa wamevumilia vya kutosha ila yeye Bw. Binafsi hakugundua hilo. Mbinu hii inamsawiri Mpya kama kiongozi msema kweli.

Umma unamsifu Mpya kwa juhudi zake za kuzungumzia na kupinga uongozi mbaya wa Binafsi:

Sauti yako inatueleza tunayooyajua. Sauti yako ni sauti yetu kwani wewe ni sisi na sisi ni wewe. Wewe na kaka zako mmefukuzwa nyumbani, lakini nyinyi mna nyumba zote za nchi hii-mnakaribishwa, karibuni (uk.75).

Kwa kurejelea takriri katika usemi huu, maneno: wewe ni sisi na sisi ni wewe yanaonekana kukinzana ukiyatazama kijuujuu. Kwa mujibu wa Mishra (2018), udenguzi huchunguza ukinzani, unyume, kinaya au utata ndani mwa matini ili kuibua maana mbalimbali. Uchunguzi wa usemi huu unaibua maana kuwa Mpya na wananchi wana mtazamo mmoja kuhusu matatizo yanayokumba nchi yao. Uradidi wa maneno: sauti yako, sisi na wewe yanasisitiza namna Mpya alivyowashawishi wananchi kupitia matendo na maneno yake hadi wakampenda na kumsifu. Takriri hizi zinamsawiri Mpya kama kiongozi mshawishi.

Picha ya mwanamke Mpya kama kiongozi mzalendo inajitokeza katika Sauti Ndani ya Kisima inayosifu tendo la Mpya la kujitokeza kwa ujasiri kupigania mabadiliko nchini. Inatumia uradidi wa maneno ‘ishara njema’ na ‘njoo’ kusisitiza hili:

*Ishara njema...Ishara njema...Ishara njema...Njema, njema njema, ishara njema.
Tulikutaraji. Sasa wakati umeshafika. Njoo uliyekuwa ukitarajiwa. Njoo uliyengojewa.
Njoo, njoo, njoo...njoo polepole, njoo kwa uhakika, njoo tukunyweshe maji ya ujasiri
(uk.21).*

Uradidi wa maneno ‘hatutaki fujo’ katika semi zifuatazo za Mpya unadhihirisha busara yake:

Kimya, wananchi kimya. Hatutaki fujo. Fujo ndiyo itakayotuharibia mambo (uk.61).

Hatutaki fujo lakini...Sisi hatutaki fujo. Hatutaki fujo (uk.72).

Uongozi wa Bw. Binafsi unapoonekana kufikia ukingoni, Mpya anawaambia wananchi:

Taifa lazima likogeshwe (uk.80)

Taifa lazima litakaswe (uk.80).

Takriri katika usemi huu wa Mpya unamsawiri Mpya kama kiongozi mwenye lengo na maono. Mpya alikuwa na maono kuwa maovu yaliyotawala taifa mathalani ufnasadi, ubinafsi, ukosefu wa usawa na njaa yafaa kuondolewa kabisa.

Mpya anauliza hadhira pamoja na Kulia na Kushoto:

Kwa nini wanapeana migongo? Kwa nini wanasuguana migongo? Kwa nini wanachagua pande tofauti kabla ya kujali taifa? Kwa nini hawasimami pamoja ingawa wana Misimamo tofauti? (uk.21-22).

Takriri ya maneno: kwa nini na migongo inaonyesha uchungu aliokuwa nao Mpya kwa sababu ya utengano uliokuwepo nchini. Anadadisi hali hii kwa lengo la kusisitiza umuhimu wa umoja katika vita vya ukombozi. Udenguzi huchunguza maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini kwa kuwa maana hufumbwa ndani mwa matini hayo (Mung'atha, 2012). Kwa mujibu wa Mdee, Njogu & Shafi (2011), mgongo ni sehemu ya nyuma ya mwili wa binadamu kati ya nyuma ya mwili shingo na kiuno. Uradidi wa neno migongo unaonyesha utengano uliokuwepo kati ya Kulia na Kushoto ambao wametumiwa na mwandishi kama viwakilishi vya wananchi. Takriri katika usemi huu inamsawiri Mpya kama kiongozi mzalendo ambaye anawatangamanisha wanajamii ili kuleta mageuzi ya kiuongozi.

Mpya anasawiriwa kama kiongozi mdadisi. Anadadisi hali iliyokuwepo nchini kwamba hakukuwa na uhuru wa kusema. Aidha, anadadisi hali kuwa mtoto wa nyumba kuu katika nchi hiyo hakuruhusiwa kujiingiza katika siasa za kupigania mabadiliko. Hili linabainika kupitia kwa mbinu ya takriri ambapo Mpya anarudia maneno: kwa nini ifuatavyo:

Kwa nini kila siku tungojee? Tungojee, tungojee mpaka lini? Kula, kulala, kuamka, kubaki ndani, kutoka nje, kwenda na kurudi, kwenda haja kubwa na ndogo, kuuza na kununua...na, na, na...kila kitu! Kwa nini?

Mpya anasema:

Niko njiani wahenga. Hatua kwa hatua. Niko njiani (uk.21).

Tazameni, tazameni enyi walimwengu.

Tazameni wana wa nchi hii.

Tazameni watoto, wajukuu, vitukuu, virembwe, virembwekeza na vinying'ina

Tazameni vijana na wazee. Tazameni...Tazameni wanawake na wanaumme (uk.23).

Takriri ya maneno: niko njiani na hatua inamsari Mpya kama kiongozi jasiri anayejitokeza kuleta mageuzi ya kiuongozi nchini mwake. Aidha, uradidi wa neno tazameni unatumiwa kusesitiza kuwa kulikuwa na makundi mbalimbali katika jamii ya Mpya. Takriri hii inamsawiri Mpya kama kiongozi mshawishi kwa kuwa Mpya anazungumza na makundi haya ili kuyashawishi kupigania uongozi bora. Njogu & Chimera (1999) wanasema kuwa taswira hutokana na maneno yaliyotumiwa katika kazi ya fasihi.

Sauti inapomwuliza Mpya yeye ni nani na kujaribu kumtambua kama mtoto wa Bw. Binafsi na Bi Shoo na mwanamke ambaye daima hawezi kuongoza, Mpya anajitambua kwa kusema:

Mimi mwananchi. Mimi mzalendo, mimi mkereketwa (uk.28).

Takriri ya neno 'mimi' inadhihirisha kuwa Mpya alijitambua na kujijua yeye mwenyewe kuwa kando ya yeye kuzaliwa katika nyumba kuu alikuwa mwananchi aliyefaa kuipigania nchi yake kwa sababu ya hisia za kizalendo alizokuwa nazo. Picha ya mwanamke kiongozi kama mtu mzalendo inabainika hapa.

Isitoshe, Mpya anasema:

Lazima mmoja wetu aanze. Lazima mmoja wetu ajitolee. Lazima mtu mmoja ajitolee mhanga (uk.21).

Maneno kwa mujibu wa udenguzi husheheni maana (Miller, 1976). Takriri ya neno 'lazima' ni ishara kuwa haikuwa rahisi kwa Mpya kujitokeza. Hali mbaya ya nchi ndiyo iliyomlazimu. Tendo la Mpya kujitokeza linamsawiri kama kiongozi mzalendo kwa kuwa linadhihirisha mapenzi aliyokuwa nayo kwa nchi yake hivi kwamba yu tayari kuifia.

Kulingana naye Kushoto na Kulia japo wana kauli zisizoafikiana wanafaa kuungana kwanza. Lengo la Mpya maishani ni nchi yake. Anaipenda nchi yake kiasi cha kujitolea kuipigania. Kwa kurejelea Kushoto na Kushoto Mpya anasema:

Tazameni mbele. Shabaha iwe nchi. Shabaha isiwe nafsi za mtu mmoja mmoja. Lengo liwe kuhifadhi na kuitunza nchi. (uk.22).

Katika usemi huu wa Mpya, takriri ya neno ‘shabaha’ na ‘nchi’ inasisitiza kuwa kiongozi bora afaa aweke maslahi ya nchi mbele ya maslahi yake mwenyewe. Asiwe mbinafsi kama Bw. Binafsi. Mpya ni mzalendo.

Katika tamthilia ya *Kigogo* (2016) Ashua anamwambia Sudi:

Kila kitu ni Tunu. Tunu, Tunu, Tunu (uk.48).

Mbinu ya takriri iliyotumiwa katika usemi huu ambapo neno ‘Tunu’ limerudiwa inasisitiza mtazamo wa Ashua kuwa Tunu ni mpenziwe Sudi. Matazamo kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi huwezesha uibuaji wa maana ndani mwa matini (Ntaragwi, 2004). Kutokana na mtazamo huu wa Ashua, Tunu anasawiriwa kama kiongozi mkakamavu ambaye anavumilia na kukiuka singizio (kuwa ana ushirikiano wa kimapenzi na mshirika wake wa kisiasa aitwaye Sudi) na kuendeleza juhudi za kuleta mabadiliko ya kiuongozi Sagamoyo.

Upendo wa Tunu kwa jamii yake unadhihirika kutokana na maneno yake kwa Sudi:

Jukumu la kulinda uhai. Kulinda haki. Kulinda uhuru (uk.18).

Tunu anazungumza maneno haya akimshauri Sudi aliyekuwa karibu kukata tamaa. Anamshauri waendeleo kupigania uongozi bora. Kwa kurudia neno ‘kulinda’ picha ya Tunu kama kiongozi mwenye lengo na maono inabainika. Tunu analenga kulinda uhai, haki na uhuru Sagamoyo.

Kila mara Tunu anamwita mamake kwa jina ‘mama’. Uradidi wa neno hili katika tamthilia ya *Kigogo* (2016) unamsawiri mwanamke huyu kama mwenye heshima:

Ma...ni ndoto. Mzee Marara (uk.53).

Mama, nisimulie kisa haraka ninataka kwenda (uk 55).

Mama, nitakwenda...Nisimulie kisa (uk.55)

Kwani walia mama? Yaishe basi! (uk.55).

Mama, nipeleke bafuni (uk.56).

Licha ya kuwa Tunu ni kiongozi anayefuatwa na wananchi wengi, bado anamheshimu mama mzazi. Aidha, Tunu anapozungumza na wananchi wa jimbo la Sagamoyo, wanamsheherekea kupitia kwa takriri:

...Tunu tosha! Tunu...uu! Tunu...uu! (uk.89).

Tunu juuuu! Tunu...uuu! Tunu...uuu! (uk.90).

Uradidi wa neno Tunu unadhihirisha namna wananchi walikuwa wameshawishika kupitia kwa matendo na maneno ya Tunu na kumfuata. Uradidi huu unaonyesha msimamo waliokuwa nao wananchi kwa kiongozi mwanamke Tunu na kumsawiri kama kiongozi mshawishi.

Kwa kurejelea *Pango* (2003) kiongozi Katango anajisawiri kama kiongozi mkakamavu na mwenye msimamo thabiti kupitia kwa kurudia maneno ‘la’ na ‘siachi’ katika jibu lake kwa mamake aliyemtaka aache kumpinga Ngwese katika uwaniaji wa uongozi wa Pango:

La! Mama La! Siachi kabisa siachi! (uk.34).

Lugha ya mwanamke Katango katika usemi huu inamsawiri kama kiongozi mkakamavu na mwenye msimamo thabiti. Hii inatokana na hali kwamba Katango anayanena maneno haya baada ya kuvamiwa njiani na Mtu I na II.

Ngwese anampoka Katango uongozi kifisadi. Baada ya tukio hili, Katango anasema kwa uchungu wakati anabaki pekee yake:

Lakini siachi katu siachi

Kulistahi pango siachi

Ndoto yangu na kizazi changu siachi, siachi!!! (uk.49).

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) Mbinu ya takriri hutumiwa kusesitiza jambo fulani. Uradidi wa neno ‘siachi’ katika dondoo hili unasisitiza ukakamavu wa Katango wa kuendelea na lengo lake la kutaka kuongoza pango. Kupitia takriri hii Katango amesawiriwa kama kiongozi mkakamavu.

Ngwese anadai kuwa wivu ndio unaomchochea Katango kumpinga katika kugombea uongozi wa Pango. Wivu huu kulingana naye Katango aliurithi kutoka kwa wazazi wake ambao walimwonea wivu babu yake (Ngwese) aliyetaka kuwa chifu. Katango anamwambia:

La! La! La! Usipoteshe ukweli. Hamna aliyemlilia ngoa kabisa. Unasikia? Hamna (uk.13).

Dhima ya takriri kwa mujibu wa Murungi (2011) ni kuleta msisitizo. Katika usemi huu, Katango anarudia maneno: la na hamna kusisitiza ukweli kuwa babu yake Ngwese alikuwa kibarakala wa wakoloni na kukosoa uongo wa Ngwese kwamba wazee wa Katango walimfanya asichaguliwe chifu. Uradidi huu unamsawiri Katango kama msema kweli hata kama ni mchungu.

Kibwana anasifu ushujaa wa Katango:

Shujaa wetu Katango.... Katango.... Katango... (uk.45).

Neno Katango linarudiwa katika usemi huu kusheherekea Katango kama kiongozi shupavu. Hili linamsawiri Katango kama kiongozi anayeheshimiwa. Taswira hii vilevile inasawiriwa wakati kundi zima la Wanapango (si vijana pekee kama ilivyokuwa awali) wanamsifu na kumsheherekea kupitia urudiaji wa maneno:

Aiwa! Aiwa! Aiwa! (uk.86).

Katango oyee! Katango oyee! Katango oyee! (uk.86).

4.3.2 Maswali ya balagha

Maswali ya balagha ni maswali ambayo hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ambayo hayahitaji majibu (Wamitila, 2003). Kwa maoni ya Nyamari (2013) jibu la swali la balagha huwa akilini mwa anayeulizwa au anayesoma kazi husika au huwa tayari analijua. Maswali ya balagha huwa na dhima ya kutoa mawazo au hisia za ndani za mhusika au kuweka jambo fulani wazi kwa hadhira (Murungi, 2013; Nyamari, 2013). Aidha, hulenga kusisitiza usemi fulani na kuwasilisha maudhui (Nyuta, 2016).

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) mwanamke ambaye anaaminika kuwa Bikisiwa anauliza:

Ni nani nyinyi mnaotafuta ushuba wangu bila kujali hisia zangu? Tuseme nyinyi ni walewale mnaotaka kuudhibiti mwili wangu... Mnachungulia nini ndani ya sura yangu? Mnatazama nini ndani ya mwili wangu. Mnataka nini ndani ya maisha yangu? Nini mnataka enhe? Mnataka, mnataka, mnataka kila kitu changu, lakini kwa nini hamtaki kujali pande zote zinazohusika katika maisha yenu na yangu? (uk.2).

Kwa nini mnanitazama kwa mbali kifichoni. Kwa nini mnajificha kizani (uk.2).

...lakini kwa nini hamtaki kujali pande zote zinazohusika katika maisha yenu na yangu? (uk.2).

Ni nani nyinyi mnaochungulia kwa siri? Ni nani nyinyi mnaojijaza tele uchu kwa kutazama pembeni pembeni ujanajike wangu? (uk.3).

Mugambi (1982) katika uhakiki wake wa tamthilia zilizochapishwa kati ya 1957-1981 alisema kuwa wanawake wamesawiriwa kama viumbe wa kuchukua maagizo kutoka kwa wanaumme bila ukinzani wala kuuliza maswali. Bikisiwa anadengua taswira hii kwa kuwadadisi wanaumme waposaji waliomjia ili kujua nia yao. Maswali haya yanamsawiri Bikisiwa kama kiongozi msaema wazi.

Bikisiwa anamsaili Sogoramaneno:

Umetoka huko kuja kuniambia upuuzi huu? (uk.55).

Katika usemi huu Sogoramaneno anamtaka Bikisiwa amruhusu asheherekee ushindi wake (wa Bikisiwa). Bikisiwa kupitia kwa swali balagha anamwambia waziwazi kuwa huu ni upuuzi.

Sogoramaneno anapojitokeza na kumwambia Bikisiwa kuwa ana haki ya kumpiga na kumbeba hadi nyumbani kwake ikiwa atakataa kuolewa naye, Bikisiwa kupitia kwa swali balagha anamwuliza:

...tuko katika karne gani Bwana Sogoramaneno? (uk.58).

Kwa mujibu wa udenguzi, maana mbalimbali zawez kuibuliwa ndani mwa matini (Bakhtin, 1981). Maana ya kwanza ni kuwa Bikisiwa anamkumbusha Sogoramaneno kuwa katika karne hii ya 21 ndoa ya lazima ni jambo lisilokubalika. Maana ya pili ni kuwa katika karne hii ya 21 taifa haliwezi kulazimishiwa uhusiano wa kimataifa kutioka nchi nyingine namna hali ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Bikisiwa kupitia usemi huu anajitokeza kama mwanamke jasiri na mtetezi wa haki zake na za wanawake wenzake.

Biss anapomjia Bikisiwa na kuanza kusifia urembo wake, Bikisiwa anamwuliza yeye ni nani. Biss anapomwambia kuwa yeye ni wa kabila takatifu, kiongozi Bikisiwa anamdadisi:

Kabila lipi si takatifu nikuulize? Hiyo pekee yake inaashiria nia yako njema, au siyo? (uk.43).

Kulingana na Mishra (2018), nadharia ya udenguzi huchunguza namna kinaya, kejeli, utata, unyume, mwachano au ukinzani ndani mwa matini unavyochangia kujenga maana. Kejeli inatokea wakati Bikisiwa anapotumia maneno yaliyotumiwa na Biss: nia njema kumkejeli Biss na kumwonyesha kuwa alikuwa mwongo. Bikisiwa alikuwa ameshatambua kutokana na usemi wa Biss kuwa alikuwa mbinafsi. Badala ya kumwambia bayana kuwa hakuwa na nia njema, Bikisiwa anaamua kutumia kejeli. Usemi huu unasawiri kama kiongozi mwenye busara.

Bikisiwa hakomei hapo na udadisi wake. Anaendelea kumsaili ili kujua hulka yake vyema:

Mbona una haraka hivyo? Unaogopa wenzako watakuwahi au unaogopa kuinyima shauku na utashi wako? Unahofu nini? (uk.44).

Mbona maneno yako yananitisha? Mbona maneno makali namna hiyo? Mbona yana sumu kali? Wewe umekuja kuposa au kuninunua na kunipora? Wewe ni mlowezi au mwindaji haramu? Au mtawala mtumia nguvu? Ni mgeni au u haramia? (uk.44).

Udadisi huu unabainisha ukweli kuwa Biss ana mtazamo wa kibepari unaomfanya kuamini kuwa yeye ni bora kuliko wengine. Picha ya kiongozi Bikisiwa inayochorwa kupitia maswali anayomwuliza Biss ni ya mwanamke msema wazi.

Vilevile, Madai ya Chachi mwanzoni anapomjia Bikisiwa kumletea posa kwamba hawapendi ndoa ya kulazimishana yanaonekana mazuri kwa Bikisiwa kwani yanaoana na msimamo wake. Hata hivyo Bikisiwa anayashuku. Anauliza maswali kutambua undani na ukweli wa maneno hayo. Bikisiwa anaendelea kumdadisi kupitia kwa maswali mbalimbali. Mathalani:

Hebu sema kweli, umevutiwa na nini? Mwili wangu au mazingira yangu? (uk.48).

Unataka kutujumuisha katika himaya zako za ndoa za kunakotua na kusikotua jua? (uk.48).

Nani atashika hatamu za utawala? (uk.49).

Usaili huu unabainisha kuwa Chachi alivutiwa na urembo wa Bikisiwa na kamwe hakujali maslahi ya nchi ya Bikisiwa alivyodai. Picha ya Bikisiwa hapa ni ya kiongozi mwenye busara kwa sababu anawadadisi waposaji ili kupata mahusiano yatakayoifaidisha jamii yake.

SS anapomwambia kuwa amemletea posa, Bikisiwa anaruka kisha anamdadisi kwa hasira kidogo:

Posa? Posa gani? Posa ya nini? Aposwaye nani? (uk.38).

Uradidi wa neno: posa katika usemi huu unadhihirisha hasira aliyokuwa nayo Bikisiwa kwa SS aliyemlelea posa. Uradidi huu unamchora Bikisiwa kama msemu wazi. Katika muktadha wa jamii za Kiafrika, mwanamke alipoletewa posa alipokea kwa heshima na furaha (Hora, 2014). Kinaya ni kuwa, Bikisiwa hapokei posa za SS. Isitoshe, badala ya kufurahi anakasirika. Picha ya Bikisiwa ni tofauti na ya mwanamke katika muktadha wa jamii ya Kiafrika.

Bikisiwa anapoelezwa na mfalme mpango wa kumtafuta binti anayefanana naye ili aozwe kwa SS baada ya kuwalinda kutokana na wavamizi. Anasema kupitia kwa balagha:

Kwa nini tatizo langu mumpagaze mwanamke mwingine? Kwa nini siku zote matatizo makubwa ana-twishwa mwanamke? (uk.35).

Maswali haya yanadhihirisha namna Bikisiwa alivyotetea hadhi ya wanawake wenzake.

Katika *Kigogo* (2016) Tunu anadadisi Ngurumo na Boza kuhusu maisha mabaya ya ulevi wanayoyaishi ili wajue ukweli kuhusu athari za ulevi. Anawauliza kupitia maswali ya balagha:

Haya ndiyo maisha mnayotaka kuishi kweli? Juzi tuliwazika wangapi kutokana na pombe hii (uk.63).

Starehe za nyani kuchezea tagaa bovu nazo ni starehe? (uk.63).

Katika usaili huu wa kibalagha, Tunu anajitokeza kama mwanamke mpenda jamii yake na msemu kweli kwa uwazi. Anawapenda wananchi wenzake na hataki wafariki kutokana na ulevi. Anawakosoa kwa uwazi.

Tunu anawaalika Ngurumo, Boza na Wanasagamoyo wengine waliokuwa kwa Mamapima wakibugia mtindi kukutanika sokoni. Ngurumo anazua madai kuwa hawezi kukosa kuhudhuria sherehe za uhuru zitakazoongozwa na kigogo Majoka ili ahudhurie mkutano wa Tunu. Tunu anamdadisi kuhusu uhalisia na ukweli wa msimamo wake.

Gani muhimu kati ya dhifa na soko? Utakula na kunywa dhifa hiyo milele? (uk 59).

Haya ni maswali ya balagha ambayo hayahitaji majibu na yanamchora kigogo Tunu kama kiongozi anayesema ukweli kwa uwazi.

Majoka anapomwambia Tunu kuwa ana mpango wa kumwoza kwa Ngao junior, Tunu anamuuliza maswali ili kusesitiza msimamo wake kwamba yeye ni mwanamke wa thamani na anayejiheshimu. Huku akiwa amekasirika, anamidadisi Majoka:

Yaani umenionaje wewe? Waona mimi ni ganda la muwa la juzi? Wadhani siwezi kusubiri kuolewa na mume nimpendaye siyo? (uk.42).

Mtazamo kama mhimili mojawapo wa nadharia ya utafiti huu huathiri maana ndani mwa matini husika (Ntaragwi, 2004). Katika usemi huu, mtazamo wa Majoka kuwa mwanamke hata akiwa kiongozi ni kiumbe duni na chombo cha mapenzi cha kuolewa tu wala si kuongoza unabainika. Mtazamo huu unamchora Tunu kama kiongozi ambaye anajiheshimu na kutetea hadhi yake katika jamii.

Kwa kutumia swali la balagha, anamsisitiza Majoka ukweli kuwa yeye ni muuaji.

Ukichinja watoto wa wenzio usiulizwe? (uk.43).

Tunu haogopi kumweleza Majoka ukweli kuwa anaendeleza kuwa yeye ni muuaji. Kiongozi Tunu anamuuliza Majoka maswali ili kujua ukweli kuhusu masuala mbalimbali. Maswali haya ya balagha yanamsawiri Tunu kama kiongozi jasiri na msema kweli kwa uwazi. Haogopi kumkabili kiongozi Majoka na kumwambia ukweli ambao ni mchungu licha ya kuwa yu ofisini mwake (Majoka) mlimo na askari na kwamba anarekodiwa.

Ngurumo na Asiya wanajaribu kuwashawishi Tunu na Sudi wanywe pombe. Asiya anapowaletea pombe akidai ni ya watu mashuhuri, Tunu habadili msimamo wake wa kutokunywa pombe. Anamkemea Asiya kupitia kwa swali balagha:

Koma! Wajua ni hatia kuuza pombe haramu? (uk.61).

Usemi huu unabainisha msimamo thabiti wa Tunu. Aidha, unaonyesha namna Tunu ni msema kweli.

Katika tamthilia ya *Pango* (2003) Ngwese anamwuliza mkewe swali balagha:

Yule mwalimu alipojitia ujasiri aliona nini? (uk.51).

Kwa kuangazia mhimili wa lugha katika nadharia ya udenguzi, lugha ni kipengele muhimu cha matini kwani kutokana kwayo maana mbalimbali ndani mwa matini huweza kuibuliwa (Miller,

1976). Lugha hujenga taswira (Njogu & Chimera, 1999). Swali la balagha lililotumiwa katika usemi huu linamhusu kiongozi Katango na linamsawiri kama mtu msomi na jasiri. Badala ya Katango kujawa na woga anapokutana na mpinzani wake mkuu wa jinsia ya kiume, Katango anajasirika na kumjibu Ngwese kwa balagha:

Je, unadhani ubabe wako utanitisha mimi? (uk.10).

Balagha hii inamchora Katango kama kiongozi jasiri.

Ngwese anapodai kuwa wazee wa Katango walimwonea wivu babu yake asifanyike chifu, Katango kwa ujasiri anabainisha ukweli wa hali hii kupitia kwa swali la balagha:

Kwani unadhani yamefichwa na yatafichwaje? Nani asiyejua kuwa alikuwa kibarakala wa wakoloni? (uk.13).

Ukweli huu unakuwa mchungu kwa Ngwese ambaye anashikwa na hasira. Picha ya mwanamke inayobainika hapa ni ya mwanamke kama kiongozi msemu kweli kwa uwazi.

Katika jamii ya Pango, mwanamke aliyejaribu kwenda kinyume na mfumo wa kitamaduni uliomdhalilisha mwanamke alisawiriwa na kutazamwa kama mwenye kiburi na mwasi. Mtu I na II wanataka kumtumia Katango kimapenzi. Kiongozi Katango anapokataa, Mtu II anamwambia:

Nini kikapacho kiburi au ni hiyo elimu yako. Ahh...unadhani ndiyo nini? Unadhani tumeona wangapi? (uk.32).

Kwa mujibu wa udenguzi, uchunguzi wa matini humwezesha mhakiki kubaini maana mbalimbali ndani mwa matini (Miller, 1976). Inabainika katika usemi huu kuwa Katango amechorwa kama msomi. Kando na hayo usemi huu unamchora Katango kama mtu mwenye kiburi. Mtazamo huu vilevile unabainika wakati babake Katango aitwaye Seki anapomwuliza Katango swali balagha:

Ndio huo usasa wenu umekupa kiburi cha kuinua kichwa na kukigotesha jabalini chini kama mjusi? (uk.20).

Inabainika kupitia kwa balagha hii kuwa ingawa Seki ana mtazamo kuwa Katango ni mwenye kiburi, Katango amesawiriwa kupitia kwa balagha hii kama mtu jasiri anayejitokeza kupinga mwanamume Ngwese katika kuwania uongozi wa Pango.

Babake Katango anamwuliza Katango swali lingine balagha:

Eeh niambie, hiyo elimu ya kizungu ndiyo iliyokupa ujasiri wa kuipuuza mila? (uk.18)

Kupitia kwa swali hili la balagha, mwanamke Katango anachorwa kama msomi na mtu jasiri. Hata hivyo, usomi na ujasiri huu unamfanya babake kumwona kama aliyeasi utamaduni wao.

Kunayo maswali mengine balagha katika *Pango* (2003) ambayo yanamchora mwanamke kama kiumbe duni na dhaifu. Seki anauliza Katango maswali ya balagha:

Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (uk.18).

Umesikia wapi mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (uk.18).

Utawezaje kufanya jambo ambalo hawafanyi wanawake? (uk.19).

Basi niambie pia si kweli unanuia kumpinga kwenye uongozi wa pango? Sema, huo pia si ukweli? (uk.19).

Kwanza nawe kwa nini unajitia ushujaa wa kwenda kinyume na utamaduni wetu? Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? (uk.35).

Kulingana na nadharia ya utafiti huu, lugha iliyotumiwa ndani mwa matini huwezesha mchanganuzi kuibua maana mbalimbali (Bakhtin, 1981). Maswali ya Seki kwa mwanamke Katango yanamsawiri mwanamke Katango kama mtu duni asiyeweza na asiyefaa kuongoza. Hata hivyo kupitia kwa maswali haya picha ya mwanamke kama kiongozi mkakamavu anayekiuka mitazamo na matendo hasi yaliyomdunisha na kuwania uongozi.

Katango anatetea haki za wanawake kupitia kwa swali la balagha:

Mwanamke ana nini, si ni mwanapango pia? Si anaweza kuongoza? (uk.27).

Isitoshe, anatetea haki yake ya kuongoza:

Sikusema mimi ndiye nifaaye; lakini ikiwa ni mimi kuna ubaya gani? (uk.21).

Aidha, anatetea haki za watoto anapomwuliza Ngwese maswali ya balagha:

Watoto gani? Hata hamnazo huachi? Hivi unadhani watu hatuna macho? ...Unadhani haya ni nini, madude ya kukamilisha urembo wa uso? Unadhani hayaoni haya? Unasikia, bwa mkubwa? Hukuwafukuza ndugu zangu waliokuja kutafuta maji wewe? Hukuwawinga kama ndege wewe? (uk.10).

Maswali ya balagha yametumiwa kumsawiri mwanamke kama mtetezi wa haki zake, za wanawake wenzake na jamii nzima kwa ujumla.

Katango anagadhabishwa na hali kwamba viongozi wabaya kama Ngwese wanasaliti juhudi za wanaukombozi waliopigania uhuru wa Pango. Anasema:

Mbona?

tunaisaliti kafara yao?

tunaisaiti Imani yao?

tunaisaliti ndoto ya waliotutangulia? (uk.9).

Taswira ya Katango inayojitokeza kupitia kwa maswali haya ya balagha ni ya kiongozi ambaye ni mzalendo.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) kiongozi Mpya anatumia maswali ya balagha ambayo yanajenga taswira yake kama kiongozi mzalendo.

Kwa nini wanapeana migongo? Kwa nini wanasuguana migongo? Kwa nini wanachagua pande tofauti kabla ya kujali taifa? (uk.22).

Vilevile Mpya anamwambia babake:

Hivi hukubaini siku zote hizi? Hukubaini kama tumechoka baba'etu mpenzi? (uk.42)

Katika usemi huu Mpya anajitokeza kama msema kweli kwa uwazi. Anamwambia babake waziwazi kuwa wamechoka na uongozi wake usiojali maslahi ya wananchi.

4.3.3 Methali

Methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe, iliyo na mizizi katika jamii na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha hekima na busara (Murungi, 2011; Mturo, 2011). Kwa kurejelea msingi wa lugha katika nadharia ya udenguzi, ni vigumu kuibua maana ndani mwa matini bila kuchunguza lugha iliyotumiwa (Ntaragwi, 2004). Njogu & Chimera wanasema kuwa taswira hutokana na maneno yaliyoteuliwa kwa ufundi katika kazi ya fasihi. Kutokana na mbinu ya methali iliyotumiwa katika tamthilia za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000, taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike inaweza kuibuliwa.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) Bikisiwa anatongoa methali:

Kula uhondo kwataka matendo, aso na matendo hula uvundo (uk.17).

Kupitia kwa methali hii, Bikisiwa anamweleza babake waziwazi ukweli kuwa Sogoramaneno hakuwa na matendo ya kudhihirisha kuwa anamjali na kujali jamii yake (Bikisiwa). Sogoramaneno alikuwa mchumba ambaye babake Bikisiwa alikuwa amempendekezea. Methali hii inamsawiri Bikisiwa kama msema wazi.

Chachi anapomshawishi Bikisiwa akubali posa yake, Bikisiwa anasema:

Nimesikia, lakini mambo haya siwezi kuyakatia shauri sasa. Nahitaji muda kutafakari vizuri. Kama ujuavyo, nyani mwenye pupa hujinasa mwenyewe (uk.50).

Methali; Mwenye pupa hujinasa mwenyewe inamsawiri Bikisiwa kama kiongozi mwenye hekima na subira kwa kuwa anachukua muda wake kuwazia kuhusu uhusiano wa ndoa kabla ya kuingia ndani. Kwa mujibu wa Nonaka & Takeuchi (2011) kiongozi bora hudhihirisha busara yake anapochukua muda wa kutathmini hatima ya uamuzi wake kabla ya kuufanya uamuzi huo. Kiongozi busara hapatii tu kufanya maamuzi kabla ya kufikiri. Bikisiwa hapatii kukubali posa kutoka kwa waposaji. Anachukua muda kutathmini posa hizo ili kufahamu ni ipi itamfaidi yeye na nchi yake. Hii ndio maana anatomia methali anapozungumza na SS aliyekuja kumposa:

Labda unapenda wasifu wa nje tu...hujui kuwa nyumba nzuri si mlango. (uk.38).

Bikisiwa anakataa kuolewa kwa Bw. Sogoramaneno, mwanamume aliyependekezewa na babake kwa kuwa ya ubinafsi wake. Anasema:

Kila shauri lazima akate yeye. Chumo lote kwa nguvu atwae yeye. Mwamba ngoma kawa, ngozi huvutia kwake kila siku (uk.22).

Methali: Mwamba ngoma huvutia ngozi kwake inabainisha ubinafsi wa mwanaume katika kufanya maamuzi na kumiliki nyenzo za kiuchumi na kisiasa. Taswira ya Bikisiwa inayodhihirika kupitia kwa methali hii ni kuwa Bikisiwa ni kiongozi mwenye busara ya kutambua kuwa Sogoramaneno hajali maslahi yake na ya nchi.

Aidha, Hassan anapjaribu kumlinganisha Bikisiwa na wanawake wengine ulimwenguni, Bikisiwa anamwambia wazi kuwa yeye hapendi kufananishwa. Anatomia methali: *Tui haliwi maziwa licha ya weupe (uk.31)* kwa maana kuwa ingawa yeye ni mwanamke ana sifa zake za

kipekee zinazomtofautisha na wanawake wengine duniani. Methali hii inamsawiri kama mtetezi wa haki zake.

Katika *Pango* (2003) Katango anajitokeza kupinga madai ya Ngwese kuwa wazee wa Katango walimzuia babuye kufanyika chifu kwa kusema:

Yeye alikuwa mbaazi uliokosa maua... akasingizia jua (uk.13).

Usemi huu unatokana na methali: Mbaazi ukikosa kuzaa husingizia jua na inamsawiri Katango kama kiongozi jasiri na msema kweli kwa uwazi. Hakubali Ngwese abadilishe ukweli kuwa babuye Ngwese alikuwa kibarakala wa wakoloni.

Uelewa wa muktadha kulingana na udenguzi husaidia mhakiki wa matini kubaini maana ndani mwa matini (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa Pango, mwanamke hakuruhusiwa kuongoza. Ni katika muktadha huu ambapo Ngwese anatumia methali: ***Kelele za chura hazimzui ndovu kunywa maji*** na ***Kelele za mlango hazimnyimi mwenye nyumba usingizi*** (uk.13). Kwa kutumia methali hizi mbili, Ngwese anasisitiza kuwa atakuwa kiongozi wa Pango licha ya upingamizi wa Katango. Anazona juhudi za Katango za kuwa kiongozi kama juhudi dhaifu zisizoweza kuzuia ndoto yake ya kuongoza Pango. Mwanamke Katango anachorwa hapa kama kiongozi mkakamavu ambaye anajibidiisha kuongoza licha ya mila na tamaduni katika jamii yake zilizompinga. Ni taswira hii inayobainika wakati Babake Katango anamtisha Katango kwa kutumia methali:

Mnyama mwenye mkia mrefu hauvuki moto; atachomeka (uk.22).

Katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) Mpya anatumia methali anapowaambia Zanga na Mussa:

Tuseme ukweli hadi udhihiri na uwongo upate kujitenga (uk.54).

Maneno haya ya Mpya yanatokana na methali: *Ukweli ukidhihirika, uongo hujitenga*. Lugha iliyotumiwa kwa mujibu wa Wanaudenguzi huibua maana ndani mwa matini (Fairclough, 1992). Kupitia kwa methali hii, Mpya anachorwa kama kiongozi msema kweli na mkakamavu. Amejitolea kusema ukweli hata ukiwa mchungu.

Kwa mujibu wa *Kigogo* (2016), Majoka anamwambia Tunu:

Yaliyopita si ndwele, tuyape mgongo (uk.39).

Majoka anasema methali: Yaliyopita si ndwele baada ya Tunu kumweleza ukweli kuhusu dhuluma ambazo Majoka alimtendea babake Tunu (uk.39). Maana inayoibuka hapa ni kuwa Majoka anakubali kuwa alimtendea babake Tunu dhuluma. Taswira ya Tunu inayobainika kupitia methali hii ni kiongozi anayesema ukweli kwa uwazi.

Aidha, Majoka anasema:

Asante ya punda ni mateke (uk.44).

Majoka anatumia methali ilii kumsingizia Tunu kama mtu asiye na shukrani. Kwa mujibu wa Mwamzandi (2013), nadharia ya udenguzi huchunguza matini kwa makini ili kubaini kivuli cha maana ndani mwa matini. Kulingana naye, kivuli cha maana ni ile sehemu ya pili ya neno au dhana ambayo huenda isizungumziwe waziwazi na mwandishi. Kwa kuchunguza methali hii tunajiuliza ikiwa Tunu alikuwa mtu asiye na shukrani. Ukweli ni kuwa Tunu alikuwa kiongozi mwenye shukrani. Mathalani anawashukuru wananchi kwa kumpa fursa kuwahutubia (uk.88). Kivuli cha maana ni kuwa Tunu amesawiriwa kupitia methali hii kama kiongozi mkakamavu kwani anavumilia singizio kutoka kwa Majoka.

Isitoshe, Tunu ananena na Majoka kupitia methali:

Mla na miwili hana mwisho mwema (uk.41).

Methali hii ina maana kuwa, mtu mbinafsi hupata hasara baadaye. Methali hii inamsawiri Tunu kama mwenye hekima kwa anatumia methali hii kukosoa ubinafsi wa Majoka. Huenda angemkasirisha Majoka iwapo angemwambia moja kwa moja kuwa alikuwa kiongozi mbinafsi.

4.3.4 Jazanda

Kulingana na Njogu & Chimera (1999) jazanda ni mbinu ambayo hutumiwa kuelezea hali ambapo hadithi inaweza kufasiriwa kwa namna tofauti. Kulingana naye, wahusika na matukio yanayopatikana katika hadithi hiyo huwa na maana nyingine zaidi ya ile ya kijuujuu. Jazanda ni sawa na kilichositiriwa (Nyuta, 2016). Kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu, lugha hutekeleza wajibu muhimu katika kuibua maana katika matini husika (Ntaragwi, 2004). Hivyo kuna haja ya kuchunguza kwa undani lugha iliyotumiwa ndani mwa matini ili kuibua maana.

Katika tamthilia ya *Pango* (2003) mbinu ya jazanda inajitokeza katika semi za wahusika mbalimbali ambayo inajenga taswira ya mwanamke kiongozi. Seki, babake Katango, anamwuliza Katango swali balagha:

Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? (uk.35).

Seki katika usemi huu anatumia jazanda ya kichwa na mkia. Kwa kurejelea mhimili wa lugha kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi, maneno ndani mwa matini husheheni maana (Miller, 1976). Kichwa ni sehemu ya mwili ambayo huongoza mwili mzima na hubeba ubongo, macho, masikio na viungo vingine. Sehemu hii huwa ya juu kwa binadamu na mbele kwa wanyama. Neno kichwa limetumiwa kijazanda kuisitiza kuwa wanaume katika Pango walifaa kuongoza jamii. Mkia kwa upande mwingine ni sehemu ya mwili ambayo hufuata mahali kichwa cha mnyama huongoza. Aghalabu sehemu hii huwa si muhimu sana ikilinganishwa na kichwa. Mathalani kuna wanyama ambao hata sehemu hii ikiondolewa, maisha yao huendelea. Kwa mfano, mkia ukiondolewa kwa kondoo, maisha yake huendelea na hata hunona zaidi. Binadamu hana mkia. Kwa kumlinganisha mwanamke (Katango) na mkia Seki ana maana kuwa kulingana na muktadha wa utamaduni wa Pango, afaa daima kuongozwa. Yeye si mtu muhimu sana kwa kuwa kama mkia jamii inaweza kuendelea bila yeye. Jazanda ya mkia katika usemi wa Ngwese inamchora mwanamke kama kiumbe duni na dhaifu ambaye hafai kuongoza jamii na ambaye daima afaa amnyenyekee na kumfuata mwanamme.

Kwa mujibu wa Mugambi (1982) mwanamke katika tamthilia za awali alisawiriwa kama kiumbe dhaifu ambaye hana upeo mkubwa wa kisiasa na ambao alitarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa waume wao bila ukinzani. Wanaudenguzi hushikilia kuwa mhakiki wa matini aweza kuibua maana mbalimbali ndani mwa matini. Jazanda hii ya mkia inaweza kumsawiri Katango kama mwanamke dhaifu asiyefaa kuongoza. Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa muktadha wa jamii ya Pango, jazanda hii inamchora Katango kama kiongozi jasiri kwa kuwa Katango anajitokeza kuwania uongozi wa Pango licha ya taasubi ya kiumbe iliyokuwepo.

Jazanda nyingine katika tamthilia hii inajitokeza Kikubi anaposema:

Eeh, Katango jiwe la mango, amchezeaye huvunjwa maungo (uk.39).

Lugha kama kipengele mojawapo muhimu cha nadharia ya udenguzi husisitiza uelewa wa lugha iliyotumiwa ndani mwa matini ili kufasiri maana (Ntaragwi, 2004). Uelewa wa jazanda; jiwe la

mango katika usemi huu ni muhimu katika kuelewa maana. Jiwe la mango ni jiwe gumu sana lenye umbo la mviringo. Jiwe hili ni imara na thabiti. Jazanda hii inasisitiza kuwa mwanamke Katango hatetereki. Msimamo thabiti wa Katango unabainika wakati anakataa kusita kuwania uongozi wa Pango na kupigania maslahi ya Wanapango licha ya changamoto nyingi anazopitia. Mwishowe, Katango anaibuka mshindi baada ya Ngwese kutiwa nguvuni. Jazanda ya jiwe la mango inamsawiri kiongozi Katango kama mwenye msimamo thabiti usiotetereka.

Katango anasema kuwa mwanamke ni nguzo (uk.27). Nguzo ni kipande cha mti au chuma kilichosimamishwa wima ardhini ili kuhimili au kushikilia kitu kingine kama vile paa la nyumba (TUKI, 2014). Nguzo huwa muhimu sana katika kuhakikisha kuwa nyumba ni imara. Pasipo na nguzo hapawezi kuwepo na nyumba. Kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi, maana hufasiriwa kwa kuchunguza mitazamo iliyopo (Ntaragwi, 2004); hivyo basi mtazamo wa Katango ni kuwa mwanamke ni kiumbe muhimu sana katika jamii na bila kuwepo mwanamke hapawezi kuwepo na jamii. Katango anatetea haki ya mwanamke kuongoza kwani anajiona kama mhimili muhimu katika maendeleo ya jamii. Kupitia kwa jazanda hii, Katango anajisawiri kama mtetezi wa jinsia ya kike.

Aidha, Katango anauambia umati wakati wa kampeni za kuwania uongozi wa Pango:

*Usisahau ni **kiwavi** anayeishia kuzaa **kipepeo** (uk.48).*

Kwa mujibu wa Derrida (1976), kila neno huwa na maana iliyojengwa ndani mwake na aghalabu huhusiana na neno lingine. Neno Kiwavi katika usemi huu wa Katango lina maana ya mdudu mwenye miguu mingi ambaye aghalabu huwa na manyoya yanayowasha na aliye katika hatua ya pili ya ukuaji wa vipepeo na nondo. Kipepeo ni mdudu mwenye umbo jembamba na mbawa pana zenye rangi mbalimbali na kupendelea kutua kwenye maua (TUKI, 2004). Kwa mujibu wa Mung'atha (2012) nadharia ya udenguzi hulenga kufichua maana ndani mwa matini ambayo huwa imefichwa na mwandishi kupitia vipengele vya lugha. Kupitia jazanda ya kiwavi na kipepeo, tunabaini kuwa Katango ni mtetezi wa haki za vijana. Anatetea haki ya vijana ya kuongoza namna afanyavyo kipepeo anapopaa.

Kijazanda, Katango analinganisha vijana na **moyo wa binadamu** na **damu ya uhai** (uk.42). Moyo ni kiungo muhimu cha uhai wa binadamu. Moyo ukikosa kufanya kazi binadamu hufa. Uhai wa kiumbe yeyote huwa katika damu yake. Mwanadamu akiishiwa damu mwilini hufa.

Kwa kutumia jazanda ya moyo na damu, Katango anatetea haki ya vijana ya kutambuliwa kuwa watu muhimu wa kuiongoza jamii kufikia malengo yake. Mbinu hii inamchora mwanamke Katango kama mtetezi wa vijana.

Kundi la vijana katika uwanja wa kampeni linatumia jazanda ya **kikaango** kumwita Katango (uk.27). Kikaango ni chombo kitumiwacho kukaangia vyakula (TUKI, 2004). Hakuna siku kikaango kitakataa kukaanga chakula. Kundi hili lina mtazamo kuwa Katango ni kikaango cha Ngwese kwa kuwa atakomesha uongozi mbaya wa Ngwese. Taswira ya kiongozi Katango inayojitokeza kutokana na jazanda hii ni kiongozi jasiri na mkakamavu.

Katango anatumia jazanda ya **jua linalotua** kwa maana kuwa mzee Ngwese afaa kustaafu kutokana na umri wake na kupeana nafasi kwa vijana kama Katango kuiongoza. Taswira ya Katango inayobainika hapa ni ya mwanamke ambaye ni msemu kweli kwa uwazi.

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008), taswira ya kiongozi Bikisiwa kama mtu mkakamavu inajengeka kupitia mbinu ya jazanda. Bikisiwa anamwambia babake:

*Mwenzangu kamwe hanijali wala hanibali. Kwake mimi ni **kiatu kibovu** (uk.22).*

Maneno kwa mujibu wa Wanaudenguzi husheheni maana (Miller, 1976). Jazanda ya kiatu kibovu katika usemi huu inatuchorea picha ya namna wanawake katika jamii ya Bikisiwa walisifiwa na wanaume ili washiriki mapenzi au ndoa nao ila baada ya wanaume kukidhi haja zao wakawatupa na kukosa kuwajali namna mtu afanyavyo na kiatu kibovu kilichomaliza kazi yake. Ifikapo kufanya maamuzi katika ndoa, mwanamke hakuwa na lake kwani mwanamume alikata kila shauri. Jazanda inabainisha namna mwanamke anavojitokeza kutetea hadhi yake katika jamii.

Biss anamwambia Bikisiwa:

*Kilichonileta ni pendo la moyoni. Wewe ni **tunda zuri lililo mtini** (uk.44).*

Kwa mujibu wa udenguzi, matini huwa na maana mbalimbali ambazo hubainishwa kupitia usomaji wa kina wa matini (Mishra, 2018). Ulinganisho wa Bikisiwa na tunda zuri lililo mtini laweza kumchora mwanamke kama chombo cha mapenzi cha kushibisha uchu wa mwanamume. Aidha, jazanda hii inamchora Bikisiwa kama kiumbe anayesisifiwa kupitia kwa maneno.

Katika *Kimya Kimya Kimya* (2011), Mpya analinganishwa na **kikaango** (uk.28):

Kikaango tokea lini kikasema? (uk.28).

Kikaango ni kifaa ambacho hutumiwa kutayarishia chakula. Kifaa hiki huwa kipo tu kupokea kila chakula cha kukaangwa bila kuchagua wala kulalamika. Kwa kumlinganisha Mpya na kikaango, taswira ya Mpya anayetetea haki yake ya kusema inadhihirika kwani mwanamke katika muktadha wa nchi ya Mpya hakufaa kujitolea na kupinga uongozi mbaya.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016), Kenga anamshauri Majoka:

Limekuwa **donda ndugu** sasa (uk.35)

Jazanda ya donda ndugu iliyotumiwa katika dondoo hili inarejelea joto la kisiasa jimboni ambapo Tunu alikuwa amefaulu kuwashawishi na kuwazindua wananchi kupinga uongozi wa Majoka na kutetea haki zao. Jazanda hii ni dhihirisho la ushawishi wa Tunu na inamsawiri Tunu kama kiongozi mshawishi.

Kinyago cha Tunu alichochonga Sudi (uk.10, 93) ni jazanda inayobainisha namna mwanamke alivyokwezwa katika jamii ya Sagamoyo. Jazanda hii inachora mwanamke Tunu kama kiongozi anayeheshimiwa.

4.3.5 Tashbihi

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili ambavyo vina sifa tofauti kwa kutumia maneno kama vile: ja, mfano wa, mithili ya, kama na sawasawa (Njogu & Chimera, 1999; Wamitila, 2003).

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) kiongozi Bikisiwa anatumia mbinu ya tashibihi anaposema:

Yeye asiye kwisha kudondokwa na ute kama mbwa mwenye njaa (uk.5).

Kwa maneno ya Mturo (2011) tashibihi ina dhima muhimu katika fasihi kwani husaidia kujenga picha kwa msomaji. Umithilishaji wa mwanamume na mbwa asiye kwisha kudondokwa na ute pindi amwonapo mwanamke katika usemi huu unatuchorea picha ya baadhi ya wanaume ambao kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Bikisiwa alimtamani mwanamke kimapenzi. Kwa mujibu

wa udenguzi, matini huwa na maana mbalimbali ambazo yafaa ziibuliwa na mhakiki (Mishra, 2018). Tashibihi iliyotumiwa katika usemi huu inamsawiri mwanamke kama chombo cha mapenzi. Aidha, mwanamke Bikisiwa anasawiriwa kupitia umithilishaji huu ni ya mwanamke mkakamavu na msema wazi ambaye anajitokeza kupinga udunishwaji.

Tashibihi nyingine inabainika wakati Bikisiwa anamwambia Hassan, mmoja wa wanaume waliokuja kumposa:

Bora niseme kinaganaga. Tusipigishane kelele bure kama sahani za kaure (uk.32).

Kwa kutumia tashibihi ya sahani za kaure, Bikisiwa anasisitiza kuwa yeye ni mtu anayesema ukweli kwa uwazi ili kuondoa migogoro na mivutano. Taswira ya mwanamke kiongozi inayobainika kupitia kwa tashibihi katika usemi huu ni ya mwanamke kama kiongozi jasiri na msema kweli kwa uwazi.

Aidha, Biss ajapo kumposa Bikisiwa, Bikisiwa anamwambia:

Na maneno ya asali matamu kuliko maji matamu... (uk.43).

Bikisiwa katika uneni huu analinganisha maneno matamu ya Biss na asali ambayo inapita utamu wa maji matamu. Ingawa maneno ya Biss ni matamu ajabu, Bikisiwa haingii mtegoni. Anaendelea kusema:

...lakini mtu lazima kwanza asikilize ladha ya baada kuonja utamu wa asali na ikiwezekana aisikilize taathira yake mapema, kabla hata hajaonja (uk.43).

Hii ina maana kuwa busara aliyo nayo Bikisiwa inampa subira ya kuwachunguza waposaji kabla ya kuingia katika nikai nao. Kwa kurejelea dhana ya kivuli cha maana katika misingi ya nadharia ya udenguzi (Mwamzandi, 2013), posa kati ya Bikisiwa na wanaumme waposaji inaashiria uhusiano wa kimataifa kati ya nchi ya Bikisiwa na nchi zingine. Bikisiwa kupitia uneni wake anadhihirisha hekima yake kwa kukataa kuingia makubaliano ya kimataifa ambayo hayataleta manufaa kwa nchi yake.

Mbinu ya tashibihi vilevile inabainika katika tamthilia ya *Pango* (2003). Mwandishi anaeleza hivi:

Wakati huu anaingia Ngwese kutoka upande wa pili. Anatembea haraka haraka lakini

anapomwona Katango anatua ghafla kama aliyemwona zimwi (uk. 8).

Kwa kurejelea msingi wa lugha katika nadharia ya udenguzi, uchunguzi wa kina wa maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini ni jambo muhimu kwa kuwa kupitia kwalo, maana ndani mwa maneno haya huibuliwa (Derrida, 1973; Miller 1976). Katango anamithilishwa na zimwi. Neno zimwi lina maana ya kiumbe adhaniwaye na kuaminiwa kuwa huishi msituni na ambaye huweza kujibadilisha katika hali mbalimbali na huweza pia kudhuru (Mdee, Njogu & Shafi, 2011). Umithilishaji huu unabainisha na kusisitiza mtazamo aliokuwa nao Ngwese kwa Katango. Ngwese ana mtazamo kuwa Katango ni nuhusi. Mtazamo huu unamsawiri mwanamke Katango kama mkosi. Mwamzandi (2013) alieleza dhana ya kivuli cha maana katika misingi ya nadharia ya udenguzi. Anasema kuwa kivuli cha maana ni ile sehemu ya pili ya dhana au neno ambayo haiwezi kubainika bila uchunguzi wa kina wa matini. Kwa kuchunguza tendo la Katango la kugombea uongozi, kivuli cha maana kinachojitokeza kutokana na maelezo haya ya mwandishi ni kuwa Katango ni kiongozi mkakamavu. Licha ya mtazamo hasi wa Ngwese unaomlinganisha na zimwi, anaendelea kupigania uongozi.

Katango katika mazungumzo yake na Ngwese anatumia tashibihi anapomwambia Ngwese:

Ni ukweli na unanyonyota ngozini kama upupu (uk.14).

Katika usemi huu, Katango anamsisitizia Ngwese kuwa babu yake hakufanyika kuwa chifu kwa kuwa alikuwa kibarakala wa wakoloni wala hakuonewa wivu na wazee wa Katango namna alivyodai Ngwese. Ngwese anakasirishwa na ukweli huu mchungu. Katango anamithilisha ukweli huu mchungu na upupu ambao ukianguka kwenye ngozi huwashawasha. Taswira ya mwanamke kiongozi ambaye anawakilishwa na Katango ni ya mtu jasiri na msema kweli kwa uwazi hata kama ukweli huu ni mchungu.

Aidha, mbinu ya tashibihi imedhihirika katika tamthilia ya *Kigogo* (2016). Tunu anamkosoa Majoka kwa uwazi:

Na wala si kuwaua watu kama kuku na kuchekacheka kama... (uk.44).

Tunu analinganisha mauaji anayoyatekeleza Majoka na mauaji ya kuku. Picha ya Tunu ambaye ni kiwakilishi cha mwanamke kiongozi inayobainika katika usemi huu ni ya mtu jasiri na msema

kweli kwa uwazi. Tunu hasiti kumkosoa Majoka kwa mauaji ya Wanasagamoyo anayoyaendeleza.

Vilevile Boza anatumia mbinu ya tashibihi anapomwambia Sudi:

Una mke na bado mnafwatana kama mtu na kivuli chake... (uk.6).

Boza anamithilisha namna Sudi anavyomwandama Tunu na mtu na kivuli chake. Kwa mujibu wa utamaduni wa jimbo la Sagamoyo, mwanamke alipoandamana na mwanamume walishiriki mapenzi. Kwa kuangazia usemi huu wa Boza kwa misingi ya mtazamo huu wa kitamaduni, Tunu anasawiriwa kama chombo cha mapenzi. Hata hivyo, kwa kuchunguza usemi huu kwa misingi ya matendo ya Tunu katika tamthilia hii, tunapata kutambua kivuli cha maana kuwa Tunu anamshawishi Sudi hadi Sudi anaambatana naye katika juhudi za kutetetea haki za Wanasagamoyo. Kulingana na Mwamzandi (2013) kivuli cha maana kwa mujibu wa udenguzi ni ile sehemu ya pili ya dhana ambayo huenda isibainishwe iwapo matini hayatachunguzwa kwa makini.

Kenga anatumia tashibihi ya nyoka ambaye twajua hutambaa kutokana na ukosefu wa miguu kuelezea hali ya Tunu:

Hana miguu kwa sasa pengine atambae kwa tumbo kama nyoka! (uk.69).

Usemi huu unaweza kumsawiri Tunu kama kiumbe dhaifu anayetendewa madhila ya kila aina. Hata hivyo kwa kuchunguza zaidi tendo la Tunu la kuendelea kutetea uongozi bora wa jimbo lao licha ya ulemavu, taswira ya Tunu kama kiongozi mkakamavu inachoreka. Kwa mujibu wa wanaudenguzi, matini husheheni maana mbalimbali ambazo huibuliwa kupitia uchunguzi wa kina wa matini (Mishra, 2018).

Kupitia tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) mwandishi anatumia mbinu ya tashibihi anaposema:

Walinzi wanamshika mkono na kumburura kama gunia la makaa! (uk.41).

Kwa kumlinganisha Mpya na gunia la makaa, mwandishi anasisitiza mtazamo wake kuhusu namna thamani ya mwanamke kiongozi ilivyodunishwa kupitia tendo hili. Picha ya mwanamke inayochorwa kupitia kwa umithilishaji huu ni ya kiumbe duni. Hata hivyo kwa kuchunguza zaidi

tunabaini kuwa tashbihi hii imemchora Mpya kama kiongozi mkakamavu anayekiuka dhuluma na kuleta mabadiliko ya kiuongoza katika jamii yake. Kulingana na udenguzi, uchunguzi wa kina wa matini huibua maana zilizofichama (Mung'atha, 2012).

4.3.6 Nahau na Misemo

Nahau ni msemu uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini huwa umesetiri maana tofauti na ile inayokuwa imebebwa na maneno hayo hayo katika matumizi ya kawaida (Senkoro 1982, Wamitila, 2003). Kulingana na Mturo (2011) misemo ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea tungo ambazo hutumia picha, ishara na tamathali kuelezea kitu au wazo kwa ufupi. Senkoro (1982) anasema kwamba misemo ni sawa na nahau kimatumizi ila nahau zenyewe ni misemo ambayo huwa imeshika mizizi zaidi katika jamii na huwa na hadhira pana kuliko misemo. Kimsingi, nahau huundwa kutokana na nomino na kitenzi (Wamitila, 2008).

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) Bikisiwa anawaambia wanaumme waposaji waache **kumpiga bodi**. Bodi ni sehemu ya gari ambamo hukaa abiria au huwekwa mizigo (TUKI, 2014). Piga bodi ni nahau iliyo na maana ya kuharakishwa au kushurutishwa. Bikisiwa kupitia kwa nahau hii anachowra kama kiongozi jasiri anayesema ukweli kwa wazi bila kuficha.

Aidha, Sogoramaneno anatumia nahau ya 'kupiga mwereka' anaposema:

Iwapo mwanamke atasitasita, basi ana haki ya kumpiga mwereka na kumbeba hadi nyumbani kwake (uk. 58).

Sogoramaneno anadai kuwa ana haki ya kumpiga Bikisiwa mwereka na kumpeleka kwake kwa lazima. Nahau 'piga mwereka' ina maana ya kumshinda au kumwangusha mtu (Mdee, Njogu & Shafi, 2011). Katika muktadha wa utamaduni wa nchi ya Bikisiwa mwanamke aliyekataa kuolewa baada ya mahari kulipwa hata bila hiari yake alipaswa kuozwa kwa lazima. Kulingana na nadharia ya udenguzi, kufahamu muktadha kunasaidia mhakiki kuelewa maana (Ntaragwi, 2004). Nahau hii inatuonyesha mitazamo hasi iliyomdunisha mwanamke katika nchi ya Bikisiwa. Mugambi (1982) alipohakiki tamthilia za kati ya mwaka 1957 na 1981 alidai kuwa mwanamke katika tamthilia teule za uhakiki wake alisawiriwa kama kiumbe duni anayepokea maagizo kutoka kwa mwanamume bila ukinzani. Picha ya kiongozi Bikisiwa inajengeka kupitia

kwa nahau hii ni ya mwanamke mkakamavu anayekataa ndoa ya lazima na kutetea uhuru wake wa kujichagulia mchumba amtakaye. Kulingana na wanaudenguzi, uhakiki wa kina wa matini huibua maana ambayo huenda ikafanana au ikatofautiana na maana ya awali (Bakhtin, 1981). Taswira ya mwanamke Bikisiwa inatofautiana na taswira ya mwanamke katika uhakiki wa Mugambi.

Boza anamwuliza kiongozi Tunu:

Wafikiri nauza nyonga kama huyo Tunu wako? (uk.64).

Nahau ‘uza nyonga’ katika swali hili balagha ina maana ya kushiriki katika biashara ya ukahaba. Boza ana mtazamo kuwa Tunu ni mpenziwe Sudi jambo ambalo twajua si kweli. Taswira ya kiongozi Tunu inayojengeka kupitia kwa nahau hii ni ya mwanamke mkakamavu na anayejiheshimu.

Isitoshe, Kenga anamwambia Majoka:

Waliota mizizi ikakita na wakamea hata pembe (uk.35).

Nahau mbili zinabainika katika usemi huu: ota mizizi na mea pembe. Kulingana na Kenga Tunu pamoja na wafuasi wake wameendelea kupinga uongozi wa Majoka hadi imekuwa vigumu kuwaondoa. Nahau hizi zinamsawiri Tunu kama kiongozi mshawishi na mkakamavu.

Kwa kurejelea *Kimya Kimya Kimya* (2011), Majoka anasema kuwa Watoto wake hawawezi **kumpaka kinyesi** kama afanyavyo Mpya (uk. 40). Nahau; paka kinyesi ina maana ya kuharibu. Picha ya Mpya inayobainika kupitia mtazamo huu wa Binafsi ni ya mwanamke mharibifu. Hata hivyo, tunapochunguza matendo ya Mpya, tunatambua kuwa Mpya hakuwa mharibifu. Anasingiziwa uharibifu na Binafsi. Hivyo, nahau hii inamsawiri Mpya kama kiongozi mkakamavu anayevumilia singizio katika juhudi zake za kupigania uongozi bora. Wanaudenguzi hulenga kubaini maana ambazo huwa zimefichama ndani mwa matini (Mung’atha, 2012). Aidha, Mpya anatumia msemu ‘haki haizami’ anaposema:

Ingawa lazima tuwaheshimu wazazi na wazee wetu, lakini pia lazima watambue haki za kila kiumbe, kwa kweli haki haizami (uk.51).

Kupitia msemu huu, taswira ya mwanamke kiongozi kama mtetezi wa haki inadhihirika.

Katika *Pango* (2003), Katango anamwambia Ngwese:

Watoto gani? Hata hamnazo huachi? (uk.10).

Msemu: **hata hamnazo** huachi unadhihirisha namna Katango alivyotetea haki za watoto.

Aidha, Katango anamwambia Mbabekazi:

Hatuwezi kushikilia tu chungu cha zamani na huku wakati unapita (uk.27).

Msemu: shikilia chungu cha zamani ni msemu unaomaanisha kujikita katika mtazamo wa kitamaduni. Anachosisitiza Katango kupitia usemi huu ni kuwa kama wanawake hawafai kushikilia mtazamo wa kitamaduni uliowadhalilisha wanawake kuhusiana na suala la uongozi; wanafaa kujitokeza na kuwania nyadhifa za uongozi. Msemu huu unamchora Katango kama kiongozi mtetezi wa haki ya wanawake ya kuongoza.

4.3.7 Kinaya na Kejeli

Kinaya ni kinyume cha jambo au matarajio. Kejeli ni kusema kwa kukebehi au kumwambia mtu maneno ya kuudhi kwa masihara (Mdee, Njogu & Shafi, 2011). Kulingana na Mishra (2018) nadharia ya udenguzi hulenga kubainsha kinaya, utata, ukinzani, unyume na mwachano ndani mwa matini kwani kupitia kwa ubainishi huu, maana mbalimbali zilizomo ndani mwa matini huibuliwa.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016) kinaya kinajitokeza wakati Tunu japo amevunjwa mguu na wahuni, anaondoka nyumbani kwao akiwa katika kiti cha magurudumu na kwenda kukabiliana na wahuni hawa (uk.56). Awali alimwambia mamake:

Mama, nisimulie kisa haraka ninataka kwenda. Nataka kukutana na majangili (uk.55).

Tunamtarajia Tunu baada ya kulemazwa kutulia nyumbani kwao na hata kuachana na juhudi za kupigania uongozi bora Sagamoyo. Kujitokeza kwa Tunu kwenda kukutana na wahuni pamoja na tendo lake la kuendelea kupigania uongozi bora ni kinyume cha matarajio. Isitoshe, ilikuwa kinyume cha matarajio ya Majoka na washauri wake kuwa Tunu alilemazwa mguu wala hakufariki. Majoka na serikali yake walitarajia kuwa mpya angekufa kwa kuwa walikuwa wamepanga njama ya kumfisha Tunu (uk.68). Kinaya hiki kinamsawiri Tunu kama kiongozi jasiri na mkakamavu.

Aidha, Tunu anapowaalika walevi wahudhurie mkutano katika lango la Chapakazi, Ngurusmo anamwambia:

Kichwa chako kizuri Tunu? Naona waota ndoto mbaya. Sisi tukose kwenda kwa kigogo wetu kwa dhifa eti tunahudhuria vitu kama hivyo? (uk.59)

Kwa mujibu wa udenguzi, matini hubeba maana mbalimbali ambazo hubainishwa na mhakiki kupitia usomaji wa kina. Katika muktadha wa kijamii, ukisema kuwa mtu hana kichwa kizuri maana tunayoipata ni kuwa mtu huyo ni mwendawazimu au hana ufahamu (mjinga). Ngurumo anapomwuliza Tunu iwapo kichwa chake ni kizuri, maana mbili zinaibuliwa. Moja ni kuwa Tunu alikuwa mjinga (alikosa ufahamu) na pili ni kuwa Tunu alikuwa mwendawazimu. Kinaya ni kuwa Tunu hakuwa mjinga wala mwendawazimu. Alifahamu haki zake na za Wanasagamoyo. Alikuwa na akili razini ambazo zilimwezesha kupigania uongozi boras. Kinaya ni kuwa Ngummo ndiye aliyekuwa mjinga (hakuwa na kichwa kizuri) kwa kuwa alimfuata Majoka kipofu tu bila ufahamu.

Isitoshe, Ngurumo anamwambia Tunu:

Mbona maringo Tunu! (uk.57).

Kulingana na Ngurumo, Tunu ana maringo kwa kuwa alikataa kunywa pombe. Tunu kupitia wimbo wa Daudi Kabaka ulioanzishwa na Ngurumo anachorwa kama msichana mrembo ambaye amelimika sana ila hajaolewa (uk.65). Msichana huyu ambaye anamithilishwa na Tunu anasemekana kuwa na maringo kwa vijana. Kinaya ni kuwa Tunu hakuwa na maringo kwani alikuja kuwaalika walevi mkutanoni. Ingawa amefikia kiwango cha juu cha elimu, Tunu anahusiana na watu wakiwemo walevi bila kujifaragua. Ukweli ni kuwa Tunu kwa kukataa kunywa pombe, ana msimamo thabiti. Taswira ya mwanamke kiongozi inyodhihirika kupitia kinaya hiki ni ya mwanamke mkakamavu anayevumilia singizio eti ni mwenye majivuno.

Isitoshe, mwandishi anatueleza kuwa Ngurumo anacheka kicheko cha kukera kinachowafanya walevi wengine kukaribia walipo Ngurumo na Boza. Baada ya kicheko hiki, Ngurumo anamkejeli Tunu:

Tunu wewe ni nani katika Sagamoyo? Babako na babu yako walikuwa nani Sagamoyo?

(uk.58).

Kicheko cha Ngurumo ni cha kumdhihaki Tunu. Kinaya ni kuwa kicheko hiki kinawavutia walevi wengine licha ya mwandishi kutueleza kuwa kilikuwa cha kukera. Kupitia kinaya na kejeli katika muktadha huu, taswira ya mwanamke kama kiongozi jasiri na mkakamavu inabainika. Tunu anajitokeza kwa ujasiri kupigania uongozi bora licha ya kejeli kutoka kwa Ngurumo.

Kwa kurejelea *Posa za Bikisiwa* (2008), Sogoramaneno anapompa Bikisiwa hongera, Bikisiwa akiwa amekasirika anakejeli hongera hizi:

Hongera...hongera ...Hongera za nini? Sema unataka nini? (uk.55).

Katika muktadha wa jamii, tunatarajia mtu kufurahi anapopewa pongezi. Kinaya ni kuwa Bikisiwa anakasirika. Hasira yake huenda ilitokana na namna mwanamke alivyokuwa akikandamizwa na kupewa sifa za kinafiki. Hii huenda ndiyo sababu alijua kuwa zilikuwa za uongo. Kinaya hiki kinamsawiri Bikisiwa kama kiongozi msema wazi.

Kinaya kingine kinajitokeza kupitia kwa kicheko cha mwanamke Bikisiwa. Mwandishi anatueleza kuwa kilikuwa kicheko kilichojaa uchungu na kilio (uk.1). Tunatarajia kicheko kudhihirisha furaha, si kilio wala uchungu. Kicheko kimedenguliwa na mwandishi ili kubaiisha machungu aliyokuwa nayo mwanamke kutokana na dhuluma alizotendewa. Kinaya hiki kinamsawiri Bikisiwa kama mtetezi wa haki za wanawake wenzake.

Katango kwa kutetea uongozi bora Pangoni anasema kuwa ni lazima kiongozi afaaye ateuliwe ili kuongoza Pango. Seki anamkejeli:

Na huyo kiongozi afaaye ni wewe sio? (uk.21).

Katango anaonyesha ujasiri na ukakamavu wake wakati Mtu I na II wanavamia njiani akiwa na Kibwana. Huku Mtu wa II akicheka kwa dharau, anamkejeli kiongozi Katango kwa kusema:

Aahh, unaogopa nini Katango? Iweje anayetaka kuwa mlinzi wa Pango awe mwoga kiasi hiki? Shh...shhh...Pango litaongozwa na mwoga hili? Jama tutapona? (uk.31).

Katika usemi huu, madai ya Mtu II kuwa Katango ni mwoga ni kinyume cha ukweli kwa kuwa, Katango alipovamiwa na Mtu wa I na II aliwakabili kijeshi na kutaka kuvua vazi alilokuwa amejifunika Mtu I. Kinaya ni kuwa, Mtu II ndiye aliyekuwa mwoga. Anaposikia Mtu I akipigwa

na Kibwana, anatumia mbio na kutoroka kwa uoga. Kinaya hiki kinamchora Katango kama kiongozi jasiri.

Kwa mujibu wa *Kimya Kimya Kimya* (2011), kinaya kinajitokeza wakati Mpya ambaye ni mtoto wa kiongozi wa nchi anapojitokeza kupinga uongozi mbaya wa babake. Jamii haikumtarajia kufanya hivi (uk.27). Kujitokeza kwake ni kinyume cha matarajio ya babake na baadhi ya wananchi walioshikilia mtazamo huu.

4.4 Hitimisho

Katika sura hii utafiti huu umechunguza namna mwanamke kiongozi alivyosawiriwa katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Imebainika kuwa mwanamke kiongozi amesawiriwa kwa njia chanya kinyume na usawiri wa mwanamke katika tafiiti nyingi za fasihi hasa za kabla mwaka wa 2000. Utafiti huu umetambua kuwa ingawa mwanamke katika tamthilia nne teule za utafiti huu amesawiriwa kama msomi, tamthilia ya *Kigogo* (2016) ndiyo tamthilia ya pekee kati ya tamthilia nne zilizoteuliwa na utafiti huu iliyomsawiri mwanamke kama kiongozi aliye na upeo wa juu sana kielimu. Isitoshe, utafiti huu umebaini kuwa mitindo ya lugha iliyotumiwa katika tamthilia teule imechangia kujenga taswira ya kiongozi wa jinsia ya kike. Utafiti huu umethibitisha msimamo wa wanaudenguzi namna ulivyoelezwa na Ntaragwi (2004) kwamba lugha ni kipengele muhimu cha matini na kupitia kwayo maana mbalimbali ndani mwa matini huibuliwa. Taswira ya mwanamke kiongozi imebainika kupitia kwa mitindo ya lugha iliyotumiwa katika tamthilia teule.

SURA YA TANO: ATHARI YA TASWIRA YA MWANAMKE KIONGOZI KWA UONGOZI WA MWANAMKE

5.1 Utangulizi

Sura hii inachunguza namna usawiri wa mwanamke kiongozi uliobainishwa katika sura ya nne ya utafiti huu unavyoathiri uongozi wa mwanamke katika tamthilia teule. Data kuhusu athari hizi ilikusanywa kupitia mbinu ya maktaba ambapo athari hizi zilinukuliwa kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi. Baadaye, data hii ilipangwa katika makundi mawili: athari chanya na hasi na kuchanganuliwa kupitia uchanganuzi wa yaliyomo. Hatimaye, matokeo yalifasiriwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo.

5.2 Athari Hasi za Taswira ya Mwanamke Kiongozi kwa Uongozi wa Mwanamke

5.2.1 Kudharauliwa na Kukejeliwa kwa Mwanamke Kiongozi

Kwa kurejelea msingi wa maana katika nadharia ya udenguzi, maneno ndani mwa matini husheheni maana mbalimbali (Miller, 1976). Kulingana na TUKI (2014) neno dharau lina maana mbili. Maana ya kwanza ni kukosa kuthamini mtu au kitu au kuvunjia heshima. Maana ya pili ni kukosa kutia maanani; kubekua; kukefya; kupuuza. Neno kejeli lina maana ya kusema maneno ya dharau; kufanyia mzaha; kukebehi. Inabainika kutokana na maana hizi kuwa mtu anaweza kumdharau mtu au kitu kupitia kwa matendo au maneno na anaweza kumkejeli kupitia kwa maneno uyasemayo.

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Pango* (2003) Katango anapojitokeza kama kiongozi jasiri kuwania uongozi wa Pango, Ngwese ambaye ni mpinzani wake mkuu anamdharau. Anapokutana na Katango njiani anamwambia:

Babu aliniambia kukumbana na mwanamke asubuhi ni kisirani, siku nzima anichafua.

Mwanamke unasaka nini hapa? (uk.10).

Ngwese anataja jina ‘mwanamke’ kabla ya kumuuliza swali hili. Hamwulizi; “Katango au Mwanapango unasaka nini hapa?” Anarudia matumizi ya neno hili. Kulingana na nadharia ya

udenguzi, lugha ni kipengele muhimu cha matini kwani kupitia kwayo maana mbalimbali zaweza kuibuliwa (Ntaragwi, 2004). Kutokana na uradidi wa neno ‘mwanamke’ katika usemi wa Ngwese, mtazamo wa Ngwese kuwa Katango ni kiumbe duni unabainika. Wanaudenguzi husisitiza kuwa mhakiki wa matini afaa kuchunguza mitazamo iliyopo kwani kupitia kwayo, changanuzi mbalimbali za matini zaweza kuibuliwa (Hooks, 1988). Mtazamo wa Ngwese kuwa mwanamke Katango hafai kuongoza unaonyesha namna Ngwese alivyomdharau Katango. Katola (2006) katika uhakiki wake wa tamthilia anadai kuwa kuna mifumo ya kijamii iliyojaa taasubi ya kiume ambayo imechangia kumdhulumu mwanamke.

Aidha, Ngwese anamdharau Katango na kumwona kuwa ni bahati mbaya. Hili linabainika kupitia kwa maelezo ya mwandishi:

Wakati huu anaingia Ngwese kutoka upande wa pili. Anatembea haraka haraka lakini anapomwona Katango anatumia ghafla kama aliyemwona zimwi. Anaukunja uso wake. Katango anageuka na kumwona (uk.8).

Tendo la Ngwese kutua ghafla ni dhahirisho la mtazamo wake kuwa mwanamke hata akiwa kiongozi ni mkosi. Isitoshe, Ngwese anaukunja uso wake pindi anapomwona Katango. Matendo huwa dhahirisho la mambo yaliyo akilini na moyoni mwa mwanadamu. Tendo la Ngwese la kukunja uso linaonyesha mtazamo wa Ngwese uliomdharau mwanamke Katango.

Aidha, Ngwese analinganisha juhudi za Katango za kuwania uongozi wa Pango, na kelele za chura ambazo hazimzui ndovu kunywa maji na kelele za mlango ambazo hazimnyimi mwenye nyumba usingizi (uk.13). Kelele za chura na za mlango hazina athari yoyote kwa ndovu na mwenye nyumba. Lugha kulingana na wanaudenguzi huibua na kukuza maana katika lugha (Ntaragwi, 2004). Inabainika kuwa Katango ana sifa za kuongoza Pango. Kwa kuchunguza maneno: kelele za chura na kelele za mlango, tunaona namna Ngwese alivyomdunisha Katango kwa kuwa yeye alikuwa mwanamke (si kwa sababu hakuwa na sifa za kiongozi bora). Kutokana na ulinganisho huu mtazamo wa Ngwese ni kuwa juhudi zote za Katango kugombea uongozi wa Pango hazina athari yoyote kwani hazitafaulu. Mtazamo huu unaonyesha namna kiongozi Katango alivyodharauliwa na Ngwese kwa misingi ya jinsia yake.

Katango anapojitokeza kutetea haki ya watoto (Susa na Sota) ya kuchota maji, Ngwese anamdharau na kudhalilisha elimu aliyoipokea Katango skwa kusema:

Wa nani mwingine si wewe mwanamke hapo ulipo? Naona babako ameshindwa nawe; labda anaistahi elimu yako lakini kwangu awe na elimu au la mwanamke ni mwanamke tu! (uk.10).

Hanitishi mwanamke kamwe! (uk.10).

Kwa mujibu wa mhimili wa lugha katika nadharia ya udenguzi, matini huwa na maana mbalimbali na maana hii hubainika kupitia kwa lugha iliyotumiwa (Bakhtin, 1981; Ntaragwi, 2004). Kutokana na maneno aliyotumia Ngwese katika usemi huu, mtazamo wake kuwa mwanamke hata kama amesoma ni mwanamke tu na daima mwanamume humpiku. Mitazamo kulingana na Wanaudenguzi huwa muhimu katika kubainisha maana ndani mwa matini (Levinas, 2003). Kutokana na mtazamo huu wa Ngwese, taswira ya namna mwanamke anavyodhalilishwa inabainika.

Katango anajitokeza kama kiongozi msema kweli kwa uwazi. Anakosoa madai potofu ya Ngwese kuwa wazee wa Katango walimwonea babuye wivu akakakosa kufanyika chifu na kumweleza ukweli kuwa haya yalitendeka kwa kuwa babuye alikuwa kibarakala wa wakoloni. Katango afanyavyo hivi, Ngwese anamkumbusha kuwa yeye ni mwanamke:

Mwanamke wewe unajua nini kuhusu matendo? (uk.13).

Sitopoteza wakati wangu kutupiana maneno na mwanamke (uk.13).

Mwamzandi (2013) alieleza kuhusu dhana ya kivuli cha maana katika nadharia ya udenguzi. Kulingana naye, kivuli cha maana ni ile maana ya pili ya neno ambayo huenda isibainike pasipokuwepo na uchunguzi wa kina wa matini. Twaweza kuchukulia tu kwamba Ngwese katika usemi huu anatumia neno ‘mwanamke’ kwa maana ya mtu wa jinsia ya kike. Hata hivyo, kwa kuchunguza muktadha wa utamaduni wa Pango, tunatambua nafasi duni aliyokuwa amepewa mwanamke. Ngwese hazungumzi tu na Katango; lazima aongeze neno ‘mwanamke’ katika usemi wake kumkumbusha kuwa yeye ni kiumbe duni.

Katango anapoangua kicheko, Ngwese kupitia kwa swali balagha anamlinganisha na mbwa abwekaye:

Ni nini unachobwekea hapa? (uk.13).

Kwa maoni ya Mung'atha (2012), nadharia ya udenguzi hulenga kuchunguza vipengele vya lugha ili kubaini maana iliyofichama. Kwa kuchunguza neno bweka ambayo ni sauti ya mbwa, tunatambua namna Ngwese alivyomdunisha kiongozi Katango kwa kumlinganisha na mbwa. Ngwese anadharau usemi wa Katango kwa kuulinganisha na sauti atoayo mbwa.

Katango anapodhihirisha hekima yake kama kiongozi katika hotuba yake kwa wananchi wakati wa kampeni, Ngwese anamkejeli kwa kumwambia:

Hili sio darasa! Sisi sio watoto wa shuleni! (uk.42).

Utambaji wa ngano katika jamii yetu hii ni wa wanawake...Lakini uongozi si ngano s(uk.46).

Baada ya Ngwese kutumia ufisadi kumpoka Katango uongozi, anamdharau Katango licha ya ujasiri, ukakamavu na usomi wake:

Ingekuwa fedheha kama ningeshindwa, tena na kijana jike eeh...Si neno hiyo elim sina...Lakini? Kwani elimu ni nini humu mwetu? (uk.50).

Yule mwalimu (Katango) alipojitia ujasiri aliona nini? (uk.51).

Babake Katango aitwaye Seki vilevile anamdharau Katango pindi tu Katango anaonyesha azma ya kuliongoza Pango. Hathamini ujasiri, ukakamavu na ushawishi wa Katango. Mtazamo wake kuwa mwanamke Katango hafai na hawezi kuongoza Pango kwa sababu ya jinsia yake unaoana na mtazamo katika muktadha wa utamaduni wa Pango ambao ulishikilia kuwa uongozi ulikuwa wa mwanamume. Maana katika lugha kwa mujibu wa wanaudenguzi huibuliwa kutokana na miktadha na mitazamo iliyopo (Ntaragwi, 2004). Kulingana na Onyoni (2012) suala la uongozi wa mwanamke halikuangaziwa katika tamthilia za kabla ya mwaka wa 2000 kwa kuwa utamaduni haukumruhusu mwanamke kuyaingilia masuala ya uongozi. Mtazamo wa Seki uliomdhalilisha kiongozi Katango unabainika kupitia kwa usemaji wake kwa Katango. Katango anapojitokeza kwa ujasiri kumpinga mwanamumme Ngwese, Seki anadharau ujasiri, juhudi, elimu na ukakamavu wake. Seki anamwambia Katango:

Mwanamke hafanyi hivyo! (uk.18).

Ehh niambie, hiyo elimu ya kizungu ndiyo iliyokupa ujasiri wa kuipuuza mila? (uk.18).

Utawezaje kufanya jambo ambalo hawafanyi wanawake? (uk.19).

Unajua kichwa cha nyoka hakistahimili kilemba wewe? (uk.20).

Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? (uk.35).

Maana kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu hujengwa na kukuzwa kupitia lugha (Berthes, 2011 Ntaragwi, 2004). Kwa mujibu wa Miller (1976) nadharia ya udenguzi hushikilia kuwa maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini hubeba maana. Neno ‘mwanamke’ pamoja na maswali balagha katika usemi huu wa Seki yanabainisha mtazamo wake uliomdharau Katango.

Katango anapotetea haki ya wanawake ya kuongoza Pango anasema kuwa kuongoza pekee hakuwezi kumshinda mwanamke. Mwanamke Mbabekazi anatoa kauli inayodhihirisha mtazamo wake uliomdhalilisha mwanamke kiongozi:

...jamii inawadharau wanawake (uk.27).

Kwa mujibu wa usemi huu wa Mbabekazi ni bayana kuwa mtazamo wa Mbabekazi ni kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiye na thamani. Mtazamo huu kulingana na Mbabekazi una misingi yake katika muktadha wa utamaduni wa Pango ambapo mila na desturi za Pango zilimdhalilisha mwanamke kwa msingi wa jinsia yake na kumpinga asijitokeze kuongoza. Kwa kurejelea kipengele cha muktadha katika nadharia ya udenguzi, uelewa wa muktadha ni muhimu kwa mhakiki wa matini kwani kupitia uelewa huu maana ya matini hubainika (Ntaragwi, 2004).

Ujasiri wa kiongozi Katango unapobainika kupitia kwa mwanamume Kikubi ambaye anasifia ujasiri huu, Mbabekazi anadharau juhudi za Katango za kugombea uongozi wa Pango. Katika majadiliano yake na Katango, Kikubi, na Kibwana, mtazamo wa Mbabekazi unabainika anaposema:

...unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe? (uk.25).

Watu watakubali uongozi wa vijana ...na hasa mwanamke? (uk.27).

Mtazamo wa Mbabekazi ni kwamba mwanamke hawezi kufaulu kufanyika kiongozi kwa sababu ya jinsia yake. Kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu, mitazamo huibua au huathiri maana ndani mwa matini (Levinas, 2003). Mtazamo huu wa mwanamke Mbabekazi unamdhalilisha kiongozi wa jinsia ya kike.

Katika majadiliano yaya haya, Katango anajitokeza kama mtetezi wa usawa anapodai kuwa mara hii asali ya pango lazima iwafaidi wote, Mbabekazi anashikilia mtazamo wake unaomdhalilisha mwanamke:

Kwa mwanamke ... itakuwa kazi... (uk.28).

Katango anapozungumza na mamake na babuye baada ya Ngwese kutwaa ushindi kwa njia ya ufisadi, anakumbuka maneno ya Mbabekazi yaliyodhalilisha juhudi zake za kugombea uongozi:

Hata wenzangu wananiambia kuwa sisi vijana hatuna nafasi kabisa. Kwanza wanawake nao... (uk.57).

Usemi huu unaonyesha namna ilivyokuwa vigumu kwa mwanamke kupigiwa kura na kufanyika kiongozi katika jamii ya Pango kwa sababu ya kudharauliwa kwa wanawake.

Katango anapodhihirisha uadilifu na msimamo wake thabiti kwa kumkemea Mtu I ili asinguse kimapenzi alivyotaka, Mtu II anamdharau Katango:

Nini kikapacho kiburi au ni hiyo elimu yako. Ahh...unadhani ndiyo nini? Mwanamke ni mwanamke...Unadhani tumeona wangapi? (uk.32).

Kwa mujibu wa Hooks (1988) kuibua maana kutoka kwa mtazamo mpana huibua maswali mapya na changanuzi mpya. Kutokana na usemi huu wa Mtu II, mtazamo wake kumhusu mwanamke kiongozi unabainika. Kulingana naye, mwanamke hata kama amesoma au kufanyika kiongozi ni kiumbe duni tu; elimu na uongozi haubadilishi hadhi yake ya chini. Mtazamo huu ulikuwa na misingi yake katika muktadha wa utamaduni wa Pango na ulimdhaliisha kiongozi wa jinsia ya kike.

Isitoshe, kiongozi Katango anapodhihirisha ukakamavu wake baada ya Katango kurusha mkono wa Mtu II uliotaka kumgusa kimapenzi na mkono huu kumpiga Mtu II shavuni, Mtu II kwa hasira anadhihirisha mtazamo wake kuwa mwanamke kamwe hafai kumpiga mwanamume (uk.33). Mtazamo huu ulikuwa na misingi yake katika muktadha wa utamaduni wa Pango. Kwa mujibu wa nadharia iliyoteuliwa na kutumika katika utafiti huu, uchunguzi wa muktadha ni jambo muhimu kwa kuwa kutokana nao maana yaweza kuibuliwa (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa Pango, mwanamume aliruhusiwa kumpiga mwanamke jinsi alivyopenda. Ngwese anamwambia Katango kuwa inafaa aolewe ili atiwe adabu na mumewe (uk.14). Mtazamo huu wa kitamaduni ulimdhaliisha mwanamke kiongozi.

Ni katika muktadha huu wa kitamaduni ambapo mwanamke hakufaa kuongoza. Uongozi ulitengewa mwanamume. Katika historia ya Pango, mwanamke hakuwai kuongoza. Mapunjo (2014) katika uhakiki wake wa tamthilia ya *Kivuli Kinaisha* (1990) alidai kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe asiyefaa kuongoza. Ujasiri wa Katango wa kutaka kuongoza unadharauliwa na Mtu I anapomtahadharisha Katango:

Kigoda cha Pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? Hilo halijawahi kutokea katika historia ya huku kwetu na halianzi nawe, unasikia? (uk.32).

Kupitia tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) kiongozi Mpya anadharauliwa kwa sababu ya jinsia yake. Bw. Binafsi anamdharau Mpya ambaye ni mwanawe kwa kuwa Mpya amejitokeza kijasiri kupinga uongozi mbaya na kutetea haki ya wananchi. Anadharau juhudi za Mpya za kuleta mabadiliko ya kiongozi nchini. Anawauliza Bw. Naona na Bw. Salimina:

Hawo vinyangarika wanajua nini kuhusu uongozi? (uk.66).

Katika swali hili la balagha, neno vinyangarika limetumiwa kama fumbo kumwashiria kiongozi Mpya na nduguze. Bw. Binafsi anamwita Mpya kinyangarika kwa kuwa anapigania nchi ipate katiba mpya. Kwa mujibu wa wanaudenguzi kilicho muhimu katika uhakiki wa matini ni usomaji wa kina wa matini ili kubaini maana iliyomo. Maana hii kulingana nao huibuliwa kwa kuchunguza maana ya maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini husika kwani maneno ndani mwa matini husheheni maana (Derrida, 1973, Miller, 1976). Kulingana na Mung'atha (2012), udenguzi hulenga kuibua maana iliyofichama ndani mwa mafumbo yaliyotumiwa katika matini. Neno kinyangarika ni fumbo lenye maana ya kitu cha kudharauliwa au kisichofaa (TUKI, 2014).

Isitoshe, Binafsi anamuuliza Mpya swali la balagha:

Mtoto wa kike ana faida gani? (uk.34).

Swali hili linabainisha mtazamo wa Binafsi kuwa mwanamke hakuwa na faida yoyote katika jamii. Kitu ambacho hakina faida huwa na hasara. Mtazamo wa Binafsi ni kuwa mwanamke Mpya kwa kujitokeza kumpinga kisiasa analeta hasara katika jamii. Mtazamo huu ulikuwa na mihimili yake katika muktadha wa utamaduni wa jamii ya Mpya. Kulingana na muktadha wa utamaduni huu, ilikuwa hasara kumzaa mtoto wa kike na faida kumzaa mtoto wa kiume.

Mtazamo huu ulimdhaliisha mwanamke. Hii ndiyo maana, katika mkutano wa familia ya Binafsi, Binafsi anawasifu wanawe wa kiume na kuwabeua Mpya ambaye ni mwanawe wa kike na Bi. Shoo ambaye ni mkewe. Aidha, Binafsi anaudharau ulumbi wa Mpya kwa kumwamrisha afunge domo lake chafu na kulinganisha mdomo wake na kijaluba.

Kwa kurejelea *Kigogo* (2016) mwanamke Tunu anajitokeza kama kiongozi kuongoza maandamano ya kuleta mageuzi ya kiuongozi. Mpinzani wake wa kisiasa anayeitwa Majoka anadharau juhudi hizi. Hamthamini Tunu. Anapoelezwa kuhusu namna anavyoendelea kuwashawishi Wanasagamoyo, anasema:

Michezo ya kitoto huchezwa kitoto. Hatutatumia bomu kuulia mbu. Hawa ni watu wadogo. Usiichoshe akili bure. Dawa yao ninayo (uk.35).

Katika usemi huu, Majoka analinganisha Tunu na wenzake na mbu ambaye mtu haihitaji bomu kumwua. Kwa kuzingatia kipengele cha lugha katika nadharia ya udenguzi, lugha hubeba maana mbalimbali na maana hizo zaweza kuibuliwa kwa kuichunguza lugha hiyo (Ntaragwi, 2004). Kutokana na umithilishaji huu wa Tunu na mbu, mtazamo wa Majoka kuwa Tunu ni mtu duni unabainika. Maana kwa kurejelea nadharia ya utafiti huu huathiriwa na mitazamo iliyopo. Mtazamo huu unamdhaliisha Tunu kwa msingi wa jinsia yake na kumfanya aonekana kama mtu duni licha ya kwamba ni kiongozi.

Isitoshe, Majoka na mshauri wake mkuu aitwaye Kenga wanakejeli elimu ya kiongozi Tunu ambaye amesoma hadi kiwango cha uzamifu na kuitwa daktari. Hawaithamini.

Majoka anasema:

*Hivi vishahada vyao wanavyovipata wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha vichwa!
Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana (uk.32).*

Mtazamo wa Majoka katika usemi huu ni kuwa elimu aliyoipata Tunu ndiyo inayomvimbisha kichwa. Kuvimbishwa kichwa katika muktadha huu ni kumfanya mtu awe na kiburi.

Kenga naye anasema:

Shahada za siku hizi! Wakati wetu mtu kuitwa kitu ilikuwa ngoma. Huyu Daktari Tunu ni daktari wa nini hasa? (uk.32).

Tunu kwa ujasiri anamwendea Majoka ili kutetea haki za Wanasagamoyo. Katika mazungumzo yao, mtazamo wa Majoka kumhusu Tunu unabainika. Kulingana na nadharia ya udenguzi,

uchunguzi wa mitazamo ni muhimu katika kubaini maana katika lugha (Levinas, 2003). Majoka ana mtazamo kuwa Tunu ni mtoto. Anamtazama Tunu kama mtoto wala si kiongozi. Mtazamo huu unamdhalilisha kiongozi Tunu. Majoka anamwambia Tunu:

Salamu kwanza, binti mdogo (uk.39).

Wewe ni msichana mdogo hata ubwabwa wa shingo haujakutoka... (uk.42).

Utoto una mambo (uk.43).

Sadakta binti mdogo! (uk.45).

Aidha, Majoka anamdharau Tunu kwa kumtaka aolewe kwa mwanawe aliyeitwa Ngao Junior. Anapokataa Majoka anamshauri Tunu:

Tafuta mume akuoe... (uk.45).

Mtazamo huu wa Majoka unaoana na mtazamo katika muktadha wa utamaduni wa Sagamoyo ambao ulimtaka mwanamke kuolewa na kuharamisha tendo la mwanamke kuwania uongozi. Muktadha na mitazamo kama mhimili wa nadharia ya udenguzi husisitiza kuwa uelewa na uibuaji wa maana katika lugha huwezekana kupitia kwa uelewa wa miktadha na mitazamo iliyopo (Ntaragwi, 2004). Ngurumo na walevi wenzake wakiwa ulevini kwa Mamapima wanambeza Tunu kupitia kwa wimbo wa Daudi Kabaka kwa sababu hajaolewa. Kwa mtazamo wao Tunu afaa kuolewa badala ya kuongoza. Mtu I katika hali yake ya ulevi anamwambia Tunu:

Nasikia Ngaaa...o Junior anakutaaa...aaka sana. Ichuuu...kue bahati hiyo bibiye, ni adimu sana (uk.65).

Mtazamo wa kitamaduni kuwa hatima kuu ya mwanamke ni kuolewa wala si kuongoza unamdhalilisha mwanamke kiongozi.

Kenga anadharau juhudi za Tunu kuongoza Jimbo la Sagamoyo anapomwuliza Sudi swali:

Sagamoyo ishawahi kuwa na mashujaa wa kike kweli? (uk.10).

Ilikuwa wazi kuwa jimbo la Sagamoyo halikuwa limewahi kuongozwa na mwanamke. Kenga anauliza swali ambalo anajua jibu lake. Kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu, mhakiki wa matini afaa kuchunguza lugha iliyotumiwa kwani lugha hiyo hubeba maana (Ntaragwi, 2004). Kutokana na swali hili balagha liliolizwa na Kenga, mtazamo wake kuwa mwanamke hakuwahi na hangewahi kuwa kiongozi unabainika. Mtazamo huu vilevile unabainika Ngurumo anapomwuliza Tunu maswali yafuatayo:

Nasikia wataka kuwa kigogo wa Sagamoyo? (uk.58).

Wewe ni nani katika Sagamoyo? (uk.58).

Mtazamo wa Kenga aidha unabainika anaposema:

Mbio za Tunu ni za sakafuni... (uk.12).

Tunu hawezi kupigiwa kura hata! (uk.33).

Ngurumo ambaye ni mfuasi sugu wa Majoka anamwambia kiongozi Tunu:

Hayo si muhimu kwa sasa. Muhimu ni kuwa mimi kura yangu simpji mtu mwingine. Kama si Majoka heri nimpe paka wake lakini si mwanamke (uk.59).

Kwa mujibu wa usemi huu wa Ngurumo, mwanamke ni kiumbe duni hasa akilinganishwa na mwanamume. Hivyo, hafai kupigiwa kura. Paka wa mwanamume ana hadhi ya juu kuliko mwanamke. Ngurumo anasema kwamba afadhali ampigie kura paka wa Majoka kuliko kumpigia mwanamke Tunu kura. Kwa mujibu wa Mung'atha (2012), udenguzi hulenga kuibua maana iliyofichama ndani mwa vipengela vya lugha. Kwa kuchunguza neno paka ambaye tujuavyo ni mnyama ambaye hufugwa na binadamu na aghalabu hupenda kula panya, mtazamo wa Ngurumo kuwa mwanamke ana hadhi ya chini sana kuliko paka unabainika. Mitazamo kulingana na wanaudenguzi huwa muhimu katika kuibua maana ndani mwa matini (Ntaragwi, 2004). Mtazamo huu unamdhalilisha mwanamke kiongozi kwa msingi wa kigezo cha jinsia.

Tunu ajitokezapo kutetea haki za Wanasagamaoyo kupitia vyombo vya habari, anadharauliwa na Kenga. Anamripotia Majoka hivi;

Aliropokwa tu maneno mengi ya kawaida (uk.32).

Kwa mujibu wa wanaudenguzi, maana huwa imefichama ndani mwa maneno (Mung'atha, 2012). Neno ropoka lina maana ya kusema maneno yasiyo na maana au kusema upuuzi (Mdee, Njagi & Shafi, 2011). Isitoshe anadai kuwa maneno haya japo yalikuwa mengi hayakuwa mapya ila yalikuwa ya kawaida. Kinaya ni kwamba maneno ya Tunu yalikuwa ya maana kwa Wanasagamoyo kwani yalitetea haki zao kama haki ya kufunguliwa kwa soko ambalo lilikuwa tegemeo lao (uk.45, 60). Mtazamo wa Kenga uliomdharau kiongozi Tunu unabainika wakati Kenga anapodai kuwa maneno ya Tunu hayakuwa na maana wala upya wowote.

Kupitia tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) Bikisiwa anadhihirisha msimamo wake thabiti anapokataa posa kutoka kwa Sogoramaneno. Sogoramaneno anamdharau kiongozi Bikisiwa na kukosa kuthamini msimamo wake thabiti pamoja na uerevu wake. Anasema:

N'najua njia ya kupita, nitakupata tu wewe. Mimi nitakupata siku moja. Usinione bwege wala usijidai mbabe sana. Werevu na maarifa yako vina ukomo (uk.60).

Sauti ambayo inaaminika kuwa ya mwanamume Sogoramaneno inamdharau kiongozi Bikisiwa:

Eeee we Bikisiwa. Ewe mwanamke. Sikiliza maneno yangu ili upulike. Mwanamke ni mwanamke tu. Uko chini yangu. Hata uwe kisiwa. Hata uwe bahari. Hata uwe bara la nchi kavu na majabali na milima. Wewe ni wangu; ni wangu, mali yangu. Na mali yangu ni yangu. Mali yangu si yako. Na yako ni yangu. Kumlalamikia baba au mama ifae nini? Ha, haha, hahaa...(uk.19)

Lugha kama msingi mojawapo muhimu wa nadharia ya udenguzi husisitiza umuhimu wa lugha katika kuibua maana mbalimbali ndani mwa matini (Bakhtin, 1981). Kutokana na usemi huu wa Sogoramaneno mtazamo wa mwanaume huyu kuwa japo Bikisiwa ni kiongozi aliyesoma na kupevuka, yeye ni kiumbe duni na daima yeye atakuwa chini ya mwanamume unadhihirika. Mitazamo na miktadha ni vipengele ambavyo huathiri maana kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi (Ntaragwi, 2004). Mtazamo wa mwanamume huyu unaoana na mtazamo wa jamii ya Bikisiwa kuwa mwanamke hata akifikia upeo wa juu wa kielimu au kiuongozi ni kiumbe duni ambaye mwanaume humpiku siku zote. Mtazamo huu unamdharau mwanamke Bikisiwa. Isitoshe, Sogoramaneno anadharau msimamo thabiti wa Bikisiwa kuwa kamwe hawezi kuolewa kwake kwa kudai kuwa kulingana na muktadha wa utamaduni wa jamii yake ana haki ya kumpiga mwereka Bikisiwa na kumbeba hadi nyumbani kwake (uk.58).

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) tendo la Mpya kujitokeza kiujasiri kupinga uongozi mbaya wa babake aitwaye Bw. Binafsi linamfanya babake kumdharau. Bw. Binafsi anamwona mwanawe Mpya kama kisirani. Anajuta kwa kukosa kumng'oa Mpya kutoka kwa tumbo la mamake Mpya kwa kuwa kulingana naye Mpya ni mtoto balaa (uk.34). Mtazamo huu unamfanya Bw. Binafsi kuagiza walinzi kumfukuza nyumbani. Isitoshe, anaitishia kumlaani Mpya kwa kuwa kulingana naye ni nuksi (uk.41).

Kiongozi Mpya anapinga kudharauliwa kwake na kuzungumza dhidi ya uongozi mbaya wa babake. Anamwambia babake Bw. Binafsi:

Tumechoka. Hivi hukubaini siku zote hizi? Hukubaini kama tumechoka baba'etu mpenzi? (uk.42).

Mwanamke Mbabekazi katika *Pango* (2003) ana mtazamo kuwa Katango hawezi kuchaguliwa kuongoza Pango kwa kuwa utamaduni wa jamii ya Pango haukumruhusu. Katango anapinga mtazamo huu:

Hamna neno mradi wenyewe hatujidharau...Hatuwezi kushikilia tu chungu cha zamani na huku wakati unapita (uk.27).

Mtazamo wa Katango ni kuwa yeye ana uwezo wa kufanyika kiongozi. Mbabekazi anapomwambia kiongozi Katango kuwa itakuwa vigumu yeye kuchaguliwa, Katango anadhihirisha mtazamo wake hivi:

Si kuongoza tu! Kuongoza kutatushinda? ...Hii ndiyo fursa aisee (uk.28).

Kiongozi Tunu kupitia *Kigogo* (2016) anajithamini na anateta dhidi ya kudharauliwa na kukejeliwa kwake. Majoka anapomdunisha kwa kumwita mtoto, Tunu anamwambia:

Na ukome kuniita mtoto; nina meno yangu yote (uk.43).

Aidha, Tunu anapinga pendekezo la Majoka la kumwoza kwa Ngao Junior kwa kuwa lingemdhalilisha:

Yaani umenionaje wewe? Waona mimi ni ganda la muwa la juzi. Wadhani siwezi kuolewa na mume nimpendaye, siyo? (uk.42).

Majoka anapomwambia atafute mume amuo, Tunu anamwuliza:

Wewe ni nani kwangu hata unishauri (uk.45).

Licha ya mwanamke kujitokeza kuongoza jamii katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016, anavunjiwa heshima, anapuuzwa na kukosa kuthaminiwa kama kiongozi na baadhi ya watu katika jamii yake. Inabainika kwamba kudharauliwa na kukejeliwa kwa mwanamke kiongozi kuna misingi yake katika muktadha wa utamaduni wa jamii yake. Muktadha kama msingi mojawapo muhimu wa nadharia ya udenguzi hushikilia kuwa maana ndani mwa matini huathiriwa na muktadha uliopo. Uelewa wa muktadha hivyo basi huleta uelewa wa maana (Ntaragwi, 2004). Katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika, mwanamke alidharauliwa na kudunishwa. Tamaduni na mila hazikumruhusu kujitokeza na kuongoza jamii (Mapunjo, 2014; Hora, 2014). Mwanamke katika muktadha wa utamaduni wa jamii za tamthilia

teule alidunishwa. Mtazamo wa baadhi ya wanajamii katika tamthilia hizi ni kuwa mwanamke hakufaa na hakuweza kuongoza kwa sababu ya jinsia yake.

Kwa mujibu wa Katola (2006) mifumo ya kijamii iliyojaa taasubi ya kiume imechangia katika kumdhulumu mwanamke. Kulingana naye, mifumo hii imechangia kumdhulumu mwanamke na kumpa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Alichomaanisha hapa Katola ni kuwa mifumo ya kijamii iliyo na taasubi ya kiume inamdhalilisha mwanamke na kumfanya asiwe mbele ya mwanamume katika nyanja mbalimbali kama siasa. Katika uhakiki wa tamthilia kati ya mwaka 1957 hadi 1981, Mugambi (1982) alidai kuwa mwanamke amedharauliwa na kuonekana kama kiumbe asiye na upeo mkubwa wa kisiasa. Keter (2013) alipofanya uhakiki wa tamthilia ya *Natala* (1997) alisema kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni asiyestahili heshima. Japo mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 anadharauliwa na kukejeliwa kwa msingi wa jinsia yake, yeye hajidharau. Isitoshe, dharau hizi hazimfanyi kuacha kupigania uongozi bora. Anaelewa uwezo wa kuongoza alionao na kuipigania nafasi ya kuongoza jamii. Kulingana na Mulila (2009) wanawake wana uwezo sawa wa kuongoza kama walivyo wanaumme.

5.2.2 Mwanamke Kiongozi Kusingiziwa maovu

Kwa mujibu wa Chacha (2013) mwanamke anatendewa matendo ya ajabu katika jamii. Katika tamthilia ya *Pango* (2003), Ngwese anapokutana na Katango njiani anamsingizia Katango kuwa alikuwa na wivu uliomfanya ampinge (Ngwese). Anasingizia Katango kwa kudai kuwa amekutana naye kwa minajili kumfanyia uchawi au uganga ili asichaguliwe kuwa kiongozi wa Pango. Hii ilikuwa baada ya Katango kutangaza azma yake ya kumpinga Ngwese katika uwaniaji wa uongozi wa Pango. Ukweli ni kwamba Katango hakuwa na wivu wowote kwa Ngwese. Mtazamo wa Ngwese kuwa Katango anamwonea wivu unabainika Ngwese anapomwambia Katango:

Ndiyo eeh, wivu unatembea kwenye damu yako, wewe na wenzio kama wewe... (uk.12).

Sema kweli yako, ulikuja kunitegea ndumba ndoto yangu iweze kupombojeka siyo?

Isitoshe, Katango anasingiziwa kuwa analiharibu Pango. Pango palikuwa mahali palipokuwa na rasilimali za jamii hii kama asali ambayo ilifaa irinwe kufaidi wanajamii wote. Uongozi mbaya wa Ngwese unafanya Pango kukosa asali na jamii kuteseka. Pindi Katango anapojitokeza kugombea uongozi wa Pango anaanza kusingiziwa na babake aitwaye Seki kuwa analiharibu Pango na kufanya nyuki wasitengeneze asali (uk.21, 72). Ukweli unadhirika baadaye kuwa Seki na Ngwese ndio waliokuwa wakiliharibu Pango kwa kurina asali na kwenda kuiuza ughaibuni (uk.85-86) kwa maslahi yao.

Katango anapodhihirisha uadilifu na msimamo wake thabiti anapopinga jaribio la Mtu I kushiriki mapenzi naye, Mtu I anamsingizia kirukanjia:

Sikiliza kirukanjia wewe! (uk.32).

Maneno yaliyotumiwa ndani mwa matini kulingana na wanaudenguzi hubeba maana (Miller, 1976). Neno kirukanjia katika usemi huu wa Mtu I limetumiwa kama fumbo lenye maana ya mwanamke ambaye haridhiki na mwanaume mmoja au mwanamke anayefanya ngono na wanaume ovyoovyo (Mdee, Njogu & Shafi, 2011). Dai hili ni la uongo kwani Katango alikuwa kiongozi mwadilifu.

Katika *Kigogo* (2016) Tunu anapojitokeza kwa ujasiri kuongoza jimbo la Sagamoyo, anasingiziwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Sudi ambaye alikuwa mshirika wake wa kisiasa. Tunu alikuwa hajaolewa naye Sudi alikuwa mume wa Ashua. Mtazamo kuwa Tunu alikuwa mpenziwe Sudi unatokana na muktadha wa utamaduni wa Sagamoyo ulioamini kuwa mwanamke hakufaa kujiingiza katika masuala ya kisiasa na kuandamana na wanaume. Kulingana na muktadha huu, jukumu la mwanamke lilikuwa kukaa nyumbani ili kutekeleza majukumu ya kinyumbani. Kwa kurejelea msingi wa muktadha katika nadharia ya udenguzi, uelewa wa muktadha husaidia mhakiki kufasiri maana ndani mwa matini (Ntaragwi, 2004). Mtazamo katika muktadha huu wa utamaduni wa Sagamoyo ni kuwa mwanaume hawezi kushirikiana na mwanamke bila kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Mtazamo huu unadhirika kupitia kwa usemaji wa Boza, Kenga, Ashua na Ngurumo. Mitazamo kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi huchangia uibuaji wa maana ndani mwa matini husika (Levinas, 2003). Boza anamwambia Sudi:

Si huyo Tunu wako. Una mke na bado mnafuatana kama mtu na kivuli chake...eti

watetezi sijui wa nini... (uk.6).

Tunu akiwa na Sudi kwa Mamapima, Boza anawaambia:

Ha-ha-ha-ha... maisha ni kufuatana wawili kwa wawili kama kumbikumbi? Oaneni yaishe bwana! (uk.63).

Anamwambia Sudi:

Wataka kuniharibia siku yangu nile nini? Wafikiri nauza nyonga kama huyo Tunu wako(uk.64).

Katika mandhari yaya haya, Ngurumo anamwambia Sudi:

Wafikiri kila mtu ametiwa ndani ya kirinda na huyu Tunu kama wewe? Ukitaka mke wa Pili mwoe uache sarakasi...(uk.64).

Kenga vilevile anadhihirisha mtazamo huu anapomwambia Sudi:

Umelishwa kiapo na huyo hawara (Tunu) wako, siyo?

Kwa mujibu wa nadharia ya utafiti huu, mhakiki katika uchanganuzi wa matini afaa kuchunguza lugha iliyotumiwa ndani mwa matini husika kwa kuwa lugha hubeba maana mbalimbali (Bakhtini, 1981). Maana hii kulingana na Miller (1976) ni zao la uchunguzi wa kina wa maneno kwani maneno huwa na maana iliyojengwa ndani mwake. Kenga katika usemi huu anatumia neno hawara kumwashiria Tunu. Neno hawara lina maana ya mwanamke au mwanamume anayekaa na mtu asiyeoana naye (TUKI, 2014).

Hata mkewe Sudi aitwaye Ashua anamsingizia Tunu kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Sudi ambaye ni mumewe. Akiwa kizuizini, Ashua anamwambia Sudi:

Nikiwa hapa sikutani nawe na huyo kirukanjia wako. Si umwoe yaishe! (uk.47).

Nenda kamnong'onezee huyo Tunu anayebubujikwa na mapenzi (uk.49)

Mawazo yako, hisia zako, nafsi yako na kila kitu chako kimesombwa na huyo Tunu (uk.49).

Neno kirukanjia lililotumiwa katika usemi huu wa Ashua limetumiwa kimafumbo. Kulingana na Mung'atha (2012), mhakiki anayetumia nadharia ya udenguzi hulenga kuibua maana mbalimbali zilizofumbwa ndani mwa neno. Neno hili lina maana tatu kulingana na Mdee, Njogu & Shafi (2011): ndege mdogo aliye na tabia ya kuruka njia kutoka upande mmoja hadi mwingine wakati wa usiku; mwanamke ambaye haridhiki na mwanaumme mmoja au mwanamke anayefanya ngono na wanaumme wengi; mtu asiyetulia mahali pamoja. Kwa kutumia neno hili, Ashua ana maana kuwa Tunu ni mpenziwe Sudi. Uhusiano wa Tunu na Sudi ulikuwa wa kisiasa tu,

haukuwa wa kimapenzi (uk.49). Hakuna mahali popote katika tamthilia nzima ambapo tunamwona Tunu wakihusiana na Tunu kimapenzi.

Tendo la Mpya katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) la kujitokeza kiujasiri na kuupinga uongozi wa babake unafanya babake kumsingizia kuwa yeye ni mkorofi, mwenye kiburi na chanzo cha matatizo yake. Babake anamwambia:

Wewe kigego, mtoto wa ukorofi... (uk34).

Umekuja duniani kuniondolea furaha (uk.34).

Wewe umekuja kubadilisha ubaba wangu humu duniani. Umekuja kubadilisha ndani na nje yangu. Umekuja kuvunja amri zangu kwa marefu na mapana! (uk.38).

Watoto wangu mwenyewe mnataka kunichakachua! Mapinduzi...mapinduzi...Mapinduzi!

Wanaleta mapinduzi nyumbani mwangu mwenyewe. Kwenye utawala wa nyumba yangu mwenyewe. Mapinduzi...Mapinduzi (uk.42).

Mtoto mdogo lakini anajifanya mkubwa wa kuchukua mamlaka yangu... (uk.41).

Mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 ni mwadilifu licha ya kusingiziwa maovu. Usingizaji huu ulikuwa na misingi katika miktadha ya utamaduni wa jamii na ulikuwa na lengo la kumkatisha tamaa ya kuwania uongozi. Hata hivyo, mwanamke kiongozi katika tamthilia teule anaendelea kuwa mwadilifu na kuendeleza juhudi zake za kuongoza jamii yake. Tunu kupitia tamthilia ya *Kigogo* (2016) anaendelea kuwa mwadilifu na kupigania haki za Wanasagamoyo licha ya kusingiziwa kuwa ni mpenzi wa Sudi. Kwa kurejela tamthilia ya *Pango* (2003) Katango anaendelea kuwania uongozi licha ya kusingiziwa kuwa analiharibu Pango. Kiongozi Mpya kupitia *Kimya Kimya Kimya* (2011) vilevile anaendelea kupigania uongozi bora wa nchi yake licha ya kusingiziwa na babake kuwa ni mkorofi.

5.2.3 Kutishwa, Kupigwa, Kukanwa na Kutengwa kwa Mwanamke Kiongozi

Kumtisha mtu ni kumtia hofu au kumwogofya (TUKI, 2014). Kwa kurejelea *Pango* (2003) Ngwese anatumia vitisho ili kumfanya Katango asiwanye uongozi. Anamtishia Katango:

Basi nitakunyamazisha mimi! Karibuni tutaona! Tutaona ni nani aotaye! Kuna siku itakuchea, siku moja nakwambia. Siku hiyo utajuta nakwambia! Utajuta karibuni

nakwambia! (uk.14).

Kwa kuangazia kipengele cha lugha katika nadharia ya udenguzi, lugha iliyotumiwa husaidia uibuaji wa maana ndani mwa matini (Bakhtin, 1981). Uradidi wa maneno: ‘tutaona’, ‘siku’ na ‘utajuta’ yanasisitiza namna Ngwese anavyomtisha kiongozi Katango. Kwa mujibu wa Mishra (2018), matini husheheni maana mbalimbali. Maana mbalimbali zaweza kuibuliwa kutokana na onyo la Ngwese kuwa atamnyamazisha Katango. Kwa kurejelea usemi huu, huenda Ngwese alikuwa akipanga kumvamia, kumwumiza, kumfisha, kumfanyia uchawi au kumfanya awe bubu. Maana hizi zote zinaonyesha namna Ngwese alivyoapa kumhasirisha kiongozi Katango.

Kwa mujibu wa udenguzi, maana mbalimbali zaweza kuibuliwa ndani mwa matini (Miller, 1976). Usemi wa Ngwese kuwa angemnyamazisha Katango unaweza kuibua maana mbili: moja ni kuwa Ngwese alinua kumwua Tunu; pili ni kuwa Ngwese alinua kumtenda Katango madhila ambayo yangemfanya kuacha kumpinga kisiasa. Siku anayosema Ngwese kuwa Katango atajuta iliwadia ambapo Ngwese alitumia Mtu I na II kumvamia Katango akiwa na Kibwana njiani. Lengo la uvamizi huu huenda lilikuwa kumuogofya au kumwumiza Katango ili aache kuwania uongozi wa Pango. Azma hii anaieleza wazi Mtu I:

Tangu leo ukome, unasikia? Usijitie kumpinga Mzee. Kigoda cha Pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? (uk.32).

Usipokoma hata tutaku... (uk32).

Kupitia usemi huu wa Mtu I, Katango anatiwa hofu na Mtu I ili asite kumpinga Ngwese katika kugombea wadhifa wa kiongozi wa Pango.

Aidha, Ngwese kwa kuambiwa ukweli na Katango kuwa amepofushwa na ushirikina, anamtisha Katango asiendeleo kusema. Kwa hasira anamwambia:

Mwanamke wee, usinitusi (uk.12).

Katango anapojitokeza kudadisi madai ya Seki (babake) kuwa mwanamke haruhusiwa kushika mishale katika jamii ya Pango, Seki anamtisha asimkate kauli kwani kitendo hiki kinaweza kumhasirisha:

La...usinikate kauli. Kitendo kama hicho kinaweza hata kukuletea nuhusi... (uk19).

Seki vilevile anamtisha Katango ili asimpinge Ngwese katika kugombea uongozi kwa kuwa utamaduni wa Pango haukuruhusu. Kulingana naye mwanamke katika muktadha wa utamaduni

wa Pango alikuwa mfuasi tu wala si kiongozi. Anamlinganisha mwanamke na mkia ambao hauwezi kuongoza kichwa.

Bw. Binafsi katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) anamkaripia Mpya:

Inamisha kichwa chako nakwambia! Wacha kunitumbulia macho yako makubwa! (uk.34).

Aidha Bw. Binafsi anamtisha Mpya wakati Mpya anapodhihirisha ulumbi wake. Anamkaripia:

Fumba kijaluba chako! Nani kakuruhusu kufungua domo lako chafu hapa? (uk.39).

Kwa mujibu wa Ntaragwi (2004), mhakiki wa matini anayetumia nadharia ya udenguzi hana budi kuchunguza lugha iliyotumiwa kwani ni kupitia kwa lugha hii ndipo maana mbalimbali zaweza kuibuliwa. Miller (1976) anadai kuwa kila neno ndani mwa matini huwa na maana ilyojengwa ndani mwake. Neno 'kijaluba' lilotumiwa katika usemi huu lina maana ya kisanduku kidogo cha kutilia vitu (TUKI, 2014). Bw. Binafsi analenga kusitisha ulumbi na utetezi haki wa kiongozi Mpya kwa kuuita mdomo wake kijaluba na kudai kuwa mdomo wake ni mchafu. Aidha, Bw. Binafsi anamtahadharisha Mpya dhidi ya kumpinga kisiasa na kudai kuwa akifanya hivyo atalaaniwa:

Mtalaaniwa nyinyi. Mtakosa radhi zangu. Mtakosa kila kitu (uk.42).

Kiongozi Bikisiwa analalamika kuwa Sogoramaneno amejaa vitisho, viapo, vikwaru na mabavu. Bikisiwa anaposhikilia msimamo wake thabiti kuwa hawezi kuolewa kwa Sogoramaneno, Sogoramaneno anamtisha:

N'najua njia ya kupita, nitakupata yu wewe. Mimi nitakupata wewe siku moja. Usinione bwege wala usijidai mbabe sana. Werevu na maarifa yako vina ukomo (uk.60).

Utamaduni wa Kiafrika ulihalalisha tendo la mwanamume kumpiga mwanamke na kuharamisha tendo la mwanamke kumpiga mwanamume (Mapunjo, 2014; Hora, 2014). Muktadha kama msingi mojawapo wa nadharia ya udenguzi husisitiza kuwa maana katika lugha huibuliwa ndani mwa muktadha fulani wa kimatumizi. Uelewa wa muktadha kulingana na wanaudenguzi ni suala la mtikati kwa mchanganuzi wa matini (Bakhtini, 1981; Onyoni, 2012). Katika tamthilia ya *Pango* (2003) muktadha wa utamaduni wa Pango ulihalalisha tendo la mwanamke kuchapwa. Ngwese ana mtazamo huu wa kitamaduni kuwa mwanamke ni chombo cha kupigwa na mwanamume.

Ngwese anamtisha Katango:

Nitakupapata makofi wewe...Unatakiwa kuolewa ili utiwe adabu na mumeo! (uk.14).

Wanaudenguzi husisitiza kuwa lugha ni kipengele muhimu cha matini na kwamba lugha hubeba maana (Derrida, 1973; Miller, 1976). Nahau: papata makofi iliyotumiwa katika usemi huu wa Ngwese inabeba maana ya kupiga mtu kwa makofi (TUKI, 2014). Nahau hii inasisitiza mtazamo wa Ngwese kuwa mwanamke katika muktadha wa kitamaduni alifaa kuchapwa ili kutiwa adabu. Kwa mujibu wa Levinas (2003) maneno huashiriwa kutokana na ulimwengu na mtazamo ambao hutazama jambo fulani. Mtazamo kuwa mwanamke ni chombo cha kupigwa vilevile unashikiliwa na Mtu I na II ambao wanamvizia kiongozi Katango njiani. Mtu I anamfinya, anambana, na kujaribu kumpiga Katango kofi.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016) Tunu anajitokeza kwa ujasiri kupinga maovu ambayo Majoka aliwatendea Wanasagamoyo. Tunu analenga kuleta wachunguzi wa kimataifa kuchunguza upya ajali ya Jabali ambaye aliuawa na serikali ya Majoka (uk.35). Uongozi wa Tunu unamfanya Majoka na washauri wake kupanga njama ya kumwua Tunu. Hata hivyo mpango huu unatibuka kwa kuwa vijana waliotumwa kutekeleza mauaji ya Tunu hawakupewa maagizo ilivyokuwa imepangwa. Kiongozi Tunu katika uvamizi huu anavunjwa mguu. Inambidi atumie kiti cha magurudumu kwa muda. Siti anabainisha madhila anayoyapitia Tunu kutokana na uvamizi huu. Anamwambia Tunu:

Maskini Tunu, bado una maumivu. Pole dadangu utapona inshallah (uk.54).

Katola (2006) Katika uhakiki wake wa tamthilia za *Hatia* (1972), *Mama eeh* (1987), *Buriani* (1983) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) alihitimisha kwamba, matokeo ya dhuluma dhidi ya mwanamke ni mitazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Dhuluma dhidi ya kiongozi Tunu zinachochea wafuasi wa Majoka kama Ngurumo kutompigia Tunu kura.

Isitoshe, Majoka anamtisha Tunu kwa kupinga uongozi wake:

Tunu, naona watia vyanda kwenye mdomo wa simba- huo ni mchezo hasi (uk.41).

Nadharia ya udenguzi husisitiza kuhusu uchunguzi wa kina wa maneno ndani mwa matini ili kubaini maana (Mishra, 2018). Neno simba lilotumiwa katika dondoo hili ni jazanda

inayomlinganisha Majoka na mnyama mkali. Majoka anamtahadharisha Tunu kuwa tendo lake la kumpinga lilikuwa likimkasirisha.

Kwa mujibu wa *Kimya Kimya Kimya* (2011) Mpya anapojasirika na kujitokeza kupinga uongozi wa babake, anatengwa na kukanwa na babake aliyeitwa Bw. Binafsi. Mwandishi anadhihirisha kutengwa kwa Mpya anapoeleza:

Familia ya Mzee Binafsi iko mezani. Mpya, mdogo wao wa miaka ishirini na moja hivi.

Kaketi upande mmoja peke yake. Kama vile katengwa na wengine (uk.26).

Bw. Binafsi anaamrisha walinzi wamburure Mpya kwa kuwa Mpya amejitokeza kupinga uongozi wake. Huku walinzi wakimburura, Bw. Binafsi anamfukuza na kumwambia:

Toka, toka, tokaaaa...Toka, toka, tokaa... (uk.41).

Mpya anapojitokeza kwa ujasiri kupinga uongozi wa babake, anamkana na kumwona kama mharibifu. Bw. Binafsi anaiambia familia yake:

*Huyu labda si mtoto wangu. Watoto wangu kweli hawawezi kunipaka **kinyesi** kama anavyonipaka yeye huyu (uk.40).*

Ukipaka mtu kinyesi utakuwa umemchafua na kumharibu. Kwa kutumia neno: kinyesi, Bw. Binafsi anamsawiri Mpya kama mtu mharibifu na chanzo cha matatizo yake.

Lengo la kumtisha, kumpiga, kumkana na kumfukuza mwanamke ni kumfanya aache juhudi za kuongoza jamii. Japo mwanamke kiongozi anatishwa na kupigwa, anaendelea kupigania nafasi yake ya kuongoza jamii. Katango katika *Pango* (2003) anapovamiwa na Mtu I na II anamwambia mamake:

Ndiyo mama, anataka (Ngwese) niache nia ya kumpinga lakini siwezi...! (uk.34).

Tunu katika *Kigogo* (2016) anaendelea kuongoza Wanasagamayo kutetea haki zao hata baada ya kupigwa na kuvunjwa mguu. Mpya katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) anaendelea kupigania haki za wananchi licha ya kufukuzwa nyumbani kwao.

Imebainika kupitia utafiti huu kuwa mwanamke kiongozi katika tamthilia nne zilizoteuliwa na utafiti huu anatishwa. Katango katika *Pango* (2003) anatishwa na Ngwese; Mtu I na Seki (uk.14, 19, 32); Bikisiwa katika *Posa za Bikisiwa* (2008) anatishwa na Sogoromaneno (uk.60); Mpya katika *Kimya Kimya Kimya* (2011) anatishwa na babake (uk.39) naye Tunu katika *Kigogo* (2016) anatishwa na Majoka (uk.41). Katika *Pango* (2003) vijana waliolipwa na Ngwese walimvamia

kiongozi Katango njiani. Katika uvamizi huu, mwanamume Kibwana ambaye alikuwa ameandamana na Katango ndiye anayepigwa kipigo cha nyuma (uk.31). Katango anamweleza mamake kuwa hakuumia kutokana na uvamizi huo (uk.33). Katika *Posa za Bikisiwa* (2008) hatumwoni Bikisiwa akipigwa au kuumizwa popote tamthiliani. Katika *Kimya Kimya Kimya* (2011), hatumwoni Mpya akipigwa popote tamthiliani. Tunachokiona ni Mpya akibururwa na walinzi kama gunia na kufukuzwa kwao (uk.41). Hata hivyo, tamthilia ya *Kigogo* (2016) ndiyo tamthilia pekee kati ya tamthilia nne teule za utafiti huu iliyomsawiri mwanamke kiongozi akipigwa, kuumizwa na kutaka kuuawa. Lengo la matendo haya lilikuwa kumwua Tunu ili asiibuke kiongozi wa Sagamoyo. Tunu anamwambia Siti aliyekuwa amemtembelea:

Inshallah! Nimeona ashekali sasa. Daktari aliniambia nitaweza kutembea vizuri bila magongo baada ya miezi mitatu. Waliniumiza mfupa na muundi (uk.54).

Mwamzandi (2013) kwa kutumia nadharia ya udenguzi alieleza kuhusu dhana ya kivuli cha maana. Kulingana naye, kivuli cha maana ni ile maana mpya ndani mwa matini ambayo huwa imejificha na aghalabu huenda isibainike iwapo matini hayatachanganyuliwa kwa kina. Kupitia uchunguzi wa *Kigogo* (2016), tendo la Tunu kupigwa na kuvunjwa mguu linaibua maana mpya. Tendo hili linamsawiri Tunu kama mwanamke anayepitia dhuluma ama changamoto ya kiwango cha juu ikikumbukwa kuwa Tunu alikuwa amepangiwa njama kuuawa (uk.35). Kinaya ni kuwa, dhuluma hii haimfanyi Tunu kuacha kupigania uongozi bora Sagamoyo.

Katola (2006) alipohakiki tamthilia nne; *Hatia* (1972), *Mama Eeh* (1987), *Buriani* (1983) na *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) alidai kuwa mifumo ya kijamii iliyojaa taasubi ya kiume imechangia kumdhulumu mwanamke. Aliibua kuwa mhusika mwanamke katika tamthilia zake teule amedhulumiwa kwa; kutishwa, kutusiwa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa. Kulingana naye, dhuluma hizi huibua mitazamo hasi kumhusu mwanamke na kufanya apewe nafasi ya pili baada ya mwanamume. Utafiti huu umebaini kwamba mwanamke kiongozi katika tamthilia za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 anapojitokeza kuongoza jamii yake anadharauliwa na kukejeliwa, anasingiziwa, anatishwa, anatusiwa, anapigwa, anakanwa na kutengwa. Hata hivyo, dhuluma hizi hazimkatishii tamaa ya kuongoza. Kiongozi wa jinsia ya kike katika tamthilia hizi anazikabili dhuluma hizi na kuibuka mshindi.

Keter (2013) alipohakiki tamthilia ya *Kifo Kisimani* (1981) na *Natala* (1997) alidai kuwa mwanamke amekabiliwa na changamoto mbalimbali katika harakati zake za kujikomboa. Baadhi

ya changamoto hizi kulingana naye ni kama vile utamaduni, uhafidhina, kutoshirikishwa katika maamuzi na hali ya kutojua miongoni mwa wanawake. Kulingana na Keter, changamoto hizi zinamzuia mwanamke kujikomboa na kujenga jamii mpya. Were (2012) katika uhakiki wake wa tamthilia za *Kilio cha Haki* (1981) na *Kijiba cha Moyo* (2012) alidai kuwa, ingawa mwanamke ana uwezo, changamoto anazozipitia humzuia kuafikia uwezo alio nao. Utafiti huu umekubaliana na Keter na Were kwamba mwanamke anakabiliwa na changamoto mbalimbali katika juhudi zake za kuongoza. Hata hivyo, utafiti huu umebaini kwamba changamoto anazokumbana nazo mwanamke kiongozi katika tamthilia za tangia 2000 hadi 2016 hazimzuii kuongoza jamii yake. Anakabiliana na changamoto hizi na kuibuka kiongozi.

5.3 Athari Chanya za Taswira ya Mwanamke Kiongozi kwa Uongozi wa Mwanamke katika Tamthilia teule za Kiswahili

5.3.1 Kubadilika kwa Mitazamo Hasi Kumhusu Mwanamke Kiongozi

Kwa mujibu wa Hooks (1998) kuibua maana kutoka kwa mtazamo mpana huibua maswali mapya na changanuzi mpya. Udenguzi kama nadharia ya utafiti huu husisitiza umuhimu wa mhakiki kuchanganua mitazamo iliyopo ili kuibua maana (Levinas, 2003).

Kwa kurejelea tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) mwanzoni, Mfalme ambaye ni babake Bikisiwa ana mtazamo kuwa ni sharti amfanyie Bikisiwa uamuzi wa mume atakayemwoa. Sogoramaneno ajapo kuleta posa za kumposa Bikisiwa, Mfalme anazipokea bila kushauriana na Bikisiwa, mkewe na wananchi (uk.17). Baada ya Bikisiwa kujitokeza kwa uwazi na kutetea haki yake ya kuolewa kwa mume amtakaye, Mfalme anabadili mtazamo wake na kuamua kumpa Bikisiwa uhuru wa kuchagua mchumba amtakaye. Anakubali pendekezo la Bikisiwa la kushauriana na umma kuhusu posa yake. Anaandaa mkutano mkubwa na wananchi kuwaeleza mtazamo wake mpya. Anawaeleza:

Sisi tumempa (Bikisiwa) uhuru kamili. Posa ni baina yake na wale watakaomposa (uk.63).

Kwa mujibu wa muktadha wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*, posa ni fumbo lililotumiwa kuashiria mahusiano ya kimataifa kati ya nchi ya Bikisiwa na nchi zingine (uk.73). Kwa msingi huu, Mfalme anamaanisha kuwa amempa Bikisiwa mamlaka ya kufanya uamuzi kuhusu

uhusiano kati ya nchi yake na nchi atakayoichagua Bikisiwa. Bikisiwa anasisitiza kwamba anataka uhusiano utakaoleta faida kwa jamii.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) Mpya anapojitokeza kwa ujasiri kuzungumzia uongozi mbaya wa babake na kupigania uongozi bora, mamake ana mtazamo hasi. Anamtazama Mpya kwa jicho kali la hasira (uk.32). Mitazamo kulingana na wanaudenguzi huwa muhimu katika kuibua maana ndani mwa matini (Ntaragwi, 2004). Mtazamo hasi wa Bi. Shoo unabadilika baada ya Mpya kudhihirisha kuwa yeye ni kiongozi jasiri, mkakamavu na mwenye msimamo thabiti. Mabadiliko ya kimtazamo yanadhihirika Bi Shoo anapomwambia mumewe:

Siwezi kumtupa mtoto wangu hasa kwa sababu ni msema kweli. Heri tuondoke sote (uk.43).

Isitoshe, anamshika Mpya mkono na kuanza kutoka naye nyumbani mwao baada ya Bw. Binafsi kuamrisha walinzi kumburura Mpya (uk.42). Tendo hili laonyesha namna mwelekeo wa Bi Shoo kwa Mpya unavyobadilika.

Mwanzoni Mussa na Zanga wanaunga mkono uongozi wa baba yao Bw. Binafsi. Mwanzoni, Mussa anadai kuwa Mpya ana utoto. Dai hili linatokana na tendo la Mpya la kujitokeza kuzungumzia ubaya wa uongozi wa babake.

Nadhani Mpya anasumbuliwa na utoto. Anatafuta mchezo tu. Anataka kucheza tu, basi! Anataka kucheza mchezo wa kuigiza! (uk.50).

Mpya anapojitokeza kuwashawishi, Mussa na Zanga wanabadili mtazamo wao na kuamua kuungana na Mpya kupigania uongozi bora. Zanga anasema:

Sasa nimeshajua (uk.55).

Mussa naye anasema;

Sasa tumeshatambua (uk.53).

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kigogo* (2016) Kenga ni mshauri mkuu wa Majoka. Mwanzoni Kenga akiwa mshauri mkuu wa Majoka anamsawiri Tunu kwa uhasi kama mtu duni na dhaifu asiyeweza kuongoza Sagamoyo. Anasema:

Tunu hawezi kupigiwa kura hata! (uk.33).

Isitoshe, Kenga anapanga njama ya kumwua Tunu (uk.35). Anakejeli shahada ya uzamifu ya Tunu (uk.32). Uongozi wa Majoka unapofika mwisho, Kenga anamwambia Majoka kuwa amekubali uongozi wa Tunu (uk.91). Kutokana na ukakamavu, uthabiti, ujasiri na ushawishi wa kiongozi Tunu, Kenga anabadili mtazamo wake kwa Tunu na kumsawiri kwa uchanya. Maneno yake yanabainisha namna mtazamo wake kumhusu Tunu ulivyobadilika. Anasema:

Yote yawezekana na Tunu (uk.87).

Tunu, Siti na Sudi wanapoenda ulevini kwa Mamapima kuwaalika watu waje kwa mkutano wake, Mamapima anawafukuza na kutishia kuwaadhibu vikali (uk.62). Tunu anaendeleza juhudi zake za kutetea uongozi bora jimboni mwake kwa bidii na ukakamavu. Inapobainika kuwa uongozi wa Majoka umefika ukingoni na Tunu kukwezwa uongozini, Mamapima anamjia kiongozi Tunu huku akilia, kuinua mikono, kutaka kumusu na kumuomba msamaha Tunu (uk.92).

Kwa kurejelea tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016, kuna baadhi ya wahusika ambao mwanzoni wana mitazamo hasi kumhusu mwanamke kiongozi ila mitazamo hii inabadilika na wanaanza kumuunga mkono. Mabadiliko ya mitazamo kutoka hasi hadi chanya yanatokana na ujasiri, ukakamavu na msimamo thabiti wa kiongozi wa jinsia ya kike.

Mulila (2009) katika uhakiki wake wa tamthilia ya *Zilizala* (2006) na *Chamchela* (2007) alihitimisha kuwa mwanamume ndiye kisiki kikubwa cha ukombozi wa mwanamke. Utafiti huu umeibua kuwa, wanaume: Ngwese na Seki katika *Pango* (2003), Bw. Binafsi katika *Kimya Kimya Kimya* (2011), wanaumme waposaji katika *Posa za Bikisiwa* (2008), Ngurumo na Majoka katika *Kigogo* (2016) wanapinga juhudi za mwanamke kuibuka na kuongoza jamii. Hata hivyo, wanaume: Kikubi katika *Pango* (2003), Sudi katika *Kigogo* wanamuunga mkono mwanamke na kumsaidia katika juhudi zake za kuongoza jamii. Kwa kuangazia tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016, utafiti huu umebaini kuwa japo kuna baadhi ya wanaume wanaomzuia na kumpinga mwanamke kupitia kwa maneno, matendo na mitazamo yao, kuna wale wanaomkweza na kuendeleza uongozi wao. Imebainika kuwa kuna baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume ambao mwanzoni walikuwa na mitazamo hasi kwa mwanamke kiongozi ila baadaye wanabadili mitazamo hii hasi na kumwunga mkono mwanamke. Mfano ni Kenga katika *Kigogo*, Mussa na Zanga katika *Kimya Kimya Kimya*, Mfalme katika *Posa za Bikisiwa*.

5.3.2 Kuheshimiwa, Kusherehekewa na Kusifiwa kwa Mwanamke Kiongozi

Kupitia *Pango* (2003), vijana wanamchezea ngoma Katango na kumsherehekea kwa udhati wa moyo kama kiongozi shupavu anayefaa kuliongoza Pango. Wakiwa katika uwanja wa kampeni wanasema:

Katango oyeee! Katango oyeee! Katango oyeee! (uk.39, 41).

Aiwa! Aiwa! Aiwa! (uk.39, 41, 43, 45)

Vijana wakiongozwa na Kibwana wanambeba juu Katango. Wanamwinua na kumbeba juu kwa juu kwa muda. Katika hali hii, mwanaume Kibwana anamsifia Katango:

Shujaa wetu Katango...Katango...Katango (uk.45).

Katika muktadha wa kisiasa, viongozi hubebwa juu aghalabu wanapotwaa ushindi. Tendo hili la kumbeba juu kiongozi wa kike ni taashira ya kuwa mwanamke ambaye kwa muda mrefu alikuwa ametwezwa sasa anakwezwa uongozini. Katango anasifiwa na kusherehekewa kwa sababu ya sifa za kiongozi bora alizo nazo kama vile ujasiri, usemaji kweli, ukakamavu, uthabiti na uzalendo. Kikubi anamsifia Katango kwa uthabiti na ukakamavu wake wakati anamlinganisha na jiwe la mango.

Si vijana tu wanaomsifu na kumsherehekea kiongozi Katango. Pindi tu ilipogunduliwa kuwa Ngwese na washirika wake walikuwa wanaliharibu Pango, kundi kubwa la wananchi wanamsifu na kumshereheka:

Aiwa! Aiwa! Aiwa! (uk.86).

Katango oyee! Katango oyee! Katango oyee! (uk.86).

Kundi hili la Wanapango linashikana mikono na kuimba kwa furaha kubwa. Katika wimbo wao wanamsifu Katango kwa kusema kuwa ni kimbunga msema kweli. Kulingana na Munga'atha (2012), mafumbo yaliyotumiwa ndani mwa matini huwa na maana fiche na mhakiki anayetumia nadharia ya udenguzi afaa kuchunguza mafumbo haya kwa makini ili kuibua mfichamo uliomo. Neno Kimbunga lina maana ya upepo wenye nguvu nyingi (TUKI, 2004). Kwa kumlinganisha Katango na dhoruba, Wanapango wanasifia ukakamavu na ujasiri wa Katango.

Kupitia tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2011), Bikisiwa anaheshimiwa na kusifiwa na wanaume waposaji. Lengo la sifa na heshima hizi ni kumshawishi kiongozi Bikisiwa akubali posa zao. Sifa na heshima hizi zinabainika kupitia kwa matendo na maneno.

Tendo la kwanza linalotuchorea sifa hii ni la kuinama. Hassan anainama kabla ya kumpa Bikisiwa kitabu kiitwacho *Fasili ya Watu wa Weusi*. Hassan mwenyewe anamwambia Bikisiwa kuwa anampa kitabu hicho kwa heshima kubwa (uk.30). SS anapomwona Bikisiwa anamwendea na kumwinamia kwa heshima kuu (uk.37). Vilevile, Biss anapoingia kuja kumposa Bikisiwa anamwinamia Bikisiwa kwa heshima na taadhima (uk.43). Baada ya Chachi kumpa Bikisiwa zawadi, anamwinamia kabla ya kumuaga na kutoweka (uk.50). Sogoramaneno vilevile anafuata mkondo huu. Anapoingia kwenye jukwaa, anainama mbele ya Bikisiwa (uk.55). Tendo hili la kuinama liliashiria heshima aliyopewa mwanamke Bikisiwa na wanaume waposaji ili akubali posa yao. Katika muktadha wa jamii nyingi, ukimwinamia mtu yamaanisha kuwa umemheshimu mtu huyo. Kwa mujibu muktadha wa utamaduni wa jamii za Afrika, ni mwiko kwa mwanamume kumwinamia mwanamke hata kama huyo mwanamke ni kiongozi. Katika muktadha wa baadhi ya jamii za Kiafrika, utamaduni humhitaji mwanamke kumwinamia mwanamume (Mosota, 2010). Hali hii imedenguliwa katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* ambapo wanaumme waposaji badala ya kuinamiwa na Bikisiwa, wanamwinamia Bikisiwa kwa taadhima.

Kando ya matendo haya, mwanamke kiongozi anasifiwa kwa maneno. Maneno huchangia kuwasawiri wahusika katika kazi ya fasihi (Mulokozi, 1996). Hassan anamsifia urembo wa Bikisiwa. Sogoramaneno vilevile anasifia uzuri wa Bikisiwa:

Na wewe kujaaliwa kuwa mwanamke mzuri kuliko wote (uk.56).

Ingawa wanaume waposaji katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) wanamsifu na kumsherehekea kiongozi Bikisiwa, wengi wao wanafanya hivi kwa maslahi yao tu ili Bikisiwa akubali posa zao na aolewe nao. Wao wana mtazamo kwamba mwanamke Bikisiwa ni chombo cha mapenzi. Kwa kuangazia kipengele cha mitazamo katika nadharia udenguzi, mitazamo husaidia kubaini maana ndani mwa matini (Hooks, 1988). Mtazamo huu wa wanaumme waposaji unamsawiri mwanamke Bikisiwa kama chombo cha mapenzi. Hassan anamsifu Bikisiwa hivi:

*Urembo wako na mapambo yako. Fuo zako za mwili. Konde za ujanajike wako... (uk.32).
Angalia bandari zako za mwili. Tazama mavuvi yako ya kike. Tafadhali Bikisiwa... (uk.32).*

Biss naye anamwambia Bikisiwa:

*Bahari izungukayo mwili wako ni shwari na ya kina. Bandari zako zote zimesitirika.
Raslimali za pekee Mungu alizokujalia ndani ya nafsi yako. Madini ni nini kuliko ardhi
ya kuotesha kila mmea ndani ya mwili wako? (uk.44).*

Chachi vilevile anamsifu Bikisiwa:

*Uso wako wenye bashasha umenitia mshawasha. Macho malegevu. Nyusi zako laini.
Kiwiliwili chako kimeumbika. Kimekufanya uwe na heba kubwa. Na si hivyo tu ...(uk.49).*

Picha ya mwanamke wanayotuchorea wanaume hawa waposaji (Hasaan, Biss na Chachi) ni ya mwanamke anayependeza kiumbo kwa lengo la kumshibisha mwanaume kimapenzi. Mule (1991) katika utafiti wake alihitimisha kuwa mwanamke amechorwa kama kiumbe duni na mtegemezi wa mwanaume. Mugambi (1982) katika utafiti wake alidai kuwa mwanamke kwa mujibu wa tamthilia zilizochapishwa nchini Kenya kati ya mwaka wa 1957 na 1981 amechorwa kama kiumbe duni anayetumiwa na mwanamume kuendeleza maslahi ya mwanaume na ambaye jukumu lake kuu ni kumhimili mwanaume. Kiongozi Bikisiwa anatambua kuwa wanaume waposaji wana mtazamo kuwa yeye ni chombo cha mapenzi cha kushibisha ashiki zao. Anatambua kuwa jukumu lake ni kuleta maongozi yatakayolinda maslahi ya nchi yake. Hivyo anakataa kupumbazwa na sifa za wanaume waposaji kwani si za dhati. Hassan anaposifia umbo lake anamweleza:

Hivyo ndivyo washairi mnavyoimba na kumvisha mwanamke kilemba cha ukoka (uk.32).

Aidha anamwambia Chachi:

*Basi tu! Umekuwa wimbo wenu nyinyi nyote. Mnadhani thamani ya mwanamke ni umbo!
Mara nywele, mara shingo, mara madodo, sijui kiuno...Mimi ni mtu bwana. Ninastahi
heshima kamili. Ninahitaji kutazamwa kama mtu siyo kitu cha kuchezea. Yataka uyaelewe
na uyashike vizuri sana (uk.49).*

Mtazamo wa Bikisiwa unaoabinika katika madondoo haya ni kwamba yeye ni mtu wa thamani anayejiheshimu. Hivyo, wanaume walio na mtazamo kuwa yeye ni chombo cha kutumiwa kimapenzi wafaa kubadili mtazamo wao na kumwona kama mtu wa thamani wa kuleta maendeleo katika jamii.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016), mwanamke kiongozi anasifiwa kidhati. Sudi anamsifu Tunu kwa kuchonga kinyago cha Tunu. Anakataa kumuundia Majoka kinyago licha ya vishawishi na vitisho vya kufanya hivyo na kuamua kuunda kinyago cha kiongozi Tunu. Kenga anapomwuliza Sudi achongacho, Sudi anamwambia kuwa anachonga shujaa halisi wa Sagamoyo, shujaa aliye mkubwa kuliko jina lake. Kitendo hiki cha Sudi kinamshangaza Kenga kwa kuwa hakuna kinyago cha mwanamke ambacho kimewahi kuchongwa Sagamoyo. Kenga anatazama kuwa shujaa huyo aliye chongwa na Sudi ni mrembo sana. Sudi anaendelea kumsifu shujaa Tunu kwa kusema kuwa urembo wake wa nafsi ni bora zaidi kuliko wa nje uonekanao. Anamsifia Tunu kwa Kenga:

Shujaa halisi wa Sagamoyo (uk.10).

Yeye ni mkubwa kuliko jina lake (uk.10).

Tendo lingine linalomsifu kiongozi wa jinsia ya kike ni la kubebwa. Kwa mujibu wa wanaudenguzi, uelewa wa muktadha ni muhimu katika kufasiri maana ndani mwa matini (Ntaragwi, 2014). Katika muktadha wa kisiasa, tendo hili lina maana ya kumsherehekea na kumsifu mtu kwa ushindi alioupata. Mathalani utapata katika muktadha huu mwanasiasa aliyeshinda uchaguzini akibebwa hobelahobela kumsifu na kumsherehekea kwa ushindi wake. Watu kwenye lango kuu la soko la Chapakazi wanambeba Tunu juujuu akiwa kwenye kiti chake (uk.88). Aidha, watu wawa hawa wanapiga makofi na kumshangilia Tunu kwa makofi na vigelegele (uk.89). Sudi anapomkabidhi Tunu kinyago chake (cha Tunu) mwenyewe akiwa na kinasa sauti, umati unashangilia (uk.93). Kiongozi Tunu anapewa sifa na kusheherekewa.

Kwa misingi ya nadharia yetu ya utafiti huu, maana katika lugha hubainika na kueleweka vyema kwa kuchunguza miktadha iliyopo. Mwanamke katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika alichorwa kama kiumbe duni ambaye kila wakati alifaa kujinyenyekesha, kumheshimu na kumtumikia mwanaume kwa utiifu mkubwa (Hora, 2014). Mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 anapojitokeza kuongoza jamii yake anaheshimiwa, anasherehekewa na kusifiwa. Baadhi ya sifa na heshima hizi ni za dhati na zingine za chati.

Kiango (1992) katika uhakiki wake wa tamthilia za Kiswahili nchini Kenya alidhihirisha namna mwanamke alivyosawiriwa kwa uhasi kama mtu mzinifu, mbaya, muuaji na maviaji mimba. Naye Keter (2013) kwa kuhakiki tamthilia za *Kifo Kisimani* (1981) na *Natala* (1997) alidai kuwa

mwanamke amechorwa kama mtu asiyestahili heshima. Imebainika kuwa, japo kuna baadhi ya wahusika katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka 2000 hadi 2016 ambao wanamdhalilisha mwanamke kiongozi, kuna wahusika ambao wanamheshimu, wanamsifu na kumshrehekea mwanamke kiongozi. Kusifiwa, kuheshimiwa na kusherehekewa kwa mwanamke kiongozi kunatokana na sifa chanya alizonazo kama vile ujasiri, ukakamavu, uadilifu na uthabiti.

5.3.3 Ushindi wa Mwanamke Kiongozi

Kupitia tamthilia ya *Pango* (2003) Katango anaibuka mshindi kama kiongozi wa Pango katika uwanja wa kampeni na kumpiku mpinzani wake Ngwese. Ushindi huu unamshangaza Ngwese (uk.45). Hata hivyo, Ngwese anatumia ufiisadi na kubatilisha ushindi huu. Baada ya kuwagawia wananchi matunda, baadhi ya wananchi wanabadili msimamo wao na kumwuunga Ngwese mkono (uk.47-48). Katango kwa ukakamavu anaendelea kupigania mabadiliko ya uongozi. Baada ya Ngwese kutangazwa mshindi, anaendeleza utepetevu na uongozi mbaya. Hata haendi kazini (uk.51). Inapodhihirika kuwa Katango alisema ukweli kuwa Ngwese analiharibu Pango na kurina asali, kundi la wananchi linamsherehekea Katango (uk.86). Katango anasongea katikati na kuanza kuongea. Ni wakati huu ndipo askari wanafika na kumtia Ngwese mbaroni kwa tuhuma za ufiisadi (uk.87). Huu unakuwa mwisho wa uongozi wa Ngwese. Kiongozi Katango anaibuka kiongozi wa Pango.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008) Bikisiwa ni binti ya mfalme. Ujasiri, uzalendo, ukakamavu na msimamo thabiti wa Bikisiwa unamfanya kumkataa Sogoramaneno na wanaume wengine waposaji (uk.64). Anafaulu kumshawishi babake kushauriana na umma kuhusu posa yake (uk.23). Nadharia ya udenguzi husisistiza kuwa matini hubeba maana mbalimbali ndani mwake na kuwa ni jukumu la mhakiki ni kuibua maana hizi kupitia usomaji wa kina wa matini Mishra, 2018). Kwa kurejelea muktadha wa tamthilia hii, posa ni fumbo linaloashiria uhusiano wa kimataifa kati ya nchi ya Bikisiwa na nchi zingine (uk.73-74). Kulingana na muktadha wa jamii ya Bikisiwa, mwana wa mfalme alitarajiwa kukabidhiwa mamlaka kutoka kwa babake. Jambo hili ndilo linalodhihirika wakati Bikisiwa anapomwambia Hassan:

Mwana wa Mfalme ni mfalme wa kesho (uk.31).

Babake Bikisiwa aitwaye Mfalme anaingia katika uhusiano na taifa lililowakilishwa na Sogoramaneno bila kushauriana na Bikisiwa wala wananchi. Kiongozi Bikisiwa anapochukua mamlaka kutoka kwa babake ya kumfanya kufanya uamuzi, anakataa uhusiano wa kimataifa uliokuwa umeanzishwa na babake na kuisistiza kuwa lazima uhusiano huu ulete faida kwa nchi yake (uk.64). Kutokana na juhudi za kuhamasisha umma kuhusu mahusiano ya kimataifa, inambidi Mfalme kumtambulisha Bikisiwa kwa umma. Bikisiwa anapewa mamlaka na babake pamoja na umma ya kuingia mahusiano na nchi ya chaguo lake. Huu ni ushindi kwa kiongozi Bikisiwa. Umma unamsherehekea ushindi huu na kuahidi kumfuata Bikisiwa kama kiongozi wao.

Kwa mujibu wa *Kimya Kimya Kimya* (2011) ujasiri, ukakamavu na uthabiti wa kiongozi Mpya unawafanya wananchi kushawishika na kumwamini. Wanamweleza Mpya:

Sauti yako inatueleza tunayoyajua. Sauti yako ni sauti yetu kwani wewe ni sisi na sisi ni wewe. Wewe na kaka zako mmefukuzwa nyumbani, lakini nyinyi mna nyumba zote za nchi hii-mnakaribishwa, karibuni (uk.75).

Mwamzandi (2013) alipoeleza kuhusu dhana ya kivuli cha maana alisema kuwa, kivuli cha maana ni maana ambayo huwa imefichwa ndani mwa matini ambayo mhakiki anayetumia udunguzi huhitajika kuibua. Katika dondo hili, wananchi wanaposema kwamba wamemkaribisha kiongozi Mpya manyumbani mwao hawamaanishi tu kumkaribisha. Wanamaanisha pia kuwa Mpya amefaulu kuwashawishi hadi wakakubali uongozi wake. Mpya anafaulu kuwashawishi wananchi kuungana pamoja na kutetea uongozi bora (uk.87). Umoja huu unasitisha uongozi mbaya babake wa aitwaye Bw. Binafsi. Mwisho wa uongozi wake unabainika wakati anashuka kwa matao ya chini huku akionekana kakata tamaa, kuhuzunika na kujuta. Bw. Binafsi anaondolewa mamalakani na Mpya kukwezwa uongozini (uk.87-88).

Kwa kuangazia tamthilia ya *Kigogo* (2016), Kiongozi Tunu anafaulu kuwashawishi wananchi kukutanika katika lango la soko la Chapakazi ili kutetea haki zao (uk.88). Wananchi wanasusia mkutano wa Majoka wa kusherehekea miaka sitini ya uhuru. Ni katika mkutano huu ambapo Majoka alinulia kumtambulisha mwanawe Ngao Junior ambaye angechukua nafasi ya kiongozi wa Sagamoyo baada yake (uk.37). Kifo cha Ngao Junior na kuporomoka kwa uongozi mbaya wa Majoka kunapisha uongozi wa Tunu. Wafuasi wa Majoka kama Kenga aliyekuwa mshauri mkuu

wa Majoka na Kingi aliyekuwa mkuu wa polisi wanabadili msimamo wao wa kisiasa na kumuunga mkono Tunu (uk.91). Awali, Kenga, Chopi, Mwango, Boza na Husda (mkewe Majoka) walikuwa wafuasi wa Majoka. Hawa wakiwa pamoja na Daktari wanamzunguka Majoka na kumtoa mamlakani. Tunu anakwezwa mamlakani (uk.93).

Ushindi wa mwanamke kiongozi katika tamthilia teule unaleta msisimko na matumaini makubwa katika jamii. Kupitia *Pango* (2003) Katango anapoibuka mshindi, wananchi wanafuatana huku wakicheza kwa furaha. Mwandishi anatueleza msisimko huu anaposema:

Wote (wananchi) wanashikana mikono na kuimba kwa furaha kubwa. Katango anaendelea kuinuliwa juu. Wanaondoka wakiimba wimbo huo kwa sauti ya juu. Mlio wa ngoma unaendelea mpaka taa zinapofifia kabisa (uk.88).

Kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi, maana mbalimbali zaeweza kuibuliwa kwa kuchunguza kwa makini lugha iliyotumiwa ndani mwa matini (Mung'atha, 2012). Kwa kuchunguza maneno yafuatayo yaliyotumiwa katika maelezo haya ya mwandishi: kuimba kwa furaha, kuinuliwa juu, sauti ya juu na mlio wa ngoma, maana mbili zinajitokeza. Moja ni kuwa Wanapango walikuwa na msisimko mkubwa kuhusu ushindi wa Katango. Pili ni kuwa walikuwa na matumaini makubwa kwa kiongozi wao Katango.

Katika *Kigogo* (2016), wananchi wa jimbo la Sagamoyo wanasimka wakati uongozi wa Majoka unapofikia ukingoni na Tunu kufanyika kiongozi. Wanamshangilia na kumwambia Tunu kuonyesha msisimko wao. Sauti ya wananchi inasema:

Hoyee...! Tunu tosha! Tunu ...uu! Tunu...uu! (uk.89).

Usemi huu unadhihirisha furaha na msisimko wa wananchi kwa kiongozi wao Tunu.

Kuna utamaushi mwanzoni mwa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011) unaotokana na uongozi mbaya wa Bw. Binafsi. Sauti Ndani ya Kisima inabainisha hili inaposema:

Hakuna uhai. Hakuna chakula. Hakuna maji. Hakuna ari ya kusema. Hakuna shime ya kutenda. Hakuna mori ya kukataa. Hakuna ushinde wa kushindana na kuchachamaa kujikwamua ... (uk.8).

Wahusika wa fasihi andishi aghalabu huwa wanadamu (Wamitila, 2008). Sauti imedenguliwa na mwandishi kama mhusika. Katika usemi huu, mwandishi hajatueleza ikiwa sauti hii ilikuwa ya jamii ya wanawake au wazee. Kwa kurejelea mhimili wa lugha katika nadharia ya udenguzi, maneno hubeba maana ambayo hubainishwa kwa uchunguzi wa kina wa maneno hayo (Derrida 1973; Miller, 1976). Takriri ya neno ‘hakuna’ katika usemi huu inasisitiza utupu na utamaushi uliokuwepo nchini. Pindi Mpya ajitokezapo kuongoza, sauti ii hii inasema:

Ishara njema...Ishara njema. Ishara njema...Njema, njema, njema, ishara njema (uk.21)
Kulingana na nadharia ya udenguzi, matini hubeba maana fiche ambayo hubainishwa na mhakiki kupitia usomaji na uchambuzi wa kina wa maneno (Mishra, 2018). Maneno: ishara njema yanaweza kuonekana kuwa maneno ya kawaida. Hata hivyo kwa kuchunguza uradidi wa neno hili, matumaini ya wananchi kwa kiongozi Mpya yanabainika. Uongozi wa Bw. Binafsi unapofika mwisho, wananchi wanasimka na kufurahia kuibuka kwa kiongozi wa jinsia ya kike. Wanasema;

Tuko sawa sisi, tuko sawa kabisa. Tuko sawa kama sahani na kawa (uk.80).

Mchezo umekwisha. Mchezo umefikia mwisho (uk.87).

Kwa kurejelea *Posa za Bikisiwa* (2008), ushindi wa Bikisiwa kama kiongozi atakayetetea maslahi ya nchi yake unawapa matumaini na kuwasisimua wananchi. Baada ya Bikisiwa kuwahutubia, wanapiga ngoma na kupiga shangwe. Wanainuka na kuanza kurukaruka na kucheza huku wakimwita Bikisiwa kwa jina mfululizo:

Bikisiwa, Bikisiwa, Bikisiwa (uk.64).

Kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi, maneno yaliyotumiwa ndani ya matini hubeba maana mbalimbali (Mishra, 2018). Maneno yafuatayo yalumiwa na mwandishi: kuinuka, kurukaruka, kucheza na kuita jina la Bikisiwa mfululizo yanabainisha furaha, msisimko na matumaini ya wananchi kwa kiongozi wao Bikisiwa.

Mulila (2009) katika uhakiki wake wa tamthilia alidai kuwa mwanamke hafaulu kujikomboa kwa sababu anapingwa na mwanamume. Katika uhakiki wa tamthilia za *Kifo Kisimani* (1981) na

Natala (1997) Keter alidhihirisha kwamba, japo mwanamke ana uwezo wa kujibidiisha vilivyo katika ujenzi wa jamii mpya, ukombozi wake unazuiliwa na changamoto zinazomkabili. Muniu (2013) alihakiki tamthilia za *Nguzo Mama* (1981) na *Mama Eeh* (1987). Kwa kutolea mifano ya Bi. Nane na Mwavita, anasema kwamba wanawake hawa wanaonekana kushindwa kwa sababu ya changamoto zilizowakabili. Isitoshe, Chacha (2013) alipofanya uhakiki wa tamthilia za *Nguzo Mama* (1981) na *Mama eeh* (1987) alihitimisha kuwa mwanamke hafaulu kupata haki kwa sababu ya changamoto anazokumbana nazo. Anatoa mfano wa wanawake Bi. Nane na Mwavita ambao wanaonekana kushindwa. Utafiti huu umebaini kuwa mwanamke kiongozi katika tamthilia za Kiswahilia tangia mwaka 2000 hadi 2016 anakumbwa na changamoto mbalimbali ila anakabiliana nazo na kuibuka mshindi. Ushindi wake unatokana na namna anavyojitokeza kama kiongozi mzalendo, jasiri, mkakamavu, mwadilifu, mshawishi, msema kweli, mwenye maono, mwenye msimamo thabiti, mwerevu na mwenye busara. Ushindi huu wa mwanamke kiongozi unaleta msisimko na matumaini makubwa kwa jamii yake.

5.4 Hitimisho

Katika sura hii, utafiti huu umeshughulikia athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Imebainika kuwa, tendo la mwanamke kiongozi kujitokeza kuongoza linamfanya adharauliwe, atishwe, atengwe, akanwe, afukuzwe, atusiwe, apigwe na kusingiziwa. Aidha tendo hili linabadilisha mitazamo hasi ya baadhi ya wanajamii na kumfanya asifiwe, asherehekehewe na kusifiwa. Japo mwanamke kiongozi anapitia changamoto mbalimbali katika azma yake ya kuongoza jamii, changamoto hizi hazididimizi juhudi zake. Mwanamke kiongozi anakabiliana nazo na kuibuka mshindi. Ushindi wake unafanya jamii kusionika na kuwa na matumaini makubwa. Imebainika kuwa mwanamke Kiongozi aitwaye Tunu katika tamthilia ya *Kigogo* (2016) ndiye anayepitia changamoto za kiwango cha juu akilinganishwa na mwanamke kiongozi katika tamthilia zingine tatu zilizoteuliwa na utafiti huu. Hata hivyo, Tunu anaibuka mshindi.

SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

6.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari wa utafiti huu. Hitimisho la utafiti huu limetolewa kwa mujibu wa matokeo yaliyojadiliwa katika sura ya nne na tano. Aidha, mapendekezo ya utafiti huu na wa baadaye yametolewa.

6.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulikuwa wa kithamano na umeshughulikia taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Katika sura ya kwanza, tasnifu jii imeshughulikia: usuli, swala, maswali, madhumuni, upeo, dhima, misingi ya uteuzi na nadharia ya utafiti. Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu: kupambanua taswira ya mwanamke kiongozi inayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016; kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kujenga taswira ya mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016; kutathmini athari ya taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke katika tamthilia za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Dira iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya udenguzi iliyoasisiwa na Derrida (1966) na kuendelezwa na Ntaragwi (2004). Mihimili mitatu ya nadharia hii ambayo ni lugha, mitazamo na muktadha ilifaa utafiti huu.

Katika sura ya pili, utafiti huu umehakiki tafiti za awali zinazohusu taswira ya mwanamke na mitindo ya lugha katika fasihi. Imebainika kuwa, nyingi ya tafiti hizi zilimsawiri mwanamke kiongozi kwa njia hasi na kwa ujumla bila kuangazia uongozi wake. Aidha, imeibuka kuwa mitindo ya lugha ni muhimu katika kuchambua maudhui ndani ya kazi ya fasihi. Sehemu hii vilevile imehakiki matumizi ya nadharia ya udenguzi katika tafiti za awali kwa lengo la kuibua vipengele muhimu vya kinadharia vya kufaulisha utafiti huu.

Katika sura ya tatu, utafiti huu umechunguza mbinu za utafiti. Utafiti huu umetumia muundo wa kiuchanganuzi na umejikita katika utanzu wa tamthilia. Kupitia kwa mbinu ya usampulishaji dhamirifu, utafiti huu uliteua na kurejelea tamthilia nne za Kiswahili zilizotungwa tangia mwaka wa 2000 hadi 2016 na ambazo zimelishughulikia suala la uongozi wa mwanamke. Tamthilia hizi

ni: *Pango* (Wamitila, 2003), *Posa za Bikisiwa* (King'ei & Mohammed, 2008), *Kimya Kimya Kimya* (Mohammed, 2011) na *Kigogo* (Kea, 2016). Mbinu ya maktaba imetumiwa kukusanya data. Kupitia mbinu hii, tamthilia teule zimesomwa huku data kuhusu sifa za mwanamke kiongozi, mitindo ya lugha na athari za taswira ya mwanamke kwa uongozi wa mwanamke ikinukuliwa kwa usaidizi wa orodha ya uchunguzi. Data kuhusu sifa za mwanamke kiongozi imetokana na matendo, lugha na mitazamo ya mwanamke kiongozi pamoja na wahusika wengine katika tamthilia teule. Data imechanganuliwa kupitia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo kwa mujibu wa muktadha wa tamthilia teule. Hatimaye, data hii imewasilishwa kupitia maelezo na matokeo kuibuliwa.

Sura ya nne na tano zimechanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Katika sura ya nne, sifa za mwanamke kiongozi zimeibuliwa na kupambanuliwa kutokana na data ilyokusanywa katika tamthilia teule. Aidha, mitindo ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi imechanganuliwa. Hatimaye, athari za taswira ya mwanamke kwa uongozi wa mwanamke imeibuliwa na kuelezwa kwa muktadha wa tamthilia teule. Katika sura ya sita, utafiti huu umeshughulikia muhtasari wa tasnifu, muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

6.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kupambanua sifa za mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili za tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Utafiti huu umeibua na kupambanua taswira ya mwanamke kiongozi. Uibuaji na upambanuzi huu uliwezekana kupitia kwa kubainisha na kuchanganua lugha, mitazamo na matendo ya mwanamke kiongozi pamoja na wahusika wengine katika tamthilia teule. Taswira ya mwanamke kiongozi iliyoibuliwa na kuelezwa na utafiti huu ni pamoja na: mwanamke kama kiongozi: mwenye msimamo thabiti; mzindushi na mtetezi wa haki; jasiri; mshawishi; msema kweli kwa uwazi; mzalendo; mkakamavu; anayejiheshimu na kuheshimu wengine; mwerevu na mwenye busara; mwenye lengo na maono; msomi na mlumbi.

Azma ya pili ya utafiti huu ilikuwa kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Utafiti huu umeweza kuchanganua mitindo mbalimbali ya lugha inayochangia katika ujenzi wa

taswira ya mwanamke kiongozi. Mitindo iliyochanganuliwa ni pamoja na: tashbiha, maswali ya balagha, takriri, methali, jazanda, nahau na misemo, kinaya na kuchanganya na kubadili msimbo.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kutathmini athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Utafiti huu umeibua na kutathmini athari chanya na hasi za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi wa mwanamke mujibu wa tamthilia teule. Athari hasi zilizoibuliwa katika utafiti huu ni: kudharauliwa, kukejeliwa, kusingiziwa, kutengwa, kukanwa, kutishwa na kupigwa kwa mwanamke kiongozi. Athari chanya zilizoibuliwa katika utafiti huu ni: kubadilika kwa mitazamo hasi kumhusu mwanamke kiongozi, kuheshimiwa, kusherehekewa, kusifiwa na hatimaye ushindi kwa mwanamke kiongozi.

6.4 Hitimisho la Utafiti

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kupambanua taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Utafiti huu unahitimisha kwamba, mwanamke katika tamthilia teule: *Pango* (2003), *Posa za Bikisiwa* (2008), *Kimya Kimya Kimya* (2011) na *Kigogo* (2016) amejitokeza kama kiongozi kuongoza jamii yake. Aidha, mitazamo, lugha na matendo ya mhusika mwanamke kiongozi pamoja na wahusika wengine katika tamthilia teule imechangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi. Utafiti huu vilevile umebaini kuwa mwanamke kiongozi kulingana na tamthilia teule amesawiriwa kwa njia chanya kinyume na tafiti za awali zilizomsawiri mwanamke kwa njia hasi. Mwanamke kiongozi katika tamthilia ya *Kigogo* (2016) amechorwa kama kiongozi mwenye upeo wa juu wa elimu. Isitoshe, imebainika kuwa mwanamke kiongozi kwa mujibu wa tamthilia teule hasubiri kupewa nafasi ya uongozi; anaipigania kwa bidii na hatimaye kufaulu kuwa kiongozi. Mwanamke kiongozi katika tamthilia teule anatumia uwezo wake kuleta mabadiliko na kuchochea maendeleo katika jamii iliyolemazwa na uongozi mbaya.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Utafiti huu umebaini kuwa mitindo ya lugha imechangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000. Kupitia uchanganuzi wa mitindo mbalimbali ya lugha katika tamthilia teule, picha ya mwanamke kiongozi imebainika.

Lengo la tatu la tasnifu hii lilikuwa kutathmini athari ya taswira ya mwanamke kwa uongozi wa mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za tangia mwaka 2000 hadi 2016. Imebainika kuwa, kujitokeza kwa mwanamke kiongozi kuongoza jamii kunaleta athari hasi na chanya kwa uongozi wake. Tendo hili linamfanya kudharauliwa, kukejeliwa, kusingiziwa, kukanwa, kutengwa, kutishwa na kupigwa. Athari hizi hasi zina misingi yake katika miktadha ya tamaduni za jamii katika tamthilia teule. Kwa upande mwingine, tendo hili linawafanya wahusika wengine kubadili mitazamo yao kumhusu mwanamke kiongozi na kumheshimu, kumsifu na kumsherehekea. Hatimaye, mwanamke kiongozi anaibuka mshindi. Ushindi wake unaleta msisimko mkubwa kwa jamii. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa, ingawa mwanamke anakumbana na changamoto mbalimbali katika juhudi zake za kusaka uongozi, changamoto hizi hazimzuii kujitokeza na kuongoza. Anazikiuka na kuibuka mshindi. Isitoshe, imebainika kuwa mwanamke kiongozi katika tamthilia ya *Kigogo* (2016) amepitia changamoto za kiwango cha juu kuliko mwanamke kiongozi katika tamthilia zingine tatu zilizoteuliwa na utafiti huu. Hata hivyo, anaibuka mshindi hatimaye.

6.5 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu unapendekeza kuwa watafiti wa kazi za fasihi wanaotafiti kuhusu taswira ya mhusika mwanamke wazingatie muktadha wa jamii husika. Hii ni kwa sababu taswira hii inaweza kubadilika kutegemea muktadha wa jamii ambamo fasihi imetungwa. Fasihi kama kioo cha jamii huakisi matukio katika jamii. Aidha, wahakiki wanaohakiki kuhusu mwanamke kiongozi katika fasihi andishi waweze kutofautisha kati ya mitindo ya lugha inayobainika kupitia usemi wa wahusika na ile inayobainika kutokana na maelezo ya mwandishi. Hii ni kwa sababu mtazamo wa mwandishi unaweza kuwa tofauti na wa wahusika katika kazi ya fasihi, hivyo kuathiri maana. Tatu ni kuwa, wanawake viongozi watumie changamoto zinazowakabili kama kichocheo cha kuendeleza uongozi wao. Wasiruhusu changamoto kulemaza au kudidimiza uongozi wao.

6.6 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye

Kuhusiana na tafiti za baadaye, utafiti huu unapendekeza watafiti wa baadaye wajitokeze kumlinganisha kiongozi wa jinsia ya kike na wa kiume ili kubaini utofauti au usawa uliopo kwa misingi ya uongozi wao. Wanaweza kujikita katika tanzu za fasihi au jamii. Aidha, watafiti wa baadaye wachunguze namna lugha ya mwanamke inavyoathiri uongozi wake au namna lugha hii inavyofanya uongozi wa mwanamke kufaulu au kudidimia. Isitoshe, watafiti wa baadaye wachunguze mchango wa wahusika wa jinsia ya kike na kiume kwa uongozi wa mwanamke. Wanaweza kuchunguza namna wahusika wanaume wanavyoendeleza au kudidimiza uongozi wa mwanamke ama namna wahusika wanawake wanavyoendeleza ama kudidimiza uongozi wa mwanamke.

MAREJELEO

- Afkhami, M. (2003). Misingi ya ujenzi wa uongozi: Uongozi bora kama shule ya mawasiliano katika C. Bwenge: *Kitabu cha Mafunzo ya Uongozi kwa Wanawake*. Bethesda: Women's Learning Partnership for Rights, Development & Peace (WLP).
- American Association of University Women (2016). *Barriers & Bias: The status of women in leadership*. Washington DC.
- Alreck, P. L. & Settle, R. B. (1995). *The survey research handbook* (2nd Ed). New York: R. R Donnelley & Sons Company.
- Althusser, L. (1971). *Lenin and philosophy and other essays*. London: New Left Books.
- Baloyi, M. E. (2009). *Patriarchal structures: A hindrance to women's right*. Saarbrücken: DDM Publishing Co.
- Bakhtin, M. (1981). *The dialogical imagination*. Austria: University of Texas Press.
- Barnett, R. C. (2008). *Gender leadership and the natural order*. Women's Studies Research Center, Brandeis University.
- Barry. P. (2011). *Beginning theory: an introduction to literary & cultural Theory*. Viva Books, 3rd Ed, India
- Bell, R. M. (2013). *Charismatic Leadership: Case Study with Ronald Reagan as Exemplar*. Regent University.
- Bensmaia, R. (2005). Post structuralism In L. Kritzan (Ed.). *The Columbia history of twentieth – century French thought*. New York: Columbia University Press.
- Berthes, R. (2011). *The death of the author*. Translated by A. Leavers, Smith & Hill, New York.
- Berthes, R. (1977). *Image, music*. Text translated by Stephen Heath, London: Fontana.
- Bertoncini, E. Z., Gromov. M. D., Khamis, S.A.M., & Wamitila K.W. (2009). *Outline of Swahili literature*. Leiden Boston: Brill.
- Brecken, D. (2004). Leadership vision and strategic direction. In the *Quality Management Forum*, vol. 30 (1).
- Carter, D. (2006). *Literary theory*. Reading: Cox & Wyman.
- Chacha, C. W. (2013). *Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Nguzo Mama na Mama Eeh*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Cheserem, S. (2011). *Female genital mutilation in Kenya: A literature review*. Tasnifu ya

Shahada, Chuo Kikuu cha Turku.

Clinton, H. (2014, March 19). *Hillary Clinton urges for equality of women & girls*. Retrieved from www.dailymail.co.uk/wires/ap/article-2575883/Hillary-clinton-urges-equality-women-girls.html on 15th November, 2015.

Creswell, J. W. (2003). *Research design: qualitative, quantitative & mixed methods approaches* (2nd Ed.). Thousand Oaks, CA: Sage Publications.

Conger. J. A., Kanungo. R. N., Menon. S. T. (2000). Charismatic leadership and follower effects. In *Journal of Organization Behavior*, 7, 747.doi: 102307/

Derrida, J. (1973). *Speech and phenomenon*. Evanston: North Western University Press.

Derrida, J. (1976) *Of grammatology*. Baltimore: John Hopkins University Press.

Derrida. J. (1977). *Structure, sign and play in the discourse of humanities: writing and difference*. Translated by A. Bass, University of Chicago, Chicago.

Donald, M. (2000). *A startup of her own*. Us News & World Report, Mei 15 2000.

Escholt, P. (1982). *Language awareness*. New York: St. Martin's Press.

Fairclough, N. L. (1992). *Discourse and social change*. Oxford: Polity Press.

Forster, E. M. (1927). *Aspects of the novel*. London: Penguin Books.

Foucault, M. (1978). *Pierre riviere*. Harmondsworth: Penguin.

Foucault, M. (1979a). *Discipline and punishment*. Harmondsworth: Penguin.

Foucault, M. (1979b). 'What is an author,' *Screen*.20 (1) (pp.13-33).

Foucault, M. (1981). *The history of sexuality* (vol.1): *An introduction*. Harmondsworth: Pelican.

Foucault, M. (1986). *The use of pleasure*. Harmondsworth: Viking.

Golafshani, N. (2003). *Understanding reliability & validity in qualitative research*. *The qualitative report*, 8(4) 597-606 nsuworks.nova.edu/.../viewcontent.cgi?...

Gikambi, H. (2012). *Said Ahmed ameandika vitabu 55, anasema mambo bado*. Retrieved from www.swahilihub.com/habari/MAKALA-/1310220/1416334/-/mpnys/-/index.html on 7th July, 2015.

Greenleaf, R. K. (2003). *The servant leader within: A Transformative path*. New York:

Panelist Press.

Groothuis, R. M. (1994). *Women caught in the conflict: The culture war between traditionalism and feminism*. Baker Books: Grand Rapids.

Hazelzet, M. (2013). *Access Denied! Girls' equal right to education in a global context, with a focus on Pakistan*. Leiden University.

Hora, E. A. (2014). Factors that affect women participation in leadership and decision making position. In *Asian Journal of Humanity, Art & Literature*, vol. No.2, Jimne University of Social Sciences, Ethiopia.

Hooks, B. (1988). *Talking back: Thinking feminist, Thinking black*. Boston: Southend Press.

Hourel, K. (2017). *Women candidates face curses and worse in Kenya elections*. Retrieved from www.reuters.com/article/us-kenys-election-women/women-candidates-face-curses-and-worse-in-kenys-election-idUSKBN1AK1E1 on 2nd September, 2017.

Hussein, J. W. (2005). The social and ethnocultural construction of masculinity and femininity in African proverbs. In *African Study Monographs*, 26(2) 59-87, Alemaya University.

Indede, F. (2011). *Mwanamke angali tata katika ushairi wa kisasa?* Retrieved from www.qucosa.de/fi/eadmin/data/qucosa/document on 3rd June, 2014.

Intezari, A. (2013). *Wisdom and decision making: Grounding theory in management practice*. Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Massey: Auckland, New Zealand.

Jalalzai, F. & Krook, M. L. (2010). Beyond Hillary and Benazir: Women's political leadership worldwide. In *International Political Science Review*. 31 (1), 8-21: Sage.

Kennedy, J. (2013). *Lessons in Leadership*. Royal Military Academy: Sandhurst.

Katola, E. (2006). *Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Keter, K. E. (2013). *Nafasi na utambulisho wa mwanamke katika Natala*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kiango, S. (1992). *Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

King'ei, K. (2002) "Suala la uana katika fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa utafiti kutoka Kenya" Katika I. Simala: *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Kinge'i, K. & Mohammed, S. A. (2008). *Posa za Bikisiwa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

- Kibera, L. (2013). *Best authors from Kenya*. Retrieved from <https://litaratureafrica.wordpress.com/tag/leonard-kibera> on 21st September, 2015.
- Kohlrieser, G. (2006). *Hostage at the table: How leaders can overcome conflict, influence others and raise performance*. Retrieved from www.imd.org/.../PFM149_LR_Kohlrieser.pdf on 5th April 2015.
- Kolzow, D. R. (2014). *Leading from within: Building organizational leadership capacity*. Haijachapishwa.
- Kombo, K. D. & Tromp L.A. D. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (1990). *Research methodology: Methods and techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.
- Kristeva, J. (1984). *Revolution in poetic language*. New York: Columbia University Press.
- Lacan, J. (1977). *Ecrits*. London: Tavistock.
- Lemer. H. (2003). The Practical qualities of effective leaders. In *the Scrivener*, vol. 12.
- Levinas, E. (2003). *Humanism of the other*. Chicago: University of Illinois Press.
- Lewis, H. H. (2012). *Barriers to women in roles of leadership in higher education: An examination of leadership texts*, George Fox University.
- Macha, F. (2012). *Kilio cha Fasihi ya Kiswahili- Mahojiano na Mwandishi stadi profesa Said Ahmed Mohammed*. Retrieved from: <https://kitoto.wordpress.com/2012/03/25/mahojiano-na-mwandishi-said-a-mohammed> on 12th August, 2015.
- Manyama, C. (2014). *Nadharia ya Udenguzi katika ujitokezaji wa wahusika wa tamthilia ya Kiswahili*. Retrieved from manyamacharles.co.ke/2014/11/nadharia-ya-udenguzi.html on 21st September, 2015.
- Mapunjo, G. C. (2014). *Usawiri wa mwanamke kama kiongozi katika tamthilia ya Kivuli Kinaisha na Nguzo Mama*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mason, M. (2010). Sample size and saturation in phd studies using qualitative interviews. *Qualitative Social Research*, 11(3).
- Matti, G. N. (2003). *Mwongozo wa kitumbua kimeingia mchanga*. Nairobi: Africanwide Network.
- Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics & Publishing

Company.

Mberia, K. (1997). *Natala*. Nairobi: Macmillan Publications.

Mbughuni, P. (1982). Images of women in Kiswahili prose fiction in *Kiswahili*, 49 (1), 80-110.

Mclaughlin, A. & Braxton, A. (Eds) (1990). *Wild women in the whirlwind Afro-American culture & contemporary literary renaissance*. New Brunswick: Rutgers University Press.

Mccullough, J. J. (2015) *Female leaders*. Retrieved from www.jjmccullough.com on 27 March, 2015.

Mdee, J. S, Njogu, K & Shafi, A. (2011). *Kamusi ya karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Meanza. A. (2009). *Factors affecting women participation in politics and decision making*. A Dissertation of M. A Thesis.

Migiro, K. (2013). *New laws ignored, so women trailed in Kenya 2013 election*. Retrieved from www.trust.org/item/20131205145820-u5bql/?source=dpaghead on 5/5/15.

Miller. J. H. (1976). Deconstruction and the Recovery of Transcendence. In G. Douglas Atkins: *Notre Dame English Journal*.vol. 13, No. 1.

Mirikau, S. A. (2011). *Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mlacha, S. A. K. (1993). *Kiswahili novels and the society*. Dar es Salaam: Education Publishers & Distributors.

Mohanty, T. C. (2003). *Feminism without borders: Decolonizing theory, practising solidarity*. Durham & London: Duke University Press.

Momanyi, C. (1998). *Usawiri wa mwanamke mwislamu katika jamii ya Waswahili inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya uzamifu; Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Momanyi, C. (2002). Suala la uana katika fasihi ya Kiswahili katika I. Simala *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Momanyi, C. (2013). *Waliochangia kukuza Kiswahili miaka 50 ya Uhuru Kenya*. Retrieved from www.swahilihub.com/habari/MAKALA/-/1310220/2110676/-/13WS64J/-/index.html on 29th September, 2015.

Moon, B. (2014, March 7). *Secretary General's speech*. Retrieved from

- www.unwoman.org/en/10/news/stories/2014/3/secretary-general-iwd-speech on 15th August, 2014.
- Moran, B. B. (1992). *Gender differences in leadership*. Library trends, 40(3), 475-491, University of Illinois.
- Morse, J. M. (2000). Determining sample size. *Qualitative Health Research*, 10(1), 3-5.
- Mosha, S. M. (2013). *Discourse analysis of gender-based violence in contemporary Kiswahili fiction: A Case study of selected novels of the past decades (1975-2004) and young Tanzanians' interpretation*. PhD Thesis: University of Waikato.
- Mosota, M. (2010). *Women thou shall kneel before thy men*. Retrieved from www.standardmedia.co.ke/business/article/20000/6047/women-thou-shall-kneel-before-thy-men on 3/7/17
- Mosoti, Z. M. (1993). *Maudhui katika tamthilia nne za Emmanuel Mbogo*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mturo, N. G. (2011). *Dhima ya Semi zilizoandikwa katika Daladala: Uchambuzi wa Vipengele vya Lugha na Dhamira*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mugambi, P. J. (1982). *Uhakiki wa maudhui katika tamthilia za Kenya zilizochapishwa*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003). *Research methods: Quantitative and Qualitative approaches*. Nairobi: African Center for Technology Studies.
- Mule, K. (1991). *Suala la mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa Kike katika njia panda*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mulila, J. L. (2009). *Usawiri chanya wa wahusika wanawake katika tamthilia za Zilizala na Chamchela*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.
- Muniu, G. G. (2011). *Ujagina wa mwanamke katika Pango*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mung'atha, R. (2012). *Ufumbuaji wa mashairi ya Kiswahili: Mfano wa Malenga wa Mvita na Malenga wa Vumba*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Munyaneza, J. (September 19, 2013). *Rwanda: women take 64 percent seats in parliament*. Retrieved from allafrica.com/stories/201309190110.html on 7/11/2015.
- Munyasia, N. & Wandiemba, C. (9th July, 2017). *Record number of women to run for elective position*. Retrieved from pawa254.org/record-number-women-run-elective-positions/ on 3rd August, 2017.
- Mureithi, F. (2015, October 29). *Rose Mwonya to take over as Egerton V. C.* Retrieved from www.nation.co.ke/news/Rose-Mwonya-to-take-over-as-Egerton-VC/-1056/29343501/1230ootwz/-/index-html on 2/12/2015.
- Murimi. M. (2015, November 26). *Gender equality ignored in cabinet reshuffle-Lichuma*. Retrieved from citizentv.co.ke/news/gender-equality-ignored-in-cabinet-reshuffle-lichuma-107238/ on 3/12/2015.
- Murungi, G. K. (2013). *Mtindo unavyoendelezwa maudhui katika Natala*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Murumba, J. B. (2011). *Mtindo katika Watu wa Gehenna*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mutua, J. (2007). *Mtazamo wa vijana na wazee kuhusu udhalimu katika tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Muthui E. K (2019). *Tathmini ya maudhui katika tamthilia teule za Kiswahili zinazotahiniwa shuleni za upili nchini Kenya: Mstahiki Meya (2009) na Kigogo (2016)*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya. Retrieved from <http://repository.seku.ac.ke/handle/123456789/4495> on 17th July, 2019.
- Mwamzandi, I. (2013). *Riwaya teule za karne ya ishirini na moja na udurusu wa nadharia za fasihi*. *Swahili Forum* 20: 48-66.
- Mwangi, D. K. (2005). *Uhakiki wa fani katika tamthilia za K.W. Wamitila*. Tasnifu ya uzamili; Chuo kikuu cha Nairobi.
- Mwanje, J. I. (2001). *Issues in social science research: Methodology series module 1*, organization of social science in Eastern & Southern Africa (OSSREA): Addis Ababa.
- Mwenderani, B. (2012). *Taswira ya mwanamke katika tamthilia ya Kilio cha Haki na Pango*. Tasnifu ya uzamili; Chuo kikuu cha Nairobi.
- Mwende. Y. (2015). *86 & counting:women leaders in Kenya's 11th parliament*. Retrieved from

www.slideshare.net/mobile/yvonnemwende//86andcounting bookweb 090315-47905028 on 2/12/2015.

- Ndungo, C. (1985). *Wanawake na mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili; Chuo kikuu cha Nairobi.
- Ngara, E. (1990). *Ideology & form in African Poetry*. Nairobi: Heinman Publishers.
- Nguta, (2011). *Fani na Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya Pango na Mama ee*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyamari, R. K. (2013). *Mtindo katika Utenzi wa Katirifu*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nyuta, W. J. (2016). *Mtindo katika kazi ya Kubuni za Lornard Sanja*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nonaka. I. & Takeuchi, H (2011). The big idea: The wise leader. In the *Harvard Business Review*. Retrieved from <https://hbr.org/2011/05/the-big-idea-the-wise-leader>.
- Ntaragwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Island: Augustina College.
- Nyamidie, J. K. E. (1999). *African proverb of the month*, September 1999. Retrieved from www.afriprov.org/african-proverb-of-the-month/25-1999 proverbs/146-sep1999.html
- Obama, B. (January 20, 2015). *State of the union address*. Retrieved from www.whitehouse.gov/the-press-office/2015/01/20/remarks-president-state-unionaddress-january-20-2015 on 15th February, 2015.
- Ogundipe-Leslie. M. (1994). *Recreating ourselves: African women & critical transformation*. Trenton: African World Press Inc.
- Ohly, R. (1990). *The Zanzibar challenge: Swahili prose in the years 1975-1981*. Windhoek, Namibia: African Studies of the Academy.
- Oluoch, F. (13th August, 2017). *More women elected in Kenya but the numbers still fall short*. Retrieved from www.theeastafrican.co.ke/news/women-elected-in-kenya-/2558-4954988-d8a9guz/index.html
- Onyoni, J. K. (2012). *Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Natala na Mama Ee*. Tasnifu ya uzamili; Chuo kikuu cha Nairobi.
- Oso, W. Y. & Onen, D. (2009). *A general guide to writing research proposal and report*.

Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Patton, M.Q. (1990). *Qualitative evaluation & research methods* (2nd Ed.). California: Sage.

Peck, J. & Coyle, M. (1984). *Literary terms and criticism*. Macmillan Education Ltd.

Randolph, J. J. (2007). *Twenty questions to methods choice*. Finland: Hamelin.

Ritchie, J. & Lewis, J. (Eds) (2003). *Qualitative research practice: A guide for social science students and researchers*. London: Sage Publications.

Rono, P. (2013). *Uhakiki wa kimaudhui na kifani katika Kidagaa Kimemwozea*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ruto, M. C. (2012). *Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sarara, M. M. (1997). *Maudhui katika tamthilia za S.A. Mohammed*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Selden, R. (1989). *Practicing theory and reading literature: An introduction*. New York: Harvest Wheatsheart.

Senzaba, E. (1997). *Tamthilia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *The prostitute in African literature*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*: Dar es Salaam, KAUTTU.

Simala, I. K. (2000). *Uhakiki wa sitiari za uana katika ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya uzamifu; Chuo Kikuu cha Moi.

Swila, I. N. (2000). Voluptuous vacuous vamps: Stereotyped representation of women in Kiswahili press. *African Study Monographs*, 21 (4), 159-171.

Syambo, B & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Trudgil, P. (1974). *Sociolinguistics: An introduction*. London: Penguin Books.

TUKI, (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

- TUKI, (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. New York: Oxford University Press.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa tamthilia: Historia na maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wandera, S.P. (2002). Utafiti wa masuala ya kijinsia katika Kiswahili katika I. Simala (mhariri). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.
- Wamalwa, D. N. (2005). *Mtoto wa kike kike katika riwaya ya Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Maseno.
- Wamitila, K. W. (2003). *Pango*. Nairobi: Focus Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Nairobi: Focus Publications.
- Wamitila, K. W. (2008). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Vide-muwa Publishers Ltd, Nairobi.
- Wanyonyi, C. M. (2011). *Uhakiki wa riwaya ya Nyuso za Mwanamke: mtazamo wa saikolojia changanuzi*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Weedon, C. (2004). *Feminist spractice and post structural theory* (2nd Ed). Malden: M.A.
- Were, E. (2012). *Fani katika tamthilia ya Kiswahili: Uchanganuzi wa Kilio cha Haki na Kijiba cha Moyo*. Tasnifu ya uzamili; Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- White. M. D & Mash. E.E (2008). *Content Analysis: A flexible methodology*. Urbana Champagne: University of Illinois.
- Woodhead, L. (2004). *Christianity: A very short introduction*. Oxford University Press.
- World Health Organisation (1998). *Female genital mutilation: An overview*. WHO, Geneva.
- Zate, K. (25th April, 2011). *Steve jobs and the importance of vision of leadership*. Retrieved from Eyes on sales: [http:// www.eyesonsales.com/contact/article-steve-jobs_the_importance_of_vision_to_leadership](http://www.eyesonsales.com/contact/article-steve-jobs_the_importance_of_vision_to_leadership).

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Sifa za Mwanamke Kiongozi

SIFA											
SIFA CHANYA						SIFA HASI					
		TAMTHILIA						TAMTHILIA			
		PS	PG	KM	KG			PS	PG	KM	KG
1.	JASIRI	√	√	√	√	1.	MGOMVI	x	x	x	x
2.	MSOMI	√	√	√	√	2.	MSALITI	x	x	x	x
3.	TAJIRI	x	x	x	x	3.	MMBEYA	x	x	x	x
4.	MLUMBI	√	√	√	√	4.	MZEMBE	x	x	x	x
5.	MPOLE	x	x	x	x	5.	DHALIMU	x	x	x	x
6.	MSHAWISHI	√	√	√	√	6.	MKALI	√	x	√	x
7.	MWEREVU	√	√	√	√	7.	MJINGA	x	x	x	x
8.	MWENYE BUSARA	√	√	√	√	8.	MBINAFSI	x	x	x	x
9.	MWENYE HURUMA	x	x	x	√	9.	MWENYE CHUKI	x	x	x	x
10.	MZALENDO	√	√	√	√	10.	MBINAFSI	x	x	x	x
11.	MWENYE KUHESHIMIWA NA KUSIFIWA	√	√	√	√	11.	MTEGEMEZI WA MWANAMUME	x	x	x	x
12.	MTETEZI WA HAKI	√	√	√	√	12.	ASIYE NA SHUKRANI	x	x	x	x
13.	MWENYE LENGU NA MAONO	√	√	√	√	13.	MWEPESI KUSHAWISHIKA	x	x	x	x
14.	MSALIHINA	x	x	x	√	14.	MPYARO	x	x	x	x
15.	MWENYE MSIMAMO THABITI	√	√	√	√	15.	ASIYEELIMIKA	x	x	x	x

MWONGOZO:

1. PS- POSA ZA BIKISIWA
2. KM- KIMYA KIMYA KIMYA
3. PG-PANGO
4. KG-KIGOGO
5. √ - NDIO
6. x - LA

Kiambatisho 2: Mitindo ya Lugha

	MITINDO YA LUGHA	PS	PG	KM	KG
1.	MBINU ZA LUGHA				
	a) Majazi	√	x	√	√
	b) Jazanda	√	√	√	√
	c) Tabaini	x	x	x	√
	d) Takriri	√	√	√	√
	e) Maswali ya balagha	√	√	√	√
	f) Methali	√	√	√	√
	g) Kubadili na kuchanganya msimbo	x	√	x	√
	h) Utohozi	√	x	x	√
	i) Semi na nahau	√	√	√	√
	j) Tashihisi	√	x	x	√
	k) Kinaya na kejeli	√	√	√	√
	l) Kweli kinzani	√	x	√	√
	m) Tanakuzi	x	x	x	x
	n) Tadmini	x	x	x	√
	o) Tasfida	x	√	x	x
	p) Mdokezo	√	√	x	√
2.	MBINU ZA SANAA				
	a) Nyimbo	x	√	x	√
	b) Taharuki	√	√	x	√
	c) Mbinu rejeshi	√	√	x	√
	d) Ndoto	x	x	x	√
	e) Sadfa	x	√	x	√
	f) Ushairi	√	√	x	√

MWONGOZO:

1. PS- POSA ZA BIKISIWA
2. KM- KIMYA KIMYA KIMYA
3. PG-PANGO
4. KG-KIGOGO
5. √ - NDIO
6. x - LA

Kiambatisho 3: Athari ya Taswira ya Mwanamke Kiongozi kwa Uongozi wa Mwanamke

TASWIRA		ATHARI	
		HASI	CHANYA
1.	MWENYE MSIMAMO THABITI	Kudharauliwa Kukejeliwa Kusingiziwa Kutishwa Kupigwa Kukanwa Kutengwa	Mtazamo hasi Kubadilika Kuheshimiwa Kusherehekewa Kusifiwa Ushindi
2.	MZINDUSHI NA MTETEZI WA HAKI		
3.	JASIRI		
4.	MSHAWISHI		
5.	MSEMA KWELI KWA UWAZI		
6.	MZALENDO		
7.	MKAKAMAVU		
8.	ANAYEJIHESHIMU NA KUHESHIMU WENGINE		
9.	MWENYE BUSARA		
	MWENYE LENGU NA MAONO		
10.	MSOMI		
11.	MLUMBI		

Kiambatisho 4: Barua ya idhini Kutoka Tume ya Kimaadili



MASENO UNIVERSITY ETHICS REVIEW COMMITTEE

Tel: +254 057 351 622 Ext: 3050
Fax: +254 057 351 221

Private Bag – 40105, Maseno, Kenya
Email: muerc-secretariat@maseno.ac.ke

FROM: Secretary - MUERC

DATE: 7th August, 2018

TO: Samuel Sinzore Ogonda
PG/MA/00042/2013
Department of Kiswahili and other African Languages
School of Arts and Social Sciences, Maseno University
P. O. Box, Private Bag, Maseno, Kenya

REF: MSU/DRPI/MUERC/00542/18

RE: Taswira ya Kiongozi Mwanamke Katika Tamphilia Teule za Kiswahili Tangia Mwaka wa 2000. Proposal Reference Number MSU/DRPI/MUERC/00542/18

This is to inform you that the Maseno University Ethics Review Committee (MUERC) determined that the ethics issues raised at the initial review were adequately addressed in the revised proposal. Consequently, the study is granted approval for implementation effective this 7th day of August, 2018 for a period of one (1) year.

Please note that authorization to conduct this study will automatically expire on 6th August, 2019. If you plan to continue with the study beyond this date, please submit an application for continuation approval to the MUERC Secretariat by 15th July, 2019.

Approval for continuation of the study will be subject to successful submission of an annual progress report that is to reach the MUERC Secretariat by 15th July, 2019.

Please note that any unanticipated problems resulting from the conduct of this study must be reported to MUERC. You are required to submit any proposed changes to this study to MUERC for review and approval prior to initiation. Please advise MUERC when the study is completed or discontinued.

Thank you.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Bonuke Anyona'.

Dr. Bonuke Anyona,
Secretary,
Maseno University Ethics Review Committee.



Cc: Chairman,
Maseno University Ethics Review Committee.

MASENO UNIVERSITY IS ISO 9001:2008 CERTIFIED



Kiambatisho 5: Barua ya Kuidhinisha Pendekezo la Utafiti



**MASENO UNIVERSITY
SCHOOL OF GRADUATE STUDIES**

Office of the Dean

Our Ref: PG/MA/00042/2013

Private Bag, MASENO, KENYA
Tel:(057)351 22/351008/351011
FAX: 254-057-351153/351221
Email: sgs@maseno.ac.ke


Date: 28th April, 2017

TO WHOM IT MAY CONCERN

**RE: PROPOSAL APPROVAL FOR SAMUEL SINZORE OGONDA —
PG/MA/00042/2013**

The above named is registered in the Master of Art in Kiswahili programme, in the School of Arts and Social Sciences, Maseno University. This is to confirm that his research proposal titled "Taswira ya Kiongozi Mwanamke katika Tamthilia za Tangu Mwaka wa 2000" has been approved for conduct of research subject to obtaining all other permissions/clearances that may be required beforehand.


Prof. J.O. Agure
DEAN, SCHOOL OF GRADUATE STUDIES



Maseno University

ISO 9001:2008 Certified

